**20 MEI, 2022**

# BUNGE LA TANZANIA

_____________

## MAJADILIANO YA BUNGE

_____________

## MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Ishirini na Saba – Tarehe 20 Mei, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. David M. Kihenzile) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa fedha 2022/2023.

**MHE. ALLY A. J. MLAGHILA K.n.y. MWENYEKITII WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, sasa namwita Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake.

Na. 228

**Kukarabati Shule za Misingi za Zamani**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukarabati Shule za Msingi za zamani katika Wilaya za Ileje na Mbozi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shule 2,147 shule za msingi kongwe nchini ambazo zilianzishwa kabla ya kupata Uhuru mwaka 1961. Hali ya miundombinu ya shule hizo ni mseto zikiwemo zenye hali nzuri na nyingine zenye miundombinu chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeanza kufanya tathmini ya hali ya miundombinu ya shule zote za msingi kupitia mradi wa *BOOST* ili kubaini mahitaji ya ujenzi wa miundombinu mipya ya shule na hali ya uchakavu wa miundombinu iliyopo. Tathmini hiyo imeanza mwezi Aprili, 2022 na itakamilika mwezi Julai, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya tathmini hiyo yatatumika kuandaa mpango wa uendelezaji na ukarabati wa miundomibinu ya Shule za Msingi kwa miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022 hadi mwaka 2025/2026.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ningependa niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; tunafahamu katika shule zetu nyingi za msingi miundombinu muhimu kama maji na umeme haipo. Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha miundombinu hii inapewa kipaumbele katika shule zetu hizi hususan katika Mkoa wangu wa Songwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; natamani kufahamu, huko kwetu shule nyingi za msingi zimekuwa

hazina vyoo, hususan kwa Mkoa wangu wa Songwe na hasa zaidi katika Wilaya yangu ya Momba? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu, Waziri David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba baadhi ya miundombinu ya maji pamoja na umeme ambayo tunayo ina changamoto kubwa. Moja ya Sera ya Serikali ni kuhakikisha sasa hivi kwenye taasisi zote hizo za kielimu zinapatiwa umeme pamoja na maji. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hilo lipo katika mpango wa Serikali na ndio maana sasa hivi unaona katika usambazaji wa umeme wa *REA,* wamekuwa wakiwapa vipaumbele taasisi hizo ambazo nimeziainisha hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusiana na maeneo mengi kukosa vyoo hususan shule zetu, katika bajeti ya mwaka huu, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyoo. Miongoni mwa vyoo tutakavyojenga ni katika Mkoa wa Songwe ambao yeye Mheshimiwa Mbunge ni Mbunge ambaye tunawakilisha pamoja. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tecla Ungele, swali la nyongeza.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi. Shule nyingi za Msingi za Mkoa wa Lindi ni za zamani, zimejengwa mwaka 1947 na zingine kabla ya hapo, ikiwepo ya Lionja, Ngunichile, Kivinje, Ntua na

kwingineko. Je, Serikali ina mkakati gani katika shule hizo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tecla, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Lindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu katika mpango ambao tathmini inafanyika ni pamoja na hizo shule ambazo ameziainisha katika Mkoa wa Lindi na tathmini yetu itakapokamilika tutaainisha maeneo yote kila mmoja ni wakati gani utatekelezeka. Kwa hiyo nimwondoe shaka kwenye hilo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jimbo la Tabora Mjini lenye kata 29 lina matatizo kama hayo, lina shule nyingi sana za msingi ambazo ni kongwe na wananchi wamekuwa wakifanya juhudi ya kuzikarabati kwa juhudi zao wenyewe. Je, ni lini hasa huo mpango utaanza huu wa kuzisaidia kukarabati hizi shule kongwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la

nyongeza la Mheshimiwa Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu umeanza mwezi Aprili mwaka huu na utakamilika mwezi Julai mwaka huu. Mara baada ya kukamilika, tunaanza utekelezaji. Nimhakikishie tu kwamba tuko ndani ya mwaka wa utekelezaji na tutafikia shule zote ikiwemo hizi ambazo yeye ameziainisha. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa George Mwenisongole. swali la nyogeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Mbozi ni moja ya Wilaya inayoongoza kuwa na shule nyingi za msingi, shule 179, lakini kiasi cha fedha za miundombinu na ukarabati zinazotoka Serikali Kuu kuja Wilaya ya Mbozi ni kidogo sana ukilinganisha na idadi ya shule 179. Sasa kwa nini Serikali isiangalie Wilaya ya Mbozi kwa jicho la tatu na kuangalia idadi ya hizi shule nyingi za msingi na kuongeza kiasi cha fedha kwa ajili ya miundombinu na ukarabati kwa ajili ya shule hizi za msingi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri David Silinde majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mwenisongole, Mbunge wa Jimbo la Mbozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba Jimbo la Mbozi lina shule nyingi na lina majengo mengi ambayo bado hayajakamilika. Nimhakikishie Mbunge tu kwamba moja ya vigezo ambavyo tutavitumia sasa hivi ni kuhakikisha yale

maeneo yenye uhitaji mkubwa tunayapa kipaumbele ikiwemo Jimbo la Mbozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, namwita Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa, aulize swali lake.

Na. 229

**Ujenzi wa Barabara za Mitaa za Halmashauri ya Mji Wa Kondoa Kupitia Mradi wa *TACTICS***

**MHE. ALLY J. MAKOA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara za mitaa ya Halmashauri ya Mji wa Kondoa kwa kiwango cha lami kupitia Miradi ya *TACTIC*?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Jimbo la Kondoa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza Mpango wa Kuboresha Miundombinu ya Msingi katika Miji Nchini, Serikali kupitia Mradi wa *Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness Project (TACTIC)* utakaotekelezwa katika miji 45. Mradi huo utatekelezwa katika Halmashauri za Majiji, Manispaa na Miji kupitia mkopo wa masharti nafuu

kutoka Benki ya Dunia wenye jumla ya Dola za Kimarekani milioni 500, baada ya kukidhi vigezo vilivyowekwa na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Kondoa ni miongoni mwa miji 45 nchini ambayo imepewa kipaumbele cha kupata ufadhili wa Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu katika Miji. Aidha, Halmashauri hii ipo kwenye kundi la tatu lenye jumla ya miji 18 ambayo inatarajiwa kuanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi iliyopendekezwa na Halmashauri husika katika mwaka wa fedha 2022/2023.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Makoa, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanz; Mji wa Kondoa Mjini una hali mbaya sana hasa kipindi cha mvua kwa kuwa na mafuriko katikati ya mji. Je, Serikali inaweza ikatupa fedha kwa ajili ya kujenga mitaro kuzuia yale mafuriko kutokea mitaa ya Uwanja wa Puma mpaka katikati ya mji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; tuna barabara ya kilomita kama moja kutoka barabara kuu kwenda katika Ofisi za Mkurugenzi maana yake majengo ya halmashauri . Je, Serikali ipo tayari kusaidia fedha kwa ajili ya kuweka lami kwa sababu ya ule muundombinu uliowekwa pale, jengo zuri la thamani kubwa lakini barabara ya tope?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo

mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Jimbo la Kondoa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba katika bajeti ambayo tumepitisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI, sehemu ya fedha ambazo tumeziweka ni pamoja na Jimbo la Kondoa na sehemu ya fedha hiyo itahusika katika ujenzi wa mitaro ambayo Mheshimiwa Mbunge ameainisha. Kwa hiyo nimwondoe shaka tu kwamba kwa kuwa tumeshapitisha bajeti, basi tutakwenda kutekeleza kama ambavyo yeye amehitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuhusiana na mahitaji ya kilomita moja kutoka barabara kuu ya lami kwenda katika jengo lao la halmashauri, niseme tu ombi hili tumelipokea japo tunatambua kwamba Mradi wa *TACTIC* sehemu mojawapo ni kutekeleza mradi huu ambao Mheshimiwa Mbunge ameainisha. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunazungumzia barabara za mitaa na halmashauri, namwita Mheshimiwa Jerry Silaa, aulize swali la nyongeza.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Serikali kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Ilala wakati ule ilijenga Barabara ya Mombasa- Mazini-Moshi Bar na kipindi hiki barabara hii imeharibika sana hasa kipande cha kuanzia pale Mombasa mpaka Transfoma. Je, Serikali haioni ni wakati sasa kufanya ukarabati wa dharura wa kipande kile cha barabara ili kuwapunguzia wananchi kero?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Jerry Silaa, Mbunge wa Jimbo la Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba ni kweli barabara ile ilijengwa na sasa hivi kwa kweli imeharibika kutokana na adha za mvua. Nimhakikishie Mbunge tu kwamba, tunawaagiza watu wa *TARURA,* Mkoa wa Dar es Salaam waende wakafanye tathmini na kutafuta fedha kwa ajili ukarabati wa barabara hiyo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Ofisi hii hii ya Rais, TAMISEMI, namwita Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 230

**Kukamilisha Miradi Iliyoanzishwa kwa Nguvu za Wananchi**

**MHE. ASIA A. HALAMGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga fedha kwa ajili ya kumalizia Miradi ya Afya iliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Manyara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua mchango wa wananchi katika ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya kote nchini. Aidha, Serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati nchi nzima katika kila jimbo. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali ilitenga fedha Shilingi bilioni 27.75 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati 555 ambapo jumla ya Shilingi bilioni 26.95 zilitolewa na Serikali kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya shilingi bilioni 38.2, zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha maboma ya zahanati 763 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi ambapo maboma 564 yanakamilishwa kwa fedha ya ruzuku ya Serikali na maboma 199 kwa fedha za halmashauri mapato ya ndani, ambapo jumla ya fedha shilingi bilioni 30.98 zimekwishatolewa mpaka sasa, ikijumuisha shilingi bilioni 26.92 ruzuku ya Serikali na shilingi Bilioni 4.06 mapato ya ndani ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga shilingi bilioni 15 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati 300.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Swali la kwanza; kwa kuwa majibu ya Serikali yanaonesha kabisa fedha iliyotengwa ni ndogo kulinganisha na miradi ya wananchi. Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya kuongeza fedha ili kuweza kumalizia miradi ambayo nguvu za wananchi zimetumika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa kuona miradi hiyo ama nguvu hizo za wananchi kwa kuanzia tuanze na Mkoa wa Manyara?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Manyara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunatambua kwamba wananchi wamefanya kazi kubwa sana ya ujenzi wa maboma na fedha ambayo tumetenga bado haikidhi, lakini Serikali inaendelea kutafuta fedha kuhakikisha kwamba tunakamilisha na kuongeza jitihada ambazo wananchi wamezifanya. Kwa hiyo nimwondoe shaka kwamba, tutaendelea kuongeza kwa mfano mwaka huu na mwakani mwaka wa fedha unaofuatia, Serikali itaongeza fedha ili kuhakikisha maboma hayo yanakamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, niko tayari kwenda kujionea hiyo miradi Mkoa wa Manyara nikiongozana na Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum pamoja na Wabunge wote wa Mkoa wa Manyara. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hussein Nassoro Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kumalizia zahanati na kuna baadhi ya zahanati ambazo tumeshakamilisha katika Wilaya ya Nyangh'wale. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza kupeleka vifaa tiba na kuweza kuzifungua zahanati hizo?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Hussein Nassoro Amar, Mbunge wa Nyangh'wale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna maeneo mengi ambayo mpaka sasa wameshamaliza vituo vya afya pamoja na zahanati. Sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tumeshafanya uagizaji wa vifaa tiba na baadhi ya *tender* zipo katika hatua za mwisho kwa ajili ya kuagiza hivyo vifaa. Kwa hiyo mara vifaa hivyo vitakapofika basi tutapeleka katika vile vituo ambavyo vimekamilika ili kuhakikisha kwamba zahanati hizo pamoja na vituo vya afya vinafunguliwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itamalizia hospitali ya Wilaya ambayo bado wodi hazijaisha. Ni lini sasa Serikali itapeleka fedha ili wodi zijengwe?

**MWENYEKITI:** Hospitali ipi?

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya ya Sumbawanga Mjini inayoitwa Isyofu, imeshajengwa lakini wodi hazijaisha, fedha haijapelekwa. Ni lini sasa Serikali itapeleka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri unayo hiari pia ya kujibu kama utakuwa huna *details* litakuja kama swali la

msingi kwa sababu pengine utakuwa huna *details exactly* ipo hatua gani.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hospitali ya Sumbawanga Mjini nilifika mimi mwenyewe pale na nilijionea adha ambayo inaendelea pale na najua bado haijakamilika. *Commitment* ya Serikali ni kuhakikisha kwamba tunatafuta fedha ili tuongezee na kuikamilisha ile hospitali kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Cosato Chumi swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Halmashauri wa Mji wa Mafinga Kata ya Bumilainga kwa kufuata maelekezo ya Serikali kwamba tutenge fedha za mapato ya ndani kujenga kituo cha afya, tumetekeleza na tuko kwenye hatua za mwisho za kukamilisha Kituo cha Afya cha Bumilainga. Je, Serikali mpo tayari kutuletea vifaa ili kituo hichi cha afya kianze kazi, ambacho kinahudumia pia Halmashauri ya Mufindi anakotoka Mheshimiwa Mwenyekiti?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI majibu kwa swali hili muhimu sana.*(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mhheshimiwa

Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Cosato Chumi Mbunge wa Mafinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu kwamba mara baada ya kituo hicho cha afya kukamilika tupo tayari kupeleka vifaatiba pamoja na Wauguzi ili kiweze kufunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI Mheshimiwa David Silinde. Tunaendelea Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, namuita Mheshimiwa Kapteni Abbas Ali Hassan Mwinyi Mbunge wa Fuoni aulize swali lake. Swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Asia Mohamed.

Na. 231

**Ufumbuzi wa Kero za Muungano**

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMED K. n. y. MHE. KAPT. ABBAS ALI MWINYI** aliuliza:-

Je, ni kero gani za Muungano bado hazijapata ufumbuzi hadi sasa; na ni jitihada gani zinafanyika ili kero zilizosalia zipate ufumbuzi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira majibu.

**WAZIRI WA NCHI, MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Kapt. Abbas Ali Hassan Mbunge wa Fuoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero za Muungano ambazo bado hazijapatiwa ufumbuzi mpaka sasa ni saba ikiwa ni pamoja na:

(i) Moja ni mgawanyo wa Mapato yatokanayo na Hisa za SMZ zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki na faida ya Benki Kuu;

(ii) Usajili wa Vyombo vya Moto;

(iii) Ongozeko la gharama za umeme kutoka *TANESCO* kwenda *ZECO*;

(iv) Malalamiko ya Wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili;

(v) Kodi ya Mapato *(PAYE)* na kodi ya Mapato inayozuiliwa *(Withholding Tax);*

(vi) Mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha;

(vii) Changamoto ya uingizaji wa sukari katika soko la Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuimarisha uratibu wa utatuzi wa hoja zilizobaki kati ya sekta zenye hoja za pande zote mbili za SMT na SMZ na kuwasilisha maamuzi kwenye Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja yenye jukumu la kufuatilia hatua za utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Pamoja na kutoa ushauri kwa sekta zenye hoja namna ya kuendelea kuzitatua hoja hizo. Aidha, Serikali za pande zote mbili zinashirikiana kwa karibu kuhakikisha vikao vya pamoja vilivyokubaliwa kwa ajili ya kupata ufumbuzi hoja zilizosalia vinaendelea kama utaratibu ulivyopangwa.

**MWENYEKITI:** Kwa niaba ya Kapteni Ali Hassan Mwinyi Mheshimiwa Asia Mohamed swali la nyongeza.

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, kuna kero Saba ambazo bado hazijapatiwa ufumbuzi na kuna kero nyingine ambazo wameanza kuzipatia ufumbuzi. Je, ni nini mpango wa Serikali kuhusiana na utoaji wa taarifa wa kero hizi ili wananchi waweze kujua tathmini na ufuatiliaji wa kero ngapi ambazo zimetatuliwa na ngapi ambazo hazijatatuliwa kwa maslahi mapana ya Taifa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira majibu.

**WAZIRI WA NCHI, MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali zuri la Dada yangu Mheshimiwa Asya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli safari yetu ya utatuzi wa hoja za muungano kama mnavyokumbuka tulikuwa na hoja 25, katika hoja hizo mwaka 2010 tulitatua hoja Mbili, mwaka 2020 tukatatua hoja Tano. Katika kipindi hichi cha mwaka mmoja chini ya Kiongozi Mama Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar Dkt. Hussein Ali Mwinyi tulitatua hoja 11. Kwa hiyo, tumefanikisha kumaliza kutatua hoja 18 za Muungano kati ya hoja 25, kwa hiyo tumebakiwa na hoja Saba. Utaratibu wetu ni kwamba tarehe 23 Agosti, 2021 jambo kubwa lililofanyika Zanzibar ilikuwa ni kuitisha vyombo vya habari na kuwaeleza wananchi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo tumejipanga kupitia vikao mbalimbali ndiyo maana katika bajeti tuliyopitisha

mwaka huu tumetoa maelekezo ya kina na kutenga bajeti maalum ya kutoa elimu ya upana kwa suala la muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo jambo hili linaendelea kuwapa wananchi katika taarifa mbalimbali kupitia runinga, vyombo vya habari mbalimbali, magazeti hali kadhalika redio zetu ikiwa ni pamoja na zile *local radio* zetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimekuona Mheshimiwa Najma Giga Murtaza swali la nyongeza.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa tafsiri ya kamusi ya Kiswahili – *English*, kero maana yake ni *a noise, a noise* ni kama maudhi ambayo ndiyo hizo kero zenyewe. Maudhi yakiendelea hata kwenye ndoa inaweza kusambaratika. Je, Serikali haioni umuhimu wa kubadilisha hili neno na kuweka japo changamoto tukizingatia kwamba hizi changamoto ni endelevu kila siku zinakuja na zingine zinaondoka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Daktari Selemani Jaffo majibu.

**WAZIRI WA NCHI, MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Dada yangu Mheshimiwa Najma Giga ambaye ni Mbunge machachari sana na Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ushauri wake ni mzuri na ndiyo maana sasa hivi tunavyopeleka taarifa sasa hivi tunaita ni hoja za Muungano siyo kero za Muungano. Kwa vile mafanikio ni makubwa zaidi kulikoni hizi hoja, kwa hiyo jambo hili Mheshimiwa Mbunge tumelichukua na tunaendelea

kulifanyia kazi na hakika ninawaomba Watanzania kwa ujumla, sasa tuendelee kuhubiri zaidi mafanikio zaidi katika utekelezaji wa mambo Katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, unaweza kwenda kuketi.

Waheshimiwa Wabunge, wakati Bunge linaendelea tunao ugeni hapa ni vizuri tuwatambulishe. Wageni wako Jukwaa la Spika ni Mheshimiwa Spika ambaye ni Spika Mstaafu wa Bunge la Kenya, Mheshimiwa Francis Ole Kaparo, akiwa na mwenyeji wake Mheshimiwa Naibu Spika wa Bunge letu, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Kaparo ameambatana na mkewe ambaye ni Mheshimiwa Sarah Paulata Korere ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Laikipia kwa vipindi viwili sasa na kwa mnaofatilia uchaguzi wa Kenya yupo kwenye kampeni tena. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Kaparo yuko Dodoma kwa ajili ya kushiriki Semina ya Chama cha Mapinduzi, Chama Tawala kesho Jumamosi tarehe 21 Mei, 2022. Mheshimiwa Kaparo karibu sana Tanzania, karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, japo tutatangaza baadae tunaye katika wageni ambao wako pale, yuko mgeni wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha Gracious Mwigulu Nchemba ambaye tutamtambulisha vizuri baadaye asimame tu apunge mkono, tutafuata utaratibu baadaye. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi sasa namuita Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 232

**Hitaji la Uwanja wa Ndege – Shinyanga**

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Uwanja wa Ndege katika Mkoa wa Shinyanga?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, *Engineer* Kasekenya Msongwe.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga kitajengwa kwa ufadhili wa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya *(European Investment Bank – EIB)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfadhili wa mradi huu tayari ameshaleta fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi. Aidha, Serikali imekwishafanya marekebisho ya mkataba na kuwasilisha kwa Mfadhili ili atoe idhini *(no objection)* kwani kutakuwa na mabadiliko ya gharama ikilinganishwa na wakati mkataba huo uliposainiwa mwaka 2017. Kazi za ujenzi wa mradi huu zitaanza mara moja tutakapopata *no objection* kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Santiel Kirumba swali la nyongeza.

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Je, kutokana na viwanja vingi vya Serikali kujengwa na makampuni ya nje. Nini kauli ya Serikali kuwajengea uwezo makampuni ya ndani ili yaweze kujenga viwanja hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kutokana na mkataba huu kusainiwa tangu umesainiwa ni miaka Mitano. Nini kauli ya Serikali itawalipa fidia lini hawa wananchi wa Shinyanga kwa sababu tangu mwaka 2017 mpaka sasa 2022 miaka mitano imepita, itawalipa fidia ya mwaka 2017 au mwaka 2022, kutokana na bidhaa nyingi kupanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Shinyanga, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge Santiel kwa jinsi anavyofuatilia ujenzi wa uwanja huu. Suala la Wakandarasi wa ndani. Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan imekuwa mara kwa mara ikihimiza na ikiwajengea uwezo Wakandarasi wote wa Tanzania ili waweze kufanya miradi mikubwa. Hii siyo tu kwa viwanja vya ndege ni pamoja na miundombinu mingine ikiwemo majengo makubwa na hata barabara. Kwa hiyo, kinachofanyika kwanza ni kuwapa elimu ya kuwaunganisha pamoja ili waweze kuwa na mitaji mikubwa pia kuwawezesha ili

waweze kupata mikopo kwa taasisi mbalimbali za fedha ikiwemo mabenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipo inafanya kazi hiyo na tunaamini kwa kuwawezesha Wakandarasi wa ndani maana yake fedha yetu nyingi itaendelea kubaki na kukuza uchumi pia kuwezesha uwezo wa hawa Makandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusu fidia. Serikali ilikwishawalipa fidia wananchi ambao wamepisha ujenzi. Kwa mujibu wa sheria zetu tunapolipa fidia tunaondoa kitu kinachoitwa uchakavu na hasa uchakavu wa majengo. Masharti ya wenzetu hawa ambao wanatoa fedha wana sharti moja kwamba ni lazima fedha ya uchakavu pia ilipwe. Kwa hiyo, Serikali imeshafanya tathmini ya uchakavu wa yale majengo na tayari yameshawasilishwa Wizara ya Fedha ili wakalipwe zile fidia za nyongeza kwa uchakavu wa yale majengo. Kwa hiyo, tayari tuko kwenye *process* na hawa watu wataongezwa fidia kwa maana ya ile ambayo sheria yetu ilikuwa inasema tusiwalipe lakini wanaotufadhili wanatuambia ni lazima pia walipwe. Kwa hiyo wananchi hawa watapata nyongeza ya fidia tofauti na waliyopata ile ya awali. Ahsante.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ritta Kabati swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Je, Serikali itamaliza lini uwanja wetu wa ndege wa Iringa, kwa sababu uwanja ule tunategemea sasa hivi Mama amehamasisha *royal tour* kwa ajili ya utalii mkubwa katika hkivutio cha Ruaha na vivutio vingine vilivyoko katika Mkoa wa Iringa na Nyanda za Juu Kusini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu kuhusu Uwanja wa Ndege wa Iringa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ritta Kabati Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Iringa, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba ujenzi huu unaendelea. Serikali inaendelea kuujenga uwanja huu na Wakandarasi wako *site*. Pengine tu ni kuwahimiza Wakandarasi waweze kuongeza *speed* na tunajenga kwa fedha ya Serikali pia wenzetu wa *World Bank* wameonesha utayari wa kuweza kusaidia ili kukamilisha ujenzi wa uwanja huu ili kuweza kuimarisha shughuli za utalii ambazo tayari Mheshimiwa Rais ameshakuwa *champion* wa hiyo kazi. Kwa hiyo tunakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba uwanja huu tutaukamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi namuita Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa Mbunge wa Handeni Vijijini aulize swali lake.

Na. 233

**Ujenzi wa Barabara ya Handeni – Kibirashi – Kondoa Hadi Singida**

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Handeni Kibirashi, Kondoa hadi Singida kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza ujenzi wa Barabara ya Handeni – Kibirashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijo Chini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro hadi Singida kwa awamu. Taratibu za manunuzi za kumpata Mkandarasi kwa sehemu ya Handeni – Mafuleta (km 20) zipo katika hatua za mwisho za kusaini mkataba. Aidha, maandalizi ya kutangaza zabuni ya ujenzi kwa sehemu ya kutoka Mafuleta – Kwediboma yenye urefu wa kilometa 30 yanaendelea na zabuni itakuwa imetangazwa kabla ya mwezi Juni, 2022. Kwa sehemu iliyobaki Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Reuben Kwagilwa swali la nyongeza.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka mwaka jana kwenye bajeti majibu ya Serikali yamekuwa ni haya haya hayabadiliki. Hatua za mwisho za kusaini mkataba. Swali

langu la msingi lilikuwa ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ipi Barabara ya Handeni - Kwa Magome, Nziha - Turiani. Ni lini Serikali pia itaanza kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu, ni lini ujenzi utaanza.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Reuben kwa jinsi anavyofuatilia barabara ambazo zinaanzia katika Jimbo lake kwenda kwenye Majimbo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyoongea nataka nimhakikishie Mheshimiwa Reuben kwamba tayari kazi ya ujenzi imeshaanza na hivi tunavyoingia huku Mkandarasi ameshapatikana na sasa ameanza *mobilization* kupeleka vifaa *site* kwa hizo kilomita 20 ambazo zilishatangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ya kutoka Handeni Mjini kuja Turiani naomba tusubiri bajeti ipitishwe halafu tuone tutakachofanya katika hiyo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, tunaendelea na Wizara ya Maji. Ninamuita Mheshimiwa Samwel Xaday Hhayuma Mbunge wa Hanang aulize swali lake.

Namwita Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, Mbunge wa Hanang' aulize swali lake.

Na. 234

**Mradi wa Maji Ziwa Basotu**

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA** aliuliza:-

Je, ni lini Mradi wa Maji kutoka Ziwa Basotu kwa ajili ya Vijiji zaidi ya tisa (9) utaanza kutekelezwa Wilayani Hanang'?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Eng. Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Samwel Xaday Hhayuma, Mbunge wa Jimbo la Hanang', kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa kutuma Ziwa Basotu kwa ajili kupeleka maji katika vijiji kumi vya Diling'ang, Wandela, Gawindu, Bassotu, Muungano, Milingori na Ming'enyi vilivyopo Wilaya ya Hanang. Utekelezaji wa awamu ya kwanza utanufaisha Kijiji cha Bassotu ambapo kazi zinazofanyika ni pamoja na ujenzi wa chanzo cha maji, vituo 13 vya kuchotea maji, na ulazaji wa bomba lenye urefu wa kilometa 14. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Julai, 2022 na utanufaisha wananchi wapatao 16,553.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2022/2023 utekelezaji wa mradi huu wa maji utaendelea katika vijiji tisa vilivyobaki ili kuimarisha huduma ya upatikanaji wa maji kwa vijiji vyote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hhayuma, swali la nyongeza.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza maji ya Ziwa Bassotu kwa siku za karibuni yamekuwa yakisambaa na kuingia kwenye mashamba ya watu na nyumba:-

Je, Wizara ya Maji iko tayari kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, (Mazingira) kuangalia na kufanya tathmini ya tatizo linalofanya hayo maji yasambae na hatimaye kulitatua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, mradi huu karibu miaka mitatu ya fedha imekuwa ikitengewa chini ya Shilingi bilioni moja na tathmini ya awali ni Shilingi bilioni 12:-

Je, Wizara sasa iko tayari kutenga fedha zaidi ili mradi huu ukamilike kwa wakati?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Eng. Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Samweli Hhayuma, Mbunge wa Hanang' kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara tunafanya kazi kwa ushirikiano na Wizara ambazo tunakuwa tunaingiliana kikazo. Hivyo tupo tayari kushirikiana ili kuondoa hiyo adha kwa wananchi na vilevile kutenga fedha zaidi. Tutaendelea kufanya hivyo na pale tunapoendelea kupata fedha tutaongeza bajeti kwenye eneo hilo ili miradi hii ikamilike.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Umekuwepo mradi wa Kwembe-King'azi wa muda mrefu ambao uliahidiwa kukamilika mwezi wa Kumi na Mbili mwaka 2021 mbele ya Mheshimiwa Waziri na mpaka sasa haujaanza:-

Je, ni lini mradi wa Kwembe-King'azi A utaanza ili wananchi wa pale waweze kupata maji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Kibamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu tunaendelea katika hatua zake za mwisho kabisa na unaelekea kwenye utekelezaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kumekuwa na tatizo kubwa la Wakandarasi kushindwa kuchimba visima. Katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu, Mkandarasi ana miezi sita, ameshindwa kuchimba visima vya Aicho, Boboa na Titimu:-

Je, Serikali imefikisha hatua gani kuleta mitambo ya kila mkoa kuchimba visima vyetu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Mbulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais, ametupatia fedha ya kutosha, taratibu zote zilishafanywa. Kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha tunatarajia mitambo ile yote iwe imeshafika Tanzania na iweze kwenda kufanya kazi inayokusudiwa.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea. Namwita Mheshimiwa Mossy Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, aulize swali lake.

Na. 235

**Uhaba wa Maji Kata ya Katuma**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka maji katika Kata ya Katuma ambayo ndiyo inatunza chanzo cha maji cha Mto Katuma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso Mbunge wa Mpanda Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali inatekeleza mradi wa maji kwa kutumia visima virefu vinne na kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa matanki matano yenye ujazo wa lita 400,000, ujenzi wa vituo 25 vya kuchotea maji na mtandao

wa bomba wenye urefu wa kilometa 30.4. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Oktoba, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo cha Mto Katuma kinanufaisha wananchi wa Kata ya Katuma kwa shughuli za kilimo ambapo Serikali imetoa vibali vitano vya kutumia maji kwa skimu za umwagiliaji wa kilimo cha mpunga. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali itaajiri Mtaalam Mshauri wa kufanya usanifu wa mradi wa maji kwa kutumia chanzo cha maji cha Ziwa Tanganyika kupeleka Mkoa wa Katavi ambapo Wilaya ya Tanganyika itanufaika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza: Mradi wa Kata ya Katuma ulipata Mkandarasi *HEMATEC* ambaye aliingia mkataba wa kufanya kazi tarehe 14 Desemba, 2021, mpaka sasa Mkandarasi huyo hajawahi kufika kwenye eneo husika:-

Je, Serikali haioni sasa ni wakati wa kuchukua hatua za dharura ku-*terminate* huo mkataba ambapo kimsingi mradi huo unatakiwa ukamilike tarehe 20 mwezi wa Sita?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili: Tunapongeza jitihada zinazofanywa na Serikali na kuleta miradi mingi kwenye eneo la kwetu. Meneja wa *RUWASA* wa Wilaya ya Tanganyika hana gari la kumsaidia kufanya kazi:-

Je, ni lini Serikali italeta fedha au kuleta gari ili liweze kusaidia kutoa huduma kwenye eneo hilo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Eng. Maryprisca Mahundi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu, maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kumpa pole Mheshimiwa Mbunge, amekuwa akifuatilia sana huyu Mkandarasi, lakini sisi kama Wizara hatutafumbia macho Mkandarasi yoyote mzembe, hata kama tumesaini mkataba, lakini ukienda kinyume na mkataba, tutakuweka pembeni kwa sababu hatuko tayari kufanya kazi na mtu anayetuchelewesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo kwa kutumia Bunge lako Tukufu, naomba nitoe wito kwa ma-*RM* wote ambao Wakandarasi wao wanalalamikiwa kama huyu *HEMATEC*, *RM* wa eneo hili. Nitapenda ulete taarifa yako kesho asubuhi ili kujua ukweli wa suala la huyu Mkandarasi na endapo itabainika ni mzembe, tutamchukulia hatua stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na *DM* wa Tanganyika kupatiwa gari, utaratibu unaendelea. Tunashukuru sana utendaji mzuri wa *Director General* wa RUWASA, *Eng.* Clement Kivegalo, ameendelea kufanya taratibu za kuona ma-*DM* wote wanapata vyombo vya usafiri. Hivyo katika magari yatakayokuja, naamini *DG* ataweka pia msisitizo kwa eneo la Tanganyika kwa umuhimu wake.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Namwita Mheshimiwa Nashoni William Bidyanguze aulize swali lake.

Na. 236

**Hitaji la Kituo cha Polisi Wilaya ya Uvinza**

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Uvinza?

**MWENYEKITI:** Majibu Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jummanne Sagini.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaanza kujenga Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Uvinza katika eneo la Lugufu baada ya eneo hilo kupimwa na kupata hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Swali la nyongeza, Mheshimiwa William Bidyanguze.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili analotolea majibu kwamba halina hati, lina kituo kidogo cha Polisi cha muda mrefu; na eneo hili halina mgogoro; sasa ni kwanini Serikali isijenge na hiyo hati ikaja kupatikana baadaye kwa sababu hakuna anayelalamikia eneo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wilaya yangu ni kubwa sana na ni mpya, lakini *OCD* hana gari ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tumpongeze Mheshimiwa Nashon kwa ufuatiliaji wake wa karibu wa masuala ya ulinzi na usalama kwenye jimbo lake. Pia tumtie moyo kwa namna anavyoshirikiana na uongozi wa Wilaya ya Kigoma na kwa sababu tunafahamu hata hili jengo linalotumika sasa ni lile ambalo Halmashauri imetoa kuiazima Jeshi la Polisi waweze kufanya shughuli zao, kwa hiyo, tunakushukuru sana Mheshimiwa Bidyanguze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa nijibu swali lako kwamba kama kweli hakuna mgogoro, basi tutamwagiza *OCD* na *RPC* wa Mkoa wa Kigoma kufuatilia kwa haraka, kwa sababu maelekezo ya Serikali ni kwamba maeneo yote ya Serikali yapate hati ili kuondoa uwezekano wa migogoro huko mbele. Kwa hiyo, hati itakapokuwa imetoka na kwa sababu hati inatolewa na Halmashauri na mahusiano yenu ni mema, bila shaka wataharakisha kutoa hii hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la gari, tumejibu hapa mara nyingi Mheshimiwa Mbunge, kwamba magari ambayo tunatarajia kuyapata ifikapo Septemba ni zaidi ya 370. Tunatarajia maeneo yenye changamoto kama hili la

kwako la Kigoma ambalo liko karibu na maeneo ya mpakani yatazingatiwa kama maeneo ya kipaombele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Wilaya ya Rorya, ni moja ya wilaya ambayo ipo kwenye kanda maalum kwa maana ya Tarime na Rorya, lakini ni wilaya ambayo haina Kituo cha Polisi cha Kiwilaya, ina Vituo vya Polisi vya Kikanda kwa maana ya Utegi, Kinesi na Shirati. Nataka nijue mpango mkakati wa Serikali wa kujenga Kituo cha Polisi cha Wilaya nzima ya Rorya, itakuwa iko kwenye mpango kule?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chege, Mbunge wa Rorya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunafahamu kwamba ziko wilaya nyingi hasa hizi wilaya mpya hazina vituo vya wilaya ya Polisi, ikiwemo hii Wilaya ya Rorya. Mpango wa Serikali kama ilivyosemwa wakati Waziri akiwasilisha hotuba yake hapa; tuna mkakati wa kujenga vituo vya Polisi kwenye mikoa ambao hawana vituo vya Polisi kwa ajili ya *RPC* na vilevile kwenye wilaya ambazo hazina Vituo Vikuu vya Polisi vya Wilaya. Kwa hiyo, mpango huo kadri tutavyokuwa tunapata fedha utaekelezwa, na Wilaya ya Rorya itakuwa ni moja ya wilaya ya vipaumbele kwa sababu iko mpakani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aloyce Kamamba, swali la nyongeza.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto inayowakabili wananchi wa Uvinza, inakwenda sambamba na Wilaya ya Kakonko. Mkuu wa Polisi wa Wilaya hana ofisi, anatumia iliyokuwa Ofisi ya Polisi ya Kata. Kwa hiyo, Waziri anaweza akaona hali halisi:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kauli ya Serikali katika kuhakikisha kwamba Wilaya ya Kakonko nayo inapata Kituo cha Polisi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye majibu ya msingi, wilaya zote mpya hazijawa na vituo vya Polisi vya ma-*OCD*. Ndiyo maana tumekuja na mkakati wa kujenga vituo hivyo kwenye maeneo ambayo hayana. Katika bajeti iliyopita tutaanza ujenzi wa vituo hivyo, lakini kipaumbele kitawekwa kwenye maeneo yaliyoko mpakani ikiwemo hii Wilaya ya Kakondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Njombe, ni miaka 10 toka umeanzishwa na mpaka leo hatuna Kituo cha Polisi kinachoendana na hadhi ya mkoa? Ni lini sasa kituo hicho cha Polisi kitajengwa katika Mji wa Njombe?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwanyika, Mbunge kutoka Njombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwishasema, tunatambua mikoa mipya iliyoanza kwenye miaka ya 2012 ukiwemo Mkoa wa Njombe, hauna kituo kikuu cha Polisi kwa maana Ofisi ya *RPC*. Kwa kweli Mkoa wa Njombe tayari uko kwenye mpango na Mheshimiwa Mbunge anajua. Katika vipaumbele ambavyo mwaka huu tunaendelea navyo, ni ujenzi wa ofisi ya *RPC* Njombe. Nadhani baada ya Bunge hili tutatembelea maeneo hayo kuona maandalizi na harakati za ujenzi zinavyoendelea Meshimiwa Mwanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chaurembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua ni lini Serikali itakijenga kwa hadhi ya Kituo cha Polisi Mbagala?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chaurembo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli swali hili ni moja ya maswali ambayo yako kwenye mpango wa kujibiwa, lakini niseme tu kwamba tunajua Mkoa wa Dar es Salaam, ikiwemo Wilaya ya Temeke, na Majimbo ya Mbagala, na majimbo mengine ya maeneo ya Kigamboni, kuna vituo vidogo vya Polisi vingi kuliko vituo vya ngazi ya wilaya. Tunaendelea na mpango mkakati wa ujenzi wa vituo hivi kwa kuangalia maeneo ambayo yana uhitaji mkubwa kutokana matukio ya uhalifu ili kuyazingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini Mbagala kwa sababu ya wigi wake wa watu, matukio ya uhalifu pia yatakuwa mengi, tutakizingatia katika mpango huu wa ujenzi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jesca swali la nyongeza.

**MHE. JESECA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa viongozi wa Wizara ya Mambo ya Ndani wana afya nzuri ya akili, ni lini sasa watatujengea nyumba za askari katika Kituo Kikuu cha Polisi pale Iringa Manispaa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru Balozi wa Afya ya Akili anatambua jinsi tulivyo timamu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi yangu ni hiyo, kwamba katika ujenzi wa vituo vya Polisi huenda sambamba na ujenzi wa nyumba za Maaskari, Wakaguzi na Maofisa. Kwa hiyo, Iringa kama alivyosema ni mjini, ukiangalia kwa vipaumbele, pale angalau watu wanaweza wakapata nyumba zenye hadhi za kupanga, lakini kuna maeneo ya vijijini kabisa

ambayo uwezekano wa kupata nyumba za kupanga ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye ujenzi wa nyumba, vipaumbele tutaweka kwenye maeneo ambayo yana changamoto kubwa za kupata makazi. Kwa hiyo, wale wa Iringa watasubiri, lakini kadri fedha zitakapopatikana na wao pia watajengewa.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Janejelly James Ntate, aulize swali lake.

Na. 237

**Hitaji la Askari Kituo cha Polisi Kata ya Kilungule – Mbagala**

**MHE. JANEJELLY J. NTATE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Askari Polisi katika Kituo cha Polisi Kata ya Kilungule - Mbagala ili wananchi wa kata hiyo wapate huduma?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janejelly James Ntate, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Dar es Salaam kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari ilishakipangia askari sita kituo kidogo cha Polisi cha Kata ya Kilungule - Mbagala na kinafanya kazi saa 24. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Janejelly.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na juhudi nzuri za Serikali za kufungua kituo hiki siku nne zilizopita, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na tishio la *panya road* waliojaa Dar es Salaam, Serikali haioni haja ya kituo hiki kufanya kazi masaa 24 kama jibu linavyosema, badala ya masaa nane ambayo kinafanya sasa hivi kuanzia saa tatu mpaka saa nane? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali haioni haja Kituo cha Kiburugwa kwa kata ya jirani kukikarabati ili kiendane na mazingira bora ya watumishi wa Polisi kufanyia kazi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ntate Mbunge wa Viti Maalum Dar es Salaam, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; hili la kufanyakazi saa 24 ndiyo maagizo ya wizara na ni maagizo ambayo *IGP* ameyapokea na kuelekezwa kwa viongozi wa Polisi Kanda, Mkoa na Wilaya za Dar es Salaam. Kwa hiyo, nitasisitiza kwamba hili lifanyike kwasababu tayari kuna askari sita na mkaguzi mmoja ambaye ni Mkuu wa Kituo hicho hakuna sababu zozote za msingi za kufanya kazi chini ya masaa ishirini na nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kukarabati kituo cha Kiburugwa kama alivyokwishasema Mheshimiwa Mbunge nakubaliana nae baadhi ya vituo vilivyo katika hali mbaya vinahitaji kukabaritiwa hii ni moja ya kuweka mazingira bora ya askari wetu kufanya kazi lakini pili kuwahudumia hawa

ambao wanapelekwa vituo wawe katika mazingira bora zaidi. Kwa hiyo, nakubaliana na wewe Mheshimiwa tutatafuta fedha kwaajili ya kukabarati vituo vilivyochakaa kikiwemo hiki cha Kiburugwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kilave swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, swali langu ni dogo sana lakini la uhakika. Je, ni lini Serikali itakipandisha hadhi Kituo cha Polisi cha Tandika ambacho tunatumia kata kama tano kwenda pale na sasa unaona kama kuna uhalifu mkubwa sana upande ule. Je, ni lini sasa mtakipandisha hadhi hata kipate *class B* ili tuweze kuona kwamba kazi nzuri inafanyika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kilave kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze kwa namna anavyofuatilia masuala ya ulinzi na usalama katika Mkoa wa Dar es Salaam mara kadhaa amenisumbua kidogo kuhusu hata njia inayokwenda Mbagala kupitia eneo la polisi na tumeshakubaliana ile njia itafunguliwa Mheshimiwa Mbunge lakini kuhusu ili la kupandisha hadhi kwa kupitia Bunge lako Tukufu namuelekeza Kamishna Kanda Maalum ya Dar es Salaam na Uongozi wa Polisi wa Mikoa ya Kipolisi Dar es Salaam kufuatilia, kupima na kufanya tathimini ya mahitaji ya kupandisha hadhi kituo hiki kama sababu alizozisema Mheshimiwa Mbunge zipo basi waone uwezekano wa kukipandisha ili kikidhi mahitaji ya eneo la Tandika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Vituo vya Polisi vidogo yaani kwamaana ya *outpost* nyingi zimechakaa sana zina hali mbaya nyingi zinavuja mapaa mbao zimeoza yaani hata hao mapolisi wanaofanyakazi huko vijijini Mungu anawalinda. Ningetaka kujua ni lini sasa Serikali itakarabati vituo hivi vidogo vyote Tanzania nzima ili viweze kuwa na hadhi ambavyo vinafaa kuwahudumia wananchi?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua na nimesema kwenye majibu yangu ya msingi kwamba tunatambua uwepo wa uchakavu kwa baadhi ya vituo vya polisi vikiwemo hivi vituo vidogo. Katika mkakati wetu wa ujenzi na ukarabati wa maeneo haya tutazingatia pia hivi vituo vidogo vya polisi kama ambavyo tumeanza kufanya kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi niliona kama Kuchauka amesimama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Naona Naibu Waziri ameondoka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri naomba umalizie nilimuita Mheshimiwa Kuchauka. *(Makofi)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Wilaya ya Liwale kijiografia imekaa vibaya sana hasa kwa ulinzi tunayoahadi ya kujengewa vituo vya polisi kwenye Tarafa ya Kibutuka, Kata ya Lilombe na Kata ya Kimambi. Nini kauli ya Serikali juu ya kutekeleza ahadi hiyo ili kuimarisha ulinzi kwenye Wilaya yetu ya Liwale? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, japo hajaniambia ahadi ilitolewa na nani lakini nikiri tu, kwanza maeneo yote ya tarafa yanahitaji kuwa na vituo vya polisi vyenye hadhi ya kutimiza majukumu ya ulinzi na usalama wa wananchi na mali zao zikiwemo hizi tarafa ulizozitaja za Liwale kwa maana ya Kibutuka na tarafa hizo nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na bajeti tuliyonayo tunakwenda kwa awamu. Kama tulivyokubaliana na Mheshimiwa Kuchauka tutafanya ziara Mkoa wa Lindi ili kuona uhitaji wa vituo hivi ili kuweka msukumo kwenye jeshi la polisi waweze kuvizingatia katika mipango yao ya ujenzi na ukarabati wa sekta nzima ya polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sasa unaweza ukaenda kuketi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Mwongozo wa Spika kutoka wapi Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Muongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kwagwila, Mheshimiwa Mpina haya naanza na Mheshimiwa Mpina.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,…

**MWENYEKITI:** Kanuni.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo kwa Kanuni ya 76 ambayo nisiisome kwa ajili ya kuokoa muda. Juzi wakati nachangia hotuba ya Waziri wa Kilimo nilihoji juu ya uhalali wa takwimu za mwenendo wa bei ya soko.

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza Mheshimiwa Mpina umesema juzi.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi.

**MWENYEKITI:** Kama unatumia Kanuni ya 76 ya Mwongozo wa Spika naomba nikusomee; inasema Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Muongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema. Ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatakayotolewa papo hapo au baadaye kadri atakavyoona inafaa. Kama ni kanuni hii likitokea leo

hapa ndiyo unaweza ukatumia kama limetokea juzi kwa kanuni hii haliwezi kwenda. *(Makofi)*

Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Nilikusikia Mheshimiwa Chege, Kwagilwa *Okay* Kwagilwa.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimesimama hapa kwa Kanuni ya 76 Mheshimiwa naomba nisiisome kwa kuokoa muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi alipokuwa akijibu swali langu amevunja kanuni yetu tuliyojiwekea Kanuni ya 53; jibu lake anasema taratibu za manunuzi za kumpata mkandarasi zipo hatua za mwisho za kutiliana saini wakati akitoa maelezo anasema mkandarasi tayari yupo *site* anafanya *mobilization* inawezekanaje mkandarasi awe *site* anafanya *mobilization* ill hali mkataba hajasaini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani sana.

**MWENYEKITI:** Haya tutalitolea majibu baadaye baada ya kusikiliza majibu ya Mheshimiwa Waziri swali lako la msingi na kilichosemwa. Tunaendelea.

Waheshimiwa Wabunge tunao wageni hapa; wageni waliopo jukwaa kuu ni wageni wa Mheshimiwa Nape Mosses Nauye Mbunge ambaye ni Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambao ni kama ifuatavyo:-

Viongozi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake; Tunae Daktari Jim Yonazi Katibu Mkuu. Tunae Ndugu Gerson Msingwa Msemaji Mkuu wa Serikali. Tunae Daktari Jones Kilimbe Mwenyekiti wa Bodi ya *TCRA*. Tunae Daktari Jabiri Bakari Mkurugenzi Mkuu *TCRA*. Ahsante. Tuna Daktari Ayubu Riyoba mkurugenzi Mkuu *TBC*, Ukweli na Uhakika. Tunae Hab Mkwizu Mwenyekiti wa Bodi ya *TSN*. Tunae Ndugu Tuma

Abdallah Kaimu Mhariri Mtendaji wa *TSN*. Tunae Richard Mayongela Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya *TTCL.* Ahsante. Tuna *Engineer* Peter Ulanga Mkurugenzi Mkuu *TTCL,* Ahsante sana. Tuna Bregedia *Generally* Mstaafu Yohana Mabongo Mwenyekiti wa Bodi ya Posta. Tuna Ndugu Marcus Mbodo Kaimu Posta Masta Mkuu wa Posta. Hatuwaoni hao. Tuna *Professor* John Mkoma Mwenyekiti wa Bodi UCSAF. Ndugu Justine Mashiba Mtendaji Mkuu wa UCSAF wale wa minara huyu wa minara amesimama hapa. *(Makofi)*

Tuna *Professor* Leonard Mselle Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya TEHAMA. Ahsante *Professor*. Tuna Daktari Nkundwe Mwasaga Mkurugenzi Mkuu Tume ya TEHAMA. Karibu sana. Tuna Ndugu Mary Shao Msuya Katibu Mtendaji Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano *TCRA-TCC*. Tuna Ndugu Deodatus Balile Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania. Karibu sana Bwana Balile. *Tuna Pasko Shelutete Mwenyekiti wa TACO.*Ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ni kutoka UMOJA wa Watoa Huduma za Mawasiliano TIGO wakiongoziwa na Ndugu Innocent Rwetabura. VODACOM Tanzania wakiongozwa na Ndugu Sitholizwa Mladose. *AIRTEL* wakiongozwa na ndugu Beatrice Singano. *SMILE* wakiongozwa na Ndugu Simoni Patrick.TSA wakiongozwa na Ndugu Zahoro Mhasi. *(Makofi)*

Pia wapo wageni kutoka Umoja wa Usafirishaji wa Vifurushi nchini (*Tanzania Couriers*) wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Aloyse Bahebe. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri wa Habari ni Wadau wa Vyombo vya Habari wasimame kwa umoja wao. Ahsante. *(Makofi)*

Wapo Pia Wawakilishi kutoka Kampuni za Ving'amuzi wakiongozwa na Ndugu Astrid Mapunda kutoka Kampuni ya *Multichoice*. *(Makofi)*

Wapo Umoja wa watoa Huduma za *Internet* Tanzania *(TISPA)* Wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji Ndugu Mzee Boma. *(Makofi)*

Yupo Mgeni Mwingine ambaye ni Mkuu wa Mawasiliano Benki ya Taifa ya Biashara (*NBC*) Ndugu Godwin Semunyu. Karibu sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wengine ambao ni Jukwaa la Wahariri. Ahsante. *(Makofi)*

Wapo MISA, *TURN*, wapo *PRST*, na *UTPC*. *(Makofi)*

Wageni Wa Mheshimiwa Mhandishi Kundo Andrea Mathew Mbunge ambaye ni Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Technolojia ya Habari ambao ni wafuatao:-

Wa kwanza ni Ndugu Kundo Grace Kidunda – Mke wake, Karibu sana Shemeji yetu, Ndugu Alvin Kundo – Mtoto wake, Ndugu Alvina Kundo – Mtoto wake, Ndugu Anna Brighton – Mama yake, Mzaa Chema, Ndugu Jane Mathew – dada yake, Ndugu James Mande – mpiga kura wake na Ndugu Basili Mathew – mdogo wake. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni 14 wa Mheshimiwa Maryprisca Mahundi Mbunge ambaye ni Naibu Waziri wa Maji ambao ni Chama cha Shule Binafsi za Udereva Tanzania wakiongozwa na Mwenyekiti Ndugu Mussa Itunku. Msimame wote na kiongozi wetu Mussa Itunku yuko wapi. Ahsanteni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Priscus Tarimo Mbunge, ambao ni *Let's Talk Finance Team* kutoka Jijini Dar es Salaam, ahsante, wakiongozwa na Ndugu Lawrence Mlaki. Huyu Bwana Mlaki Mjumbe wa Baraza Kuu la Vijana la CCM huyu. *(Makofi)*

Wageni nane wa Mheshimiwa Godfrey Kasekenya Mbunge ambao ni wafanyakazi Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Karibuni Sana Watendaji wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimiwa Jesca Msambatavangu Mbunge ambao ni Wahariri na Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Iringa. Karibuni Sana. *(Makofi)*

Wageni 20 wa Mheshimiwa Jesca Msambatavangu ambao ni Watendaji wa Kata za Iringa Manispaa kutoka Mkoani Iringa. Watendaji wa Kata kutoka Iringa Manispaa wako wapi aah *ok* sawa. *(Makofi)*

Wageni 09 wa Mheshimiwa Pauline Gekul Mbunge ambaye ni Naibu Waziri Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo, ambao ni Viongozi wa Chama cha *Netball* Tanzania (CHANETA) kutoka Dar es Salaam. Chaneta Karibuni Sana namuona Shayrose Banji pale. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis Mbunge ambao ni Viongozi wa Taasisi ya Zardefo kutoka Mjini Magharibi Zanzibar. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Ighondo Abeid Mbunge ambao ni Mwenyekiti na Katibu wa Baraza la Wazee Mkoa wa Singida kutoka Kaskazini Mkoa wa Singida. Wageni wa Mheshimiwa Ighondo Abed *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Amina Yussuf Mbunge, ambae ni Daktari wa Hospitali ya *DCMC* Ntyuka Dodoma Daktari Bugondo Leonard Bugondo. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; Wanafunzi 107 kutoka Feza *Primary School* ya Jijini Dar es Salaam.Wanafunzi kutoka Feza na walimu na wafanyakazi pamoja na timu nzima. Lakini pia nimeambiwa pia wapo na

watoto wa viongozi akiwemo Grashiani Mwingulu Nchemba pale, akiwemo Aziza Tamika Kikwete ambaye ni mtoto wa Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete nimeambiwa yuko hapo na wengine wengi ambao wako pale. *(Makofi)*

Lakini pia tuna Wanafunzi 100 na Walimu 12 kutoka shule ya Santhome *Primary* ya Dodoma Mjini. Karibuni sana wanafunzi na walimu na timu nzima ambayo mmeambatana nayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nina matangazo machache hapa; tangazo la kwanza; tangazo muhimu sana tusikilizane Waheshimiwa Wabunge natangaza tangazo muhimu sana hili limetoka kwa Katibu wa Bunge anasema; uwatangazie Wabunge wote kuwa Wizara ya Habari na Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imepanga kufanya maonyesho ya miradi mikubwa inayosimamiwa na wizara ikiwemo mradi wa kitaifa wa anuani za makazi Tanzania ya kidigitali *digital* Tanzania, Mkongo wa Taifa, *National ICT Back born,* Usalama wa Mifumo Mitandao kwajumla pamoja na mambo mengine. Maonyesho haya yafanyika tarehe 20,22 na 23 Mei nyuma ya Ukumbi wa Msekwa.

Si mnafahamu tarehe 21 kuna jambo eeh imerukwa hapo 20,22 na 23 Mei Wizara ya Habari. Kwa hiyo, tuhudhurie wote nyuma ya Ukumbi wa Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa katika maonyesho hayo ili kufahamu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na wizara ikiwa ni pamoja na miradi mikubwa ya kitaifa.

Aidha, Katibu wa Bunge anasema uwatangazie Wabunge wote kuwa leo siku ya Ijumaa tarehe 20 kuanzia saa saba na nusu mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa kutakuwa na semina itakayoondeshwa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kuhusu Utendaji wa Kazi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *TPA* na Shirika la Reli Tanzaniza *TRC.* Semina hiyo itahusu kuwajengea uwezo jinsi mashirika

hayo yanavyochangia katika ukuaji wa uchumi wa Pato la Taifa. Waheshimiwa Wabunge wote wanakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu.

Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, namwita sasa Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa ajili ya kuwasilisha hotuba yake.

Waheshimiwa Wabunge naomba tusikilize, Mheshimiwa Waziri wetu wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari anaanza kuwasilisha hotuba yake sasa. Karibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa humu Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Naomba hotuba

yangu yote iingie kwenye kumbukumbu za Bunge kama ilivyowasilishwa mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano huu wa Saba wa Bunge la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote, nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake madhubuti katika kipindi hiki cha zaidi ya mwaka mmoja ambacho kimekuwa na maendeleo ya uwekezaji mkubwa katika sekta zote zinazogusa maendeleo ya watu nchini. Kwa hakika katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wake kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameonesha uzalendo, uwezo, ujasiri, uhodari na mapenzi yake makubwa kwa nchi yetu na wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua kadhaa za kisera, kiutendaji alizochukua katika kipindi kifupi cha uongozi wake zimekuwa na mwangwi mkubwa uliopeleka matumaini kwa waliokata tamaa, umepeleka upendo mahali paliponyemelewa na chuki, umepeleka heshima mahali paliponyemelewa na dharau. Utendaji huu uliotukuka umezigusa pia Sekta za Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na wadau wake. Mheshimiwa Rais kwa makusudi tarehe 12 Septemba, 2021 alianzisha Wizara inayojitegemea kwa ajili ya kushughulikia Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari muundo ambao umeongeza ufanisi katika kuzihudumia sekta hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatambua matarajio makubwa waliyonayo wananchi ya kufikishiwa huduma za habari na mawasiliano kama ilivyofafanuliwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025.

Wizara hii ndiyo inayosimamia mapinduzi ya kidijitali nchini. Mapinduzi ya kidijitali ndiyo yanayoweka msingi wa kulipeleka Taifa kwenye uchumi wa kidijitali unaowezeshwa na kuendeshwa na TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchumi wa kidigitali, sekta zote hufanya kazi kwa pamoja, kwa ushirikiano, mwingiliano zikiwezeshwa na mazingira bora ya kidigitali. Mapinduzi haya yanawezeshwa na misingi muhimu ikiwemo Teknolojia ya Habari na Mawasiliano yaani TEHAMA na mifumo ya mawasiliano. Mifumo hii imerahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi ikiwemo utunzaji, utumiaji na upokeaji wa fedha yaani *financial inclusion,* usambazaji wa bidhaa, uwepo wa vyombo vya kisasa vya upashanaji habari pamoja na uhimara na uhuru wake. Aidha, uchumi wa kidigitali umewekewa mazingira bora ya kiudhibiti, kiuwekezaji na atamizi kwa ajili ya uanzishwaji na uendelezaji wa kampuni changa za ubunifu yaani *Startups*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina jukumu la kutunga na kusimamia Sera zinazohusiana na masuala ya Habari, Mawasiliano, na Teknolojia ya Habari; Kuratibu na kusimamia vyombo vya habari, mawasiliano ya posta na simu; Kuendeleza tafiti na ubunifu kwenye masuala ya TEHAMA; Kuendeleza wataalam wa TEHAMA; na Kuendeleza na kusimamia miundombinu ya mawasiliano nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu haya kutaiwezesha Tanzania kuimarika katika kushiriki uchumi wa kidijitali na kufikia Mapinduzi ya Nne ya Viwanda yaani *($4^{th}$ Industrial Revolution)* yanayowezeshwa na kuendeshwa na TEHAMA na pia kuwa na jamii inayopata taarifa sahihi kama Mheshimiwa Rais alivyobainisha kwenye hotuba yake aliyoitoa hapa Bungeni tarehe 22 Aprili, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kuchaguliwa na

Waheshimiwa Wabunge kuongoza Bunge la Kumi na Mbili. Niwapongeze Wenyeviti na Viongozi wote wa Bunge hili. Napenda kulishukuru Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano wao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa mbalimbali kuhusu Wizara. Napenda kuwahakikishia kuwa, Wizara yangu itaendelea kutoa ushirikiano unaohitajika ili kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa na ya mwananchi mmojammoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari itaendelea kuhimiza matumizi ya TEHAMA katika kuharakisha utoaji huduma, kufanya biashara, uzalishaji viwandani na kutoa elimu kwa wananchi ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kujiletea maendeleo binafsi na ya Taifa kwa ujumla. Aidha, kwa namna ya pekee, nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kuniteua kuongoza Wizara hii. Mheshimiwa Rais nakushukuru na nakuahidi sitakuangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwashukuru wapiga kura wa Jimbo langu la uchaguzi la Mtama kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kujiletea maendeleo kwenye Jimbo letu. Nawashukuru wadau mbalimbali kwa ushirikiano wao wakati wa kutimiza kazi zangu. Bila kuisahau familia yangu ikiongozwa na mke wangu mpenzi Roby, mwanangu Jaydan, Jayson na binti yangu Jailer kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upekee niishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inayoongozwa na Mheshimiwa Seleman Moshi Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki. Wizara imenufaika sana na umahiri, uzoefu, umakini na ushirikiano wa Kamati hii katika kuchambua, kushauri, kufuatilia majukumu yanayosimamiwa na Wizara. Napenda

kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa kikamilifu katika hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Philip Mpango pamoja na Waziri Mkuu ndugu yangu Majaliwa kwa usimamizi na maelekezo yao ambayo kwa pamoja yamesaidia sana katika utekelezaji wa majukumu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki na wananchi kwa kuondokewa na viongozi mbalimbali wakiwemo aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mbunge wa Jimbo la Ushetu kwa tiketi ya CCM, Elias John Kwandikwa; aliyekuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu na Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro kwa tiketi ya CCM, William Ole Nasha; aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Konde Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha *ACT*-Wazalendo, Khatib Said Haji; na aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum kupitia CCM, Mkoa wa Rukwa, Irene Alex Ndyamkama. Naomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inasimamia taasisi nane zilizogawanyika kwenye umahususi wa huduma, udhibiti, mfuko, mashirika ya kibiashara na taasisi wezeshi. Taasisi hizi ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)*, Shirika la Mawasiliano Tanzania *(TTCL)*, Shirika la Posta Tanzania *(TPC)*, Shirika la Utangazaji *(TBC)*, Kampuni ya Magazeti ya Serikali *(TSN)*, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)*, Tume ya TEHAMA *(ICTC)* na Baraza la Ushauri la Watumiaji Huduma za Mawasiliano *(TCRA-CCC)*. Hotuba hii itaelezea kwa ufupi masuala mbalimbali yanayotekelezwa na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na taasisi tunazosimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa Sekta ya Mawasiliano na Habari, kulingana na kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa cha mwaka 2020, Sekta ya Habari na Mawasiliano imekuwa kwa kasi ya asilimia 8.4 mwaka 2020. Ukuaji huu umethibitishwa na ongezeko la upatikanaji wa matumizi ya huduma za mawasiliano na kusambaa kwa huduma zitolewazo na vyombo vya habari. Kulingana na uchambuzi uliofanywa na Wizara mwaka 2021 asilimia 69 ya ardhi ya Tanzania inafikiwa na huduma za mawasiliano ya simu za kiganjani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mawasiliano imeendelea kukua, takwimu zifuatazo zinaonesha kuwa laini za simu zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka 52,965,816 mwezi Aprili, 2021 hadi kufikia laini za simu 55,365,229 mwezi Aprili, 2022, sawa na ongezeko la asilimia 4.5. Watumiaji wa *internet* wameongezeka kutoka milioni 29.1 mwezi Aprili, 2021 hadi kufikia milioni 29 mwezi Aprili mwaka huu sawa na ongezeko la asilimia 2.7. Watumiaji wa huduma za kutuma na kupokea pesa kwa njia ya mtandao wa simu wameongezeka kutoka milioni 27.3 mwezi Aprili, 2021 hadi kufikia milioni 35.7 mwezi Aprili, 2022 sawa na ongezeko la asilimia 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, watoa huduma wa miundombinu ya mawasiliano wamefikia 23 ukilinganisha na watoa huduma 19 mwezi Aprili, 2021 hii ni sawa na ongezeko la asilimia 21. Watoa huduma wa huduma ya ziada yaani *application services and value-added services* wamefikia 102 ukilinganisha na 66 mwaka 2021, hii ni sawasawa na ongezeko la asilimia 54.5. Pia, bei ya mwingiliano kati ya watoa huduma yaani *voice interconnection charges* imeshuka kutoka Shilingi 2.6 kwa dakika mwaka 2021 hadi Shilingi 2.0 kwa dakika mwaka 2022, hili ni punguzo la asilimia 23.1. Vituo vya kurusha matangazo ya redio vimeongezeka kutoka vituo 200 mwaka 2021 hadi kufikia vituo 210 mwaka

2022 na vituo vya kurusha matangazo ya runinga vimeongezeka kutoka 50 mpaka vituo 56 mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *cable television* zimeongezeka kutoka 40 mwaka 2021 mwezi wa nne na kufikia 59 mwezi wa nne mwaka huu na magazeti yameongezeka kutoka 272 na kufikia 284 mwezi Aprili mwaka huu. Serikali imeendelea kuweka mazingira rafiki ya matumizi ya teknolojia za utangazaji hasa maudhui ya mtandaoni ambayo pia yamechangia kuongeza ajira kwa vijana. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2022, televisheni mtandaoni zimeongezeka kutoka 552 hadi 663, sawa na ongezeko la asilimia 20.1, *blog* zimeongezeka kutoka 134 hadi 148, sawa na ongezeko la asilimia 10 na redio mtandaoni zimeongezeka kutoka 25 mpaka 27 sawa na ongezeko la asilimia nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za mwezi Aprili, 2022 zinaonesha kuwa asilimia 95 ya Watanzania kwenye maeneo yenye mtandao wenye uwezo wa kutoa huduma za simu, sauti na jumbe fupi yaani *2G network* kupitia minara 12,268, idadi ya asilimia 95 sasa imefikiwa. Aidha, asilimia 68 ya Watanzania wako kwenye maeneo yenye mtandao wenye uwezo wa kutoa huduma za *internet* ya kasi ya *3G* kupitia minara 11,753 na asilimia 45 ya watanzania wapo kwenye maeneo ya mtandao wa *4G* kupitia minara 6,656.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pamoja na kwamba asilimia 68 wapo kwenye maeneo ya huduma ya *internet,* jambo la kusikitisha ni asilimia 27 tu ya watumiaji wa huduma za mawasiliano wenye uwezo wa simu janja au vifaa vingine vya mawasiliano yaani *laptop, tablet, iPads* na kadhalika vyenye uwezo wa kutumia *internet*. Jitihada za Serikali za kuondoa kodi kwenye vifaa vya simu katika mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na watoa huduma kutengeneza taratibu mbalimbali za kuwakopesha wateja wao simu kumeongeza idadi ya simu janja kuwa takribani

asilimia mbili tu na kulinganisha na mwaka uliopitia kabla ya maamuzi haya hayajapitiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya TEHAMA; pamoja na teknolojia zinazoibukia kama *artificial intelligent, internet of things, block chain* na nyinginezo yanawezesha ujenzi wa miji ya kisasa na endelevu haya yote yanahitaji miundombinu thabiti ya *internet* ya kasi. Upatikanaji na utumiaji wa huduma ya *internet* ya *4G* kwa wananchi wengi unatarajiwa kuleta mageuzi makubwa katika uchumi wa kidigitali. Serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa watoa huduma au wawekezaji kujenga miundombinu ya mawasiliano ya *internet* ya kasi ili kuongeza wigo *(coverage)* wa mitandao na kuimarisha ubora wa huduma za mawasiliano ili kufikisha *internet* ya kasi kwa asilimia 80 ya Watanzania ifikapo mwaka 2025. Hii ni kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uwezo wa kuridhisha wa *internet* ya *4G* na uwekezaji unaoendelea, Serikali kupitia *TCRA* imeshachukua hatua za kutengeneza mkakati wa kuchochea miundombinu inayowezesha *internet* ya kasi yaani *5G*. Mkakati huu unahusisha pamoja na mambo mengine kupanga na kuweka masafa yatakayowezesha uwekezaji kwenye mitandao ya *5G* hapa nchini. Serikali kupitia *TCRA* ipo tayari kutoa masafa kwa watoa huduma ambao wangependa kufanya majaribio ya teknolojia ya *5G* yaani *5G trials.* Utaratibu wa kugawa masafa uliobainishwa kutumika kwa teknolojia ya *5G* utakuwa wa ushindani (*transparent and competitive process)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato na ukusanyaji wake; hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 Wizara imekusanya jumla ya Sh.41,098,558,762.5 kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambayo ni sawa na asilimia 82.2 na makadirio ya makusanyo ya Shilingi Bilioni 50 na kiasi cha Shilingi Bilioni 8.6 kutokana na tozo ya kuongeza

salio kwenye laini za simu. Aidha, Idara ya Habari - Maelezo imekusanya Sh.354,190,750 kutokana na mauzo ya picha za Viongozi Wakuu wa Nchi na picha ya Baba wa Taifa, vitambulisho, machapisho na ada ya mwaka ya magazeti sawa na asilimia 199 ya lengo la Shilingi Milioni 178.2. Kuvuka kwa malengo ya makusanyo kumetokana na kuuzwa kwa wingi kwa picha ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mara baada ya kuapishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka 2021/2022; katika huo wa fedha, iliyokuwa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa kutumia kiasi cha Sh.246,384,551,000. Kati ya fedha hizo Sh.4,984,770,000 ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.241,399,781,000 ziliidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, Idara ya Habari - Maelezo na Taasisi za *TBC* na *TSN* zilikuwa zimetengewa bajeti ya jumla ya Sh.23,744,630,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, ambapo Sh.17,743,630,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.6,000,000,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022, Wizara imepokea na kutumia Sh.6,946,838,745.79 sawa na asilimia 84 ya fedha zilizotengwa. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa Sh.2,288,345,600 ni mishahara na Shilingi Bilioni 4.6 ni matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maendeleo; hadi kufika tarehe 30 Aprili, 2022, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Fungu 68 imepokea jumla ya Sh.129,713,798,179.86 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo ni sawa na asilimia 53.7 ya fedha zilizotengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya

kufikisha huduma za mawasiliano vijijini na mijini kusiko na mvuto kibiashara. Hadi sasa utekelezaji wa miradi hiyo upo katika hatua mbalimbali ambapo ujenzi wa minara 181 *passive part* umekamilika. Kwa sasa hivi watoa huduma wapo katika hatua za kuingiza vifaa vya kurushia mawimbi ya simu na hatimaye kuwashwa kwa minara hiyo. Minara hii inategemewa kuwashwa kabla ya mwezi Oktoba mwaka huu 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Serikali kupitia *UCSAF* imeingia makubaliana na watoa huduma za mawasiliano kwa ajili ya kujenga minara 161 Tanzania Bara na Visiwani minara hii inajengwa katika maeneo ya mipakani, maeneo ya Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri ambazo zilikuwa hazina huduma za mawasiliano pamoja na Zanzibar, ujenzi wa minara hii upo katika hatua mbalimbali. Kwa upande wa Zanzibar ujenzi wa minara 42 upo katika hatua za ukamilishwaji, ambapo ujenzi wa minara hiyo unatarajiwa kukamilika mwezi Juni mwaka huu. Kwa upande wa miradi mingine 119 ujenzi upo katika hatua za awali ikiwa ni pamoja na kutafuta maeneo kwa ajili ya ujenzi pamoja na kutafuta Wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu katika maeneo mengine. Katika Mwaka wa Fedha 2022 wizara katika eneo la mawasiliano imetekeleza majukumu yafuatayo:-

Moja, kuanza maandalizi ya kuhuisha Sera ya Mawasiliano ya Simu ya Mwaka 1997 na mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya *TEHAMA;*

Mbili, kuendelea kuratibu ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Umoja wa Posta Afrika ambao tumefikia asilimia 65;

Tatu, kuendeleza mashirikiano ya Kikanda na Kimataifa ambapo Wizara imeshiriki Mikutano Mikuu mbalimbali na tumepewa dhamana ya kuongoza baadhi ya taasisi hizi,

Nne, kuendelea kuratibu jitihada za ufikishaji wa huduma za mawasiliano na simu katika maeneo ambayo bado hayajafikiwa na yenye mawasiliano hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala yaliyofanyika ni pamoja na ukaguzi wa mawasiliano katika maeneo mbalimbali ikiwemo eneo la Pori Tengefu la Loliondo lenye Kata 15 Visiwa 171 vya Ziwa Victoria, maeneo ya Kanda ya Ziwa, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Kati na Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yaliyobainishwa yatafikishiwa huduma kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote. Aidha, katika kuratibu jitihada hizi za ufikishaji wa huduma za mawasiliano wizara imeandaa mkakati wa kuimarisha mawasiliano kwa kipindi cha miaka Minne ili kuboresha huduma za mawasiliano nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tano, kufanya mapitio ya sekta ndogo ya utangazaji na mfumo wa leseni ili kuweka mazingira wezeshi kwa maendeleo ya sekta. Wizara imetoa leseni 25 kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali kupitia Sekta ya Mawasiliano na TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara imetekeleza majukumu mengine yafuatayo:-

i) Kukamilisha uaandaaji wa Mkakati wa Taifa wa intaneti yenye kasi yaani *National broadband Strategy*;

ii) Kuandaa Mwongozo wa Kitaifa wa kushughulikia masuala ya uhalifu mtandaoni unaongeza uratibu wa pamoja kwa taasisi zote zinazoshughulikia masuala ya uhalifu ya kimtandao.

iii) Kuingia mkataba wa mashikiriano na *TANESCO* kwa ajili ya kufanya kazi pamoja ya kupitisha miundombinu ya mawasiliano kwenye nguzo za umeme kwa lengo la kuongeza mtandao wa mawasiliano. Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii imepunguza gharama za ujenzi wa Mkongo na kuharakisha mradi huu ambapo zilikuwa zijengwe Kilomita 1,880 lakini kutokana na Mkataba huu zitajengwa Kilomita 4,442 na kufikisha jumla ya Kilomita 12,761 za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

iv) Kuratibu utengenezaji wa mfumo wa kutunza na kuchakata taarifa za kesi na matukio ya uhalifu wa usalama mtandao yaani *cybercrimes module* inayowezesha matukio ya uhalifu kutunzwa, kufuatilia mwenendo wa mashtaka husika hadi pale inapokamilika *process* nzima.

v) Kutoa mafunzo kwa Waendesha Mashtaka, Wachunguzi na Wapelelezi zaidi ya 197 pamoja na mafunzo ya kutumia *cybercrimes module* kwa watumishi 470 wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

vi) Kukamilisha uandaaji wa rasimu ya Mkakati wa Uchumi wa kidijitali *Digital Economy Strategic Framework* kwa ajili ya kuchochea matumizi ya *TEHAMA* kwenye sekta za uchumi, kukamilisha uandaaji wa mwongozo wa mageuzi ya kidijitali yaani *Digital Transformation Guideline* kwa ajili ya kutoa mwongozo wa taasisi zote nchini wa kuelekea kwenye uchumi wa kidijitali.

vii) Kamilishwaji wa Mkakati wa Taifa wa Elimu kwa Umma wa Usalama Mtandaoni (*National Cyber Security Communication Strategy)*.

viii) Kukamilisha na kuingia makubaliano na ushirikiano kwenye maeneo ya TEHAMA na nchi ya Rwanda aidha, majadiliano na nchi ya Kidemokrasia ya Kongo, Uganda, Kenya, Marekani, Ujerumani, Uturuki na Falme za Kiarabu yanaendelea.

ix) Kuanza mchakato wa kuhamishia shughuli za ujenzi, usimamizi na uendeshaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa Shirika La Mawasiliano la Taifa (*TTCL)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Habari Maelezo. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara imetekeleza majukumu yafuatayo:-

i) Kuisemea Serikali kuhusu utekelezaji wa Sera, Mikakati, Miradi mbalimbali;

ii) Kuratibu ratiba za Mawaziri na Viongozi kuzungumza kupitia runinga na pia kukutana na Waandishi wa Habari kuelezea mafanikio na utekelezaji wa Serikali ya Awamu ya Sita;

iii) Kuandaa, kuchapisha na kusambaza nakala zaidi ya 5,000 za jarida la nchi yetu, kukusanya na kusambaza habari kuhusu utekelezaji wa miradi ya Serikali, kuendelea kuhamasisha Vyombo vya Habari vya nje na ndani kutangaza Tanzania vyombo vya habari vya nje ambavyo vimeshirikishwa ni pamoja na *CCTV, DW, BBC, Voice of America*, *Xinhua* na *CGTV* vilishiriki katika kuitangaza Tanzania katika shughuli mbalimbali;

iv) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha uhuru wa vyombo vya Habari, Serikali imetoa jumla ya leseni mpya 19 kwa magazeti hivyo kufanya jumla ya Vyombo vya Habari vilivyosajiliwa kufikia 285;

v) Kuhuisha Kanuni za utangazaji kwa njia ya kidijitali za mwaka 2018 ili kuruhusu watoa huduma wanaotoa maudhui ya bila malipo kwa wananchi *free to air* kubebwa katika visimbuzi vya kulipia;

vi) Kuendelea kuratibu maandalizi ya mkakati wa Taifa wa mawasiliano *(National Communication Strategy);*

vii) Mwisho, kuratibu mkutano wa siku ya uhuru wa vyombo vya habari duniani ambao kwa Bara zima la Afrika ulifanyika Jijini Arusha hapa Tanzania na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan alikuwa mgeni rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2021/2022 tunaoumaliza Wizara imetekeleza majukumu mengi ikiwa ni pamoja na kuhuishwa Sheria Tatu na Kanuni Nne.

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**MWENYEKITI:** Kengele ya kwanza Mheshimiwa Waziri kwa hiyo anza kuhitimisha.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria zilizohuishwa ni pamoja na *EPOCA* ya mwaka 2010, Sheria ya Mfuko wa Mawasiliano *UCSAF* ya mwaka 2016, Sheria ya Posta ya mwaka 1993. Sheria hizi zimehuishwa hili kuboresha utendaji wa taasisi husika mazingira ya utoaji huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni zilizohuishwa ni pamoja na leseni za mwaka 2018 kanuni za utangazaji kidijitali za mwaka 2018, kanuni za maudhui ya mtandaoni ya mwaka 2020, na kanuni za utangazaji redioni na kwenye luninga. Kuratibu na kusimamia uandaaji wa nyaraka za Baraza la Mawaziri kuhuisha mpango wa mkakati wa Wizara kwa kipindi cha miaka mitano, kuajiri watumishi kadhaa, kuandaa mpango wa vihatarishi wa Wizara na rejesta vihatarishi *(risk register)*, Bodi za Wakurugenzi wa taasisi tatu zimeundwa, usimamizi na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Wizara pale Mtumba lenye ghorofa Saba ambapo hivi sasa liko katika hatua za ghorofa ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mbalimbali iliyotekelezwa ya maendeleo. Kwanza ni mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano umekusudiwa kupanua mawasiliano ya simu na *internet* nchini na nchi zinazotuzunguka katika kufanikisha mapinduzi ya kidijitali. Katika kipindi kinachoishia mwezi Aprili kazi zifuatazo zimefanyika.

i) Kukamilisha kwa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano KM 165 kutoka Itigi – Manyoni - Rungwa);

ii) Kukamilika kwa Ujenzi wa Kilomita 72 za Mkongo wa kuunganisha Ofisi za Serikali yaani Kikombo – Mtumba pale Msalato;

iii) Kukamilika kwa Ujenzi wa Kilomita 72 za Mkongo wa Taifa, kwenye eneo la Mtambaswala kuunganisha Tanzania na Msumbiji;

iv) Kukamilika kwa Upembuzi yakinifu kuunganisha Mkongo wa Taifa na nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (*DRC)* na nyaraka ya zabuni zimeandaliwa, kwa hiyo mpango huko

tayari tuko tayari kuungana na Congo kuwapa huduma ya mkongo.

v) Kukamilika kwa kazi ya kukarabati Kilomita 105 za ujenzi wa mkongo kutoka Arusha - Namanga kupitia miundombinu ya *TANESCO*;

vi) Kukamilika kwa Ujenzi wa Kituo cha Kutolea Huduma za Mkongo wa Taifa kwenye Mji wa Serikali yaani Mtumba;

vii) Kukamilika kwa taratibu za manunuzi za kuwezesha ujenzi wa Kilomita 4,442 za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, upanuzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kutoka kiwango cha 200G hadi 800G na kujenga vituo vipya 37 na upanuzi wa vituo 75 vya kutolea huduma za Mkongo, ambapo mikataba 22 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 141 imesainiwa. Aidha, utekelezaji huu utafikisha Mkongo katika Wilaya 23.

viii) Kukamilika kwa Upanuzi wa Mkongo wa Taifa kwenye vituo Vitano vya Kigoma, Arusha, Babati, Tunduma na Mbeya vyenye jumla ya kadi za kuchakata huduma *line processing cards* 30;

ix) Kukamilika kwa kazi ya kuhamisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano wenye urefu wa Mita 250 eneo la makazi ya watu kule Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa mfumo wa Anwani za Makazi. Kufuatia malengo ya Serikali ya kukamilisha Anwani za Makazi kabla ya Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika Mwezi Agosti tarehe 23, katika Kikao kazi cha Wakuu wa Mikoa kilichofanyika tarehe 08 Februari, 2022, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alielekeza Mfumo wa

Anwani za Makazi kutekelezwa kwa Mfumo wa Operesheni, aliyoipa jina la ‘‘Operesheni Anwani za Makazi’’.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI zimeendelea na utekelezaji wa mradi huu chini uratibu mzuri na hodari wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Waziri Mkuu mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2022 shughuli nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na:

(i) Kuunda programu tumizi *(Mobile application)* ya mfumo iliyoongeza ufanisi katika matumizi ya utekelezaji wa mfumo.

(ii) Semina ya kujengea uwezo watu ambao walikuwa wanahusika na utekelezaji na viongozi mbalimbali kwenye ngazi zetu za Mikoa hadi kufikia tarehe 18 Mei, jumla ya anuani za makazi 12,339,471 zimekusanywa na kuingizwa kwenye *program* tumizi idadi ya anuani zilizokusanywa ni asilimia 106.53 ya lengo la anuani zilizotakiwa kukusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kazi ya kuweka alama kwa maana ya namba za nyumba na vibao inaendelea, nayo inakwenda kwa kasi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Tanzania ya kidijitali una thamani ya Dola za Marekani Milioni 150 na ulisainiwa tarehe 19 Agosti, 2021. Mradi huu unalenga kuboresha na kukuza maunganisho ya ndani na ya kimataifa ili kuweza kufikisha huduma za mawasiliano pamoja na utoaji wa huduma mbalimbali za Serikali kwa wananchi. Kazi zilizotekelezwa katika mradi huu, moja ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya mradi katika eneo la *Area D* na kuanza kutumika, kukamilisha usanifu na kuandaa mahitaji ya

kuwezesha ununuzi wa bando la intaneti ya Serikali *(Government Internet Bandwidth)*, kukamilisha usanifu na kuandaa mahitaji ya kuwezesha kujenga na kuboresha mtandao wa TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilisha ukusanyaji wa mahitaji kuwezesha kujenga na kupandisha hadhi minara 150 ya mawasiliano kutoka teknolojia ya 2G kwenda 3G/4G ili kuwezesha huduma za intaneti yenye kasi, kukamilisha manunuzi ya vifaa na programu endeshi, kufanya tathmini ya maeneo ya kujengewa uwezo kwa watumishi wa TEHAMA Serikalini, kufanya maandalizi ya kuwezesha ujenzi wa Chuo cha TEHAMA ambapo eneo lenye ukubwa wa Hekta 400 limepatikana eneo hapa Nala Jijini Dodoma ambacho chuo hiki kitajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya Wizara kwa kwa Mwaka wa Fedha 2022 katika Mwaka wa Fedha Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia Habari Fungu 68 inakaribia kukusanya kiasi cha Shilingi Bilioni mia moja na Hamsini, Mia Saba Elfu (150,700,000,000) ambazo zinatokana na mauzo ya huduma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri omba fedha sasa.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 282,056,786,000 kwa mchanganuo ufuatao:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha Shilingi 26,279,346,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo Shilingi 17,249,317,000 ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi 9,030,029,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kiasi cha fedha cha Shilingi 255,777,440,000 kinaombwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ambapo Shilingi

215,777,440,000 ni fedha za ndani na Shilingi Bilioni 40 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii inapatikana kwenye tovuti ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## HOTUBA YA WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI MHESHIMIWA NAPE MOSES NNAUYE (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIOYA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### A. UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia taarifa iliyowasilishwa humu Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2021/22. Aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2022/23.

**2.** ***Mheshimiwa Spika***, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema; na kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano huu wa saba wa Bunge la kumi na mbili.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake madhubuti katika kipindi hiki cha zaidi ya mwaka mmoja ambacho kimekuwa na maendeleo na uwekezaji mkubwa katika Sekta ya Habari,

Mawasiliano na TEHAMA. Wizara inatambua matarajio makubwa waliyonayo wananchi ya kufikishiwa huduma za Habari na Mawasiliano kama ilivyofafanuliwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025. Kwa kutambua matarajio haya Mheshimiwa Rais alianzisha Wizara hii mpya **tarehe 12 Septemba, 2021** ili kuharakisha ufikishaji huduma kwa wananchi.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara hii ndio inayosimamia Mapinduzi ya Kidijitali nchini. Mapinduzi ya Kidijitali ndio yanayoweka msingi wa kulipeleka Taifa kwenye Uchumi wa Kidijitali unaowezeshwa na kuendeshwa na TEHAMA. Katika uchumi wa kidigitali, Sekta zote hufanya kazi kwa pamoja, kwa ushirikiano na muingiliano zikiwezeshwa na mazingira bora ya kidigiti. Mapinduzi haya yanawezeshwa na misingi muhimu ikiwemo TEHAMA, Mifumo ya Mawasiliano, tendaji, fedha, usambazaji kwa njia ya posta, Uwepo wa vyombo vya upashanaji Habari pamoja na uimara wa uhuru husika. Aidha, Uchumi wa Kidigitali unawekewa mazingira bora ya kiudhibiti, kiuwekezaji na atamizi kwa ajili ya uanzishwaji na uendelezaji wa Kampuni changa (Startups).

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kutunga na kusimamia Sera zinazohusiana na masuala ya Habari, Mawasiliano, na Teknolojia ya Habari kuratibu na kusimamia vyombo vya Habari, Mawasiliano ya Posta na Simu; kuendeleza tafiti na ubunifu kwenye masuala ya TEHAMA; kuendeleza wataalam wa TEHAMA, na kuendeleza na kusimamia miundombinu ya Mawasiliano nchini. Utekelezaji wa majukumu haya kutaiwezesha Tanzania kuimarika kushiriki uchumi wa kidijitali katika kufikia Mapinduzi ya Nne ya Viwanda ($4^{th}$ *Industrial Revolution*) yanayowezeshwa na kuendeshwa na TEHAMA na pia kuwa na jamii inayopata taarifa sahihi kama Mheshimiwa Rais alivyobainisha kwenye Hotuba yake aliyotoa hapa kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 22 Aprili, 2021.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba nikupongeze wewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuchaguliwa na Waheshimiwa Wabunge kuongoza Bunge la Kumi na Mbili. Ninapenda kuwashukuru Watendaji wa Ofisi ya Bunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano wao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu pamoja na wakati wa kuwasilisha taarifa mbalimbali kuhusu Wizara. Ninapenda kuwahakikishia kuwa, Wizara yangu itaendelea kutoa ushirikiano unaohitajika ili kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa na ya mwananchi mmoja mmoja kijamii na kiuchumi. Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari itaendelea kuhimiza matumizi ya TEHAMA katika kuharakisha utoaji huduma, kufanya biashara, uzalishaji viwandani na kutoa elimu kwa wananchi ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kujiletea maendeleo binafsi na ya Taifa kwa ujumla. Aidha, kwa namna ya pekee nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuongoza Wizara hii wezeshi na mtambuka katika kuivusha nchi kuelekea katika mapinduzi ya Uchumi wa Kidijitali yanayowezeshwa na kuendeshwa TEHAMA. Naomba kuwashukuru wapiga kura wa Jimbo langu la Uchaguzi la Mtama kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kujiletea maendeleo kwenye Jimbo letu; bila kuisahau familia yangu kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu kwa Watanzania.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** ninachukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inayoongozwa na **Mheshimiwa Seleman Moshi Kakoso** Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini na Makamu Mwenyekiti **Mheshimiwa Anne Kilango Malecela** Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki. Wizara imenufaika sana na umahiri, umakini na ushirikiano wa Kamati hiyo katika kuchambua, kushauri na kufuatilia majukumu yanayosimamiwa na Wizara. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba maoni,

ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa kikamilifu katika Hotuba hii.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa ndugu, jamaa, marafiki na wananchi kwa kuondokewa na viongozi mbalimbali wakiwemo aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mbunge wa Jimbo la Ushetu kwa tiketi ya CCM Elias John Kwandikwa, aliyekuwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu na Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro kwa tiketi ya CCM William Ole Nasha, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Konde Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha ACT-Wazalendo, Khatib Said Haji na ailyekuwa Mbunge wa Viti Maalum kupitia CCM, Mkoa wa Rukwa, Irene Alex Ndyamkama. Ninaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Fungu 68) inasimamia Taasisi Nane zilizogawanyika kwenye umahsusi wa Huduma, udhibiti, mfuko, mashirika ya kibiashara na taasisi wezeshi. Taasisi hizo ni: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA); Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL); Shirika la Posta Tanzania (TPC); Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC); Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN); Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF); Tume ya TEHAMA (ICTC); na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA-CCC). Hotuba hii itaelezea kwa ufupi masuala mbalimbali yanayotekelezwa na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na taasisi inazosimamia.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ina jukumu kuu la udhibiti wa huduma za Mawasiliano kama ilivyoainishwa kwa Sheria ya Mamalaka ya Mawasiliano Tanzania Sura Na. 172 (*Tanzania Communications Regulatory Act CAP. 172*) ambapo pamoja na mambo mengine, Mamlaka imekabidhiwa majukumu ya:-

i) Kutoa leseni za watoa huduma za mawasiliano nchini;
ii) Kuongeza muda wa leseni na kufuta leseni pale ambapo masharti ya leseni husika hayakufuatwa;
iii) Kuweka viwango kwa bidhaa na huduma zinazosimamiwa kama gharama za maunganisho kati ya mtandao mmoja na mwingine;
iv) Kulinda watumiaji wa huduma za mawasiliano;
v) Kusimamia rasilimali adimu za mawasiliano ikiwemo masafa, namba na majina ya vikoa;
vi) Kufuatilia utendaji wa sekta zinazodhibitiwa ikiwa ni pamoja na;
    a) Viwango vya uwekezaji;
    b) Upatikanaji, ubora na viwango vya huduma;
    c) Gharama za huduma; na
    d) Ufanisi wa uzalishaji na usambazaji wa huduma.
vii) Kukuza ushindani katika sekta;
viii) Kusambaza taarifa zinazohusu kazi na majukumu ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania; na
ix) Kushauriana na mamlaka nyingine za udhibiti katika kutekeleza majukumu sawa na yale ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***11 Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Posta Tanzania lilianzishwa kwa Sheria Sura Na. 303 na lilianza kazi rasmi tarehe 1 Januari, 1994 baada ya kuvunjwa kwa lililokuwa Shirika la Posta na Simu Tanzania. Baada ya kuvunjwa, iliundwa Kampuni ya Simu Tanzania na Shirika la Posta Tanzania kwa mgawanyo wa mali wa asilimia 70 kwa 30 mtawalia. Shirika la Posta linamilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia 100. Shirika lina majukumu makuu manne kama ifuatavyo:-

i) Kutoa huduma za Posta ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

ii) Kutosheleza mahitaji ya kitaifa ya huduma za Posta katika sekta za viwanda, biashara na jamii kwa ujumla kwa ufanisi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

iii) Kutoa huduma za kutuma na kulipa fedha kwa njia ya hawala za Posta (*Money Order* na *Postal Order*), au kwa kutumia njia nyingine zinazoonekana zinafaa; na

iv) Kutoa huduma za Kaunta kwa ajili ya Shirika na Huduma za Serikali bila kuathiri majukumu mengine yaliyotajwa katika Sheria ya uanzishwaji wa Shirika.

***12 Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL Corporation) ni Shirika la Umma lenye jukumu la kutoa huduma za mawasiliano kwa jamii na kusimamia uendeshaji wa Miundombinu ya Kimkakati kwa usalama wa nchi. Shirika lilianzishwa kupitia Sheria Na. 12 ya Bunge ya mwaka 2017 (*Tanzania Telecommunications Corporation Act, No. 12 of 2017*). Kwa mujibu wa sheria hiyo, Shirika la Mawasiliano Tanzania lina majukumu ya msingi yafuatayo: -

i) Kuimarisha ulinzi na usalama wa huduma za mawasiliano ya simu nchini na utoaji wa huduma ya mawasiliano ya simu kibiashara na kiuchumi;
ii) Kutoa huduma za mawasiliano ya simu kwa mujibu wa Sheria;
iii) Kujenga na kuendesha miundombinu ya mawasiliano ya kimkakati kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana;
iv) Kutoa huduma ya miamala ya kifedha inayohusiana na mawasiliano ya simu;
v) Kuendesha mifumo na huduma ya mawasiliano ya simu ikiwemo mfumo wa TEHAMA ndani na nje ya nchi;
vi) Kutoa huduma za mawasiliano kwa njia ya sauti na picha;

vii) Kutoa ushauri wa kitaalamu katika masuala yanayohusu TEHAMA kwenye mashirika, Taasisi za umma na kwa wajasiriamali; na
viii) Kukuza uwekezaji wa huduma za mawasiliano ya simu ndani na nje ya nchi.

***13 Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) ni taasisi ya huduma kwa umma iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika ya Umma, Sura ya 257 (2002). Kabla ya kuanzishwa TBC kupitia Tangazo la Serikali Na.186 la Mwaka 2007, taasisi hii ilijulikana kama Taasisi ya Utangazaji Tanzania (TUT) ambayo ilitokana na muungano wa iliyokuwa Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD) na Televisheni ya Taifa (TVT). Shirika linatekeleza majukumu yake kupitia vyombo vyake vya habari vikiwemo:

a. Redio (***TBCTaifa, TBCFM, na TBCIntentational***);
b. Televisheni ($TBC_1$, $TBC_2$, na $TBC_3$ (au Tanzania *Safari Chaneli);*
c. TBC Mtandao (Tovuti ya www.tbc.go.tz, Programu Tumizi ya TBC Live, ***Facebook***, ***Instagram*** na ***Twitter***. Shirika pia lina Tovuti na Programu Tumizi ya *Tanzania Safari Channel (**www. tanzaniasafarichannel.go.tz**);*
d. Studio za redio za Kanda (Magharibi – **Kigoma**; Kaskazini – **Arusha**; Makao Makuu – **Dodoma**; na Ziwa Nyasa - **Songea**).

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** Majukumu makuu ya TBC ni kuhabarisha, kuelimisha, kuburudisha na kutafakarisha kwa kuzingatia kaulimbiu ya **'*Ukweli na Uhakika*'.** Chombo cha Utangazaji cha Umma (*Public Service Boradcaster* - PSB) kina sifa na majukumu yafuatayo:

(i) Kuwafikia wananchi wote nchini bila kujali umbali, idadi ya wakazi au gharama;
(ii) Kuandaa maudhui yanayohusu na kugusa maisha ya makundi yote ya jamii na kwa kuzingatia utamaduni;

(iii) Kuendesha huduma ya utangazaji kwa fedha zinazotokana na bajeti au vyanzo vingine;
(iv) Kulinda, kuendeleza na kudumisha utamaduni wa Taifa;
(v) Kulinda, kutetea na kusimamia rasilimali za Taifa kama vile maliasili, madini, gesi, mafuta, mazingira na urithi wa kihistoria;
(vi) Kukuza na kudumisha uzalendo, kutetea na kusimamia maslahi ya Taifa; na
(vii) Kulinda, kutetea na kujenga taswira chanya ya Taifa.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) ilianzishwa kwa Tamko la Rais la mwaka 1970 na imetokana na utaifishaji wa iliyokuwa Tanganyika Standard Newspapers Limited. Kampuni hii inasimamiwa na kuendeshwa chini ya Sheria ya Makampuni Sura ya 212. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitia Msajili wa Hazina inamiliki asilimia 99 ya hisa na Mhariri Mtendaji anamiliki asilimia 1 ya hisa kwa minajili ya kukidhi matakwa ya Sheria. Kampuni hii huchapisha magazeti mbalimbali kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Magazeti yanayochapwa kwa lugha ya Kiingereza ni Daily News na Sunday News na yale ya Kiswahili ni HabariLeo pamoja na gazeti la Michezo la Spotileo ambalo huchapishwa mara mbili kwa wiki. Pamoja na magazeti hayo, Kampuni pia hutoa vijarida mbalimbali vinavyolenga makundi maalum, kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza. TSN pia inatumia njia ya mtandao kusambaza habari mbalimbali ndani na nje ya nchi kupitia tovuti pamoja na mitandao ya kijamii kama vile *Facebook*, *Twitter*, *Instagram* na *Youtube*. Aidha, Kampuni inamiliki kiwanda cha uchapaji ambacho hutumika kwa ajili ya kuchapa magazeti yake na pia kufanya uchapaji wa kibiashara kwa kutumia mtambo mdogo wa kidijitali.

Kampuni lina majukumu makuu manne kama ifuatavyo: -

i) Kuwa chombo cha mawasiliano kati ya Serikali na wananchi na wananchi na Serikali yao;

ii) Kuunga mkono sera na mipango ya serikali na kuhabarisha na kuelimisha umma juu ya sera na mipango hiyo;
iii) Kutafuta na kuandika habari sahihi zenye michango mbalimbali katika sayansi, jamii, siasa, uchumi na utamaduni; na
iv) Kuwa kiini cha kutoa habari kwa lengo la kukuza uchumi na kueneza amani na mshikamano kwa Watanzania.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ulianzishwa kwa Sheria Namba 11 ya Mwaka 2006, Sura ya 422, kwa lengo la kupeleka na kufikisha huduma ya mawasiliano kwa wananchi waishio katika maeneo ya mijini na maeneo ya vijijini yasiyo na mvuto wa kibiashara kwa kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano. Mwaka 2009 kanuni za Mfuko zilipitishwa na Mfuko kuanza kazi tarehe 1 Julai, 2009.

Malengo ya Mfuko yaliyoainishwa na sheria ya uanzishwaji wake yamejikita katika maeneo yafuatayo:
i) Kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya mawasiliano katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mijini yenye mawasiliano hafifu;
ii) Kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi na Serikali katika utoaji wa huduma za mawasiliano kwa wote katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mijini yenye mawasiliano hafifu;
iii) Kuhamasisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mijini yenye mawasiliano hafifu;
iv) Kutengeneza mfumo kwa ajili ya upatikanaji wa mitandao ya mawasiliano na huduma rahisi na zenye ufanisi katika uzalishaji na upatikanaji katika soko la kiushindani;
v) Kuhamasisha utoaji wa huduma bora katika viwango nafuu na kuhakikisha kuwa Teknolojia ya Habari na

Mawasiliano inapatikana vijijini na sehemu za mijini zenye mawasiliano hafifu kwa bei nafuu; na

vi) Kuhakikisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano kupitia ushiriki wa sekta binafsi.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya TEHAMA ilianzishwa kwa Amri ya Rais kupitia Tangazo Namba 532 lililochapishwa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 20 Novemba, 2015. Uanzishwaji wa Tume ya TEHAMA nchini ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA ya Mwaka 2003 na maelekezo ya Baraza la Mawaziri yaliyotolewa Juni, 2012 kuhusu kuunda Tume ya Kitaifa ya kuratibu, kusimamia na kuendeleza Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) nchini.

Kwa mujibu wa Amri iliyoanzisha Tume ya TEHAMA, majukumu yake ni pamoja na:-

i) Kukuza uwekezaji katika TEHAMA;
ii) Kujenga uwezo na kukuza utaalamu na viwango katika fani ya TEHAMA;
iii) Kushauri na kushirikiana na wadau wengine kwenye masuala ya tafiti na kuweka viwango na mwelekeo;
iv) Kuhifadhi na kuendeleza miundombinu na programu za TEHAMA; na
v) Kufanya kazi nyingine zozote zitakazoainishwa na Sheria.

**18. Mheshimiwa Spika,** Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano limeanzishwa kwa Sheria ya Mamalaka ya Mawasiliano Tanzania Sura Na. 172 (*Tanzania Communications Regulatory Act CAP. 172*) Kifungu cha 37. Kulingana na Sheria iliyoanzisha Baraza, Kifungu cha 38 kinalipa Baraza majukumu yafuatayo:

i) Kuwakilisha maslahi ya watumiaji wa huduma za mawasiliano zinazosimamiwa kisheria kwa kushauriana na TCRA, Waziri mwenye dhamana ya mawasiliano na watoa huduma.

ii) Kupokea na kusambaza taarifa na maoni kuhusu masuala ya msingi ya watumiaji wa huduma za mawasiliano;
iii) Kuanzisha kamati za watumiaji katika ngazi za mikoa, wilaya na sekta na kushauriana na kamati hizo; na
iv) Kufanya mashauriano na wahusika katika sekta, Serikali na makundi mengine ya watumiaji wa huduma kuhusiana na masuala ya msingi ya watumiaji wa huduma zinazosimamiwa kisheria.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22

### Ukuaji wa Sekta ya Habari na Mawasiliano

**19.** ***Mheshimiwa Spika***, kulingana na Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa cha mwaka 2020, Sekta ya Habari na Mawasiliano imekua kwa kasi ya **asilimia 8.4** mwaka 2020. Ukuaji huu unathibitishwa na ongezeko la upatikanaji na matumizi ya huduma za mawasiliano na kusambaa kwa huduma zitolewazo na vyombo vya habari. Kulingana na uchambuzi uliofanywa na Wizara Mwaka 2021 **asilimia 69** ya ardhi ya Tanzania (*Geographical Coverage*) inafikiwa na huduma ya mawasiliano ya simu za kiganjani. Sekta hii huchangia katika uchumi moja kwa moja na kupitia sekta zingine zote kama nyenzo ya uwezeshaji katika kuongeza ufanisi wa utendaji kupitia Teknolojia ya Habari.

**20.** ***Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Mawasiliano imeendelea kukua, takwimu zinaonyesha kuwa laini za simu zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka **52,965,816** Mwezi Aprili, 2021 hadi kufikia laini **55,365,239** Mwezi **Aprili**, 2022 sawa na ongezeko la **asilimia 4.5**. Watumiaji wa intaneti wameongezeka kutoka Milioni 29.1 Mwezi Aprili, 2021 hadi kufikia **Milioni 29.9** Mwezi Aprili, 2022 sawa na ongezeko la **asilimia 2.7**. Watumiaji wa huduma za kutuma na kupokea pesa kwa

njia ya mtandao wa simu wameongezeka kutoka **27,326,938** Mwezi Aprili, 2021 hadi kufikia **35,749,298** mwezi Aprili, 2022 sawa na ongezeko la **asilimia 30.8.** Aidha, Watoa huduma wa Miundombinu ya Mawasiliano wamefikia **23** ukilinganisha na watoa huduma **19** Mwezi Aprili, 2021 (hii ni sawa na ongezeko la asilimia **21.1**). Watoa huduma wa huduma za ziada (Application Services and Value Added Services) wamefikia **102** ukilinganisha na watoa huduma **66** Mwezi Aprilii, 2021 (ongezeko la asilimia 54.5). Pia, Bei ya mwingiliano kati ya watoa huduma (Voice interconnection Charges) imeshuka kutoka **Shilingi 2.6** kwa dakika mwaka 2021 hadi **Shilingi 2.0** kwa dakika mwaka 2022 sawa na punguzo la asilimia **23.1**. Vituo vya kurusha matangazo ya redio vimeongezeka kutoka vituo **200** mwaka 2021 hadi kufikia vituo **210** Mwezi Aprili, 2022 sawa na ongezeko la asilimia 5 na vituo vya kurusha matangazo ya runinga vimeongezeka kutoka vituo **50** mwaka 2021 na kufikia vituo **56** Mwezi Aprili, 2022 sawa na ongezeko la asilimia 12. *Cable Television* zimeongezeka kutoka **40** Mwezi Aprili, 2021 na kufikia **59** Mwezi Aprili, 2022 sawa na ongezeko la asilimia 47.5 na magazeti yameongezeka kutoka **272** na kufikia **284** Mwezi Aprili, 2022 sawa na ongezeko la asilimia **4.4**. Serikali imeendelea kuweka mazingira rafiki ya matumizi ya teknolojia za Utangazaji hasa maudhui mtandaoni ambayo pia yamechangia kuongeza ajira kwa vijana. Kufikia Mwezi April**i, 2022** televisheni mtandao zimeongezeka kutoka **552** hadi **663** sawa na ongezeko la asilimia **20.1**, blogu zimeongezeka kutoka **134** hadi **148** sawa na ongezeko la asilimia **10.4** na redio mtandao zimeongezeka kutoka **25** hadi **27** sawa na ongezeko la asilimia **8.0**.

**Ukusanyaji wa Mapato**

**21**. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 446,306,000,000**

ambapo **Shilingi 396,306,000,000** ilikadiriwa kutokana na tozo ya kuongeza salio kwenye laini za simu na **Shilingi 50,000,000,000** ni kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa mawasiliano. Aidha, Idara ya Habari-MAELEZO ilikadiriwa kukusanya kiasi cha **Shilingi 178,017,222** kutokana na mauzo ya picha, vitambulisho, machapisho na Ada ya mwaka ya magazeti.
Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 Wizara imekusanya jumla ya **Shilingi 41,098,538,762.15** kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambayo ni sawa na asilimia 82.2 ya makadirio ya makusanyo; na kiasi cha **Shilingi 8,621,793,488** kutokana na tozo ya kuongeza salio kwenye laini za simu sawa na asilimia 2.2 ya lengo. Aidha, Idara ya HabariMAELEZO imekusanya **Shilingi 354,190,750** kutokana na mauzo ya picha za Viongozi Wakuu wa nchi na picha ya Baba wa Taifa, vitambulisho, machapisho na ada ya mwaka ya magazeti sawa na asilimia 199. Kuvuka kwa malengo ya makusanyo kumetokana na kuuzwa kwa wingi kwa picha za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kuapishwa.

**Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge Mwaka wa Fedha 2021/22**

**22**. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika Mwaka wa Fedha 2021/22 iliyokuwa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa kutumia kiasi cha **Shilingi 246,384,551,000.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 4,984,770,000** iliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 241,399,781,000** iliidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Aidha, Idara ya Habari - MAELEZO na Taasisi za TBC na TSN zilikuwa zimetengewa bajeti ya jumla ya **Shilingi 23,744,630,000** kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, ambapo **Shilingi 17,743,630,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi **6,001,000,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Bajeti ya Matumizi ya Kawaida**

**23**. ***Mheshimiwa Spika,*** Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 Wizara imepokea na kutumia jumla ya **Shilingi 6,947,838,745.79** sawa na **asilimia 84 ya** fedha zilizotengwa. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa **Shilingi 2,288,345,600.00** ni za Mishahara na **Shilingi 4,659,493,145.79** ni Matumizi Mengineyo.

**Bajeti ya Miradi ya Maendeleo**

**24**. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia **tarehe 30 Aprili, 2022** Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (**Fungu 68**) imepokea jumla ya **Shilingi 129,713,798,179.86** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambayo ni **asilimia 53.7** ya fedha zilizotengwa.

**Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara Eneo la Mawasiliano**

**25**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imetekeleza majukumu yafuatayo:

i) Kujenga Vituo viwili vya Huduma Pamoja katika Mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma ambapo aina ya huduma 12 zinatolewa na taasisi 10;
ii) Kuanza maandalizi ya kuhuisha Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA na mahuisho ya Sera ya Mawasiliano ya Simu ya Mwaka 1997. Hadidu za rejea, mpango kazi na bajeti zimeandaliwa ikiwa ni pamoja na kuanza taratibu za manunuzi ya kumpata mshauri mwelekezi kwa ajili ya kufanya kazi hizi;
iii) Kuendelea kuratibu ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Umoja wa Posta la Afrika (Pan Africa Postal Union – PAPU) jijini Arusha lenye urefu wa ghorofa 18. Ujenzi wa jengo (structural works) umekamilika kwa asilimia 100. Aidha, maendeleo ya kazi za kumalizia jengo kwa

ujumla wake (overall contruction progress) umefikia asilimia **65**;

iv) Kuendeleza mashirikiano ya Kikanda na Kimataifa ambapo Wizara imeshiriki Mkutano Mkuu wa Umoja wa Posta Duniani (UPU) uliofanyika tarehe 9 – 27 Agosti, 2021 Abidjan, Ivory Coast; ambapo chaguzi mbalimbali za viongozi na Mabaraza zilifanyika na Tanzania kufanikiwa kushinda nafasi ya Ujumbe wa Baraza la Utawala (*The Council of Administration* - CA); na Baraza la Uendeshaji la Posta (The Postal Operations Council - POC) kwa kipindi cha miaka minne (2021 - 2025). Sambamba na hilo, Tanzania imepata nafasi ya Kuongoza Kamati ya Huduma za Posta na Biashara Mtandao (Physical Services and E-Commerce) ambayo ni mojawapo ya Kamati zilizo chini ya Baraza la Uendeshaji la Posta (POC) chini ya Umoja wa Posta Duniani. Aidha, kwa upande wa Umoja wa Posta Afrika -PAPU), Tanzania ni mjumbe wa kudumu wa Baraza la Utawala na Tanzania pia imegombea na kupata nafasi ya kuongoza Kamati ya Fedha na Utawala ambayo ni mojawapo ya Kamati zilizo chini ya Umoja wa Posta Afrika – (PAPU). Aidha, Katika kuimarisha masuala haya ya Kikanda na Kimataifa, Wizara imeandaa Mkakati wa kuimarisha ushiriki wa Tanzania Kikanda na Kimataifa katika Sekta ya Mawasiliano ili kujipanga kimkakati na kunufaika zaidi na ushiriki huo. Ushiriki wa nchi katika Mabaraza ya Kikanda na Kimataifa kuna manufaa makubwa kwa nchi ikiwa ni pamoja na kushiriki kupitisha maamuzi mbalimbali yatakayokuwa na maslahi kwa nchi; kupata fursa za miradi inayotangazwa kwa ajili ya nchi zinazoendelea; kupata uzoefu kutoka nchi nyingine namna zinavyotumia teknolojia katika utoaji huduma za posta; na kutoa uzoefu wa nchi katika huduma na miradi inayotekelezwa katika Sekta ya Posta.

v) Kuendelea kuratibu jitihada za ufikishaji wa huduma za mawasiliano ya simu katika maeneo ambayo bado

hayajafikiwa na yenye mawasiliano hafifu. Masuala yaliyofanyika ni pamoja na: ukaguzi wa hali ya mawasiliano katika maeneo mbalimbali ikiwemo eneo la Pori Tengefu

la Loliondo lenye kata 15, visiwa 171 vya Ziwa Victoria, maeneo ya Kanda ya Ziwa, Kanda ya Juu Kusini, Kanda ya Kati na Pwani. Maeneo yaliyobainishwa yatafikishiwa huduma kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. Aidha, zabuni kwa ajili ya kufikisha Mawasiliano katika Shehia 38 ambapo minara 42 itajengwa Zanzibar kwa ajili ya kumaliza changamoto ya Mawasiliano Zanzibar imetolewa. Mradi huu utatekelezwa kwa kutumia ruzuku inayotolewa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), kusaini mikataba kwa ajili ya kufikisha mawasiliano katika kata 85 za maeneo ya mipakani na maeneo maalum Mwezi Februari, 2022. Aidha, katika kuratibu jitihada hizi za ufikishaji wa huduma za mawasiliano, Wizara imeandaa Mkakati wa Kuimarisha Mawasiliano wa kipindi cha miaka minne (2021/22 - 2024/25) ili kuboresha huduma za mawasiliano nchini.

vi) Kuendelea kusimamia utendaji kazi wa taasisi za Sekta zilizopo chini ya Wizara ambazo ni TCRA, TTCL, TPC, UCSAF, ICTC, TBC, TSN na TCRA-CCC. Wizara imekuwa ikipokea taarifa za utendaji za robo mwaka, kuzipitia na kutoa maelekezo. Vilevile, vikao baina ya Wizara na taasisi hizo vimefanyika kwa lengo la kuimarisha utendaji;

vii) Kufanya mapitio ya sekta ndogo ya utangazaji na mfumo wa leseni ili kuweka mazingira wezeshi kwa maendeleo ya sekta. Matokeo ya kazi hii ni kuhuisha Kanuni za Utangazaji kwa njia ya kidijitali na Kanuni za Leseni ambapo pamoja na masuala mengine kupitia marekebisho ya kanuni za leseni, ada za baadhi ya leseni zimepunguzwa ili kuvutia uwekezaji.

viii) Wizara imetoa leseni 25 kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali kupitia Sekta ya Mawasiliano na TEHAMA

nchini. Leseni hizi zitawezesha kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za TEHAMA, kuongeza aina ya huduma zinazotolewa kupitia TEHAMA nchini na pia kuleta ajira kwa wananchi.

**Eneo la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)**

**26**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imetekeleza majukumu yafuatayo:-

i) Kukamilisha uaandaaji wa Mkakati wa Taifa wa intaneti yenye kasi (*National broadband Strategy*);
ii) Kuandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Kushughulikia masuala ya uhalifu wa mtandao unaowezesha uratibu wa pamoja kwa taasisi zote zinazoshughulikia masuala ya uhalifu ya kimtandao. Aidha, kutokana na jitihada zinazofanywa na taasisi hizo na kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Shirika la Mawasiliano Duniani (International Telecommunication Union – ITU) kwenye utafiti wao ujulikanao kama Global Cybersecurity Index (GCI), Tanzania inashika nafasi ya pili (2) barani Afrika na nafasi ya 37 duniani katika masuala ya usalama wa mtandao (cybersecurity);
iii) Kuingia Mkataba wa Mashirikiano na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa ajili ya kufanya kazi pamoja ya kupitisha miundombinu ya mawasiliano kwenye nguzo za umeme kwa lengo la kuongeza mtandao wa mawasiliano na wa umeme. Hatua hii imepunguza gharama za ujenzi wa Mkongo na kuharakisha mradi huu ambapo zilikuwa zijengwe Kilomita **1,880** lakini kutokana na Mkataba huu zitajengwa Kilomita **4,442** na kufikisha jumla ya Kilomita **12,761** za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ujenzi utakapokamilika Mwezi Disemba, 2022; iv) Kuratibu utengenezaji wa Mfumo wa kutunza na kuchakata taarifa za kesi na matukio ya uhalifu wa usalama mtandao "cybercrimes module" inayowezesha

matukio ya uhalifu kutunzwa na kufuatilia mwenendo wa mashtaka husika hadi ukamilifu wake;

v) Kutoa Mafunzo kwa Waendesha Mashtaka, Wachunguzi na Wapelelezi 197 pamoja na mafunzo ya kutumia "cybercrimes module" kwa watumishi 470 wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;

vi) Kukamilisha uandaaji wa rasimu ya Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali (Digital Economy Strategic Framework) kwa ajili ya kuchochea matumizi ya TEHAMA kwenye sekta zote za uchumi;

vii) Kukamilisha uandaaji wa Mwongozo wa Mageuzi ya Kidijitali (Digital Transformation Guideline) kwa ajili ya kutoa mwongozo wa Taasisi zote nchini wa kuelekea uchumi wa kidijitali;

viii) Kukamilisha uandaaji wa Programu ya Mafunzo ya TEHAMA yatakayopelekea kuongeza ujuzi na ubobezi wa wataalamu wa ndani ili kuendana na mahitaji ya sasa ya Uchumi wa Kidijitali kufikia Mapinduzi ya Nne ya Viwanda ($4^{th}$ Industrial Revolution);

ix) Ukamilishwaji wa Mkakati wa Taifa wa Elimu kwa Umma wa Usalama Mtandao (National Cyber Security Communication Strategy), 2021/22 – 2024/25; na

x) Kukamilisha na kuingia Makubaliano ya Ushirikiano kwenye maeneo ya TEHAMA na nchi ya Rwanda yanayojumuisha ushirikiano kwenye kutengeneza Sera za TEHAMA na mikakati ya utekelezaji; ujenzi wa miundombinu ya TEHAMA na utoaji huduma; matumizi ya teknolojia zinazochipukia na kuboresha mazingira ya mfumo mzima wa ubunifu; kukuza vipaji katika TEHAMA, kujenga uwezo na kuboresha mifumo ya taasisi; matumizi ya teknolojia janja (smart technologies); utambuzi wa kidijitali na miundombinu ya Saini Salama za Kielektroniki (Public Key Infrastructure); utengenezaji wa mifumo ya kielektroniki ya kutolea huduma; usalama wa mtandao, ulinzi wa taarifa (privacy), usafirishaji wa taarifa nje ya mipaka ya nchi, na utafiti na maendeleo ya TEHAMA. Aidha, majadiliano na nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia

ya Kongo, Uganda, Kenya, Marekani, Ujerumani, Uturuki na Falme za Kiarabu yanaendelea.

**Eneo la Habari-MAELEZO**

**27**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imetekeleza majukumu yafuatayo:-

i) Kuisemea Serikali kuhusu utekelezaji wa Sera, Mikakati, Miradi na Programu zinazotekelezwa na Serikali kupitia Msemaji Mkuu wa Serikali. Jumla ya taarifa 18 zimetolewa kupitia vyombo vya habari kuhusu utekelezaji wa Serikali sambamba na kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali ikiwemo kujibu hoja na maswali yanayoulizwa na wananchi. Aidha, Msemaji Mkuu wa Serikali alitembelea vyombo vya habari 34 vikiwemo Runinga, Redio, magazeti na mitandao vya kijamii kwa lengo la kutoa ufafanuzi na kuuhabarisha umma kuhusu utekelezaji wa Shughuli za Serikali. Taarifa hizi alizitoa kwa kuzunguka katika mikoa mbalimbali pamoja Jiji la Los Angels nchini Marekani ambapo alitoa taarifa kwa kuongea na Watanzania waishio Marekani na zilirushwa mubashara na vyombo vya habari;

ii) Kuratibu ratiba za Mawaziri na Viongozi kuzungumza kupitia Runinga na pia kukutana na Waandishi wa Habari kuelezea mafanikio na utekelezaji wa Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Wizara zao, katika kuadhimisha kipindi cha Siku 100 na pia mwaka mmoja tangu Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani. Aidha, Wizara iliandaa na kusimamia Kipindi Maalum cha **KAZI IENDELEE** kinachorushwa na Televisheni ya TBC1;

iii) Kuratibu ratiba ya Waheshimiwa Mawaziri kuongea na Waandishi wa Habari kuelezea mafanikio ya Serikali katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara na Sherehe za Mapinduzi ikiwemo Waandishi wa

Habari kutembelea miradi ya mfano ya kila Wizara kuona utekelezaji ili kuhabarisha wananchi kwa ufanisi;

iv) Kuandaa, kuchapisha na kusambaza nakala 5,000 za Jarida la Nchi Yetu lenye kuelezea mafanikio na utekelezaji wa mwaka mmoja wa Serikali ya Awamu ya Sita tangu iingie madarakani tarehe 19 Machi, 2021. Kutokana na mahitaji ya toleo hili kuwa makubwa, Wizara imechapisha nakala nyingine 10,000 na kuzisambaza katika ofisi mbalimbali za Serikali, Sekta binafsi pamoja na kuwapatia wananchi;

v) Kukusanya na kusambaza habari kuhusu utekelezaji wa miradi ya Serikali, ambapo Jumla ya habari 3,411, Makala 37, habari picha 529 katika magazeti, habari 49 katika Runinga, habari 1,600 katika "*blogs*" na mitandao ya kijamii zilichapishwa na kutangazwa;

vi) Kuendelea kuhamasisha Vyombo vya Habari vya Nje ya nchi kuitangaza Tanzania ambapo vyombo vya habari vya nje vikiwemo CCTV, DW, BBC, Voice of Amerika, Xinhua na CGTV vilishiriki katika kuitangaza Tanzania na shughuli za utekelezaji wa Serikali;

vii) Katika kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari; Serikali imetoa jumla ya leseni mpya 19 kwa magazeti hivyo kufanya Jumla ya vyombo vya Habari vilivyosajiliwa kufikia 285. Aidha, Serikali imeyafungulia magazeti manne (4) ya Mseto, Mawio, Tanzania Daima na Mwanahalisi na kuwapatia leseni za kuendelea kufanya kazi katika kuimarisha wigo wa vyombo vya Habari;

viii) Kuhuisha Kanuni za Utangazaji kwa njia ya Kidijitali za Mwaka 2018 ili kuruhusu watoa huduma wanaotoa maudhui ya bila malipo kwa wananchi (Free to Air – FTA) kubebwa katika visimbuzi vya kulipia; na

ix) Kuendelea kuratibu maandalizi ya Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano (National Communication Strategy – NCS).

## Utekelezaji wa Masuala Mengine

**28. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imetekeleza majukumu mengine kama ifuatavyo:

i) Kuhuisha Mpango Mkakati wa Wizara kwa kipindi cha miaka mitano (2021/22 –025/26) kujumuiasha Idara ya Habari-MAELEZO;
ii) Kuhuisha sheria tatu (3) na Kanuni nne (4) za Sekta; sheria zilizohuishwa ni Sheria ya EPOCA ya Mwaka 2010; Sheria ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ya Mwaka 2006; na Sheria ya Posta ya Mwaka 1993. Sheria hizi zimehuishwa ili kuboresha utendaji wa Taasisi husika na mazingira ya huduma za mawasiliano. Kanuni zilizohuishwa ni Kanuni za Leseni za Mwaka 2018; Kanuni za Utangazaji Kidijitali za Mwaka 2018; Kanuni za Maudhui ya Mtandaoni za Mwaka 2020; na Kanuni za Utangazaji Redioni na kwenye Runinga. Marekebisho ya kanuni hizo ni pamoja na; kuruhusu watoa huduma wa maudhui ya bila malipo kwa wananchi (Free to Air - FTA) kubebwa katika visimbuzi vya kulipia; kuondoa leseni katika huduma za maudhui ya mtandao isipokuwa katika eneo la habari na matukio (news and current affairs) kwa lengo la kukuza fursa na vipaji; kuanzisha leseni kwa vituo vya kutunzia kumbukumbu kwa vituo ambavyo tayari vinafanya kazi hadi kanuni zilipoanza kutumika, na; kuondoa zuio kwa matangazo ya kubahatisha (online betting);
iii) Kuratibu na kusimamia uandaaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri za kutunga Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (Personal Data protection) na Sheria ya TEHAMA na kuhuisha Sheria ya Huduma ya Habari. Pia kuendelea kuboresha Kanuni za Usajili wa laini za Simu, Tozo za Muda wa Maongezi wa simu, Kanuni za Masafa na Kanuni za Kushirikiana katika Miundombinu ya Mawasiliano;

iv) Kuajiri Mtumishi mmoja (1), kupandisha vyeo watumishi 46, kufanyika uhamisho wa watumishi 27 kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali. Aidha, Muundo mpya wa Wizara umeandaliwa baada ya kuanzishwa kwa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari;
v) Kuandaa Mpango wa vihatarishi wa Wizara na rejesta ya vihatarishi (risk register) na Mafunzo ya vihatarishi kwa watumishi wote wa Wizara yametolewa;
vi) Bodi za Wakurugenzi wa Taasisi tatu (3) ambazo ni Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Tume ya TEHAMA, na Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) zimeteuliwa; na vii) Usimamizi wa ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Wizara – Mtumba, lenye ghorofa saba ambapo hivi sasa lipo katika hatua ya ghorofa ya kwanza unaendelea.

**Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**29**. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Miradi inayotekelezwa na Wizara ni Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano uliotengewa **Shilingi 171,399,781,000,** Mfumo wa Anwani za Makazi wenye jumla ya **Shilingi 45,000,000,000,** Mradi wa Tanzania ya Kidijitali uliotengewa **Shilingi 25,000,000,000** na Mradi wa Elimu kwa Umma uliotengewa jumla ya **Shilingi 1,000,000,000.**

**Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano**

**30**. ***Mheshimiwa Spika***, Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano umekusudiwa kupanua mawasiliano ya simu na intaneti nchini na nchi zinazotuzunguka katika kufanikisha mapinduzi ya kidijitali. Mradi huu unajumuisha ujenzi wa mkongo wa mawasiliano na vituo vya utoaji huduma. Katika kipindi kinachoishia Mwezi Aprili, 2022 kazi zifuatazo zimefanyika:

(i) Kukamilika kwa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano Kilomita 265 (Itigi – Manyoni - Rungwa);

(ii) Kukamilika kwa Ujenzi wa Kilomita 72 za Mkongo wa kuunganisha Ofisi za Serikali (Kikombo – Mtumba – Msalato);
(iii) Kukamilika kwa Ujenzi wa Kilomita 72 za Mkongo wa Taifa kwenye eneo la Mtambaswala kuunganisha Tanzania na Msumbiji;
(iv) Kukamilika kwa Upembuzi yakinifu (feasibility study, designing and Cost estimates) kuunganisha Mkongo wa Taifa na nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na nyaraka ya zabuni zimeandaliwa. Baada ya kuunganisha nchi ya DRC tutakuwa tumekamilisha maunganisho na nchi zote nane (8) zilizopakana na Tanzania;
(v) Kukamilika kwa kazi ya kukarabati Kilomita 105 za ujenzi wa mkongo Arusha – Namanga kupitia miundombinu ya TANESCO;
(vi) Kukamilika kwa Ujenzi wa Kituo cha Kutolea Huduma za Mkongo wa Taifa kwenye Mji wa Serikali Mtumba;
(vii) Kukamilika kwa taratibu za manunuzi za kuwezesha ujenzi wa **Kilomita 4,442** za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, upanuzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kutoka kiwango cha 200G hadi 800G na kujenga vituo vipya 37 na upanuzi wa vituo 75 vya kutolea huduma za Mkongo ambapo mikataba 22 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 141 imesainiwa. Aidha, utekelezaji huu utafikisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano katika Wilaya 23 nchini. Hii itapelekea ujenzi wa Mkongo kufikia Wilaya 66 kati ya Wilaya 139. Wilaya zitakazojengwa Mkongo wa Taifa ni Karagwe, Uvinza, Chunya, Manyoni, Igunga, Bunda, Bariadi, Mlimba, Namtumbo, Tunduru, Masasi, Ikwiriri - Rufiji, Kilosa, Kongwa, Ruangwa, Kondoa, Korogwe, Bagamoyo, Kibaha, Kasulu, Chato, Urambo na Buhigwe. Wakandarasi wameshaanza kazi za kuchimba mitaro, kusambaza na kusimika nguzo za zege na vifaa vimeshazalishwa tayari kusafirishwa kuja nchini. Aidha, ujenzi kati ya Shinyanga na Kahama umefikia asilimia 40.

(viii) Kukamilika kwa Upanuzi wa Mkongo wa Taifa kwenye vituo 5 vya Kigoma, Arusha, Babati, Tunduma na Mbeya vyenye jumla ya kadi za kuchakata huduma (line processing cards) 30; na
(ix) Kukamilika kwa kazi ya kuhamisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano wenye urefu wa Mita 250 eneo la Mkazi – Katavi kutokana na kujengwa kwenye eneo la makazi ya watu.

***Mradi wa Mfumo wa Anwani za Makazi***

**31**. ***Mheshimiwa Spika,*** Mfumo wa Anwani za Makazi ni Mfumo unaotoa taarifa sahihi ya anapopatikana mwananchi na utambulisho wa matumizi ya eneo husika. Taarifa hizo zinarahisisha utoaji na ufikishaji wa huduma za kiuchumi na kijamii mahali alipo mwananchi sambamba na kuwezesha biashara mtandao (e-Commerce). Kufuatia malengo ya Serikali ya kukamilisha Anwani za Makazi kabla ya Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika Mwezi Agosti, 2022, katika Kikao kazi cha Wakuu wa Mikoa kilichofanyika tarehe 08 Februari, 2022; Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alielekeza Mfumo wa Anwani za Makazi kutekelezwa kwa Mfumo wa Operesheni, aliyoipa jina la "**OPERESHENI ANWANI ZA MAKAZI**". Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea na utekelezaji wa Mradi chini uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Katika Mwaka wa Fedha 2021/22 shughuli nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na:

i) Kuunda Programu Tumizi (Mobile application) ya Mfumo iliyoongeza ufanisi katika matumizi na utekelezaji wa Mfumo. Programu Tumizi imetumika katika kukusanya taarifa za barabara/ mitaa/ njia, makazi na wakazi sambamba na kumuongoza mtu kutoka anwani ya makazi moja kwenda anwani ya makazi nyingine;
ii) Semina ya kuwajengea uelewa kuhusu Mfumo wa Anwani za Makazi imetolewa kwa Viongozi 483 ambao

ni Wakuu wa Mikoa; Katibu Tawala wa Mikoa; Wenyeviti na Wakurugenzi wa Halmashauri; na Wajumbe wa ALAT;

iii) Wataalam 616 wa Mikoa na Halmashauri wamejengewa uwezo kuhusu namna bora ya kutekeleza Mfumo wa Anwani za Makazi ili wasimamie ipasavyo katika maeneo yao;

iv) Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 jumla ya anwani za makazi 12,171,320 zimekusanywa na kuingizwa kwenye Programu Tumizi. Idadi ya Anwani zilizokusanywa ni asilimia 104.3 ya lengo la jumla ya Anwani 11,676,891 zilizopangwa kukusanywa katika Mikoa yote nchini. Matumizi ya programu tumizi yamewezesha kubaini maeneo mengineyo yaliyokuwa hayajabainishwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Mradi wa Tanzania ya Kidijitali**

**32**. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ilifanikisha kusainiwa kwa Mkataba kati ya Serikali na Benki ya Dunia wenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 150 na ulisainiwa rasmi tarehe **19 Agosti, 2021** na Mradi kuanza rasmi kutekelezwa Mwezi **Novemba, 2021**. Mradi huu unalenga kuboresha na kukuza maunganisho ya ndani na ya kimataifa ili kuweza kufikisha huduma za mawasiliano pamoja na utoaji wa huduma mbalimbali za Serikali kwa Wananchi. Vilevile, mradi huu unalenga kuboresha ubunifu pamoja na kuwajengea uwezo wataalam wa TEHAMA nchini. Kazi zilizotekelezwa ni:-

i) Ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mradi katika eneo la Area D na kuanza kutumika rasmi tarehe **01 Oktoba, 2021;**

ii) Kukamilisha usanifu na kuandaa mahitaji ya kuwezesha ununuzi wa bando la intaneti ya Serikali (Government internet bandwidth) kwa ajili ya matumizi ya Taasisi za Umma;

iii) Kukamilisha usanifu na kuandaa mahitaji kuwezesha kujenga na kuboresha Mtandao wa TEHAMA unaounganisha Taasisi za Serikali (GovNET);
iv) Kukamilisha mpango wa kuelimisha umma kuhusu shughuli za mradi;
v) Kukamilisha ukusanyaji wa mahitaji kuwezesha kujenga na kupandisha hadhi minara 150 ya mawasiliano kutoka teknolojia ya 2G kwenda 3G/4G ili kuwezesha huduma za intaneti yenye kasi kwenye maeneo hayo;
vi) Kukamilisha manunuzi ya vifaa na programu endeshi za kuboresha vituo mahiri vya kuhifadhia Data (National Internet Data Centre - NIDC na Government Data Centre);
vii) Kufanya tathmini ya maeneo ya kujengewa uwezo kwa watumishi wa TEHAMA Serikalini ambapo jumla ya watumishi **450** watapatiwa mafunzo ya muda mfupi na watumishi **50** watapatiwa mafunzo ya muda mrefu; na
viii) Kufanya maandalizi ya kuwezesha ujenzi wa Chuo cha TEHAMA ambapo eneo lenye ukubwa wa Hekta **400** limepatikana eneo la Nala, Jijini Dodoma.

**Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Taasisi zilizo chini ya Wizara zilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 453,092,090,266.** Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 Taasisi zimekusanya jumla ya **Shilingi 326,477,155,532.89** sawa na **asilimia 68.8** ya lengo.

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa kila Taasisi ni kama ifuatavyo:-

**Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)**

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Mamlaka ilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 150,067,415,286.65.** Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 Mamlaka ilifanikiwa kukusanya **Shilingi 141,887,325,293**

sawa na asilimia 95 ya makadirio ya mwaka. Vyanzo vya mapato ya Mamlaka ni pamoja na ada za leseni, ada za matumizi ya masafa, mrabaha (asilimia moja ya pato ghafi la watoa huduma za mawasiliano), ada za usimikaji na ukarabati wa mitambo ya mawasiliano, ada za uingizaji na usambazaji wa vifaa vya TEHAMA na makusanyo kutokana na mtambo wa *Teletraffic Management System (TTMS)*.

**36.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kusimamia Mfumo wa *Teletraffic Management System (TTMS)* wenye uwezo wa kubaini takwimu mbalimbali zinazopita katika mitandao ya mawasiliano nchini. Mfumo huu unaiwezesha Serikali kupata mapato stahiki kutokana na huduma za mawasiliano.

**37.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022, Wizara kupitia Mamlaka kupitia mfumo wa TTMS imefanya yafuatayo:-

i) Kutambua mapato na takwimu za miamala ya fedha mtandao, ambapo jumla ya miamala **3,261,152,614** ilifanyika kupitia mitandao ya simu na kiasi cha **Shilingi 162,841,588,091,516** kilipita kwenye miamala ya simu katika kipindi hicho; ii) Kuzuia mianya ya upotevu wa mapato yanayotokana na mawasiliano ya simu za kimataifa zinazoingia hapa nchini ambapo jumla ya simu za ulaghai zipatazo **920** zilibainika. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilifanya kaguzi tatu **(3)** kwenye mikoa ya Arusha, Kagera na Morogoro na kuwezesha kukamata vifaa viwili (2) vya uchepushaji wa mawasiliano ya simu za kimataifa na kukamata watuhumiwa nane (8) waliokuwa wakijihusisha na uchepushaji huo. Watuhumiwa wote walifikishwa kwenye vyombo vya sheria na kesi zao zinaendelea kusikilizwa mahakamani; na

ii) Mfumo wa TTMS umewezesha Serikali kupata mapato yanayotokana na mawasiliano ya simu za kimataifa

zinazoingia na kuishia hapa nchini ambapo kiasi cha **Shilingi 7,962,091,841.56** kilikusanywa.

**38.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kuendesha na kuboresha kanzidata ya usajili wa laini za simu kwa njia ya kibiometria. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 laini zote za simu **55,365,239** zimesajiliwa kwa alama za vidole sawa na asilimia **100** ya laini zote zinazotumika.

**39.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kukabiliana na changamoto za ukuaji wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) hapa nchini. Mamlaka kwa kutumia *National Computer Emergency Response Team* (TZ-CERT) imeendelea kukabiliana na majanga yatokanayo na Kompyuta na mifumo ya Mawasiliano. Katika kipindi cha Mwezi Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 Serikali kupitia TCRA imetekeleza majukumu yafuatayo: -

i) Kufanya tathmini na uchambuzi wa vihatarishi vya usalama katika mtandao na mifumo ya kompyuta kwa lengo la kubaini mapungufu yaliyopo dhidi ya mashambulio ya mtandao (cyber-attacks) ambapo tahadhari za usalama (security alert) **875** na mashauri ya usalama mtandaoni (security advisories) **726** yalitolewa ili hatua stahiki ziweze kuchukulia kuimarisha usalama wa mtandao na mifumo; na
ii) Kutoa mafunzo kwa washiriki **83** wa taasisi mbalimbali juu ya utayari wa kuitikia matukio ya usalama wa mifumo na miundombinu (Cybersecurity Incident Response Training*)*.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea na jukumu la kukagua na kuhakiki ubora wa viwango wa vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki hapa nchini kwa lengo la kulinda usalama na afya za wananchi. Katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 jumla ya maombi **505** yamepokelewa

kwa ajili ya uhakiki wa ubora na usalama wa matumizi ya vifaa vya kielektroniki. Kati ya hayo, maombi **431** yamekaguliwa na kukidhi vigezo vya ubora na usalama kwa matumizi, maombi **60** yako kwenye hatua za mwisho za ukaguzi na maombi 10 yamekataliwa.

**41.** ***Mheshimiwa Spika*,** Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano imeendelea kuhakikisha uwepo wa rasilimali zinazowezesha mawasiliano ya simu, intaneti, redio na runinga. Rasilimali hizi ni pamoja na masafa, namba na vikoa (domain names). Usimamizi mzuri wa rasilimali hizi umewezesha kuhakikisha kuwa hakuna mwingiliano katika huduma na kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa zinakidhi viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa. Usimamizi wa rasilimali hizi umetokana na:

i) Uwepo wa nyenzo za kisasa pamoja na Sera, Sheria na Kanuni zinazoendana na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya nchi hivyo kuwezesha upangaji mzuri wa rasilimali za mawasiliano; na

ii) Upangaji na usimamizi mzuri wa rasilimali za mawasiliano (masafa na namba), umewezesha upatikanaji wa huduma za mawasiliano pamoja na huduma za pesa mtandao. Mamlaka ya Mawasiliano hupanga na kutoa namba zinazotumika katika mawasiliano pamoja na namba fupi (short codes) zinazotumika katika kufanya miamala ya kifedha na zinazotumika kwenye maisha na usalama wa raia mfano 112 - kwa ajili ya Polisi, 114 - Zima moto n.k.

    Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeweka utaratibu na kutenga rasilimali maalum ambazo watapewa bure vijana wanaojishughulisha na ubunifu katika TEHAMA ili waweze kufanya majaribio ya vumbuzi zao wakishirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia.

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kuhimiza matumizi ya kikoa cha kitaifa cha *dot tz* (*country code Top Level Domain*

- *cc-TLD*) ambacho ni rasilimali muhimu ya Taifa kwenye mawasiliano ya intaneti kama ilivyo namba +255 kwenye Mawasiliano ya simu. Mamlaka ya Mawasiliano inapanga na kuratibu matumizi ya kikoa hiki nchini kwa ajili ya kutumika kwenye anwani za kielektroniki kwenye mawasiliano ya intaneti mfano tovuti au barua pepe. Anwani zenye kikoa cha kitaifa zinasaidia:-

i) Kutoa utambulisho wa Tanzania kwenye mtandao (*cyber space*);
ii) Kuongeza uhakika na usalama kwenye matumizi ya mtandao;
iii) Masuala ya kibiashara ya kikoa cha kitaifa yanatatuliwa na sheria zetu tofauti na vikoa vingine kama "*dot com*"; na
iv) Kupatikana kirahisi kwenye *search engines* kama *Google*.

Aidha, kuanzia tarehe 1 Machi, 2022, Mamlaka ya Mawasiliano imeanza usajili wa vikoa vya ngazi ya pili (Second level Domain names) ili kuendana na mahitaji ya kiteknolojia na pia kuruhusu taasisi na kampuni mbalimbali za Kitanzania kuwa na vikoa vifupi. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 jumla vikoa vya kati 293 vimesajiliwa.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2021 matumizi ya anwani za kikoa cha kitaifa (dot tz) yameongezeka na hivyo kufanya jumla ya anwani za kikoa kuongezeka kutoka **22,184** Mwezi Julai, **2021** na kufikia anwani za kikoa **23,820** Mwezi Aprili, 2022 sawa na ongezeko la **asilimia saba (7).**

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kushirikiana na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA-CCC) kwa kutoa elimu juu ya sheria, haki na wajibu wa mtumiaji, uhakiki wa usajili wa laini za simu za mkononi, wajibu wa mtumiaji katika masuala ya tahadhari dhidi ya

uhalifu kupitia mtandao na kufanikisha ufumbuzi wa malalamiko kati ya watumiaji na watoa huduma za Mawasiliano.

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka imeweka utaratibu mahsusi wa kushughulikia malalamiko kati ya watumiaji na watoa huduma. Vilevile, mamlaka ya Mawasiliano inaendelea kutoa elimu juu ya wajibu na haki za watumiaji na watoa huduma za mawasiliano. Kuanzia Mwezi Julai, 2021 hadi kufikia Mwezi Aprili, 2022, Mamlaka ilikuwa imepokea na kushughulikia jumla ya malalamiko 3,033 ambapo malalamiko 2,996 sawa na asilimia 98.8 yameshughulikiwa na kupatiwa ufumbuzi na malalamiko 37 sawa na asilimia 1.22 yako kwenye hatua ya utatuzi.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kusimamia Sheria na kuboresha mfumo wa utoaji leseni unaowezeshwa kwa njia ya mtandao. Katika kipindi cha kuanzia tarehe 1 Julai, 2021 hadi 30 Aprili, 2022 jumla ya Leseni **657** zimetolewa. Leseni ambazo zimetolewa zinajumuisha leseni za maudhui ya redio 51, leseni za maudhui ya televisheni 13, leseni ndogo za madaraja mbalimbali (Class Licences) 558, leseni za Huduma za Mawasiliano (Application Service Licences) 31 na Leseni za Miundombinu ya Mawasiliano (Network Facilities Licences) 4.

**47.** ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2021 hadi Aprili, 2022, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kufanya kazi ya ukaguzi wa matumizi ya rasilimali masafa ili kuhakikisha kuwa yanatumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Zoezi hili linafanyika kuhakikisha watoa huduma wa mawasiliano wamezingatia matumizi ya masafa ya mawasiliano (Radio frequency Spectrum) kulingana na leseni walizopewa. Hili linafanyika kulingana na upangaji masafa wa Shirika la Umoja wa Mawasiliano ya Simu Duniani (International Telecommunications Union - ITU).

**48.** ***Mheshimiwa Spika****,* Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inaendelea kufanya tathmini ya gharama za huduma za mawasiliano pamoja na kuwashirikisha wadau muhimu ili iweze kuchukua hatua stahiki zinazolenga kuhakikisha kuwa mahitaji ya wadau wa pande zote (Serikali, watoa huduma na watumiaji wa huduma) yanafikiwa kupitia huduma husika.

**Miradi ya Maendeleo Iliyotekelezwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) (a) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Pan African Postal Union (PAPU House)**

**49**. ***Mheshimiwa Spika****,* Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inaendelea na ujenzi wa Jengo la Umoja wa Posta Afrika (Pan African Postal Union - PAPU House) jijini Arusha lenye ghorofa 18. Ujenzi huu unagharimu **Shilingi 39,706,626,131.05.** Mradi huu unatekelezwa kwa ubia kati ya Serikali ya Tanzania (**asilimia 40**) na Umoja wa Posta Afrika (**asilimia 60**). Jengo hili litatumika kama Makao Makuu ya Umoja wa Posta la Afrika na Ofisi za Kanda ya Kaskazini za Mamlaka ya Mawasiliano. Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2022, ujenzi huu umefikia **asilimia 65.**

**(b) Mradi wa Muundombinu wa Kitaifa wa Saini za Kieletroniki (National Public Key Infrastratucture)**

**50**. ***Mheshimiwa Spika****,* Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inaendelea na mradi wa Muundombinu wa Kitaifa wa Saini za Kielektroniki (National Public Key Infrastratucture). Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2022 mchakato wa kupata wazabuni mwenye sifa na uzoefu wa kusimika mifumo ya aina hii katika hatua ya *Pre-qualification* umekwisha kamilika. Hatua zinazofuata ni kuzialika kampuni hizi katika mchakato wa manunuzi. Mradi huu utakapokamilika utaongeza usalama wa mifumo na miamala ya kielektroniki dhidi ya matishio ya usalama mtandaoni.

**(c) Maabara ya Ukaguzi wa Vifaa vya Mawasiliano (Type Approval Laboratory)**

**51**. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inaendelea na mradi wa ujenzi wa Maabara za kupima ubora wa vifaa vya mawasiliano; hadi kufikia Mwezi Aprili, 2022 hatua ya kupata wazabuni wenye sifa na vifaa vya maabara umeanza. Mradi huu unajumuisha maabara nne (4) zenye kupima masafa ya kifaa (radio frequency), unyonyaji wa mionzi ya simu (Specific absorption rate), kupima vifaa vya utangazaji (broadcasting equipment) na mionzi ya sumakuumeme (Electromagnetic Field - EMF). Mradi huu utakapokamilika utaongeza usalama kwa watumiaji wa huduma za mawasiliano kwa kutumia vifaa bora na kuboresha huduma za mawasiliano.

**(d) Mradi wa vifaa vya TEHAMA Mashuleni**

**52**. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kutekeleza mradi wa kufadhili vifaa vya TEHAMA mashuleni ili kuwezesha Wanafunzi na Walimu kutumia mifumo ya TEHAMA kupata taarifa za masomo kwenye tovuti mbalimbali duniani. Kwa Mwaka wa Fedha 2021/22, Serikali kupitia TCRA imekamilisha taratibu za manunuzi ili kufikisha vifaa vya TEHAMA kwenye shule mbili (2) za Sekondari za wasichana na moja ya mchanganyiko zilizopo katika mikoa ya Pwani, Lindi, na Pemba. Vifaa hivyo ni Kompyuta 30, ambazo zitagawiwa kwa uwiano wa kompyuta 10 kila shule, Mashine ya kudurufu moja kwa kila shule, vitunza umeme (UPS) 10 kwa kila shule na kuunganisha shule zote na mfumo wa intaneti. Shule hizo ni Sekondari ya Makoongwe (Pemba), Sekondari ya Wasichana Kibaha (Pwani) na Sekondari ya wasichana Ilulu (Lindi).

**(e) Mradi wa kutoa Elimu kwa Umma**

**53**. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kutekeleza mradi wa

kuelimisha wananchi masuala yanayohusiana na Sekta ya Mawasiliano kupitia vipindi vya redio, runinga na mitandao. Katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 TCRA imerusha vipindi **526** vya Elimu kwa Umma kupitia redio, runinga na mitandao na kuwafikia takriban watu **30,141,597.**

**Shirika la Posta Tanzania (TPC)**

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 Shirika la Posta Tanzania lilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 40,761,234,400.** Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 Shirika lilizalisha jumla ya Shilingi **25,648,180,486** sawa na asilimia **63** ya lengo kutoka katika vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni usafirishaji wa barua na vipeto, Usafirishaji wa nyaraka kwa njia ya haraka (EMS), fedha na uwakala, biashara mtandao, pamoja na miliki. Aidha, kutofikiwa kwa malengo ya mapato ni kutokana na athari za mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO ambao ulipelekea kusitishwa kwa safari za ndege kwa baadhi ya nchi. Sababu nyingine ni zuio maalumu (Embago) la Mwezi Novemba, 2021 lililositisha kupeleka mizigo Marekani na Japan.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Shirika lilipanga kuzalisha faida kabla ya kodi ya **Shilingi 3,029,269,206.** Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2022 Shirika limefanikiwa kuzalisha faida kabla ya kodi **Shilingi2,661,477,261** ikiwa ni **asilimia 88** ya lengo.

**56.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 Shirika limefanikiwa kutengeneza Ramani ya Kidijitali (Postal Digital Map) ili kuimarisha usambazaji wa barua, vifurushi na vipeto pamoja na usafirishaji wa sampuli za maabara. Ramani hii inaendelea kufanyiwa maboresho ikiwemo kuunganishwa na Mfumo wa Anwani za Makazi kabla ya utekelezaji wake.

**57.** ***Mheshimiwa Spika***, katika uboreshaji wa utoaji wa huduma Shirika limefanikiwa kufanya usimikaji na kuanza utekelezaji wa matumizi ya Mfumo wa Ofisi Mtandao (e-Office) ambapo shughuli zote za kiutendaji kwa ngazi za makao makuu na mikoa zinatumia mfumo wa e-office sambamba na mfumo wa ulipaji (MUSE) ambao umeunganishwa katika mikoa yote.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limekamilisha ukarabati wa majengo makuu mawili ya ofisi za Posta Kuu Mwanza na Tanga ili kuboresha muonekano wa majengo na kuongeza mvuto wa kibiashara.

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeunganisha Mfumo wa Ukusanyaji Mapato wa Posta (Posta Revenue Collection System) na mfumo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kuwezesha kutumia vifaa vya kielektroniki vya kufanyia mauzo (Point of Sale - POS) katika maeneo ya kutolea huduma za Posta pamoja na mfumo wake wenyewe wa kusimamia uendeshaji wa maduka ya kununua na kuuza fedha za kigeni (Posta Bureau De Change System). Mfumo huu umeunganishwa na mifumo ya Benki Kuu kwa lengo la kufuatilia miamala yote ya ununuzi na uuzwaji wa fedha za kigeni kupitia maduka haya.

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea kutoa huduma za Posta Mlangoni katika maeneo yenye miundombinu ya Anwani za Makazi katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Kilimanjaro, Morogoro, Mwanza, Shinyanga, Geita, Pwani pamoja na Zanzibar. Shirika pia linatoa huduma ya Posta Mlangoni kwa mahakama zote za Tanzania Bara.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuwasogezea wananchi huduma, Shirika limefanya maboresho ya mfumo wa kutolea huduma ya Posta Kiganjani na kutengeneza programu tumizi ya androidi (Android mobile application) ambayo inafanyiwa mapitio ya kiufundi kabla ya kuanza kutumika.

Aidha, programu hii ina uwezo wa kutoa huduma za masanduku, kubadilisha anwani, kufuatilia mwenendo wa barua, vifurushi na vipeto, kufuatilia Ankara zinazolipwa, ukusanyaji na usambazaji wa barua, vifurushi na vipeto, utumaji wa pesa kutoka ofisi moja kwenda nyingine (posta cash app) na huduma nyinginezo za Shirika.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea kusimamia na kuendesha vituo vya Huduma Pamoja kupitia mradi wa Tanzania ya kidijitali. Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2022 vituo viwili vimeanza kutoa huduma ambapo jumla ya wananchi 22,506 wamepata huduma katika vituo hivi katika Mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma kwa kutoa huduma zifuatazo;

a) Cheti cha kuzaliwa - RITA;
b) Hati ya kusafiria (Passsport) - Uhamiaji;
c) Kitambulisho cha Taifa - NIDA;
d) Usajili wa Kampuni za Biashara - BRELA;
e) Namba ya Mlipa Kodi (TIN) - TRA;
f) Leseni za Biashara za Halmashauri - Halmashauri ya Ilala, Kigamboni, Kinondoni na Temeke;
g) Bima ya Afya - NHIF;
h) Taarifa za Pensheni ya Uzeeni – PSSSF na NSSF; na
i) Taarifa za Upotevu wa Mali – Jeshi la Polisi Tanzania.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kutekeleza Operesheni Anwani za Makazi kama ilivyoelekezwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Shirika la Posta Tanzania limefanikiwa kutengeneza na kusimika vibao vya anwani za makazi katika ofisi 50 za Shirika la Posta Tanzania nchini.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuboresha mahusiano ya Kitaifa na Kimataifa katika utoaji wa huduma za Posta, Shirika la Posta Tanzania limefanikiwa kupata fursa ya kuwa Mwenyekiti Mwenza wa kuongoza kamati muhimu ya Baraza la Uendeshaji katika Kamati ya Huduma za Posta na Biashara Mtandao (Physical Services and e-Commerce

Committee). Aidha, kama Mwenyekiti mwenza wa Kamati hiyo Tanzania inanufaika katika nyanja mbalimbali kama ifuatavyo:-

i) Kuingia kwenye Menejimenti ya Baraza la Uendeshaji la Umoja wa Posta Duniani kunaifanya Tanzania kuwa kwenye maamuzi yote yatakayopitishwa au yanayoweza kupitishwa yenye maslahi ya nchi kama vile miradi mbalimbali inayotekelezwa na Umoja wa Posta Duniani kupitia programu mbalimbali.
ii) Tanzania imechaguliwa kuingia kwenye Kamati maalumu ya Mfuko wa Kuendeleza huduma za Posta wa nchi zinazoendelea *(Quality of Service Special Fund for LDCs);* hii itasaidia nchi kupata nafasi katika miradi inayoenda kutekelezwa kwenye nchi zinazoendelea; na
iii) Kuongoza vikao na mijadala mbalimbali inayoweka mustakabali wa nchi kwenye mada zenye maslahi kwa nchi hasa za utendaji na uboreshaji huduma.

**65. *Mheshimiwa Spika,*** Katika jitihada za kuboresha na kuimarisha ulinzi na usalama wa mizigo na mali za wateja, Shirika la Posta Tanzania limeimarisha miundombinu ya ulinzi na usalama wa mali za wateja zinazosafirishwa kwa njia ya Posta kwa kusimika mitambo mipya mitatu (3) ya kukagua mizigo (baggage Scanners) katika Ofisi Kuu ya Posta Dar es Salaam na kusimika kamera za usalama 44 (CCTV Camera) katika ofisi za Shangani na Kijangwani Zanzibar.

**66. *Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kuboresha huduma kwa kutumia teknolojia za kisasa, Shirika la Posta Tanzania limefanikiwa kuzindua jukwaa la kuuza na kununua bidhaa kwa njia ya mtandao *(*e-shop platform) ambapo jumla ya maduka 800 yamesajiliwa kwa ajili ya kuuza na kununua bidhaa mbalimbali ndani na nje ya Tanzania. Jukwaa hilo linapatikana kwa njia ya mtandao kupitia tovuti zifuatazo https://www.postashoptz.post na https://stamps.tz.post.

**Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL)**

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Shirika lilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 232,388,423,127.57**. Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2022 Shirika limefanikiwa kukusanya **Shilingi 112,096,049,434.15** sawa na asilimia 48.2 ya makadirio ya mwaka kutokana na huduma za Shirika ambazo ni simu, data na kupangisha maeneo kwa ajili ya vyombo vya mawasiliano.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limefanya upanuzi na uboreshaji wa Mifumo ya Mtandao Mhimili (Core Network Systems), Usafirishaji wa Data (Transmission/Transport Networks) na mawasiliano ya Simu za Mkononi (Radio Access Network). Hatua hii imewezesha Shirika kuongeza uwezo wake katika kutoa huduma.

**69.** ***Mheshimiwa Spika***, Shirika limefanikiwa kuongeza wateja kutoka wateja **1,300,295** Mwezi Julai, 2021 hadi kufikia wateja 2,033,2451 Mwezi Aprili, 2022 ikiwa ni ongezeko la wateja **732,950** sawa na asilimia 56. Ongezeko hili ni sawa pia na asilimia 96 ya lengo na hivyo kulifanya Shirika kumiliki asilimia 3.4 ya soko la mawasiliano. Aidha, Shirika linatarajia kufikisha wateja 2,114,051 ifikapo Mwezi Juni, 2022.

**70.** ***Mheshimiwa Spika***, Shirika limeendelea kuimarisha mkakati wa uuzaji na usambazaji wa muda wa maongezi. Sambamba na maduka yaliyopo katika ofisi za Shirika la Mawasiliano nchi nzima, Shirika limeendelea kuboresha upatikanaji wa muda wa maongezi kwa:-

i) Kuongeza idadi ya wasambazaji wa vocha kutoka 6,836 Mwezi Julai, 2021 hadi kufikia wasambazaji 7,512 Mwezi Aprili, 2022 sawa na ongezeko la asilimia 10;
ii) Kuwaelimisha na kuwaunganisha wateja wake na huduma ya T-PESA ili waweze kununua muda wa

maongezi kwa njia ya kielektroniki kupitia T-PESA na benki pindi wanapohitaji kununua muda wa maongezi bila kufika ofisi za Shirika au Wakala; na

iii) Shirika limeingia makubaliano na Shirika la Posta kwa ajili ya kutoa huduma za uwakala mkuu wa T-PESA, usambazaji wa vocha na usajili wa wateja wapya wa TTCL. Hivyo, huduma za TTCL zinapatikana kila palipo na ofisi za Shirika la Posta Tanzania.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika linaendelea kufanya maboresho ili kuhakikisha huduma inazotoa zinakidhi viwango kwa kuboresha mitambo na kuongeza vituo vya huduma kwa wateja. Kwa upande wa huduma kwa wateja maboresho haya ni kama ifuatavyo: kuhakikisha kituo cha huduma kwa wateja (call centre) kinakuwa thabiti na kupatikana ndani ya muda wote; T-PESA imeanzisha namba maalum ya kupiga simu bure (**0800 110095)** kwa ajili ya kuwahudumia Mawakala wake ili kupunguza msongamano na kuchelewesha kupata huduma kwa wakati; kuongeza vituo vya huduma kwa wateja (customer service centres) katika Mikoa na Wilaya ili kuhakikisha huduma zinawafikia wananchi kote nchini kwa ukaribu zaidi.

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea kutoa huduma ya T-HAKIKI inayowezesha kuthibitisha ubora wa mbegu na viuatilifu. Huduma hii inalenga kuwasaidia wakulima kubaini mbegu na viuatilifu visivyokidhi viwango au vilivyopitwa na muda wa matumizi. Huduma hii inatolewa bure na inatumiwa na wakulima, taasisi za udhibiti ubora wa pembejeo za kilimo na wauzaji wa mbegu na kemikali za kilimo. Hivyo, watumiaji wote wa simu za mkononi waliosajiliwa nchini wanaweza kuhakiki ubora wa pembejeo kupitia namba ***148*52#**. Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2022 huduma hii imeweza kufikia watumiaji **41,665** kutoka watumiaji **12,291** Mwezi Julai, 2021 sawa na

ongezeko la asilimia 239. Shirika linaendelea kutoa elimu kwa wananchi ya namna ya kutumia huduma hii.

**73.** ***Mheshimiwa Spika***, Shirika limeendelea kusimamia na kuendesha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano likiwa na vituo **27** vinavyotoa huduma za matengenezo ya kiufundi kupitia kwa wataalam wa Shirika pamoja na vituo **44** vinavyounganisha huduma za wateja waliopo ndani na nje ya nchi sita (6) za Rwanda, Burundi, Malawi, Zambia, Kenya na Uganda kupitia vituo vilivyojengwa mipakani.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea kuendesha Kampuni Tanzu ya TTCL Pesa (T-PESA) ambapo watumiaji wa huduma za T-PESA wameongezeka kutoka wateja **948,446** Mwezi Julai, 2021 hadi kufikia wateja **1,439,2831** Mwezi Aprili, 2022 sawa na ongezeko la asilimia **52.** Kwa upande wa mawakala ambao wanafanya miamala, wameongezeka kutoka mawakala **3,200** walio hai kwa kipindi cha siku 90 zilizopita Mwezi Julai, 2021 hadi kufikia mawakala **6,764** Mwezi Aprili, 2022. Wateja na mawakala hawa wamekamilisha taratibu zote za kiusajili kwa mujibu wa Sheria. Aidha, T-PESA imeunganishwa kwenye Mfumo wa Malipo wa Serikali (GePG), mifumo ya ki-benki ya CRDB, NMB, NBC, Azania, Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) na watoa huduma za mawasiliano wengineo ili kumwezesha mteja kufanya malipo mbalimbali kupitia T-PESA.

**Kituo cha Data cha Taifa (*National Internet Data Centre - NIDC*)**

**75.** ***Mheshimiwa Spika***, Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data Kimtandao (NIDC) kilianzishwa Mwaka 2015 ikiwa ni sehemu ya mradi wa Mkongo wa Taifa na kina hadhi ya daraja la tatu (tier 3) kwenye viwango vya kimataifa. Huduma zinazotolewa na Kituo ni upangishaji wa vifaa (collocation), upangishaji wa nafasi kwenye mashine (virtual servers), upangishaji wa mashine kubwa (dedicated servers), kutunza

data kwa matumizi ya baadae (storage and backups), kutengeneza mifumo na huduma za kuweka tovuti za wateja ili zipatikane kwenye wavuti ulimwengu (web hosting). Aidha, NIDC inatarajia kuanzisha huduma mpya ya *Cloud Computing* ambayo ina uwezo wa kuhudumia wateja wengi kwa kutumia rasilimali chache na kwa gharama nafuu. Huduma za *Cloud Computing* ni ufumbuzi bora wa matumizi mazuri ya miundombinu ya Kituo kwani hutumia nafasi ndogo kwa matokeo makubwa.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo kimefanikiwa kuunganisha wateja **209** ambao kinaendelea kuwahudumia toka kuanzishwa kwake, kati ya hao wateja **106** ni Taasisi na Idara za Serikali na wateja **103** ni taasisi au kampuni binafsi. Katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 **Shilingi 3,803,340,531.983** zimekusanywa kupitia huduma zitolewazo na Kituo. Hii ni asilimia 107.4 ya lengo la kukusanya **Shilingi 3,542,959,084.36** hadi kufikia Mwezi Juni, 2022.

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data (NIDC) kwa kushirikiana na T-PESA kimeanzisha kadi ya malipo maalum ijulikanayo kama N-CARD inayotumiwa na wateja waliosajiliwa na mitandao yote ya simu ili kuwawezesha watumiaji kulipia bidhaa na huduma mbalimbali. Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2022 mfumo wa N-CARD una jumla ya wateja **1,500,000** wanaotumia N-CARD kuingia viwanja vya mpira wa miguu na kwenye maonesho ya biashara, kulipia nauli za vivuko na huduma za uanachama wa klabu ya mpira Yanga.

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kimetengeneza mfumo wa ukataji tiketi za mabasi kwa njia ya kielektroniki (Tiketi Mtandao). Mfumo huu unamwezesha abiria kukata tiketi ya kielektroniki pasipo kulazimika kwenda kwenye vituo vya mabasi. Abiria kwa kutumia programu

tumizi (Mobile Application) inayopatikana katika simu janja (smart phone) ataweza kukata tiketi na kulipia kwa kutumia njia za pesa mtandao zilizopo. Aidha, tiketi zitaweza kukatwa kupitia mawakala wa mabenki na makampuni ya simu waliosambaa kote nchini kwani mfumo umeunganishwa na mifumo ya mauzo ya makampuni ya simu na mabenki.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfumo wa Tiketi Mtandao umeunganishwa na Mfumo wa kusimamia Risiti za Kielektroniki (EFDMS) wa TRA pamoja na mifumo shirikishi ya watoa huduma (vendors). Mfumo *umeanza* kufanyiwa majaribio tangu tarehe 01 Aprili, 2022 ambapo katika kipindi hiki wamiliki wa mabasi wana fursa ya kujiunga kwenye mifumo ya watoa huduma za tiketi ikiwa ni pamoja na kufanya usajili wa mabasi yao kwenye mfumo mkuu wa Tiketi Mtandao. Matokeo mazuri ya majaribio yatapelekea mfumo huu kuanza rasmi kutumika ifikapo tarehe 01 Julai, 2022 na hivyo kuwawezesha abiria kupata huduma ya tiketi wakiwa mahali popote ikiwa ni pamoja na kuwezesha urasimishaji wa ajira za madereva na watendaji wengine wa mabasi.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha Taifa Kuhifadhi Data (NIDC) kimekuwa kikiendelea kufanya maboresho na usimamizi wa mfumo wa ukusanyaji kodi kwa njia ya kielektroniki ujulikanao kama *Electronic Revenue Collection System* (e-RCS). Mfumo huu unakusanya kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na Ushuru wa Bidhaa (Excise Duty) kutoka kwenye miamala inayofanywa kupitia Kampuni za simu Nchini. Mfumo wa e-RCS umekuwa ni msaada mkubwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kwani umeondoa ile dhana ya mfanyabiashara kujifanyia makadirio ya kiwango cha kulipa kodi (Self Assessment) katika eneo la ulipaji kodi.

**Miradi ya Maendeleo Iliyotekelezwa na Shirika la Mawasiliano Tanzania**

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limekamilisha usimikaji wa mfumo mpya wa Ankara (Billing System), na uanzishwaji wa *self-care portal* mpya inayowezesha wateja kujihudumia, na kukamilika kwa maunganisho (integration) kati ya mfumo wa ankara na mfumo wa malipo ya Serikali GePG. Maunganisho haya yameanza kufanyika kuanzia Mwezi Julai 2021. Pia, Shirika limekamilisha uboreshwaji (optimization) wa miundombinu ya 4G LTE TDD kwenye maeneo **17** tofauti ndani ya Jiji la Dar es Salaam.

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limekamilisha usimikaji wa vituo 88 vilivyo jengwa kupitia miradi ya UCSAF kwenye maeneo ya yasiyo na mvuto kibiashara kwenye mikoa ya Mtwara, Lindi, Tabora, Rukwa, Geita, Dodoma, Iringa, Njombe, Ruvuma, Mbeya, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Mara, Kigoma, Singida, Morogoro, Pwani, Kusini Pemba, na Kaskazini Pemba.

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeanza kutekeleza mradi wa upanuzi wa mkongo wa baharini wa EASSy awamu ya nne ambao Shirika ni mbia. Shirika limechangia Dola za Marekani 136,195 kwenye upanuzi wa awamu ya nne ya Mkongo wa EASSy. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Mwezi Juni, 2022. Aidha, Shirika limekamilisha upanuzi wa njia za kimataifa za mawasiliano ya intaneti kutoka kiwango cha 12.7Gbps hadi 18.7Gbps sawa na ongezeko la asilimia 47. Upanuzi wa njia umelenga kuboresha huduma za intaneti zinazotolewa na Shirika kwa taasisi za Serikali na wateja wengine binafsi. Vilevile, Shirika limekamilisha upanuzi wa miundombinu ya mawasiwliano (kupitia NICTBB) inayounganisha Majiji ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya na Dodoma.

**Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)**

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) lilipanga kukusanya kiasi cha Shilingi **14,044,500,000** kutoka katika vyanzo vyake vya mapato vya ndani, ambavyo ni matangazo ya biashara, udhamini wa vipindi na matangazo mubashara kupitia vyombo vyake vya redio, runinga na mitandao ya kijamii. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 TBC ilikusanya jumla ya Shilingi **9,478,016,712.20** sawa na **asilimia 67.5** ya lengo.

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TBC imeendelea na ujenzi wa mitambo ya redio masafa ya FM kwa fedha za maendeleo. Kufikia Mwezi Aprili, 2022 utekelezaji ulifikia hatua mbalimbali kama ifuatavyo: Wilaya za Same (80%), Sikonge (90%), Kahama (90)%), Bunda (95%), Nkasi (90%), Kasulu (80%) na Karagwe (90%). Aidha, kupitia fedha za UCSAF imeendelea na ujenzi wa mitambo ya redio ya FM ni katika Wilaya za Mlele (70%), Makete (70%), Uvinza (50%), Mbinga (75%) na Ngorongoro (70%). Pia, Shirika limeendelea na ujenzi wa mitambo kwa ajili ya kuongeza mawanda na usikivu kupitia ufadhili wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ambapo umekamilika katika Wilaya za Ngara (100%), Ruangwa (100%) na Kilombero (100%) na utekelezaji katika Wilaya za Ludewa na Kyela zimefikia hatua zifuatazo 90% na 50% mtawalia.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** Miradi mingine ya upanuzi wa usikivu inayotekelezwa na TBC kwa fedha za maendeleo kwa kipindi cha 2021/22 ni ujenzi wa vituo na ufungaji wa mitambo ya redio masafa ya FM visiwa vya Unguja na Pemba, mikoa ya Njombe, Songwe na Simiyu pamoja na Wilaya za Kilwa na Serengeti. Utekelezaji wa miradi hii imefikia asilimia 40 na inatarajiwa kukamilika ifikapo Mwezi Septemba, 2022.

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TBC imeendelea kuboresha studio za redio na runinga kwa kufunga mitambo ya kidijitali inayoendana na mabadiliko ya teknolojia. Studio za redio Barabara ya Nyerere Jijini Dar es Salaam zimefungwa mitambo na vifaa vya kisasa vya kidijiti kwa Shilingi Bilioni 2.03 kwa kuondoa mitambo na vifaa vya analojia vilivyokuwa vikitumika hapo awali. Aidha, jengo na studio za televisheni kwa ajili ya TBC2 zimejengwa Mikocheni jijini Dar es Salaam kwa Shilingi Bilioni 3.48 kwa ufadhili wa Serikali ya Korea Kusini ambapo Serikali ya Tanzania ilichangia Shilingi Milioni 726. Studio hizi ni mahsusi kwa ajili ya kuandaa vipindi vya burudani, elimu na michezo. Kwa upande mwingine, TBC imekamilisha ujenzi wa studio za redio jamii jijini Dodoma na kuzinduliwa rasmi Mwezi Julai, 2021 ambayo imekuwa ni msaada kwa wananchi wanaoishi makao Makuu ya nchi Dodoma pamoja na kurusha sehemu ya taarifa ya Habari na matukio ya kitaifa kutokea Dodoma.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuhakikisha kuwa TBC inabeba wajibu wake wa kuhabarisha umma, maboresho ya maudhui pamoja na mwonekano wa vipindi vya redio na runinga yamefanyika. Mathalani, kipindi cha Jambo Tanzania kupitia TBC1 kimekuwa na mvuto wa aina yake kwa kutumia mtindo wa kisasa wa upashanaji habari. Kwa upande wa redio, TBCTaifa huandaa vipindi vyenye maudhui kutoka maktaba za TBC (Tafakuri, Wosia wa Baba, Ndivyo ilivyokuwa, Nyota wa wiki, na Lulu za Kiswahili). TBC imeendelea kutangaza na kuonesha mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita na kuibua changamoto zinazowakabili wananchi ili zifanyiwe kazi na mamlaka husika.

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kutokana na mageuzi ya teknolojia ya habari TBC imeendelea kujiimarisha kupasha habari wananchi kwa njia ya mitandao ya kijamii kupitia TBConline na matangazo mubashara ya redio na runinga. Kupitia majukwaa haya TBC hurusha mubashara matangazo kuonesha utekelezaji wa miradi ya kimkakati inayotekelezwa

na Serikali na ile inayoshirikisha wadau wa sekta binafsi wa ndani na nje ya nchi huku ikitekeleza kaulimbiu yake ya Ukweli na Uhakika. Hivi karibuni, TBC itazindua chaneli ya televisheni ya itakayotangaza kwa lugha ya Kiingereza mtandaoni ili iweze kuitangaza nchi kimataifa.

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** TBC kupitia chaneli yake ya Televisheni ya Tanzania Safari imeendelea kuandaa na kutangaza maudhui yanayohusiana na fursa za utalii zilizopo nchini. Chaneli hii imekuwa ni kichocheo muhimu katika kukuza pato la utalii nchini ikiwemo kufundisha vijana wa kitanzania kuhusu rasilimali zilizopo nchini. Kwa upande mwingine, TBC imefanikiwa kupata haki ya kurusha matangazo ya mpira wa miguu Ligi Kuu ya Soka Tanzania Bara kwa kipindi cha miaka kumi mfululizo (2021/22 – 2030/31) kwa upande wa redio na mitandao ya kijamii. Hatua hii inaifanya TBC kuendelea kuwa kinara na tegemeo kwa watazania katika kuwapasha habari za burudani na michezo hasa matangazo ya soka hapa nchini.

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** Naomba nilitaarifu Bunge lako tukufu kuwa, zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi 45 waliopisha eneo la takriban ekari 53 kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya TBC katika kata ya Mtumba limekamilika, michoro kwa ajili ya majengo na miundombinu ya utangazaji ya TBC imekamilika na hatua inayoendelea kwa sasa kuandaa gharama za ujenzi (detailed design). Ujenzi unatarajia kuanza Mwezi Juni, 2022 na fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi huu ni Shilingi Bilioni 1.46.

**Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN)**

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) ilipanga kukusanya kiasi cha **Shilingi 14,343,823,000.00** kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni mauzo ya matangazo, nakala za magazeti, uchapaji kibiashara, kodi za pango na

ushauri wa kimedia. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 Kampuni ilifanikiwa kukusanya **Shilingi 6,973,776,024.63** sawa na asilimia 49 ya lengo.

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni imeendelea kuwa daraja muhimu na la kuaminika la mawasiliano kati ya Serikali na wananchi. Kupitia magazeti yake ya Kiswahili na Kiingereza, majarida na huduma za habari kwa njia ya mtandao, TSN imeendelea kuwa nyenzo ya utoaji wa habari sahihi na za kuaminika zinazozingatia weledi na maadili ya taaluma ya uandishi wa habari. Katika kutekeleza majukumu yake, TSN imefanya juhudi kubwa za kuboresha magazeti yake kimwonekano na kimaudhui ili kuvutia wasomaji na watangazaji zaidi. Katika kipindi hiki mkazo mkubwa uliwekwa kwenye uandishi wa habari za kimaendeleo zinazoangazia kwa kiasi kikubwa namna Serikali ya Awamu ya Sita inavyotekeleza majukumu yake.

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni imechapisha machapisho maalum (special supplements) tisa (9) ambayo yameiingizia Kampuni kiasi cha Shilingi 948,744,410.00. Machapisho haya maalum yalibeba habari za kina kuhusu matukio mbalimbali ya Kitaifa yakiwemo maadhimisho ya Miaka 60 ya Uhuru, Miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mwaka Mmoja wa Uongozi wa Awamu ya Sita na Miaka 58 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Aidha, Kampuni iliendelea kuchapisha majarida maalum yenye maudhui yanayolenga makundi mbalimbali katika jamii ikiwemo vijana, wanawake na wafanyabiashara.

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na changamoto za kutetereka kwa soko la habari chapishi nchini na duniani kote kwa kubuni na kuendeleza vyanzo mbadala vya mapato. Katika kipindi hiki uchapaji wa kibiashara (Commecial Printing) pamoja na utoaji wa huduma za kitaalam za kimedia (Media Consultancy Services)

zimepewa msukumo mkubwa na kwa pamoja zimeweza kuiingizia Kampuni zaidi ya Shilingi Bilioni moja (1). Uchapaji huu ambao umefanyika kwa kutumia mtambo mdogo wa uchapaji kidijitali (digital printing machine) umeonyesha matumaini makubwa ya biashara baada ya kutangaza huduma hii kwenye vyombo vya habari.

**96. *Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi hiki Kampuni ilitekeleza Mradi wa Kimedia wa kutangaza shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) kwa njia ya makala kwa kutumia magazeti yake ya Daily news na HabariLEO. Mradi huu wenye thamani ya Shilingi Milioni 345.8 ambao utekelezaji wake ulianza Mwezi Disemba 2021 na utakamilika Mwezi Juni 30, 2022 unahusisha uandishi wa Habari na Makala pamoja na uandaaji na uchapaji wa jarida yla kila Mwezi na jingine linalotoka kila baada ya miezi mitatu . Aidha, Kampuni iliendelea kutekeleza mradi wa kusaidia Maendeleo ya Elimu ya Msingi na Sekondari nchini (TSN Education Initiative) ambao unahusisha uandaaji na uchapaji wa majarida maalum ya kila wiki ya Elimika (HabariLEO) na Academy (Daily News). Uchapaji wa majarida haya umefanyika kwa ufadhili wa Ubalozi wa China nchini wa Dola za Marekani 30,000 (sawa na Shilingi Milioni 70).

**97. *Mheshimiwa Spika,*** katika hatua ya kuendana na mabadiliko katika teknolojia ya upashanaji habari, Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) imeanzisha Programu Tumizi (Application) ili kuwezesha magazeti yake kupatikana pia kwa njia ya mtandao. Katika kipindi hiki, TSN imeendelea kutangaza Mobile application yake pamoja na kuimarisha uuzaji wa magazeti yake kwa njia ya mtandao. Hadi kufikia mwishoni mwa Mwezi Aprili, 2022, Kampuni ilikuwa imefanikiwa kupata wasomaji wapya 818 wa magazeti kwa njia ya mtandao pamoja na Taasisi 45 ambao waliingizia Kampuni Shilingi Milioni 56.2 ikilinganishwa na wateja 672 ambao waliingiza Shilingi Milioni 31.8 katika kipindi kama hiki

mwaka uliotangulia. Wakati huo huo, Kampuni iliendelea kuimarisha utoaji wa huduma ya habari mtandao kwa kuongeza upatikanaji wa habari katika mitandao ya kijamii. Juhudi hizi zimewezesha jumuiya ya wasomaji na wafuatiliaji mtandaoni kuendelea kuongezeka na hadi kufikia Mwezi Aprili 2022 wasomaji/ wafuatiliaji Milioni 266 waliweza kuona/ kuangalia video na habari za TSN ikilinganishwa na wasomaji/ wafuatiliaji Milioni 175 Mwezi Juni 2021.

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni pia imeongeza uchapishaji wa habari na kurusha matangazo mubashara hususani yanayohusu matukio ya kitaifa na kiserikali ambapo kwa sasa wastani wa matangazo ya moja kwa moja yamefikia 20 kwa Mwezi kutoka wastani wa matangazo matatu Mwezi Juni, 2021. Kutokana na mafanikio haya Mwezi Agosti, 2021 Kampuni ilitunukiwa tuzo ya maudhui mtandaoni na kampuni ya Marekani ya *YouTube*. Pamoja na hayo, Kampuni imeboresha mifumo, tovuti na programu mbalimbali ili kuongeza ufanisi katika utendaji na utoaji huduma. Maboresho hayo yamefanyika kwenye Programu Tumizi (Mobile Application) ambayo inawawezesha wasomaji kununua magazeti ya TSN kwa njia ya mtandao popote duniani na mfumo wa kuuza nafasi za matangazo kwenye magazeti na tovuti zake tatu - www.dailynews.co.tz, www. habarileo.co.tz na www.spotileo.co.tz

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuunga mkono jitihada za Serikali katika kutoa ajira, Kampuni ilitoa ajira zisizo rasmi zaidi ya 600 nchi nzima kwa mawakala wa magazeti, wauzaji wadogo wadogo (street vendors), wasafirishaji wa magazeti, mawakala wa kuuza matangazo pamoja na wauzaji wa matangazo binafsi (Freelancers) ambao hupata *commission* ya hadi asilimia 30 ya mauzo wanayofanya.

**Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)**

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Mfuko ulipanga kukusanya kiasi cha **Shilingi 34,086,331,975**

kutoka katika vyanzo vyake vya mapato, ambavyo ni Ruzuku toka Serikalini, Tozo ya huduma, ruzuku toka TCRA na wadau wa maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022, UCSAF ilifanikiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 28,893,129,482** sawa na asilimia 84.8 ya lengo.

**Miradi ya kufikisha huduma za mawasiliano vijijini katika Kata 532**

**101. Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2021/22 UCSAF, ilipanga kufikisha huduma za mawasiliano ya simu za mkononi kwenye Kata 532 zenye vijiji 1,100 na wakazi takriban 5,213,686 ambapo jumla ya fedha za ruzuku kiasi cha Shilingi Bilioni 82.2 kitatumika katika kufikisha huduma za mawasiliano. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 Kata 123 zenye Vijiji 314 na wakazi wapatao 1,375,198 tayari zimefikishiwa huduma za mawasiliano. Minara katika Kata zilizobaki 409 utekelezaji wake upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Mwezi Juni, 2022.

**102. Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Serikali kupitia UCSAF inatekeleza miradi mipya mitatu ya kufikisha huduma za mawasiliano vijijini kama ifuatavyo.

**Mradi wa Kupeleka Huduma za Mawasiliano Awamu ya 6**

**103. Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Serikali kupitia UCSAF ilitangaza zabuni ya kufikisha huduma za mawasiliano katika Kata 190 zenye Vijiji 380 vya maeneo ya mipakani na kanda maalum ambapo baada ya tathmini ya zabuni hiyo, Kata 85 zenye Vijiji 179 na wakazi takriban 816,090 zimepata watoa huduma. Mikataba ya kufikisha huduma za mawasiliano kupitia mradi huu imesainiwa Mwezi Februari, 2022. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kukamilika Mwezi Novemba, 2022.

**104. *Mheshimiwa Spika*,** Katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Serikali kupitia UCSAF iliingia makubaliano na Shirika la

Mawasiliano TTCL kufikisha huduma za mawasiliano katika Ofisi za Halmashauri 11 ambazo ni Mbogwe, Tanganyika, Kakonko, Malinyi, Mtwara DC, Msalala DC, Bariadi, Nzega, Kilindi, Rorya na Pangani. Mkataba wa kutekeleza mradi huo ulisainiwa tarehe 25 Oktoba, 2021 na kwamba mradi huu unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Mwezi Juni, 2022.

**Mradi wa Kupeleka Huduma za Mawasiliano Zanzibar**

**105**. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia UCSAF inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kufikisha huduma za mawasiliano Zanzibar. Mkataba wa kupeleka mawasiliano Zanzibar ulisainiwa tarehe 20 Januari, 2022 ambapo kupitia mkataba huo, Shehia 38 zenye vijiji 78 zitajengwa minara 42 ambapo vitapata huduma za mawasiliano. Mradi huu ukikamilika wakazi wapatao 211,000 waliokuwa wamebaki bila huduma za mawasiliano watapata huduma za mawasiliano na kwamba mradi huu unatarajiwa kukamilika Mwezi Oktoba, 2022.

**Kuzipatia Shule vifaa vya TEHAMA na Kuunganisha na mtandao wa intaneti**

**106. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia UCSAF ilipanga kupeleka vifaa vya TEHAMA kwenye shule 150 ambapo kila shule itapata kompyuta 5, printa moja na projekta moja pamoja na kuziunganisha shule hizo na mtandao wa intaneti. Lengo la mradi huu ni kuongeza matumizi ya TEHAMA kwa wanafunzi wanaosoma katika shule za Serikali. Aidha, UCSAF inakamilisha kazi ya kuwapata wazabuni kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu unaotarajiwa kukamilika ifikapo Mwezi Juni, 2022.

**107. Mheshimiwa Spika**, Katika kukuza uwezo wa matumizi ya TEHAMA kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, Serikali kupitia UCSAF ilipanga kupeleka vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya Shule 10 za wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Utekelezaji umeanza kwa Shule za Sekondari nane (8) za Mpwapwa (Mpwapwa), Mkolani (Nyamagana), Kashaulili (Mpanda), Morogoro Sekondari (Morogoro Manispaa), Shinyanga (Kishapu), Songea Wavulana (Songea Manispaa) Kazima (Tabora Manispaa) na Haile Selassie (Mjini Magharibi). Mradi huu ambao unatarajiwa kukamilika Mwezi Juni, 2022.

**Kuboresha usikivu wa matangazo ya Redio katika maeneo ya mipakani**

**108**. **Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Serikali kupitia UCSAF kwa ushirikiano na Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) imekamilisha mradi wa uboreshaji usikivu wa matangazo ya redio ya TBC katika Wilaya za Mlimba, Ludewa, Ruangwa na Ngara. Aidha, usikivu huu umewezesha watanzania takriban 622,462 wanaoishi katika wilaya hizi kupata usikivu wa Redio yetu ya Taifa ya TBC. Vilevile, UCSAF imeingia makubaliano mengine na TBC kwa ajili ya kuboresha usikivu wa redio katika Wilaya za Kyerwa na Lushoto. Mradi huu ukikamilika wananchi takriban 813,467 waishio katika Wilaya hizi mbili watapata usikivu wa maudhui ya Kitanzania kupitia redio ya TBC. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Mwezi Disemba, 2022.

**Kutoa Mafunzo ya TEHAMA kwa Walimu**

**109**. **Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Serikali kupitia UCSAF imetoa mafunzo ya TEHAMA kwa Walimu 621 (569 toka Tanzania Bara na 52 toka Zanzibar) wa shule za umma ambazo zimenufaika na mradi wa kufikishiwa vifaa vya TEHAMA. Nia ya mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo Walimu kuweza kutatua changamoto za kiufundi zinazoweza tokea katika vifaa vya TEHAMA vinavyotolewa na Mfuko. Aidha, madhumuni mengine ya mafunzo hayo ni kuboresha ufundishaji kwa kutumia njia ya TEHAMA. Mafunzo hayo yalifanyika tarehe 25 – 29 Oktoba, 2021 katika vituo vitatu (3) ambavyo ni Taasisi ya Teknolojia

ya Dar es Salaam (DIT), Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST).

**Mradi wa Kituo cha TEHAMA katika Wilaya ya Mjini – Zanzibar**

**110**. **Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Serikali kupitia UCSAF ilipanga kujenga kituo cha TEHAMA katika Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi katika eneo la Fumba. Ujenzi wa kituo hiki upo katika hatua za mwisho za ukamilishaji. Huu ni mwendelezo wa ujenzi wa vituo 10 vilivyojengwa Zanzibar ambapo kituo kimoja kimejengwa kwa kila Wilaya. Kituo tajwa ni kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kupata huduma za TEHAMA ambapo hupata taarifa mbalimbali kupitia mtandao pamoja na mafunzo mbalimbali ya TEHAMA.

**Ujenzi wa Kituo cha Miito ya Dharura**

**111**. ***Mheshimiwa Spika***, Katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Serikali kupitia UCSAF imefadhili uanzishaji wa Kituo cha Miito ya Dharura, ambapo wananchi wataweza kutoa taarifa za maafa na majanga mfano moto, mlipuko wa magonjwa mbalimbali na kadhalika. Kituo hicho kina mfumo wenye uwezo wa kupokea simu 500 kwa wakati mmoja. Lengo la kufadhili kituo hichi ni kuwawezesha wakazi kuweza kutoa taarifa za dharura na kusaidiwa katika kutatuliwa kwa changamoto zao za majanga. Aidha kituo hicho kimekamilika na kukabidhiwa kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi (SMZ) tarehe 07 Machi, 2022. Kituo hicho kipo eneo la Kiembesamaki.

**Uanzishwaji wa Vituo vya Wazi vya Intaneti**

**112**. ***Mheshimiwa Spika***, Katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Serikali kupitia UCSAF inatarajiwa kukamilisha mradi wa uanzishwaji wa Vituo vya wazi vya intaneti (*Hotspot*) katika maeneo matano (5) kwa lengo la kuongeza matumizi ya intaneti kwa wananchi kwenye maeneo ya wazi. Utekelezaji wa mradi huu upo katika hatua ya kumpata mtoa huduma

kupitia tathmini ya zabuni iliyotangazwa. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Mwezi Juni, 2022.

**Mradi wa Tiba Mtandao (Telemedicine)**

**113**. **Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Serikali kupitia UCSAF inatekeleza mradi wa Tiba Mtandao katika Hospitali za Mnazi Mmoja (Unguja) na Abdallah Mzee (Pemba) ambazo zinatarajiwa kuunganishwa na Hospitali za Jakaya Kikwete Cadiac Institute (JKCI), Hospitali ya Ocean Road, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) na Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI). Mkandarasi wa Mradi ameshapatikana kwa ajili ya utekelezaji. Mradi huu unatarajiwa kukamilika Mwezi Juni, 2022. Lengo la mradi huu ni kuwezesha wananchi kupata huduma za kibingwa kwa njia ya mtandao bila kuwa na haja ya kusafiri na hivyo kupunguza gharama za rufaa kwa wagonjwa husika.

**Tume ya TEHAMA (ICTC)**

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Tume ilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 2,107,622,000.** Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 Tume ilifanikiwa kukusanya **Shilingi 903,985,434.41** sawa na **asilimia 42.9** ya makadirio ya mwaka kutoka katika vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni mgao kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, ada za usajili na uendelezaji wa Wataalam wa TEHAMA na washirika wa maendeleo.

**115.** ***Mheshimiwa Spika***, Tume ya TEHAMA imeendelea kusajili Wataalam wa TEHAMA nchini kwa lengo la kuwatambua na kuwaendeleza kulingana na Mwongozo wa usajili wa wataalam wa TEHAMA uliozinduliwa tarehe 7 Oktoba, 2020. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 wataalam wa TEHAMA **546** walikuwa wamesajiliwa na kufanya idadi ya wataalam waliosajiliwa kuongezeka kutoka **415** Mwezi Machi 2021 na kufikia **961**.

**116.** ***Mheshimiwa Spika***, Tume imeendelea kutekeleza Mwongozo wa Kitaifa wa Kuendeleza Ujuzi wa TEHAMA *(National ICT skills Development Framework)* kwa kuratibu mafunzo ya Utaalam wa TEHAMA. Kwa kipindi cha Mwezi Julai, 2021 hadi tarehe 30 Aprili, 2022, Wataalam **222** walishiriki mafunzo na kufanya idadi ya washiriki wa mafunzo kuongezeka kutoka **90** Mwaka 2021 na kufikia **312.** Mafunzo yalitolewa mwenye maeneo ya: *Cyber Security Specialists (29), Cloud Computing (18), Big Data Analytics (19), Data Analysis for Business Management and Governance (60), Certified Network Defender (45), Information Technology Infrastructure Library – ITIL (15), Cisco Certified Network Associate (4), na Fibre Optic Professional Technician Certification (13)*. Aidha, jumla ya wataalam 33 wamefanya mitihani ya Kimataifa ya kitaalam inayotolewa na *EC – Council* pamoja na *Fibre Optic Association*. Wataalamu 20 wanatambulika kama *Cyber Security Specialists* na wataalam 13 wanatambulika kama *Certified Fibre Optic Technicians.*

**117.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendeleza ubunifu TEHAMA nchini, Tume inaratibu utekelezaji wa programu ya kukuza Kampuni changa za TEHAMA (Startups) ili kuwezesha bidhaa za TEHAMA kuingia katika soko la biashara na kuchangia katika kukuza uchumi ikiwepo kutengeneza ajira kwa vijana. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 Tume kupitia kanzidata ya ubunifu TEHAMA imepokea maombi 320 ya wabunifu TEHAMA ya kutaka bunifu zao zitambuliwe ili waweze kuingia katika soko la biashara. Kwa kulitambua hili, Tume imeandaa rasimu ya Mwongozo *(Regulatory Sandbox Framework for Digital Innovators, ICT Products and Solutions)* utakaoweka mazingira wezeshi kuruhusu kampuni changa za TEHAMA na wabunifu TEHAMA kufanya majaribio ya bunifu zao bila gharama kabla ya bidhaa kuingia sokoni. Mwongozo huu utaanza kutumika katika mwaka ujao wa fedha.

**118.** ***Mheshimiwa Spika***, katika eneo la utafiti, Tume ya TEHAMA kwaq kushirikiana na Taasisi ya TEHAMA ya Estonia zimekubaliana kufanya tathmini ya mazingira ya TEHAMA *(*ICT landscape assessment*)* nchini ikiwa ni utekelezaji wa Hati ya Makubaliano (MoU) baina ya nchi hizi mbili. Tathmini itafanyika kuanzia Mwezi Juni, 2022.

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika juhudi za kuendeleza TEHAMA nchini, Tume imeandaa na kuwezesha yafuatayo:

i) Kongamano la Tano la Mwaka la TEHAMA nchini (*5th Tanzania Annual ICT Conference* - TAIC) lililofanyika Jijini Arusha Mwezi Oktoba, 2021 na kuhudhuriwa na washiriki **816**. Kongamano lilifunguliwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa (Mb.) ambapo pamoja na mambo mengine lilitengeneza agenda ya Mwaka ya TEHAMA inayosema: **Kujenga Taifa la Kidijitali** (Building a Digital Nation). Tume ya TEHAMA inaendelea kuratibu maazimio yaliyotolewa na wadau katika Kongamano hilo.

ii) Katika kuhamasisha matumizi ya TEHAMA kwa jamii, Tume ya TEHAMA ilianzisha Tuzo za TEHAMA Tanzania (Tanzania ICT Award) ambayo kilele chake kilikuwa tarehe 22 Oktoba, 2021. Jumla ya makundi 18 yalikabidhiwa Tuzo za TEHAMA na Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tuzo hizi zitakuwa chachu ya matumizi ya TEHAMA katika taasisi mbalimbali na jamii kwa ujumla.

iii) Tume katika kutekeleza jukumu lake ya kukuza uwekezaji katika TEHAMA nchini, imeanzisha jukwaa la uwekezaji katika TEHAMA lililofanyika Jijini Arusha tarehe 20 Oktoba, 2021 ambapo wadau kutoka ndani na nje ya nchi walishiriki kujadili masuala mbalimbali kuhusu uwekezaji nchini.

iv) Kadhalika, katika kuendeleza ujuzi wa TEHAMA kwa vijana, Tume ya TEHAMA kwa kushirikiana na Shirika la

Kimataifa la Fursa za Kidijitali *(*Digital Opportunity Trust – DOT*)* iliandaa mkutano wa kidijitali wa vijana Tanzania katika mikoa 10 ambapo vijana 2,716 walishiriki kwa njia ya mtandao na kuelimishwa kuhusu fursa za ajira kupitia TEHAMA.

**Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano Tanzania (TCRA CCC)**

**120.** ***Mheshimiwa Spika***, Baraza limeendelea kutekeleza majukumu yake ya kuwakilisha maslahi ya watumiaji wa huduma za mawasiliano. Chanzo kikuu cha mapato ya Baraza ni ruzuku kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 Baraza limepokea **Shilingi 600,000,000** sawa na asilimia **100** ya ruzuku toka TCRA.

**121.** ***Mheshimiwa Spika***, Baraza limeendelea kutekeleza jukumu lake la kuanzisha Kamati za Watumiaji na kushauriana nazo. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/22 Baraza limeanzisha Kamati za Watumiaji katika Mikoa ya Kigoma na Tabora na kufikia mwisho wa Mwaka wa Fedha Baraza litaanzisha Kamati nyingine katika Mkoa wa Rukwa. Baraza limeendelea kushauriana na Kamati za watumiaji katika mikoa ya Arusha, Tanga, Morogoro, Mbeya, Iringa, Mwanza, Kagera, Mtwara, Lindi, Mjini Magharibi, Dodoma na Kusini Pemba. Aidha, Baraza limeendelea kuzijengea Kamati za Watumiaji uwezo wa kutekeleza majukumu ya kutoa elimu, kuhamasisha na kupokea maoni ya watumiaji.

**122.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Baraza limeendelea kutekeleza jukumu lake la kupokea na kusambaza taarifa muhimu zinazohusu masuala ya watumiaji. Kupitia mikutano na wawakilishi wa watumiaji kutoka makundi ya watu wenye ulemavu, wajasiriamali, wanawake, vijana, viongozi wa dini, Serikali za Mitaa na Waandishi wa Habari katika Mikoa ya Dar es Salaam, Geita,

Arusha, Kigoma, Tabora, Tanga, Morogoro, Mbeya, Iringa, Mwanza, Kagera, Mtwara, Lindi, Mjini Magharibi, Dodoma na Kusini Pemba ambapo takribani watumiaji **45,569** wakiwemo watumiaji **2,241** wenye ulemavu walifikiwa na kutoa maoni.

**123.** ***Mheshimiwa Spika***, Baraza kupitia vyombo vya habari ikiwemo; redio, magazeti, blogu, runinga, tovuti na kurasa za mitandao ya kijamii limeendelea kutoa elimu na kuhamasisha upokeaji wa maoni kutoka kwa watumiaji. Baraza limeendesha vipindi 24 kupitia redio na runinga kwa lengo la kuelimisha na kuhamasisha watumiaji wa huduma za mawasiliano. Aidha, Mfumo wa e-mrejesho umetumika kupokea maoni na changamoto za watumiaji pamoja na kutoa mrejesho kwa watumiaji. Kurasa za Mitandao ya kijamii ya *Facebook, Instagram* na *Twitter* zimehuishwa kwa kuwekwa taarifa mbalimbali na kuwafikia watumiaji takriban **527,269**. Aidha, Baraza linaendelea kukamilisha utengenezaji wa Programu Tumizi (Mobile application) itakayowasaidia watumiaji kujua na kuhakiki taarifa za matumizi ya data na kuwasilisha malalamiko endapo hawataridhika na taarifa za matumizi yao. Vilevile, Baraza limeendelea kushauriana na Wizara, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania na Watoa huduma kuhusiana na masuala muhimu ya watumiaji kwa lengo la kuondoa changamoto na kuboresha huduma za mawasiliano.

## C. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

### Makadirio ya Mapato ya Wizara

**124**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Fungu 68) inakadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 150,700,000,000** ambazo zitatokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, tozo itokanayo na kuongeza salio la simu, usajili wa Magazeti, ada ya mwaka

ya Magazeti, vitambulisho vya Waandishi wa Habari na machapisho ya picha, mabango na majarida.

**MALENGO YA BAJETI YA WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**

**124.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara yangu inasimamia Mapinduzi ya Kidijitali na kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari nchini. Mapinduzi ya Kidijitali ndio yanayoweka Msingi wa kulipeleka Taifa kwenye Uchumi wa Kidijitali unaowezeshwa na kuendeshwa na TEHAMA. Ili kuwezesha mageuzi na mapinduzi haya kwenye Sekta zote za Uchumi na Kijamii, Wizara imepanga kufanya mabadiliko na maboresho makubwa kwenye Sekta ili kuendana na mageuzi kwa kuharakisha uendelezaji na usimamiaji miundombinu ya TEHAMA, Mawasiliano, Posta na Habari inayojumuisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, anwani za makazi, mitambo ya utangazaji na Posta. Vilevile, kufanya mapinduzi kwenye Taasisi za Sekta; kuimarisha mashirikiano na Sekta binafsi, kuendeleza tafiti na ubunifu kwenye masuala ya TEHAMA, kuwajengea uwezo watumishi kuendana na mapinduzi haya, kuwezesha Sekta nyingine kuelekea kwenye mapinduzi ya kidijitali na kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari. Aidha, Wizara imekusudia kufanya mageuzi kwenye taasisi zake ili ziweze kutoa huduma zake kwa ufanisi zaidi. Shughuli nyinginezo zitakazotekelezwa kuharakisha mapinduzi ya kidijitali katika kila Eneo la Sekta Ndogo ni kama ifuatavyo:

**Eneo la Mawasiliano**

**126**. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Wizara imepanga kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

i) Kuandaa Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA ya Mwaka 2016;
ii) Kusimamia utendaji wa Taasisi zilizo chini ya Wizara zinazohusika na mawasiliano ya simu na Posta;

iii) Kuimarisha ushirikiano wa Sekta Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;
iv) Kusimamia uboreshaji wa huduma za mawasiliano ya simu na Posta ili kufikia wananchi wote;
v) Kuendelea kutekeleza Mfumo wa Anwani za Makazi nchini;
vi) Kusimamia utekelezaji wa mradi wa Huduma Pamoja (One Stop Community Centre);
vii) Kusimamia upembuzi yakinifu utakaowezesha biashara Mtandao (e-Commerce);
viii) Kufanya mapitio ya Sheria za Kisekta na Kanuni zake;
iv) Kuratibu masuala ya kukuza uwekezaji katika Sekta ya Mawasiliano;
v) Kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu ya Mwaka 1997; na
xii) Kukamilisha kazi ya kuhuisha Sera ya Taifa ya Posta ya Mwaka 2003 na maandalizi ya Mkakati wa utekelezaji.

**Eneo la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)**

**127**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inatarajia kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

i) Kuendeleza Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kufikisha huduma ya Mkongo kwenye Wilaya 15 na kuongeza huduma za Mkongo kutoka Wilaya 66 hadi 81 (kati ya Wilaya 139);
ii) Kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Tanzania ya Kidijitali (Digital Tanzania Program);
iii) Kukamilisha uandaaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Uchumi wa Kidijitali (National Digital Economy Strategy) na kusimamia utekelezaji wake;
iv) Kuratibu na kuwezesha ujenzi wa Mfumo wa TEHAMA kuratibu utendaji kazi wa Wizara;
v) Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Usalama wa Mitandao (National Cyber Security Strategy);

vi) Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Mtandao wa TEHAMA wenye kasi zaidi (National Broadband Strategy) ili kuongeza msambao wa intaneti (penetration) kutoka asilimia 50 hadi kufikia asilimia 60 Mwaka 2023;
vii) Kuendelea kuwaendeleza wataalamu 200 kwenye maeneo ya TEHAMA yenye uhaba wa ujuzi;
viii) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Miongozo ya kuimarisha masuala ya utafiti na ubunifu katika TEHAMA;
ix) Kuendelea kuimarisha usalama wa mitandao, kuongeza udhibiti wa matumizi ya taarifa binafsi na kupunguza uhalifu wa mitandao kwa kushirikiana na Vyombo vya Usalama; na
x) Kuimarisha mashirikiano na mashirika ya mawasiliano ya Kikanda na Kimataifa.

**Eneo la Habari – MAELEZO**

**128.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Wizara imepanga kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

i) Kukusanya taarifa na kuisemea Serikali kuhusu utekelezaji wa Sera, Mikakati, Miradi na Programu inazozitekeleza;
ii) Kuanzisha Bodi ya Ithibati ya Wanahabari, Baraza Huru la Habari na Mfuko wa Mafunzo kwa Wanahabari;
iii) Kufanya mapitio ya Sera ya Habari na Utangazaji ya Mwaka 2003 ili kuifanya iendane na mabadiliko katika Sekta ya Habari;
iv) Kufanya mapitio ya baadhi ya vifungu katika Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016 na Kanuni zake za Mwaka 2017;
v) Kuchapa nakala 12,794 za Picha za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nakala 12,794 za Picha za Baba wa Taifa Mwl. Julius K. Nyerere, nakala 4,000 za Jarida la Nchi Yetu na nakala 2000 za Bango la Baraza la Mawaziri (Cabinet posters);

vi) Kuchapa na kutoa leseni za magazeti na vitambulisho vya waandishi wa Habari;
vii) Kutoa miongozo na kufanya tathmini ya utoaji taarifa kwa umma kwa kila Taasisi;
viii) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Habari na Utangazaji ya Mwaka 2003, Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016 na Kanuni zake za Mwaka 2017 ili kuhakikisha maadili na uzingatiwaji wa Sheria katika Tasnia ya Habari;
ix) Kuratibu mkutano wa Mwaka wa Maafisa Mawasiliano Serikalini;
x) Kuratibu Vyombo vya Habari katika matukio mbalimbali ya kitaifa;
xi) Kuhamasisha Vyombo vya Habari vya nje ya nchi katika kuitangaza Tanzania;
xii) Kuanza Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano (National Communication Strategy – NCS); xiii) Kuanzisha Kipindi Maalum cha Ongea na Waziri; na
xiv) Kujenga Studio maalum kwa ajili ya Vipindi vya Moja kwa Moja vya redio na runinga.

**Miradi Itakayotekelezwa na Wizara**

**I: Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano**

**129. *Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara imekadiria kutumia **Shilingi 149,700,000,000** ambapo **Shilingi 149,000,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 700,000,000** ni fedha za nje kwa ajili ya kutekeleza kazi ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Fedha hizi zitatumika kujenga Kilomita 1,600 za Mkongo na Vituo vipya **15** vya kutolea huduma za Mkongo ili kuongeza wigo wa utoaji wa huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano hadi kufikisha ngazi za Wilaya nchini. Ujenzi huu utawezesha kufikisha huduma za Mkongo kutoka Wilaya 81 kati ya Wilaya 139.

**130. *Mheshimiwa Spika***, shughuli nyingine zitakazotekelezwa kwenye Mradi huu ni:

i) Kufanya Ujenzi wa Mkongo wa Majini kiasi cha Kilomita 60 kuunganisha Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kupitia Ziwa Tanganyika;
ii) Kufanya tathmini ya Ujenzi wa Kituo cha kuhifadhi Data Zanzibar;
iii) Kuwajengea uwezo wataalam 150 kwenye TEHAMA;
iv) Kuendelea kuimarisha usalama wa mitandao, kuongeza udhibiti wa matumizi ya taarifa binafsi na kupunguza uhalifu wa mitandao kwa kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama;
v) Kukamilisha Nyaraka za Baraza la Mawaziri kuhusu Mapendekezo ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sheria ya TEHAMA na Mkataba wa Jumuiya ya Umoja wa Afrika wa Usalama wa Mtandao na Ulinzi wa Taarifa Binafsi (Malabo Convention);
vi) Kuelimisha umma kuhusu Mkakati wa Usalama Mtandaoni;
vii) Kuwezesha utendaji kazi wa Kamati za Kiufundi kwa ajili ya usimamizi wa Mradi wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano;
viii) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mradi pamoja na ununuzi wa vitendea kazi kwa ajili ya usimamizi wa mradi; na
ix) Kuandaa Mpango Mkuu *(*Master Plan*)* wa utekelezaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

**II: Mfumo wa Anwani za Makazi**

**131.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara imekadiria kutumia **Shilingi 40,000,000,000** fedha za ndani kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi. Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na:

i. Kuhakiki miundombinu iliyowekwa wakati wa Operesheni Anwani za Makazi ili kuhakikisha viwango vimezingatiwa ili Mfumo uwe na tija kwa wananchi na kuwa endelevu;
ii. Kuhakiki taarifa zilizokusanywa kwenye operesheni maalum ya utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi;

iii. Kuboresha Kanzidata na Programu Tumizi ya Mfumo;
iv. Kuendelea kuunganisha Mfumo wa Anwani za Makazi na Mifumo mingine ya kutoa huduma muhimu za kijamii;
v. Kutoa elimu kwa umma; makundi maalum ya kijamii kuhusu manufaa na matumizi sahihi ya Mfumo na kujengea uwezo Taasisi za umma na binafsi kutoa huduma kupitia Mfumo;
vi. Kutunga Sheria ndogo za kuwezesha ujenzi na matumizi ya Mfumo, mapitio ya Sheria ya EPOCA na Kanuni zake kuwezesha matumizi ya Mfumo;
vii. Kununua *servers* mbili (2) kwa ajili ya kuhifadhi taarifa za Mfumo na vifaa vya kuwezesha matumizi ya Mfumo;
viii. Kuandaa mwongozo wa kufanya maboresho ya namna mpya ya kufanya biashara kwa kutumia Mfumo;
ix. Kutengeneza Mkakati wa usimamizi, uendeshaji na uendelezaji wa Mfumo; na
x. Kuwezesha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mfumo.

**III: Mradi wa Tanzania ya Kidijitali (Digital Tanzania)**

**132.** ***Mheshimiwa Spika***, Mradi wa Tanzania ya Kidijitali unalenga kuleta mabadiliko ya Kidijitali kwa kuwezesha maunganisho ya Kijiditali ya Kikanda na Kimataifa na hatimaye kukuza Uchumi wa Kidijitali (*Digital Economy*). Matokeo ya mradi huu ni pamoja na kuongeza na kubuni ajira zitakazotokana na ubunifu wa TEHAMA, ukuzaji wa viwanda vidogo vidogo (SMEs na SMMEs); kukuza ustadi wa wataalamu wa ndani ya Serikali na waliopo nje ya Serikali; na kuongeza uwezo wa utoaji wa Huduma za Serikali kwa kuwezesha uwepo wa intaneti bora ya bei nafuu na ya uhakika kwa ajili ya matumizi ya Serikali ili kumnufaisha mwananchi.

**133.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara inakadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 39,300,000,000** ikiwa ni fedha za nje kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i) Kujenga kituo kimoja (1) cha kukuza taaluma na ubunifu katika TEHAMA na vituo vidogo vitano (5) kwenye kila Kanda;
ii) Kuwezesha ununuzi, ugavi na ufungaji wa vifaa katika kituo kimoja (1) kikubwa na vituo vidogo vitano (5) vya kukuza taaluma na ubunifu katika TEHAMA;
iii) Kuwezesha ununuzi wa 'bandwidth' kwa ajili ya matumizi ya intaneti ya Serikali;
iv) Kusimika mitambo kwa ajili ya kuboresha Kituo cha Taifa cha Kutunzia Data (NIDC);
v) Kukarabati vituo 10 vya Huduma Pamoja;vi) Kujenga mfumo wa kitaifa utakaorahisisha ukusanyaji wa takwimu za masuala ya TEHAMA;
vii) Kujenga, kupanua na kuboresha miundombinu iliyopo ya intaneti yenye kasi (broadband) inayomilikiwa na Serikali (GovNET) na kuunganisha taasisi 100 kwenye Miundombinu hiyo na kufikisha taasisi 390 zilizounganishwa;
viii) Kutekeleza programu ya uelimishaji umma kuhusu mradi;
ix) Kujenga maabara tatu (3) kwa ajili ya kufufua (refurbishment) vifaa vya TEHAMA katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Mwanza;
x) Kujenga minara ya mawasiliano 150 kwenye Kata 150 ili kuwezesha huduma za mawasiliano nchini;
xi) Kufanya mapitio na kuhuisha Sera, Sheria na Kanuni mbalimbali za TEHAMA;
xii) Kuwajengea uwezo wataalam wa TEHAMA nchini kwa kuwapatia watalaam 200 mafunzo ya muda mfupi na wataalam 10 mafunzo ya muda mrefu; na
xiii) Kufanya tathmini ya kuainisha mahitaji na usanifu wa kujenga mfumo wa kuwezesha biashara mtandao.

**IV: Mradi wa Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA**

**134**. ***Mheshimiwa Spika***, Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 3,300,000,000** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Kuendeleza Ubunifu

na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA. Fedha hizo zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

i) Kujenga Kituo cha Kuendeleza Wataalam, tafiti na ubunifu wa TEHAMA na kufanya maandalizi ya ujenzi wa makao makuu ya Tume ya TEHAMA;
ii) Kukiendeleza kituo cha kuendeleza kampuni changa za TEHAMA (ICT startups) cha Dar es Salaam (Soft Centre) na kujenga vituo viwili (2) vya Kanda vya kutengeneza bidhaa za TEHAMA;
iii) Kuanzisha Vituo vya Ubunifu na Atamizi TEHAMA katika Wilaya mbili (2) nchini;
iv) Kutengeneza mfumo jumuishi utakaounganisha usajili na uendelezaji wa wataalam na wabunifu TEHAMA nchini (ICT human capital development system); na
v) Kuwezesha shughuli za ufuatiliaji na tathmini ya Mradi.

**V: Mradi wa Upanuzi wa Usikivu kwa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)**

**135**. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Upanuzi wa Usikivu kwa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) unalenga kuboresha upanuzi wa usikivu wa Shirika Nchi nzima. Kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 13,136,500,000** kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo.

i. Upanuzi wa Usikivu redio za TBC kwenye maeneo yasiyokuwa na ausikivu nchini;
ii. Ukarabati wa ofisi, ununuzi wa Mitambo na vifaa vya utangazaji vya Chaneli ya Tanzania Safari;
iii. Kuimarisha muonekano wa Televisheni kwa kuongeza ung'aavu wa picha (improvement of Television Channels Outlook);
iv. Kuwezesha ununuzi na ufungaji wa mfumo wa kupokea na kuchanganya picha studio na matukio ya nje (Tricaster System, CG and Monitoring);
v. Ujenzi jengo la Makao Makuu ya TBC Dodoma na ukarabati wa majengo ya Ofisi yaliyopo;
vi. Kuwezesha ununuzi wa Magari ya kurushia matangazo mubashara ya Redio (TBCTaifa naTBCFM) na Televisheni

(TBC1, TB2 na TBConline) na pia Magari kwa ajili ya Shughuli nyingine za Utangazaji;

vii. Kuwezesha ununuzi wa vifaa 18 vya kurushia Matangazo mubashara ya Redio nje ya studio;

viii. Ununuzi wa mitambo 10 na vifaa vya kurushia matangazo mubashara ya Televisheni (TBC1, TBC2 na Ofisi za Kanda);

ix. Ukarabati, uhifadhi, uhamishaji na uboreshaji wa studio za Ukombozi wa Nchi Kusini mwa Afrika katika jengo la utangazaji Barabara ya Nyerere kwa ajili ya Makumbusho ya maktaba ya picha na sauti;

x. Ufungaji wa mifumo ya uhariri, upokeaji na urushaji wa Matangazo kupitia mifumo ya TEHAMA (Robotic Intergrated News system with international news Monitoring); na xi. Kuwezesha ununuzi wa mitambo na vifaa kwa ajili ya TBC Mtandaoni na televisheni ya Kiingereza ya *online*.

**VI: Mradi wa Kufunga Mtambo Mpya wa Kisasa wa Uchapaji**

**136**. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu unalenga kuwezesha Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) kufunga mtambo mpya na wa kisasa wa uchapaji ambao utakuwa ni chanzo kikubwa cha mapato ya Kampuni. Mtambo huu unatarajiwa kuboresha mwonekano wa magazeti ya Serikali na hivyo kuvutia wasomaji na watangazaji na pia kufanya uchapaji wa kibiashara kwa bidhaa mbalimbali chapishi kwa wateja wa ndani na nje ya nchi. Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara inakadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 9,400,940,000** fedha za ndani kwa ajili ya kuwezesha ufungaji wa mitambo tajwa**.**

**VII: Mradi wa Habari kwa Umma**

**137**. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu unalenga kukusanya, kuchakata, kuandaa na kusambaza habari na taarifa kwa wananchi kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa shughuli za Serikali ikiwemo Sera, Mikakati, Miradi na Programu zinazotekelezwa na Serikali. Vilevile, mradi unakusanya taarifa za mrejesho kutoka kwa wananchi kwa lengo la

kupata maoni ya wananchi katika utekelezaji wa majukumu yake. Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara inakadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 940,940,000** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza mradi huu.

**Mipango ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

**138**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/23, taasisi zilizo chini ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari zimekadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 469,027,236,767** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali. Mchanganuo wa makusanyo na shughuli zitakazotekelezwa na kila taasisi ni kama ifuatavyo:

**Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA**)

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inakadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 155,897,258,292.00** ambazo zitatokana na vyanzo mbalimbali ikiwemo ada za leseni, ada za matumizi ya masafa, mrabaha (asilimia 1 ya pato ghafi ya watoa huduma za mawasiliano), ada za usimikaji na ukarabati wa mitambo ya mawasiliano, ada za uingizaji na usambazaji wa vifaa vya TEHAMA na makusanyo yatokanayo na mtambo wa TTMS.

**140.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

i) Kuendelea kuwapa wafanyakazi wa TCRA mafunzo endelevu ili kukuza uwezo wao kwa utekelezaji wa kazi za udhibiti;
ii) Kuimarisha ukusanyaji wa mapato kwa kufanya ukaguzi wa ufuatiliaji na kuhakikisha kuwa huduma za mawasiliano zinatolewa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na kwa kuzingatia masharti ya leseni;
iii) Kuimarisha usimamizi wa Mfumo wa utoaji leseni na rasilimali za mawasiliano;

iv) Kutoa elimu kwa watumiaji na wadau wengine wa huduma za mawasiliano ili kuongeza uelewa juu ya haki na wajibu wao;
v) Utekelezaji wa Miundombinu ya Kitaifa ya Mawasiliano ya Mtandao wa Umma (NPKI) ili kuhakikisha usalama wa miamala ya kielektroniki inayofanyika nchini;
vi) Kukamilisha ujenzi wa Jengo la Ofisi za PAPU na ofisi za Kanda ya Kaskazini ya TCRA (TCRA – PAPU House) na kuanza ujenzi wa ofisi ya TCRA Makao Makuu – Dodoma;
vii) Kujenga Maabara ya kukagua na kuhakiki viwango vya vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki nchini;
viii) Kuendelea kuimarisha Mifumo ya ndani ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi;
ix) Kufuatilia, kujibu na kuripoti matukio ya usalama wa kompyuta ili kupunguza mashambulizi ya kimtandao;
x) Usimamizi wa kanzidata ya Usajili ya CEIR na namba za SIM (Management of CEIR and SIM Card Registration Database)
xi) Kuendelea kusimamia Mfumo wa Uhakiki wa Mapato ya Mawasiliano ya Simu (TRAS), mfumo uliobuniwa na kutekelezwa chini ya mradi wa (TTMS) kuwezesha ukusanyaji wa takwimu za huduma za mawasiliano zinazotolewa kwa wateja na watoa huduma za mawasiliano. Mfumo huu umewezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuhakiki usahihi wa mapato unaolenga kuisaidia Serikali kuthibitisha mapato yaliyotangazwa na watoa huduma;
xii) Kufuatilia na kudhibiti gharama za huduma zinazotolewa na watoa huduma ili kulinda maslahi ya watumiaji (Billing verification system);
xiii) Kuendelea kusimamia ubora wa huduma za mawasiliano ili kutoa huduma za udhibiti kwa usahihi zaidi;
xiv) Kudhibiti ulaghai katika mitandao ya mawasiliano ili kuhakikisha upatikanaji wa mapato ya Serikali kutoka

kwa miamala ya simu za kutoka nje ya nchi (*International Incoming traffic*).

**Shirika la Posta Tanzania (TPC)**

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Shirika linatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 40,943,300,000** kutokana na biashara za usafirishaji wa barua na vipeto, usafirishaji wa nyaraka kwa njia ya haraka (EMS), fedha na uwakala, biashara mtandao pamoja na miliki.

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Shirika limepanga kutekeleza mambo yafuatayo:

i. Kuimarisha miundombinu na mifumo ya TEHAMA sambamba na kuboresha miundombinu ya mtandao wa eneo mahsusi (Local Area Network – LAN) katika Ofisi za Posta 40 ili kukuza matumizi ya TEHAMA na kuboresha utoaji wa huduma za posta zinazokidhi matakwa ya walaji;
ii. Kukarabati na kubadilisha mwonekano wa majengo sita (6) ya ofisi za Posta za Mtaa wa Libya, Sokoine, Meru, Pamba Road, Makambako na Mpwapwa;
iii. Kuanzisha Ofisi ya kubadilishana barua, vifurushi na vipeto kimataifa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere;
iv. Kutengeneza programu tumizi (Mobile application) ya duka mtandao la Posta;
v. Kuanza kutumia ramani ya kidijitali (Postal Digital Map) kwa ajili ya kuboresha ufikishaji wa huduma za Posta kwa wananchi kwa kupitia Mfumo wa Anwani za Makazi; na
vi. Kuendelea kusimamia vituo vya Huduma Pamoja vilivyopo ndani ya Shirika la Posta Tanzania.

**Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL)**

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Shirika linatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 202,851,880,319** kutokana na huduma za Shirika ambazo ni simu, data na kupangisha maeneo kwa ajili ya vyombo vya mawasiliano.

**144.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Shirika la Mawasiliano Tanzania limepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

i) Kuboresha mbinu za kuuza na kusambaza muda wa maongezi na kuhakikisha huduma za muda wa maongezi zinawafikia watumiaji wa mtandao wa TTCL katika ngazi zote;

ii) Kuendelea kuendesha kampuni tanzu ya TTCL Pesa (T-PESA) kwa kutekeleza yafuatayo;

a) Kuongeza idadi ya mawakala wa T-PESA kutoka **14,399** walisajiliwa (biometric registered) Mwezi Aprili, 2022 hadi kufikia mawakala **18,000** ifikapo Mwezi Juni, 2023;

b) Kuongeza wigo wa watumiaji wa T-PESA kutoka watumiaji **1,383,284** wa Mwezi Aprili 2022 hadi watumiaji **1,500,000** ifikapo Mwezi Juni, 2023; na

c) Kutanua wigo wa uwakala wa kuuza muda wa maongezi, matumizi ya N-CARD na huduma za tiketi mtandao kwa kushirikiana na wadau.

iii) Shirika la Mawasiliano Tanzania linaendelea na mpango mahususi wa Kuboresha mtandao wa 2G kwenda 4G ili Kuongeza wigo na matumizi ya mawasiliano ya intaneti ya kasi (broadband), kuweza kuongeza watumiaji wa intaneti pia kuongeza matumizi ya TEHAMA;

iv) Kuendelea kujenga, kusimamia na kuendesha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (NICTBB) na Kituo cha Taifa cha Kutunza Data (NIDC);

v) Kuendelea na uboreshaji wa makusanyo ya mapato na madeni ya Shirika yatokanayo na huduma ya wateja;

vi) Kuongeza idadi ya wateja kufikia 2,918,785 watumiao huduma za simu za kiganjani na zile za mezani.

vii) Kuboresha usambazaji wa vocha kwa kuongeza idadi ya mawakala kutoka 7,501 hadi kufikia 8,250 sawa na ongezeko la asilimia 10 kwa mwaka.

viii) Ujenzi wa kilomita 5,000 za mkongo kwenda kwa watumiaji (Milestone).

**Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC)**

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Shirika la Utangazaji Tanzania linakadiria kukusanya **Shilingi 42,842,649,000** ambapo Shilingi **15,809,165,000** ni makusanyo ya ndani na **Shilingi 27,033,484,000** ni kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Vyanzo vya mapato ya ndani ni pamoja na matangazo ya biashara, udhamini wa vipindi na matangazo mubashara kupitia vyombo vyake vya redio, runinga na mitandao ya kijamii.

**146.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TBC imepanga kutekeleza miradi ya upanuzi wa usikivu kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 ikiwa ni pamoja na ununuzi wa mitambo na vifaa vya utangazaji vya redio, runinga na mitandao ya kijamii. Miradi hiyo ni pamoja na:

(i) Upanuzi wa usikivu kwa kufunga mitambo ya masafa ya FM katika Wilaya (14) nchini: Kalambo (Rukwa), Kiteto (Manyara), Chunya (Mbeya), Liwale (Lindi), Rufiji (Pwani), Babati (Manyara), Chemba (Dodoma), Kakonko (Kigoma), Mufindi (Iringa), Itigi (Singida), Igunga (Tabora), Rombo (Kilimanjaro), Kongwa (Dodoma) na Kilindi (Tanga);

(ii) Ujenzi wa Makao Makuu ya TBC eneo la Vikonje jijini Dodoma;

(iii) Ununuzi wa Magari ishirini (20) kwa ajili ya shughuli za Utangazaji;

(iv) Ununuzi na ufungaji wa mfumo wa kupokea na kuchanganya picha studio na matukio ya nje (Tricaster System, CG and Monitoring);

(v) Ununuzi wa Magari mawili (2) ya kurushia matangazo mubashara – Redio: TBCTaifa, TBCFM;

(vi) Ununuzi wa Magari maalumu matatu (3) ya kurushia matangazo Mubashara – Televisheni: TBC1, TB2 na TBConline;

(vii) Ununuzi wa vifaa 18 vya kurushia Matangazo mubashara ya Redio nje ya studio;

(viii) Ununuzi wa mitambo na vifaa vya kurushia matangazo mubashara ya Televisheni (TBC1, TBC2 na Ofisi za Kanda);
(ix) Ukarabati, uhifadhi, uhamishaji na uboreshaji wa studio za Ukombozi wa Nchi Kusini Mwa Afrika katika jengo la utangazaji Barabara ya Nyerere kwa ajili ya Makumbusho ya maktaba ya picha na Sauti;
(x) Ufungaji wa Mitambo ya redio na TEHAMA katika studio za redio Barabara ya Nyerere pamoja na jengo la TBC2 awamu ya pili;
(xi) Ufungaji wa mifumo ya uhariri, upokeaji na urushaji wa Matangazo kupitia mifumo ya TEHAMA (Robotic Intergrated News System with international news monitoring feature); na
(xii) Ununuzi wa mitambo na vifaa kwa ajili ya TBC Mtandaoni na televisheni ya Kiingereza ya online.

**Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN)**
**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 16,506,945,000.00** kutokana na mauzo ya bidhaa na huduma zake za mauzo ya matangazo, nakala za magazeti, uchapaji kibiashara, kodi za pango na ushauri wa kimedia.

**148.** ***Mheshimiwa Spika*** Kampuni ya Magazeti ya Serikali imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo katika Mwaka wa Fedha 2022/23:

i. Kufunga mitambo mipya na ya kisasa ya uchapaji kibiashara;
ii. Kuongeza ubora wa bidhaa na huduma za kihabari zinazotolewa na Kampuni kwa Kurudisha uchapaji wa magazeti wenye tija na kuongeza maudhui ya ndani kufikia asilimia 80 ya maudhui yote;
iii. Kuboresha mauzo na ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa madeni ili kuongeza ukwasi wa Kampuni kwa asilimia 10;

iv. Kuboresha na kuongeza maudhui ya habari mitandaoni ili kuongeza idadi ya wasomaji/ wafuatiliaji wa habari za Kampuni mtandaoni kwa asilimia 20;
v. Kuongeza mauzo ya gazeti mtandao kwa asilimia 10;
vi. Kuanzisha studio ya kisasa (Multimedia Digital Studio) jijini Dar es Salaam;
vii. Kuongeza ufanisi wa rasilimali watu kwa kuimarisha na kuboresha mifumo na mazingira ya kazi kwa kuwapatia watumishi wasiopungua 50 mafunzo ya muda mfupi na mrefu na kununua vitendea kazi yakiwemo magari 15;
viii. Kuanza utekelezaji wa miradi ya Elimu ya Uraia na Matumizi Bora na Sahihi ya TEHAMA;
ix. Kuimarisha ushirikiano na wadau wa ndani na nje ya nchi vikiwemo vyombo vingine vya habari, Balozi na Taasisi za Kimataifa na kutia saini Mikataba ya Ushirikiano wa hiyari isiyopungua 5; na
x. Kuboresha mwonekano wa majengo ya Kampuni kwa kukarabati nyumba zake za Samora jijini Dar es Salaam na Chinangali na Makole jijini Dodoma.

**Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)**

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) unatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 34,760,583,156** kutoka katika vyanzo vyake vya mapato, ambavyo ni Tozo ya huduma na tengeo toka TCRA.

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) umepanga kutekeleza yafuatayo:

i) Kuendelea kutathmini mahitaji ya huduma za mawasiliano katika maeneo yasiyo na mvuto kibiashara nchini kwa lengo la kuyajumuisha katika miradi inayotekelezwa na Mfuko;
ii) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya kufikisha huduma za mawasiliano katika Kata 1,223 ili kuona

huduma iliyokusudiwa inawafikia wananchi katika viwango vinavyokubalika;

iii) Kufikisha huduma za mawasiliano ya simu katika maeneo 150 yasiyo na huduma za mawasiliano kupitia fedha za Benki ya Dunia;
iv) Kuboresha teknolojia ya mawasiliano ya simu katika maeneo 150 kutoka "2G" kwenda "3G/4G" kupitia fedha za Mkopo kutoka Benki ya Dunia;
v) Kufikisha huduma za mawasiliano katika maeneo maalum 89;
vi) Kuunganisha shule 150 za umma kwenye mtandao wa intaneti na kuzipatia vifaa vya TEHAMA;
vii) Kupeleka vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa shule tano (5);
viii) Kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa Walimu 650 wa shule za umma;
ix) Kuboresha matangazo ya TBC Redio katika maeneo matatu (3) ya mipakani;
x) Kufunga intaneti kwa matumizi ya umma katika maeneo matano (5) ya wazi; na
xi) Kuboresha usikivu wa redio jamii katika maeneo manne (4).

**Tume ya TEHAMA (ICTC)**

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Tume ya TEHAMA inatarajia kutumia kiasi cha **Shilingi 5,468,105,000,** ambapo **Shilingi 3,922,897,000** ni mgao wa Serikali na **Shilingi 1,545,208,000** ni vyanzo vya ndani na wadau wa maendeleo.

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Tume ya TEHAMA imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

i) Kujenga kituo cha Kitaifa cha kuendeleza wataalam, tafiti na bunifu za TEHAMA;
ii) Kuanzisha kituo kimoja cha ubunifu TEHAMA (Softcentre) Zanzibar, Vituo vinne vya Kanda katika majiji ya Arusha,

Dodoma, Mwanza na Mbeya; na kuendeleza kituo cha Dar es Salaam kwa ajili ya kuendeleza kampuni changa za TEHAMA ili kukuza kiwango cha uzalishaji wa bidhaa za TEHAMA, kuongeza ajira na kukuza uchumi wa nchi;

iii) Kuanzisha kituo cha kutengeneza na kuboresha vifaa vya TEHAMA *(*ICT refurbishment and assembly centre*)*;

iv) Kuwezesha uanzishaji wa vituo vya majaribio vya ubunifu TEHAMA *(*District ICT Innovation hubs*)* katika Wilaya mbili (2) nchini;

v) Kuwezesha mafunzo maalum ya TEHAMA kwa watu 500 ili kukuza na kuendeleza ujuzi wa TEHAMA nchini, utengenezaji wa vitabu 50 vya kidijitali vya shule za sekondari;

vi) Kuhamasisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kufundishia na kujifunzia kwa Vyuo Vikuu vitatu (3) na kuzifikishia Shule 10 za Sekondari mfumo wa TEHAMA wa kufundishia, kujifunzia na wazazi kufuatilia maendeleo ya watoto shuleni (Schoolaby);

vii) Kuwezesha mijadala miwili (2) ya wadau kutoka sekta ya Umma na binafsi inayohusu maboresho ya sheria katika sekta ya TEHAMA na kuvutia uwekezaji ili kuharakisha ukuaji wa sekta kwa kuihusisha sekta binafsi;

viii) Kutengeneza mfumo jumuishi utakaounganisha usajili na uendelezaji wa wataalam na wabunifu TEHAMA nchini (ICT Human Capital Development System)*;* ix) Kuendelea kusajili wataalam wa TEHAMA kufikia Wataalam 1,600 na kuandaa Mkutano wa Mwaka wa TEHAMA (TAIC); na

x) Kuandaa Tuzo ya Mwaka ya TEHAMA Tanzania *(*Tanzania ICT Award*)*.

**Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA – CCC)**

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA - CCC) linatarajia kupokea kiasi cha **Shilingi 710,000,000** kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

**154. *Mheshimiwa Spika,*** Shughuli zilizopangwa kutekelezwa na Baraza ni kama ifuatavyo:-

i) Kuanzisha Kamati za watumiaji katika Mikoa ya Simiyu, Pwani na Ruvuma;
ii) Kujengea uwezo Kamati za watumiaji katika Mikoa ya Mjini Magharibi, Kusini Pemba, Tanga, Lindi na Mtwara ili kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yao;
iii) Kuziwezesha Kamati za Watumiaji katika Mikoa 18 kwa kuzipatia vitendea kazi kwa ajili ya kutekeleza majukumu;
iv) Kuimarisha mifumo ya mawasiliano ya kidijitali ili kuboresha utendaji kazi wa Baraza na kuimarisha mawasiliano na watumiaji;
v) Kufanya mashauriano na wadau wa sekta kwa lengo la kutatua changamoto za watumiaji na kuboresha huduma;
vi) Kuandaa na kutoa elimu, uhamasishaji na kupokea maoni ya watumiaji kupitia redio, runinga, mitandao ya kijamii, Maadhimisho ya Wiki ya Mtumiaji, maonesho na matukio ya Kitaifa ili kuongeza uelewa wa watumiaji; na
vii) Kushiriki katika Mikutano na mashauriano na TCRA, Watoa huduma na Mabaraza mengine ya Watumiaji.

## D. SHUKRANI

**155. *Mheshimiwa Spika,*** kwa moyo wa dhati ninapenda kuwashukuru wale wote walioshiriki kunisaidia kutekeleza majukumu yangu katika Wizara hii. Kipekee niwashukuru Mheshimiwa **Mhandisi Kundo Andrea Mathew (Mb.),** Naibu Waziri; **Dkt. Jim Yonazi,** Katibu Mkuu na, **Mohammed Khamis** Naibu Katibu Mkuu. Aidha, nawashukuru Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo katika Wizara yangu, Wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi za Taasisi zilizo chini ya Wizara; Viongozi wa Taasisi na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi kwa kufanya kazi kwa bidii kuhakikisha kuwa Wizara yetu inakuwa chachu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kupitia Habari na TEHAMA.

**156. *Mheshimiwa Spika,*** naomba nichukue fursa hii kwa upekee niweze kuwashukuru Washirika wa Maendeleo ambao Serikali imekuwa ikishirikiana nao katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo zinazohusiana na Sekta za Habari na Mawasiliano. Washirika hao ni: Shirika la Umoja wa Mataifa la Mawasiliano (ITU); Shirika la Umoja wa Posta Duniani (UPU); Shirika la Umoja wa Posta Afrika (PAPU); Benki ya Dunia (WB) kupitia dirisha la Wakala wa Maendeleo ya Kimataifa (IDA), Ubalozi wa China nchini na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD).

**157. *Mheshimiwa Spika,*** ningependa kuchukua fursa hii kuzishukuru Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kwa ushirikiano katika masuala ya Kikanda yanayohusu Sekta hii. Kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/23, Wizara yangu itaendelea kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo na wadau wengine ili kuhakikisha kuwa Sekta ya Mawasiliano inachangia katika kutimiza Dira ya Taifa ya kufikia Uchumi wa Kati wa Juu ifikapo Mwaka 2025.

## E. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2022/23

**158**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2022/23, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 282,056,786,000.00** kwa mchanganuo ufuatao:-

i) Kiasi cha **Shilingi 26,279,346,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 17,249,317,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 9,030,029,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.
ii) Kiasi cha **Shilingi 255,777,440,000.00** kinaombwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambapo

**Shilingi 215,777,440,000.00** ni Fedha za Ndani na **Shilingi 40,000,000,000.00** ni Fedha za Nje.

**159.** ***Mheshimiwa Spika***, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni http://www.mawasiliano.go.tz.

**160.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, hoja imetolewa na imeungwa mkono sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Miundombinu ambae kwa niaba yake namuona Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA - MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchache wa muda naomba taarifa yote iingie kwenye *Hansard* kama ilivyowasilishwa mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka Fedha wa 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2022/ 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusoma taarifa hii kwa muhtasari lakini taarifa yote iingie kwenye Taarifa Rasmi za Majadiliano ya Bunge kwa kumbukumbuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulijulisha Bunge kuwa taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya Kwanza ni maelezo ya jumla kuonesha msingi, muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi. Sehemu ya Pili ni uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti, makusanyo ya maduhuli, upatikanaji wa fedha za bajeti ya kawaida, miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri wa Kamati Bungeni. Sehemu ya Tatu makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Sehemu ya Nne inayohusu majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati. Sehemu ya Tano inahitimisha na kulishauri Bunge kuhusu hoja iliyowasilisha na Waziri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotembelewa na Kamati. Mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Shirika la Mawasiliano Tanzania, kukamilika kwa mradi huu kutafanikisha lengo la kufikisha mawasiliano ya kasi kwa wananchi, Kamati imebaini kuna changamoto ya uendeshaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, watoa huduma binafsi wa mawasiliano wasiruhusiwe kumiliki Mkongo wa Mawasiliano ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha kufikia Februari 2022. Kwa mujibu wa taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 247.4 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, hadi Mwezi Februari, 2022 shilingi bilioni 81. 2 sawa na asilimia 32.8 zilipatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa hizo unaonyesha kwamba kwa ujumla upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo siyo wa kiwango kizuri, hali hii inaweza kuathiri lengo la miradi iliyopangwa kutekelezwa na kufikisha manufaa yaliyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa utekelezaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka 2021/2022. Kamati ilifuatilia utekelezaji na kuchambua taarifa za utekelezaji, matokeo ya uchambuzi huo yameonesha kwamba baadhi ya malengo yaliyopangwa hayakukamilika katika utekelezaji na mengine yametekelezwa ilivyostahili. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara ililenga kukamilisha ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano kiasi cha KM 1,880 lengo hili halikukamilika na linahitaji kuendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi, Kamati ilichambua Makadirio ya Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ikilinganishwa na utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Aidha, Malengo ya Mpango wa Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ikilinganishwa na utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2021/2022, ni miongoni mwa vigezo vilivyotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara na taasisi zake imelenga kukusanya mapato ya shilingi bilioni 682.651 Sawa na asilimia 41.3 ya bajeti yake ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa licha ya Wizara kushindwa kufikia lengo la ukusanyaji hadi mwezi Februari, 2022, kwani ilikusanya asilimia 5.5 ya lengo, taarifa zinaonesha kuwa bado imelenga kukusanya kiasi ambacho ni sawa na asilimia 33.7 ya lengo la mwaka 2021/2022. Kwa kuwa vyanzo ni vile vile vya mwaka wa fedha 2021/2022, lengo linalowekwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 linaweza kukosa uhalisia na lisitekelezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wa mpango na Bajeti ya Wizara hii, Kamati ilizingatia umuhimu wa malengo makuu ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Miongoni mwa malengo hayo ni ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, uboreshaji wa usikivu wa TBC na uendelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi. Matokeo ya uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya shilingi bilioni 255.777 zinaombwa kwa ajili ya kugharimia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa maoni na ushauri unaotokana na uchanganuzi uliofanyika. Katika maoni, Kamati inaonesha maelezo kuhusu mtazamo wake juu ya mambo yaliyojitokeza katika uchambuzi. Kwa kuzingatia mtazamo huo pamoja na hali halisi inayolinganishwa na matarajio ya wananchi, Kamati inatoa ushauri wa kuzingatiwa katika utekelezaji wa Bajeti ya sekta hii kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi uliofanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 117 ya Kanuni za Bunge, umeipa Kamati nafasi ya kutoa maoni ambayo ni mtazamo unaotokana na taarifa zilizowasilishwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi wa maoni yaliyobainishwa awali, Kamati inatoa ushauri kuwa Serikali iendelee kuwekeza fedha za maendeleo kwenye Shirika la Utangazaji Tanzania, Kampuni ya Magazeti ya Serikali na Idara ya Habari na Maelezo. Aidha, Serikali ione namna ya kupandisha makusanyo kwenye baadhi ya taasisi zilizo chini yake ambazo zimekusanya mapato chini ya asilimia 50. Mfano wa taasisi hizo ni *TTCL, UCSAF* na *TBC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri, Serikali ihakikishe taasisi zote zinazopata huduma kutoka TTCL zilipie huduma na madeni kwa wakati na Serikali iisaidie TTCL kujiendesha kibiashara ili kusaidia kukuza uchumi wa nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri;Serikali kupitia UCSAF iisimamie TTCL na Halotel kumaliza miradi yao kwa wakati. UCSAF ipewe fedha za kutosha ili iweze kutekeleza miradi yake ili huduma iweze kufika maeneo mengi zaidi hasa mipakani. Kamati inashauri fedha inayopatikana kutoka kwa mtoa huduma (CSR) irudi kwa UCSAF na kuendeleza utekelezaji wa miradi mingine; na minara yote ambayo Serikali imewekeza fedha ni vyema iwekwe nembo ya mfuko. Aidha, wananchi wana jukumu la kulinda minara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, Kamati inashauri Serikali ikae kwa pamoja na TTCL ili wajadili namna ya kuendesha Mkongo wa Taifa na kuiachia TTCL uendeshaji wa Mkongo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Anwani za Makazi na Postikodi Kamati inashauri, Serikali itoe fedha za kutosha za kufanikisha mradi na iwaunganishe wadau wote muhimu katika Wizara ili kufanikisha mradi huu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Posta – TPC, Kamati inashauri, Shirika la Posta Tanzania lipewe mtaji wa kutosha ili liweze kujiendesha kibiashara na kuhimili ushindani; Shirika la Posta liwezeshwe kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za kifedha; Serikali ilisimamie Shirika liweze kulipwa pesa kutoka kwa watoa huduma za kusafirisha mizigo kama mabasi, malori na kadhalika; na Shirika lisaidiwe kulipa na kulipwa madeni kwani limeendelea kuelemewa na deni la Shilingi bilioni 26.8 ambazo asilimia kubwa ni madeni ya taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu TBC na TSN, Kamati inashauri, Serikali iwekeze fedha za kutosha ikiwemo ruzuku ili kuisaidia TBC na TSN; Serikali ihakikishe TBC na TSN zinapata watumishi wa kutosha na kuboresha maslahi yao ili kuepusha kuacha kazi au kuhamia kwenye taasisi nyingine; Serikali itoe fedha kwa wakati kwa TBC na ihakikishe inapata gari la matangazo kwa kila Mkoa; TBC na TSN zijiendeshe kibiashara kwa kuanzisha miradi ya maendeleo; Serikali ihakikishe taasisi zake zinalipa madeni ya mashirika haya mfano, deni la TSN limefikia Shilingi bilioni 11. Serikali ihakikishe StarTimes inaendelea kutoa gawio kwa TBC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, uwekezaji katika sekta ya mawasiliano ni chachu kubwa ya maendeleo ya uchumi na kijamii kama ilivyo katika uwekezaji wa huduma nyingine. Hivyo ni muhimu Serikali kuhakikisha sekta hii inastawi na inachangia kwa kiwango kikubwa zaidi maendeleo ya uchumi wa nchi kama inavyoeleza katika ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kuiwezesha Kamati hii kutimiza majukumu yake. Namshukuru Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Mbunge na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Eng. Andrea Mathew Kundo, Mbunge na Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kuipa Kamati ushirikiano stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kumwezesha Waziri na Naibu Waziri kutoa ushirikiano kwa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge - Ndugu Nenelwa Joyce Mwihambi kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Aidha, shukrani maalumu ziende kwa Mkurugenzi wa Kamati za Bunge - Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi - Ndugu Gerald Singano Magili pamoja na Makatibu wa Kamati; Ndugu Janeth Julian Malangu, Ndugu Victory Eliackim Mrema na Msaidizi wa Kamati Ndugu Grace Samwel Gwivaha pamoja na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao ulioiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango waliyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti pamoja na kuandaa taarifa hii. Kutokana na muda sitawataja majina yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha

2022/2023 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA HABARI MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2021/2022; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2022/2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### SEHEMU YA KWANZA

### *1.0 MAELEZO YA JUMLA*

***Utangulizi***

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2022/ 2023.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kufuatilia mtiririko wa uwasilishaji wangu, naomba kulijulisha Bunge kuwa Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu zifuatazo:-

a) Sehemu ya **Kwanza** inayotoa maelezo ya jumla kuonesha msingi, muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

b) Sehemu ya **Pili** inayoripoti uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa kuangalia makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Bajeti ya kawaida, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri wa Kamati Bungeni;

c) Sehemu ya **Tatu** inayoripoti uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023;

d) Sehemu ya **Nne** inayohusu majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati; na

e) Sehemu ya **Tano** na ya mwisho inahitimisha na kulishauri Bunge kuhusu hoja ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

### *1.0 Msingi wa Uchambuzi wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** msingi wa Kamati kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ni Masharti ya Kanuni za Bunge. Kifungu cha 6(8) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 117(4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yaliyotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Wizara hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa na kwamba, naliomba Bunge hili lijadili hoja ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa pamoja na Taarifa hii.

### *1.2.1 Mawanda ya Uchambuzi*

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, inagusa taasisi nane

zilizokasimiwa katika Fungu 68. Naomba kulijulisha Bunge kwamba, Kamati ilichambua taarifa za Wizara na taasisi zake tarehe 23 – 24 Machi, 2022, taasisi hizo ni:-

i) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania - TCRA;
ii) Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano Tanzania - TCRA – CCC;
iii) Shirika la Mawasiliano Tanzania - TTCL;
iv) Tume ya Taifa ya TEHAMA - ICTC;
v) Shirika la Posta Tanzania - TPC;
vi) Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote - UCSAF;
vii) Shirika la Utangazaji Tanzania - TBC; na
viii) Kampuni ya Magazeti ya Tanzania - TSN.

### *1.2.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo*

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na taarifa hizo, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Bunge, na kutembelea miradi mitatu (3) iliyotengewa fedha kwenye bajeti ya maendeleo, miradi hiyo ni:-

(a) Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (Mradi Na.4283);
(b) Mradi wa Uwekaji wa Anwani za Makazi na Postikodi (Mradi Na. Na. 4234); na
(c) Mradi wa Tanzania ya Kidigitali (Na. 4280).

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya ukaguzi wa miradi hiyo yanafafanuliwa kama ifuatavyo:-

### *1.2.3 Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (Mradi Na.4283)*

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 16 Machi 2022, Kamati ilitembelea mradi huu na kupata taarifa zinazohusu mradi. Miongoni mwa shughuli hizo ni ujenzi wa kilomita **1880** za Mkongo wa Taifa na ujenzi wa vituo vipya **17** vya kutolea huduma za

Mkongo. Taarifa za Wizara zimeonesha kuwa hadi Kamati ilipokagua na kuchambua taarifa za utekelezaji, jumla ya kilomita **409** sawa na asilimia **21.8** ya lengo zilijengwa. Aidha, kazi ya ujenzi wa vituo vipya **17** haijakamilika tofauti na ilivyotarajiwa. Kwa taarifa hizo Kamati imebaini yafuatayo:-

(a) Kasi ndogo ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa ikilinganishwa na lengo kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Hata hivyo, hatua za Wizara kuingia mkataba wa maelewano na Shirika la Umeme Tanzania kwa ajili ya kufanya kazi pamoja, zinaweza kuongeza ufanisi. Kwa mfano, mkataba huo utawezesha ujenzi wa kilomita **4,442** badala ya kilomita **1,880** zilizokuwa zimepangwa. Vilevile, vitajengwa vituo **37** vya kutolea huduma za mkongo badala ya vituo **17** vilivyokuwa vimepangwa awali;

(b) Upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa mradi hadi mwezi Februari, 2022 haukuwa wa matumaini. Kiasi cha fedha kilichopatikana ni asilimia **19.3** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa kipindi cha robo tatu ya muda wa utekelezaji; na

**Mheshimiwa Spika**, Ujenzi wa Mkongo wa Taifa ukikamilika utaendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) TTCL kudai madeni kwenye baadhi ya taasisi za Serikali ambazo huchelewa kulipa madeni yao kwa wakati, jambo linaloipunguzia uwezo katika uendeshaji wa Mkongo;

(ii) TTCL kushindwa kujiendesha kibiashara kutokana na kutokuwa na mtaji wa kutosha na hivyo kuchelewesha utekelezaji wa miradi;

(iii) TTCL kutokuwa na mamlaka ya kuumiliki Mkongo wa Taifa kutokana na Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kuendelea kuumiliki moja kwa moja, jambo linalosababisha mkanganyiko wa kiutendaji; na

(iv) Sheria ya manunuzi irekebishwe kwani inazuia TTCL kununua vifaa toka Kampuni nyingine inapouza mitambo yake pale inapofunga biashara hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kuna haja na umuhimu wa kutatua changamoto hizo ili kuongeza ufanisi katika uendeshaji na usimamizi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kuongeza mchango wa Sekta ya Mawasiliano kwenye Pato la Taifa na matumizi ya TEHAMA kama inavyoeleza kwenye Ilani *ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020,* katika aya ya 60(d) ukurasa wa 98.

***1.2.4 Mradi wa Uwekaji wa Anwani za Makazi na Postikodi (Na. 4234)***

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulilenga kutoa Anwani za Makazi ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi, sambamba na kuwezesha biashara mtandao. Matokeo ya ukaguzi na uchambuzi wa taarifa yanabainisha kasi inayoridhisha ya utekelezaji wa mradi. Aidha, ilibainika kuwa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mradi huo umekuwa wa kuridhisha kadiri ilivyopangwa.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Februari, 2022, mradi ulipata fedha kiasi cha asilimia **91.7.** Kwa mujibu wa randama iliyotumika wakati wa uchambuzi, kiasi cha fedha ambacho kimewekwa katika utekelezaji ni asilimia **100**. Hali hii inaonesha kuwa upatikanaji wa fedha kwa mradi huu ni wa kuridhisha kwa kiwango kikubwa na matumizi kwa fedha zinazopokewa unaenda vizuri kama iliyotarajiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inaipongeza Serikali kwa kuwekeza fedha nyingi katika mradi huu.

### *1.2.5 Mradi wa Tanzania ya Kidigitali (Na. 4280)*

**Mheshimiwa Spika**, kusudio la mradi wa Tanzania ya Kidigitali ni kuleta mabadiliko ya kidigitali kwa kuunganisha Tanzania na nchi nyingine lengo la kukuza uchumi wa kidigitali. Hata hivyo, pamoja na umuhimu wa mradi huo kwa mustakabali wa Taifa na uchumi wake, fedha zote zilizoidhinshwa na Bunge zilitegemewa kutoka Benki ya Dunia. Hadi kufikia mwezi Februari, 2022, mradi huu ulipokea asilimia **25.4** tu ya bajeti ya mradi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa mradi huo. Naomba kulijulisha Bunge kwamba utekelezaji wa mradi ulichelewa kuanza. Kwa mujibu wa taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati, mkataba kati ya Serikali na Benki ya Dunia ulisainiwa tarehe 19 Agosti, 2021. Utekelezaji wa mkataba huo ulianza mwezi Novemba, 2021. Kwa hali hiyo, isingelikuwa rahisi kuanza kutekeleza mradi mapema. Aidha, taarifa zaidi za utekelezaji zilizoripotiwa zinaonesha kuwa mradi upo katika hatua za mwanzo kwani fedha iliyotumika ni asilimia **23.4**.

**Mheshimiwa Spika**, hali hiyo ya utekelezaji wa mradi imetokana na kutegemea fedha za nje, randama inaonesha kuwa Bajeti yote iliyoidhinishwa kwa mradi huu ni fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto nyingine katika mradi huu ni kasi ndogo ya utekelezaji kwa fedha zilizopatikana. Taarifa inaonesha kuwa hadi Mwezi Februari, 2022 ni asilimia **23** tu ya fedha iliyopatikana ndiyo iliyoingizwa kwenye utekelezaji. Hali hiyo inaashiria kasi ndogo ya kutekeleza shughuli zinazofanikisha Tanzania ya Kidigitali.

**Mheshimiwa Spika,** ni maoni ya Kamati kwamba, upatikanaji wa fedha usio na uhakika pamoja na kasi ndogo ya

utekelezaji wa mpango kazi kwa miradi ya maendeleo ni mambo yanayoweza kuathiri maendeleo ya nchi.

### *1.2.6 Mradi wa Habari kwa Umma (Na. 6567)*

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ni mahususi kwa ajili ya kuuhabarisha umma kuhusu mafanikio ya utendaji wa Serikali. Azma hiyo inasaidia kuwaweka wananchi katika nafasi nzuri ya kupima mafanikio yanayofikiwa na kulinganisha na matarajio waliyonayo. Kutokana na umuhimu huo, Kamati ilifuatilia hatua za utekelezaji wa mradi. Naomba kulijulisha Bunge kuwa taarifa za utekelezaji zilionesha kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2022 mradi huu ulipokea asilimia **55** ya fedha zilizopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaona kwamba kwa mwenendo huo zipo ishara kuwa wananchi hawataweza kufahamu utendaji wa Serikali yao.

### *1.2.7 Mradi wa Upanuzi wa Usikivu TBC (Na. 4279)*

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ni kwa ajili ya kuboresha usikivu wa TBC maeneo ya pembezoni na mipakani, ili kuwafanya wananchi wapate habari sahihi kwa maslahi ya Taifa lao. Pamoja na umuhimu huo, hadi kufikia mwezi Februari, 2022, Mradi huu haukupokea fedha yoyote kwa ajili ya utekelezaji. Hali hii inaashiria kuwa usikivu hafifu wa TBC katika maeneo ya nchi yaliyo mipakani na pembezoni utaendelea.

**Mheshimiwa Spika,** ni maoni ya Kamati kuwa, kuchelewa kutekeleza mradi huu ni kuendeleza athari za usikivu duni wa TBC kwa wananchi wanaoishi maeneo ya mipakani.

## *1.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na Kamati ni kama ifuatavyo*

**a) Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Shirika la Mawasiliano Tanzania**

i) Mradi huu ni muhimu katika kufikisha mawasiliano ya kasi kwa wananchi:-

ii) Kamati imebaini Kuna changamoto ya uendeshaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;

iii) Watoa huduma binafsi wa mawasiliano wasiruhusiwe kumiliki Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa.

**b) Mradi wa Uwekaji wa Anwani za Makazi na Postikodi** Kamati imebaini kuwa:-

i) Kukamilika kwa mradi huu utasaidia sana katika zoezi la Sensa ya Makazi itakayofanyika mwezi Agosti, 2022:-

ii) Zoezi hili bado linakabiliwa na changamoto kwa baadhi ya Mikoa katika utekelezaji wake;

iii) Changamoto ya utowepo kwa mfumo wa usajili na uhuwishaji wa Taarifa.

**c) Mradi wa upanuzi wa usikivu - TBC** na **TSN**

i) Mradi wa TBC ni muhimu sana kwa nchi katika kuboresha usikivu maeneo ya pembezoni na mipakani;
ii) Kuna upungufu wa fedha zinazopelekea kushindwa kujiendesha kibiashara;
iii) Kuna changamoto kubwa ya madeni ;
iv) Kuna uhaba wa upungufu wa watumishi;
v) Kuna tatizo kubwa la kutolipwa madeni kwa wakati; na
vi) Shirika la Star times halitoi gawio kwa TBC.

**d) Mradi wa Tanzania ya Kidigitali**

Mradi huu umechelewa kukamilika kutokana na sababu mbalimbali kama vile:-

i) Kutegemea fedha za nje zaidi katika utekelezaji; na
ii) Changamoto ya kuchelewa kutolewa kwa fedha hizo kunaathari utekelezaji wa mradi.

**SEHEMU YA PILI**

***2.0 UCHAMBUZI WA BAJETI***

***UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI PAMOJA NA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022***

**Mheshimiwa Spika**, katika Taarifa ya Kamati kuhusu uchambuzi wa Bajeti ya Mwaka 2021/2022 ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari **(Fungu 68),** Kamati ilitoa maoni ili kuboresha utendaji kazi wa Wizara na Serikali kwa ujumla. Kamati imepitia Taarifa ya utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati na kubaini kwa kiasi kikubwa Wizara imetekeleza Maoni, Ushauri na Mapendekezo hayo ya Kamati. Kwa maeneo ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu au utekelezaji wake unaendelea. Kamati inayasisitiza katika Taarifa hii likiwemo suala la TBC na TSN kuwezeshwa ili kuweza kujiendesha kibiashara.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti na Majukumu ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari **(Fungu 68)** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ulijikita katika maeneo makuu manne (4) ambayo ni:-

a) Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

b) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kuhusu ukusanyaji wa Maduhuli;

c) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kuhusu upatikanaji wa fedha; na

d) Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kwa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

### 2.1.1 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara

**Mheshimiwa Spika,** jukumu kuu la Wizara ni kusimamia, kuandaa na kuratibu masuala ya Habari, Mawasiliano Teknolojia ya Habari (TEHAMA) ili kuhakikisha kuwa TEHAMA inachangia kikamilifu katika maendeleo ya nchi yetu na pia kuhakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa za Serikali za utekelezaji wa Sera mipango na miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ina ilijiwekea vipaumbele kama vile:-

i) Kuandaa, kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera zinazohusu Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Posta na Mawasiliano ya Simu;
ii) Kuratibu na kusimamia vyombo vya Habari nchini;
iii) Kufanya tafiti, maendeleo na ubunifu kwenye TEHAMA;
iv) Kuendeleza wataalam wa TEHAMA;
v) Kuanzisha na kusimamia Postikodi;
vi) Kusimamia ujenzi na uendeshaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; na
vii) Ulinzi na usalama wa mtandao;

**Mheshimiwa Spika,** kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa malengo umekuwa na mafanikio kiasi kwani umefanikisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa Sekta hii katika Pato la Taifa, pia Wizara imefanikiwa kuendeleza ujenzi wa Mkongo Taifa wa Mawasiliano kwa kilomita 409 sawa na

asilimia 21.8 na miradi ya kufikisha mawasiliano vijini kwa kata 112 zenye vijiji 218. Sekta hii imejipanga kuongeza wigo wa matumizi ya mawasiliano ya kasi kutoka asilimia 45 kwa mwaka 2020 hadi asilimia 80 mwaka 2025.

**Mheshimiwa Spika,** mchango wa sekta ya Habari na Mawasiliano kwenye Pato la Taifa ni mkubwa kwani inaonyesha imeweza kuchangia kwa wastani wa asilimia **8.4** katika kipindi cha mwaka 2020/2021. Mwenendo huu wa mchango unatoa mwelekeo chanya kuwa Sekta ya Habari na Mawasiliano (Kama inavyoonesha katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Aya ya 61 (a-o)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatoa pongezi kwa Serikali na inasisitiza juhudi zaidi zinahitajika katika ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kuendelea na miradi ya kufikisha huduma za mawasiliano vijijini.

### *2.1.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2021/2022 kuhusu ukusanyaji wa Maduhuli*

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara hii kwa pamoja na taasisi zake, ilipaswa kukusanya jumla ya **Sh. 907,176,107,206.65.** Kati ya fedha hizo, **Sh. 446,484,017,206.65** sawa na asilimia 49.2 ya lengo la makusanyo ni kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, tozo ya kuongeza salio kwenye simu na mapato yanayokusanywa na Idara ya Habari Maelezo**. Sh. 460,692,089,984.65** sawa na asilimia **50.8** zilipangwa kukusanywa na taasisi saba za Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa zilionesha kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2022, kiasi kilichokusanywa ni **Sh. 376,541,865,079.51** sawa na asilimia **41.5** ya lengo la jumla la makusanyo kwa Wizara.
Mchanganuo wa makusanyo kwa Wizara na taasisi zake unaonekana katika jedwali Na.01 linahusu makusanyo ya taasisi na jedwali Na. 02 linalohusu ulinganisho wa makusanyo kutokana na vyanzo vya Wizara.

**Jedwali Na. 01 Kiasi cha Fedha Kilichokadiriwa Kukusanywa na Kiasi Kilichokusanywa kwa Mashirika/Taasisi kwa mwaka 2021/ 2022**

| NA | TAASISI | MAKADIRIO YA MAKUSANYO kwa 2021/2022 | % JUMLA KWA YA MAKADIRIO | MAKUSANYO HADI FEBRUARI, 2022 | % LENGO LA MAKUSANYO YA TAASISI | % JUMLA YA MAKUSA-NYO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (a) | (b) | (c) | (d) | (e) | (f) | (g) |
| 1. | TCRA | 150,067,415,286.65 | 32.6 | 119,269,301,118.82 | 79.48 | 33.89 |
| 2. | TTCL | 206,240,680,323.00 | 44.8 | 184,270,289,173 | 89.35 | 52.36 |
| 3. | ICTC | 1,148,105,000.00 | 0.2 | 881,885,434.41 | 76.81 | 0.25 |
| 4. | POSTA | 40,761,234,400.00 | 8.8 | 20,703,158,568 | 50.79 | 5.88 |
| 5. | UCSAF | 34,086,331,975.00 | 7.4 | 16,024,342,078 | 47.01 | 4.55 |
| 6. | TBC | 14,044,500,000.00 | 3.0 | 5,311,742,860.52 | 37.82 | 1.51 |
| 7. | TSN | 14,343,823,000.00 | 3.1 | 5,469,097,483 | 38.13 | 1.55 |
| | | **460,692,089,984.65** | | **351,929,816,715.75** | **76.39** | |

**Chanzo:** Randama ya Wizara

**Jedwali Na. 02: Ulinganisho wa Makusanyo kutokana na Vyanzo vya Wizara kwa mwaka 2021/2022**

| CHANZO CHA MAPATO | LENGO | MAKUSANYO HADI FEBRUARI | % LENGO |
|---|---|---|---|
| Mauzo ya Huduma za Mkongo wa Taifa | 50,000,000,000.00 | 19,453,656,271.76 | 38.9 |
| Tozo ya Kuongeza Salio kwenye Simu | 396,306,000,000.00 | 4,804,201,342.00 | 1.2 |
| Mauzo ya Picha, Vitambulisho, Machapisho na Ada ya mwaka ya magazeti | 178,017,222.00 | 354,190,750.00 | 199.0 |
| **JUMLA** | **446,484,017,222.00** | **24,612,048,363.76** | **5.5** |

**Chanzo:** Randama ya Wizara

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa makusanyo ya maduhuli unaonesha kwamba:-

i) Jumla ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Wizara na taasisi zake hadi kufikia mwezi Februari, 2022 ni asilimia **41.5** ya lengo. Makusanyo hayo yamepatikana ndani ya robo tatu (yaani asilima 75) za kipindi cha utekelezaji wa majukumu. Hali hiyo ni ishara ya kutofikia lengo lililowekwa;

ii) Makusanyo ya Wizara bila taasisi au mashirika yake yamepatikana kwa asilimia **5.5** ya lengo lake. Hii imetokana na kutokukusanywa kwa tozo ya kuongeza salio kwenye simu tofauti na ilivyotarajiwa;

iii) Makusanyo kutokana na Huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano yamekuwa kidogo ikilinganishwa na lengo. Chanzo hiki kimewezesha ukusanyaji wa asilimia **38.9** ya lengo. Kwa matokeo hayo, ni dhahiri kuwa kuna jambo la kufanyiwa kazi katika huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;

iv) Mwenendo wa ufikiaji lengo la makusanyo kwa TCRA na ICTC umevuka lengo kwa wastani wa makusanyo ya asilimia **89.35,** asilimia **79.48** na asilimia **76.81** mtawalia; na

v) Mwenendo wa ufikiaji lengo la makusanyo kwa Shirika la Posta, UCSAF, TBC na TSN yamekuwa chini ikilinganishwa na wastani wa makusanyo ya taasisi zote.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wake na kubaini kuwa wastani wa makusanyo ya mapato si mbaya kwa taasisi zilizo chini ya Wizara hii. Hata hivyo, Shirika la Posta, UCSAF, TBC na TSN zinaonekana kuwa na shida katika ukusanyaji wa mapato au uwekaji wa malengo ya makusanyo. Aidha, lengo la makusanyo kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano linahitaji

kuangaliwa vizuri sambamba na kuboresha ukusanyaji wa mapato yanayohusika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kuwa kuweka malengo yasiyofikiwa si jambo jema na athari yake si nzuri katika utekelezaji wa bajeti.

***2.1.3 Uchambuzi wa Upatikanaji wa Fedha kufikia Februari, 2022***

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara hii iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 247,400,781,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hadi mwezi Februari, 2022, **Sh. 81,257,893,336.87** sawa na asilimia **32.8** zilipatikana. Mchanganuo wa bajeti hiyo na upatikanaji wa fedha unaonekana katika Jedwali Na. 03.

**Jedwali Na.3: Upatikanaji wa fedha za maendeleo hadi kufikia Februari, 2021/2022**

| NA. | MRADI | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | % JUMLA MAENDELEO | FEDHA ILIYOPATIKANA | % YA IDHINI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa Mkongo | 171,399,781,000.00 | 69.3 | 33,024,492,723.23 | 19.3 |
| 2. | Anwani za Makazi na Postikodi | 45,000,000,000.00 | 18.2 | 41,282,160,613.64 | 91.7 |
| 3. | Tanzania ya Kidijitali | 25,000,000,000.00 | 10.1 | 6,400,000,000.00 | 25.6 |
| 4. | Habari Maelezo | 6,001,000,000.00 | 2.4 | 551,240,000.00 | 9.2 |
| **Jumla** | | **247,400,781,000.00** | | **81,257,893,336.87** | **32.8** |

**Chanzo:** Randama ya Wizara

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa taarifa hizo unaonesha kwamba:-

a) Kwa ujumla upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharimia miradi ya maendeleo si wa kiwango kizuri. Hali hii inaweza kuathiri lengo la miradi iliyopangwa kutekelezwa na kufifisha manufaa yaliyotarajiwa;

b) Mradi wa Anuani za Makazi umepata fedha za kutosha kuendana na utekelezaji wa mradi huo. Mwenendo huu unaonesha ishara nzuri ya kurahisisha zoezi muhimu la sensa ya watu na makazi ifikapo Mwezi Agosti, 2022; na

c) Fedha za utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Tanzania ya Kidijitali zimepatikana kwa kiasi kidogo. Hadi kufikia mwezi Februari, 2022 kiasi kilichopatikana ni asilimia **19.3** na asilimia **25.6** mtawalia. Hali hiyo ni dalili ya kutofanikiwa kwa lengo la ujenzi wa Mkongo wa Taifa na kushindwa kuiwezesha Tanzania kuwa ya Kidigitali.

**Mheshimiwa Spika,** ni rai ya Kamati kuwa, Serikali iendele kutoa fedha kwa wakati ili kukamilisha utekelezaji wa miradi.

### *2.1.4 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka 2021/2022*

**Mheshimiwa Spika,** wakati Bunge lako lilipopitisha Bajeti ya **Fungu 68** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, lilizingatia malengo ya mpango wa Wizara yaliyowasilishwa Bungeni. Ili kuliwezesha Bunge kujiridhisha kama utekelezaji wa malengo hayo unaendana na azma ya Bunge kupitisha bajeti kwa mwaka wa fedha unaohusika, Kamati ilifuatilia utekelezaji na kuchambua taarifa za utekelezaji. Matokeo ya uchambuzi huo yameonesha kwamba, baadhi ya malengo yaliyopangwa hayakukamilika katika utekelezaji na mengine yametekelezwa ilivyostahili. Kwa mfano, katika mwaka wa

fedha 2021/2022, Wizara ililenga kukamilisha ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kiasi cha km **1880** lengo hili halikukamilika na linahitaji kuendelea kufanyiwa kazi**.**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ililenga kukamilisha uwekaji wa Anwani za Makazi na Postikodi nchini. Taarifa ya utekelezaji ilionesha kuwa operesheni ya anwani ya makazi ilizinduliwa tarehe 08 Februari, 2022 ikiwa na lengo kwamba, ifikapo mwezi Mei, 2022, kila mwananchi apate anwani ya makazi. Hatua hii ya utekelezaji inatoa matumaini ya jumla kuhusu kufanikisha azma ya Bunge katika kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

### *2.2 Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara (Fungu 68) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023*

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi, Kamati ilichambua Makadirio ya Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ikilinganishwa na utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Aidha, Malengo ya Mpango wa Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ikilinganishwa na utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2021/2022, ni miongoni mwa vigezo vilivyotumika kufanya uchambuzi. Jambo jingine muhimu lililofanyiwa kazi ni Makadirio ya Bajeti ya kugharimia miradi ya maendeleo ikilinganishwa na Ilani ya Uchaguzi na Mpango wa Maendeleo na hatua ya utekelezaji iliyofikiwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

**Mheshimiwa Spika**, ni maoni ya Kamati kuwa vipaumbele hivi vitekelezwe kikamilifu ili Sekta hii iendelee kutoa mchango mzuri katika uchumi wa Taifa letu.

### *2.2.1 Uchambuzi wa Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa Taarifa ya Wizara kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi yake kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na kubaini kuwa, Bajeti hii ya Wizara imezingatia mambo mbalimbali kama vile Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya Mwaka 2020 – 2025, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na Mpango wa Taifa wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26. Wizara imepanga kutekeleza vipaumbele saba (7) vya maendeleo kwa Mwaka 2022/2023. Vipaumbele hivyo ni kama vifuatavyo:-

i) Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;
ii) Mradi wa Anuani za Makazi na postikodi;
iii) Kuendelea na mradi wa Kidigitali Tanzania;
iv) Kuendeleza ubunifu na utengenezaji wa vifaa vya TEHAMA;
v) Upanuzi wa usikivu kwa shirika la utangazaji Tanzania;
vi) Kufunga mtambo mpya wa kisasa wa uchapaji; na
vii) Kuendeleza mradi wa habari kwa umma.

**Mheshimiwa Spika**, ni maoni ya Kamati kuwa vipaumbele hivi vitekelezwe kikamilifu ili Sekta hii iendelee kutoa mchango mzuri katika kukuza uchumi.

### *2.2.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2022/2023*

**Mheshimiwa Spika,** Wizara na taasisi zake imelenga kukusanya mapato ya **Sh. 682,651,883,495** Sawa na asilimia **41.3** ya bajeti yake ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**Jedwali Na. 04: Mchanganuo wa Lengo la Mapato**

| TAASISI | LENGO KWA MWAKA 2021/2022 | UKUSANYAJI HADI FEBRUARI, 2022 | % LENGO | LENGO KWA MWAKA 2022/2023 |
|---|---|---|---|---|
| Wizara | 446,484,017,222.00 | 24,612,048,363.76 | 5.5 | 150,700,000,000.00 |
| TCRA | 150,067,415,286.65 | 119,269,301,118.2 | 79.48 | 155,897,258,292.00 |
| TTCL | 206,240,680,323.00 | 184,270,289,173,00 | 89.35 | 254,115,588,048.00 |
| TPC | 40,761,234,400.00 | 20,703,158,568.00 | 50.79 | 40,943,300,000.00 |
| ICTC | 1,148,105,000.00 | 881,885,434.41 | 76.81 | 1,984,725,000.00 |
| UCSAF | 34,086,331,975.00 | 16,024,342,078.00 | 47.01 | 34,760,583,156.00 |
| TBC | 14,044,500,000.00 | 5,311,742,860.52 | 37.82 | 27,033,484,000.00 |
| TSN | 14,343,826,000.00 | 5,469,097,483.00 | 38.13 | 16,506,945,000.00 |
| **JUMLA** | **907,176,110,206.65** | **192,271,575,905.89** | **21.1** | **681,941,883,496.00** |

**Chanzo:** Randama ya Wizara

**Mheshimiwa Spika**, ulinganisho wa lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na utekelezaji hadi kufikia mwezi Februari, 2022 unaweza kuonesha uwezekano wa kufikia lengo linalowekwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa licha ya Wizara kutofikia lengo la ukusanyaji kwani imekusanya asilimia **5.5**, hadi kufikia mwezi Februari, 2022. Mwaka 2022/2023 Wizara imelenga kukusanya kiasi sawa na asilimia **33.7** ya lengo la mwaka 2021/2022. Kwa kuwa vyanzo ni vile vile vya mwaka wa fedha 2021/2022, lengo linalowekwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 linaweza kukosa uhalisia na lisitekelezeke.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara iliweka lengo ambalo hadi kufikia mwezi Feburari, 2022, lilifikiwa kwa asilimia **37.8** tu. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa, lengo la makusanyo kwa TBC limeongezeka kwa asilimia **92.** Hali hiyo inaweza kutafsiriwa kuwa, vyanzo vya mapato kwa TBC vimeongezeka au kuna matarajio ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Jambo muhimu katika hilo, ni kuhakikisha kuwa malengo ya ukusanyaji hayapangwi kwa majaribio, bali yanahitaji kuzingatia uzoefu wa bajeti iliyopita.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Tume ya Taifa ya TEHAMA na

Shirika la Mawasiliano Tanzania, malengo yaliyowekwa yanaakisi uzingatiwaji wa uzouefu wa makusanyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa hali hiyo, Kamati ina maoni kuwa upangaji wa lengo la makusanyo kwenye taasisi hizo ungeweza kuwa mfano kwa taasisi nyingine chini ya Wizara hii.

***2.2.3 Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023***

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wa mpango na Bajeti ya Wizara hii, Kamati ilizingatia umuhimu wa malengo makuu ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Miongoni mwa malengo hayo ni ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, uboreshaji wa usikivu wa TBC na uendelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi. Malengo mengine ni kama yalivyobainishwa na mtoa hoja. Ili kuona uhalisia kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na kuoanisha na matarajio ya wananchi kuhusu malengo hayo, Kamati ilifanya ulinganisho na mwaka wa fedha 2021/2022. Matokeo ya uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

***a) Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023***

**Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Sh. 255,777,440,000.00** zinaombwa kwa ajili ya kugharimia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka **2022/2023**. Miradi hiyo na bajeti yake inaonekana katika Jedwali Na. 05.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa makadirio ya matumizi ya kugharimia miradi mitatu yameongezeka kwa asilimia **3.27** ikilinganishwa na mwaka wa fedha wa 2021/2022. Miradi hiyo ni mradi wa Anwani za Makazi na Postikodi, mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa na

mradi wa Elimu kwa Umma kuhusu mafanikio ya Serikali. Uchambuzi unabainisha kwamba, isipokuwa Mradi wa Anwani ya Makazi, Bajeti kwa ajili ya miradi ya Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Programu ya Elimu kwa Umma zimeshuka kwa asilimia **13** na asilimia **6** mtawalia.

***b) Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka wa fedha 2022/2023***

**Mheshimiwa Spika**, makadirio ya matumizi ya kawaida nayo yalilinganishwa na Bajeti inayoisha tarehe 30 Juni, 2022. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Bunge liliidhinisha jumla ya **Sh. 22,728,400,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Wizara hii na taasisi zake. Katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, Bunge lako tukufu linaombwa kuidhinisha jumla ya **Sh. 26,279,346,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa Wizara hii na taasisi zake. Kiasi hicho ni ongezeko la asilimia **13.51**

**Mheshimiwa Spika,** ili kulinganisha makadirio ya matumizi na shughuli zinazotarajiwa kufanyika, Kamati ilifanya uchambuzi zaidi kwa kuchanganua makadirio ya kila taasisi ikiwemo Wizara yenyewe. Matokeo ya uchanganuzi huo yameoneshwa katika Jedwali Na . 06

***Jedwali Na. 06 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida ya Taasisi kwa mwaka wa fedha 2022/2023***

| Na | Taasisi | Makadirio ya Matumizi 2021/2022 | Makadirio ya Matumizi 2022/2023 | % Ongezeko |
|---|---|---|---|---|
| **(a)** | **(b)** | **(c)** | **(d)** | **(e)** |
| 1. | TCRA | 150,067,415,286.65 | 155,897,258,292 | 3.74 |
| 2. | TTCL | 206,240,680,323.00 | 254,115,588,048 | 18.84 |
| 3. | ICTC | 1,148,105,000.00 | 5,407,622,000 | 78.77 |
| 4. | POSTA | 40,761,234,400.00 | 37,843,300,000 | -7.7 |
| 5. | UCSAF | 34,086,331,975.00 | 34,760,583,155 | 1.9 |
| 6. | TBC | 14,044,500,000.00 | 42,842,649,000 | 67.22 |
| 7. | TSN | 14,343,823,000.00 | 16,506,945,000 | 13.10 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 8. | TCRA-CCC | 710,000,000 | 710,000,000 | 0 |
| | | **531,951,883,495.00** | **548,083,945,495.00** | **2.9** |

**Chanzo:** Limetayarishwa kutokana na Randama iliyowasilishwa kwenye Kama

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchanganuzi huo, Kamati inabainisha yafuatayo:-

*a) Matumizi ya kawaida kwa mwaka 2022/2023 yameongezeka kwa asilimia **13.15** ukilinganisha na mwaka 2021/2022;*

*b) Makadirio ya matumizi kwa taasisi yameongeza kwa asilimia **2.9** kwa mwaka 2022/2023 ukilinganisha na mwaka 2021/2022;*

*c) Hadi kufikia mwezi Februari, 2022 fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa ni asilimia **31.8***

***2.2.4 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Jumla ya Wizara na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2022/2023***

**Mheshimiwa Spika**, makadirio ya matumizi ya jumla ya Wizara hii yanaonesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara hii ilitengewa jumla ya **Sh. 270,129,181,000.00.** Kati ya fedha hizo, Wizara yenyewe ilitengewa **Sh. 246,384,551,000.00** na taasisi zake zilitengewa jumla ya **Sh. 23,744,630,000.00.**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara yenyewe inaombewa **Sh. 255,777,440,000.00 fedha za maendeleo** sawa na ongezeko la asilimia **5.62** na Taasisi za Wizara hii zinaombewa jumla ya **Sh. 26,279,346,000.00** . Jumla ya bajeti nzima inayoombwa ni **Sh. 282,156,746,000.00** sawa na ongezeko la asilimia **4.23**

Mchanganuo wa makadirio hayo unaonekana ongezeko katika Jedwali Na. 05.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi unaonesha kuwa makadirio ya fedha yameongezeka kwa mwaka 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kusisitiza kuwa fedha zikitengwa zitolewe kwa wakati ili ziweze kutekeleza malengo yalivyopangwa.

**Jedwli Na: 5 Mchanganuo wa Makadirio ya fedha za maendeleo kwa mwaka 2021/2022 na 2022/2023**

| NA. MRADI | JINA LA MRADI | BAJETI KWA MWAKA 2021/2022 | BAJETI KWA MWAKA 2022/2023 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 4283 | Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano | 171,399,781,000.00 | 149,700,000,000.00 | -14.4 |
| 4234 | Anwani za Makazi na Postikodi | 45,000,000,000.00 | 40,000,000,000.00 | -12.5 |
| 4280 | Tanzania ya Kidigitali | 25,000,000,000.00 | 39,000,000,000.00 | 35.89 |
| 4279 | TBC | 5,000,000,000, | 13,136,500,000.00 | 61.93 |
| 6226 | Vifaa vya TEHAMA | - | 3,300,000,000.00 | |
| 6505 | TSN | 1,000,000, | 9,400,940,000.00 | |
| 6567 | Habari kwa Umma | 1,000,000,000 | 940,000,000.00 | |
| | **JUMLA** | **241,3999,781,000** | **255,777,400,000** | **5.62** |

**Chanzo:** Randama ya Wizara

a) **Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi unaonesha kuwa makadirio ya fedha za maendeleo zimeongezeka kwa asilimia **5.62** kwa mwaka 2022/2023,

b) **Mradi wa** Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano, Tanzania ya Kidigitali fedha zake zimepungua kwa asilimia **14.4** asilimia **12.5** mtawalia.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kushauri kuwa Serikali iendelee kuwekeza fedha kwenye miradi hii kwani ni muhimu kwa mustakabali wa nchi na wananchi.

## SEHEMU YA TATU

### *3.0 MAONI NA USHAURI*

### *3.1 Maelezo ya Jumla*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatoa maoni na ushauri unaotokana na uchanganuzi uliofanyika. Katika maoni, Kamati inaonesha maelezo kuhusu mtazamo wake juu ya mambo yaliyojitokeza katika uchambuzi. Kwa kuzingatia mtazamo huo pamoja na hali halisi inayolinganishwa na matarajio ya wananchi, Kamati inatoa ushauri wa kuzingatiwa katika utekelezaji wa Bajeti ya sekta hii kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

### *3.2 Majumuisho ya Maoni*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 117 ya Kanuni za Bunge, umeipa Kamati nafasi ya kutoa maoni ambayo ni mtazamo unaotokana na taarifa zilizowasilishwa kama ifuatavyo:

### *3.3 Ushauri wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi wa maoni yaliyobainishwa awali, Kamati inatoa ushauri kuwa Serikali iendelee kuwekeza fedha za maendeleo kwenye Shirika la Utangazaji Tanzania, Kampuni ya Magazeti ya Serikali na Idara ya Habari na Maelezo. Aidha Serikali ione namna ya kupandisha makusanyo kwenye baadhi ya taasisi zilizo chini yake ambazo zimekusanya mapato chini ya asilimia **50** mfano wa taasisi hizo ni TTCL, UCSAF na TBC.

***3.3.1 Mheshimiwa Spika,*** *kuhusu TCRA Kamati inashauri;*

1. Serikali kupitia Mamlaka hii iendelee kuwaelemisha wananchi juu ya umuhimu wa kutunza miundombinu ya Mawasiliano;

2. TCRA iendelee na utaratibu wa kupanga masafa kwa kuzingatia vipaumbele na ukuaji wa teknolojia;

3. TCRA kwa kushirikiana na Jeshi la polisi liendelee kudhibiti uhalifu wa kimtandao;

4. Serikali isimamie suala la watumiaji wa line za simu zilizosajiliwa tayari, ili kuondoa usumbufu wa kupokea ujumbe wa kutakiwa kuhakiki line zao; na

5. TCRA ikae pamoja na makampuni ya simu kuangalia matumizi ya bando ambayo yanalalamikiwa na watumiaji.

***3.3.2 Mheshimiwa Spika,*** *kuhusu Shirika la TTCL Kamati inashauri;*
1. Serikali ihakikishe taasisi zote zinazopata huduma kutoka TTCL zilipie huduma na madeni kwa wakati; na

2. Serikali iisaidie TTCL kujiendesha kibiashara ili kusaidia kukuza uchumi wa nchi.

***3.3.3 Mheshimiwa Spika,*** *kuhusu Mfuko wa la UCSAF Kamati inashauri;*
1. Serikali kupitia UCSAF iisimamie TTCL na Halotel kumaliza miradi yao kwa wakati;

2. UCSAF ipewe fedha za kutosha ili iweze kutekeleza miradi yake ili huduma iweze kufika maeneo mengi zaidi hasa mipakani;

3. Kamati inashauri fedha inayopatikana kutoka kwa mtoa huduma (CSR) irudi kwa UCSAF na kuendeleza utekelezaji wa miradi mingine; na

4. Minara yote ambayo Serikali imewekeza fedha ni vyema iwekwe nembo ya mfuko, aidha, wananchi wanajukumu la kulinda minara hiyo.

***3.3.4 Mheshimiwa Spika,*** *kuhusu Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano Kamati inashauri;*

1. Serikali ikae kwa pamoja na TTCL ili wajadili namna ya kuendesha Mkongo wa Taifa na kuiachia TTCL uendeshaji wa Mkongo; na

2. Serikali iendelee kuwekeza kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na watoa huduma binafsi wasiruhusiwe kumiliki Mkongo wa Mawasiliano hii ni kwa ajili ya usalama wa Taifa letu.

***3.3.5 Mheshimiwa Spika,*** *kuhusu Anwani za Makazi na Postikodi Kamati inashauri;*

1. Serikali itoe fedha za kutosha za kufanikisha mradi na iwaunganishe wadau wote muhimu katika Wizara ili kufanikisha mradi huu;

2. Maeneo mapya yapimwe na kupangwa ili kurahisisha wakati wa uwekezaji wa Anwani za Makazi;

3. Serikali itoe zawadi kwa Mkoa utakaofanya vizuri kwa kutekeleza mradi wa Anwani za Makazi na Postikodi na Mikoa ambayo inasuasua katika utekelezaji wasimamiwe ili wakamilishe kwa wakati; na

4. Serikali iharakishe mfumo wa usajili na uhuwishaji wa taarifa za Wananchi wanapohama kutoka eneo moja kwenda sehemu nyingine.

***3.3.6 Mheshimiwa Spika,*** *kuhusu Shirika la Posta - TPC Kamati inashauri;*

1. Shirika la Posta Tanzania lipewe mtaji wa kutosha ili liweze kujiendesha kibiashara na kuhimili ushindani;

2. Shirika la Posta liwezeshwe kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za kifedha;

3. Serikali ilisimamie Shirika liweze kulipwa pesa kutoka kwa watoa huduma za kusafirisha mizigo kama mabasi, malori nk; na

4. Shirika lisaidiwe kulipa na kulipwa madeni kwani limeendelea kuelemewa na deni la **Sh. bilioni 26.8** ambazo asilimia kubwa ni madeni ya taasisi za Serikali.

**3.3.7** ***Mheshimiwa Spika,*** *kuhusu TBC na TSN Kamati inashauri;*
1. Serikali iwekeze fedha za kutosha ikiwemo Ruzuku ili kuisaidia TBC na TSN;

2. Serikali ihakikishe TBC na TSN inapata watumishi wa kutosha na kuboresha maslahi yao ili kuepusha kuacha kazi au kuhamia kwenye taasisi zingine;

3. Serikali itoe fedha kwa wakati kwa TBC na ihakikishe inapata gari la matangazo kwa kila Mkoa;

4. TBC na TSN zijiendeshe kibiashara kwa kuanzisha miradi ya maendeleo;

5. Serikali ihakikishe taasisi zake zinalipa madeni ya mashirika haya mfano, deni la TSN limefikia **Sh**. **bilioni 11;** na

6. Serikali ihakikishe Star times inaendelea kutoa gawio kwa TBC.

## SEHEMU YA NNE

### *4.0 HITIMISHO*

### *4.1 Maelezo ya Kuhitimisha*

**Mheshimiwa Spika**, sekta ya Habari na Mawasiliano ni muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi kwani sekta hii

huwezesha sekta nyingine zote kuweza kufikia malengo. Uwekezaji katika sekta ya mawasiliano ni chachu kubwa ya maendeleo ya uchumi na kijamii kama ilivyo katika uwekezaji wa huduma nyingine. Hivyo ni muhimu Serikali kuhakikisha sekta hii inastawi na inachangia kwa kiwango kikubwa zaidi maendeleo ya uchumi wa nchi kama inavyoeleza katika ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 Ibara ya 61 (a - o).

### *4.2 Shukrani na Wasilisho*

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba kukushukuru kwa dhati Mhe Spika na Naibu Spika kwa kuiwezesha Kamati hii kutimiza majukumu yake, namshukuru Mhe. Nape Moses Nnauye (Mb) Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Eng. Kundo Andrea Mathew (Mb), Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kuipa Kamati ushirikiano stahiki.

**Mheshimiwa Spika,** nawashukuru pia Makatibu wakuu, Naibu Makatibu wakuu na Watendaji wote wa Wizara ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kumuwezesha Waziri na Naibu Waziri kutoa ushirikiano kwa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Joyce Mwihambi kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Aidha, shukrani maalumu ziende kwa Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu. Gerald Singano Magili pamoja na Makatibu wa Kamati Ndugu Janeth Julian Malangu, Ndugu Victory Eliackim Mrema na Msaidizi wa Kamati Ndugu Grace Samwel Gwivaha pamoja na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao ulioiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango waliyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti pamoja na kuandaa taarifa hii. Naomba kuwatambua wajumbe wa kamati hii kwa kuwataja majina kama ifuatavyo: -

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Moshi Seleman Kakoso, Mb | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb | - | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka, Mb | | " |
| 5. | Mhe. Capt. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb | | " |
| 6. | Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu, Mb | | " |
| 7. | Mhe. Fredrick Edward Lowassa, Mb | | " |
| 8. | Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mb | | " |
| 9. | Mhe. Mohamed Maulid Ali, Mb | | " |
| 10. | Mhe. Innocent Edward Kalogeris, Mb | | " |
| 11. | Mhe. Mbarouk Juma Khatib, Mb | | " |
| 12. | Mhe. Masache Njelu Kasaka, Mb | | " |
| 13. | Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb | | " |
| 14. | Mhe. Amina Ali Mzee, Mb | | " |
| 15. | Mhe. Rose Vicent Busiga, Mb | | " |
| 16. | Mhe. Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila, Mb | | " |
| 17. | Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb | | " |
| 18. | Mhe. Stella Simon Fiyao, Mb | | " |
| 19. | Mhe. Aeshi Khalfan Hilaly, Mb | | " |
| 20. | Mhe. Abdulaziz M. Abood, Mb | | " |
| 21. | Mhe. Innocent Sebba Bilakwate, Mb | | " |
| 22. | Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb | | " |
| 23. | Mhe. Ahmed Yahya Abdulwakil, Mb | | " |
| 24. | Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb | | " |
| 25. | Mhe. Angelina Malembeka, Mb | | " |

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kama

ilivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Moshi Seleman Kakoso, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU**
**YA BUNGE YA MIUNDOMBINU**

20 Mei, 2022

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anne kilango Malecela kwa taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na uchangiaji. Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Jerry William Silaa akifuatiwa na Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mheshimiwa Stella Martin Manyanya, kisha atakuja Mheshimiwa Salome Makamba na wakati huo Mheshimiwa Esther Bulaya ajiandae.

Mchango ni dakika tano tu na kengele ni moja; ikigonga Mheshimiwa Mbunge tunakuomba uketi. Ahsante.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa kwanza. Kwa kuwa muda ni mchache, kwanza nimpongeze kipekee Mheshimiwa Nape Moses Nauye, Waziri; tokea ateuliwe kushika nafasi hii, amerejesha heshima, amani na utulivu kwenye Sekta ya Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kwenye eneo moja tu la TEHAMA na katika hilo nitajikita kwenye kuwa na mfumo mmoja wa kieletroniki katika kuendesha shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na kauli nyingi na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais ambaye mara tatu akiapisha Makatibu Wakuu, akipokea Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu mwaka 2021 na vilevile akipokea Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali mwaka huu tarehe 30 mwezi Machi, amesisitiza jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo hatua kubwa sana iliyofanywa na Serikali katika uwekezaji kwenye Sekta ya *TEHAMA*. Tunacho kituo cha *National Internet Data Center (NIDC)* ambacho kina miundombinu mikubwa na ya kisasa kabisa katika suala la *TEHAMA,* lakini Serikali kupitia sheria Na.10 ya mwaka 2019 imeanzisha wakala *e-GA (e-government)* ambaye anafanya kazi ya kusimamia mifumo ya TEHAMA kwenye Serikali. Pia asilimia 100 Serikali ina *political will* katika kuhakikisha Sekta ya TEHAMA ina *flourish* na kwa kufanya hivyo imeanzisha wizara maalumu kwa ajili ya Teknolojia ya Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake ametueleza kwenye *mobile connectivity* kwamba sasa tunawatumiaji zaidi ya milioni 55 wa simu na milioni 29 wa mitandao ya *internet.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchache, upo upungufu. Upungufu wa kwanza, nchi yetu haina *central database system* ambayo ina taarifa zote za Mtanzania. Kwenye Taifa letu tunayo *NIDA* wanaandikisha vitambulisho, tunayo *RITA* wanatoa vyeti vya kuzaliwa, tunayo *TRA* wanatoa *TIN Number;* na hii kuipata siyo mchezo, upeleke nyaraka nyingine toka taasisi nyingine; Tunaye humu ndani Seif Gulamali anatoa Kadi za Yanga; tunao *CRDB* nao wanatoa kadi zao kwa wateja wao; tunayo Tume ya Uchaguzi na yenyewe inaandikisha Watanzania hao hao; tunao *NHIF* mmeona wanatibia wanaume mpaka ujazito kwa kutoa vitambulisho vyao na kuandisha watu; una leseni ya udereva;

una kadi ya Chama cha Mapinduzi; kwa utaratibu huu hatuwezi kufikia pale tunapotaka kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwa kuwa muda ni mdogo, niyaseme machache. Leo Mtanzania akiomba mkopo, ataombwa nyaraka hii, ataombwa nyaraka nyingine kwa sababu hakuna sehemu moja ambapo benki inaweza ikaenda ikakuta taarifa zote za Mtanzania huyu za kuweza kumsaidia. Hata huo mkopo ukiwa *approved;* juzi nilienda ofisini kwa mtu mmoja nikakuta anasaini nyaraka za mikopo, alikuwa na nyaraka siyo chini ya 40 amesaini *signature* 219, kitu ambacho tungekuwa na mfumo wa kieletroniki, angesaini tu pale kieletroniki *agreed,* angepata mkopo wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *e-GA* ipo chini ya Ofisi ya Rais, Utumishi. Leo Waziri anawasilisha hapa TEHAMA, yupo Wizara nyingine na hilo nalo ni tatizo kwenye mfumo wa kisheria wa nchi yetu. Nimeenda *e-GA* vijana wale wanafanya kazi nzuri, nawapongeza sana, lakini wakati naondoka nikashangaa, nikapewa nyaraka hizi. Wewe una mamlaka ya kieletroniki, una-*print* nyaraka za nini? Kama kweli tuna nia ya kwenda kietroniki, leo hapa nani amewahi kuprintiwa nyaraka na *face book?* Nani kaprintiwa nyaraka na *Instagram?* Nani amewahi kuprintiwa nyaraka yoyote na simu yake ya mkononi au anamjua hata meneja wa kampuni ya simu anayoitumia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuseme mifumo ifuatayo kwa ufupi wake. Tunao mfumo wa *TANePS*. Huu siyo mfumo, ni kitu kimetengenezwa cha kumsaidia tu Mtanzania, mzabuni asi-*print* nyaraka za *PDF* ofisini kwake, bali azi-*upload* ziende kule zikafanyiwe kazi. Ingekuwa ni mfumo, ulitakiwa kieletroniki umtambue mzabuni, utangaze zabuni, ufanye *evaluation,* uandae mkataba, ukafanye *vetting* mkataba uliozidi Shilingi bilioni moja, uende ukafanye maombi ya msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani *(VAT),* ufanye *contractor management,* uandae *certificate,* umlipe

mkandarasi, tusipate zile hasara alizozionesha *CAG* za ucheleweshaji wa malipo kwa kuwa kazi zinafanyika kwenye *manual system. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi nitaje hasara zinazopatikana nchi katika mifumo ya kieletroniki. Ukisoma ripoti ya *CAG* ukurasa wa 348 *TANROAD* peke yake wamelipa Shilingi bilioni 224 kwa ukosefu wa mifumo ya kulipa hii, wanalipa kwa *manual system.* Leo Bodi ya Mikopo inao wadaiwa 155,722 wanaodaiwa Shilingi bilioni 422 hawajui wako wapi? Yaani kuna Watanzania wamesoma *degree,* halafu Bodi ya Mikopo haijui itawapata wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tukisema Bima ya Afya kwa watu wote bila kuwa na mfumo wa kieletroniki ambapo Watanzania wote wanapatikana, itakuwa ni ndoto. Kama tu hii *NHIF* inashindwa kutibia watu na inajiendesha kwa harasa, hatuwezi kufika. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika tano ni chache, nitachangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *senior* anasema uniongeze kidogo Mwenyekiti ukiridhia.

**MWENYEKITI:** Nilishakuongeza sekunde karibu 40 mpaka sasa. Kwa hiyo, nikushukuru kwa mchango wako.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Asha Abdullah Juma aweze kuchangia.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nami namshukuru Mungu kwa kunipa uwezo leo hii nikasimama hapa kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri *Comrade* Nape Moses Nauye na timu yake kwa jinsi anavyofanya kazi nzuri ya kutoa huduma katika Wizara hii. Kazi yake inapimika, inaonekana na inaeleweka na ipo wazi kabisa kila mtu anaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia kazi kubwa sana iliyoweza kufanywa na mfuko huu wa *UCSAF,* Mawasiliano kwa Wote. Mfuko huu umefanya kazi kubwa hasa kwa upande wa Zanzibar. Umeweza kusimika minara 42 iliyotiwa mkataba tarehe 20 Januari na mpaka sasa hivi kwa mujibu wa ripoti ya juzi aliyokwenda kufanya ziara Mheshimiwa Waziri, minara 38 imeshakamilika. Hiyo ni muda kama wa miezi minne. Itakapofika mwezi Juni tunategemea minara yote hii itaweza kuwa tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, minara hii itaweza kuleta *excess* kwa sehemu ambazo sisi kwa lugha yetu Kiingereza tunaita *very remote places,* kama Fundo, Nungwi kule mwisho, Msuka, Kwa Pemba, Chaani, Unguja, kote huko minara hii itakamilika, kwa hiyo, italeta mawasiliano kwa urahisi kwa wananchi wetu na kutuweka Tanzania katika huduma ya endelevu kidijitali. Hapo nawapa kongole sana watu wa mfuko ambao wamefanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tunategemea hiyo minara hiyo mingine 119 ya huku Bara itakamilika, lakini haya yote pia nitoe pongezi kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa elekezo lake lililoelekeza kwamba kusiwe na ucheleweshaji katika kutoa vibali vya kukamilisha kazi hizi. Kwa hiyo, Mheshimiwa

Dkt. Hussein amefanya vizuri na nchi yetu inakuwa *communicated* kidijitali. Namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii nzuri pia imeweza kufanikishwa kwa juhudi za pamoja za mfuko na pamoja na Zantel na zikifanywa vizuri pia na *contractor* wetu *Helios Tower*. Kwa hivyo nawapongeza sana kazi hiyo iliyofanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko huu pia umeweza kukamilisha vituo vya *TEHAMA* katika wilaya 10 za Zanzibar na wilaya 11 inakamilika. Na vilevile mafunzo yanatolewa ya matumizi haya ya *TEHAMA* kwa Masheha wote na watu wote na vituo hivi vipo karibu na watu kwa hivyo vitakuwa *access* kirahisi na watu. Kwa hiyo, ni kazi nzuri inayofanywa na mfuko huu, kwa sababu hiyo pia naona kwamba mfuko huo uweze kuongezewa fedha ili uweze kufanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo jingine ambalo ni la muhimu vilevile ni hili la kuhakikisha kwamba mfuko huu umeweza kutengeneza kitu cha milio ya dharura ambao unaweza kupiga 190 na Kituo hichi kipo Kiembesamaki na kinafanya vizuri. Mtu unaweza ukapata shida baharini, ukapata ajali, ukapata ugonjwa ukapiga hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine liliofanywa na Wizara hii ni kuhakikisha kwamba kuunganisha tiba kwa kupitia *TEHAMA* kwa mtandao, kwa mfano Abdalla Mzee itaunganishwa moja kwa moja na *MOI*, Jakaya Mrisho na Muhimbili kwa hivyo itapunguza gharama kwa Serikali na wananchi wenyewe kwa kusafiri kwenda kutafuta huduma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo nchi yetu kila kukicha inakwenda kupaa zaidi kidigitali. Na haya yamesemwa jana pia na Mheshimiwa Rais Mama yetu alipokuwa anasema kwamba katika siku zijazo za mbele tutajikuta Tanzania imepaa zaidi kimaendeleo. Na

maendeleo hayawezi kuja kama huna tekonolojia kwenye *TEHEMA* na kwenye *digital* na jambo hili limeshikwa vizuri sana Wizara hii, tunatoa hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunaweza kupata mawasiliano kwa kupitia Televisheni zetu zote ambazo zinafanya vizuri na tunashuhudia na hapo ndiyo tunaweza kupata taarifa ya Habari. Nchi haiwezi kuendelea kama haiwezi kupata taarifa za Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu anuani ya makazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Juma.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Naam.

**MWENYEKITI:** Kengele imeshagongwa.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sijaisikia, samahani naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge ninasisitiza sana ukiwa unazungumza kiangalie kiti na kusikiliza kengele. Nilimuita Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya aweze kuchangia.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianzie kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya toka amekaa kwenye hicho kiti lakini pamoja na timu yake yote ya Wizara hii pamoja na Naibu wake kwa kweli wanajitahidi sana. Na nakupongeza kwa jinsi ambavyo umesimamia suala la anuani ya makazi, tumekuona

ukizunguka huku ukitoa maelekezo hayo ndiyo tunayoyahitaji sisi watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze sana kwa namna ya kipekee Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mkazo wa matumizi ya *TEHAMA* katika kufanya shughuli zetu mbalimbali. Na hivi sasa kuna shule za Sekondari zinajengwa kila Mkoa tena za wasichana kwa ajili ya kuwezesha katika masuala ya *TEHAMA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende pia kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Spika wetu wa Bunge la Tanzania kwa jinsi ambavyo ameamua kuendelea kuboresha huduma za Maktaba ili sasa Wabunge pamoja na wadau wote wanaopenda kufuatilia shughuli za Bunge waweze kupata taarifa mbalimbali za Bunge pamoja na kujisomea majarida mbalimbali au vitabu mbalimbali kupitia mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini kwamba Wizara hii itashirikiana na Bunge letu hili Tukufu kuhakikisha kwamba linakuwa ni kweli Bunge la kimtandao. Kwa sababu hata wakati tunaanza hivi vishikwambi watu walisema hivi itawezekana, lakini imeshawezekana sisi wote tunatumia vishikwambi na shuhguli za Bunge zinaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina suala moja zito sana kwa kuliangalia linaweza kuwa ni la kawaida lakini ni zito. Waheshimiwa Wabunge wengi wanashindwa kuhudhuria vikao vya Baraza katika halmashauri zetu kutokana na shughuli hizo kugongana na shughuli hizo ambazo zinatakiwa ziendeshwe kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati Mheshimiwa Mbunge analazimika kutembea usiku kucha kwa ajili ya kuwahi kikao cha Baraza na kurudi, jambo ambalo linagharimu lakini pia ni hatari kwa maisha yake kwa sababu

anakuwa amechoka hata madereva wanakuwa wamechoka. Sasa nilikuwa najiuliza kwa sababu hii Mihimili ya Dola inafanya kazi kwa ushindani lakini pia kwa kuhakikisha wanatoa huduma zinazotakiwa kwa wananchi. Sisi Wabunge tunapokosa kuhudhuria Mabaraza yetu yanapokaa ni kwamba ni mambo mengi tunashindwa kuchangia na kuweza kusimamia halmashauri zetu inavyopaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nasema niiombe sana Wizara hii ya Habari, Mawasilinao na Teknolojia ya *TEHAMA* pamoja na Bunge letu Tukufu kuanzisha kona ya Madiwani nikimaanisha Wabunge hapahapa Bungeni. Sisi tunavyokuwa hapa tuweze kuhudhuria vikao vyetu vya Baraza vya halmashauri wakati tukiwa tunaendelea na shuhguli za Kibunge kwa njia ya Mtandao. Kule kwenye halmashauri zetu bado hazijafungwa zile huduma za kuwezesha hayo mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana na hilo leo mchango wangu hasa unajikita hapo. Niwaombe kuna mfuko huu ambao ni wa mawasiliano kwa wote ambao umefanya kazi nzuri sana wa kusaidia kwenye maeneo yetu hata huko Vijijini, nawapongeza sana. Lakini pia vyombo vya Habari vinajitahidi, lakini katika hili naomba Wizara yetu hii chini ya wewe Mheshimiwa Waziri Nape Nnauye pamoja na Mheshimiwa Spika wetu sisi tunahitaji hiyo huduma ili tuhudhurie vikao vyetu vya Mabaraza bila kukosa. Haiwezekani Mbunge inafikia unahudhuria vikao viwili tu au pengine kimoja na pengine usihudhurie kabisa *simply* kwa sababu unakosa mawasiliano kama haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia inapotekea tatizo ni mwanzo wa kufikiri juu fursa nyingine. Kuna tatizo la upandaji wa bei ya mafuta sasa kwa nini tutembeze gari kutwa, usiku kutwa mara mbili, mara tano, wakati pengine kwa kutumia mtandao tu tungeweza kutekeleza hayo majukumu yetu

vizuri kabisa. Na nikisema hivyo simaanishi kwamba sisi Wabunge sasa tutakuwa hatuendi kwenye Majimbo yetu. Tunazungumzia kipindi tunachokuwa Bungeni tunataka tuweze kuwasiliana na watu, tuweze kukaa kwenye vikao vyetu vinavyohitajika ili na sisi tuweze kuchangia na kutoa tija kwa wananchi wetu. Hili nalinzungumza kwa kweli nikiwa *serious* kwa sababu kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. ENG. STELLA M. MAYANYA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu anatumia sana mtandao katika kuwasiliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya kwa mchango wako naamini Mheshimiwa Nape ameupokea. Nilimuita Mheshimiwa Salome Makamba wakati huo Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira wanajiandaa.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tarehe 13 Mei, 2022 niliuliza swali hapa Bungeni juu ya Makampuni ya simu kukata muda wa maongezi wa watanzania ambao haujatumika kwa maana kwamba *bundle* lime-*expire*. Na Waziri wakati ananijibu alisema kwamba wameelekeza Makampuni ya simu mtu kama *bundle* lake lime-*expire* basi akinunua *bundle* lingine ule muda uliyopita arudishiwe. Hiyo ninahesabu kama ni dhulma kwa watanzania kama ndivyo wanavyofanya basi Mheshimiwa Waziri haujatenda haki kwa watanzania.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka niweke sawa jambo hili kwamba ukizungumzia *bundle* linakuwa *limited* kama ni siku 30 kama ni siku 15. Lakini nafurahia Waziri alisema kwamba kama ukiongeza linavyokaribia kwisha unaongezea muda wa mazungumzo. Kwa hiyo ndiyo *business model* yaani ndiyo biashara iko namna hiyo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo ndiyo taarifa. Mheshimiwa Salome unapokea taarifa.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei na namshauri Mheshimiwa Mbunge atulie, asubiri nifafanue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kasema *clear* hapa kwamba watanzania asilimia 95 wana-*access* ya mtandao kwa maana ya kwamba wana-*access* ya minara ya simu. Kwa hiyo, wanaweza kutumia simu, kwa maana hiyo wanaweza kujiunga kwenye vifurushi vya kupiga simu. Na amesema asilimia 68 ya watanzania wanauwezo wa kujiunga kwenye vifurishi vya *internet* yaani wanaweza kupata *access* ya *internet*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, ukijiunga kwenye kifurushi cha *internet* au *bundle* lile *bundle* unatakiwa ulitumie ndani ya siku moja. Ikitokea kwa namna yoyote ambazo mara nyingi mtu anashindwa kutumia *bundle* lile kwa sababu ya kukosa mtandao kwa sababu maeneo mengi bado hayana *access* ya mtandao au anashindwa kutumia *bundle* lile kwa sababu ya changamoto za kampuni za simu. Kwa sababu hizo sasa yule mtu ambaye *bundle* lake

lime-*expire* hawezi kurudishiwa hiyo pesa ambayo ime-*expire*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa mantiki hiyo, kama mtu yule analazimishwa ili arudishiwe ile pesa yake ambayo ime-*expire* ni lazima ajiunge dakika chache kabla yaku-*expire* kwa *bundle* lile au muda wake wa maongezi kama analazimishwa kufanya hivyo ni kumlazimisha mtu kufanya matumizi ambayo hakuyapanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni ya simu yakifanikiwa kukata shilingi 200 tu kwa watanzania Milioni 50 ambao Mheshimiwa Waziri amesema, wakifanikiwa kukata shilingi 200 tu kwa siku kwa maana ya kwamba bando lime-*expire* au kifurushi cha muda wa maongezi kime-*expire* kwa siku moja wanauwezo wa kukusanya zaidi ya shilingi bilioni 10. Kwa mwezi wanakusanya zaidi ya bilioni 300. Mheshimiwa Waziri hapa ameomba hapa hela anayoomba kwa ajili ya Wizara yake, ameomba shilingi bilioni 282. Kwa hiyo, pesa hiyo wanaweza kukusanyia ndani ya mwezi mmoja tu wakakupatia na ukafanya kazi za Wizara yako zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuwe makini sana. Bilioni 300 za watanzania zinaweza kupotea ndani ya mwezi mmoja kwa sababu ya *bundle* lime-*expire* au muda wa maongezi umeisha muda wake na wakati siyo kosa la watanzania kushindwa kutumia muda wa maongezi. Kusema kwamba hiyo ni biashara, biashara ni nguvu ya *negotiation* na kazi kubwa ya Wizara ni kuwalinda watanzania wasiibiwe na makampuni ya simu. Na Mheshimiwa Mbunge ananipa taarifa, kwa taarifa yake na mimi nimpe taarifa, hiyo biashara ya *bundle* ku-*expire* huko duniani ilishapitwa na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zilizoendelea hakuna biashara ya *bundle* ku-*expire*. Nchi zinazoendelea hakuna biashara ya *bundle* ku-*expire*. Kwa nini Tanzania tunaruhusu

makampuni ya simu yaibe pesa za watanzania kwa sababu *bundle* lime-*expire? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Bashe kwenye Wizara ya Kilimo wakati anaomba hela, ameomba bilioni 750. Hiyo pesa makampuni ya simu yanakusanya ndani ya miezi mitatu tu. Miezi mitatu tu wanakusanya, sisi tunatafuta mwaka mzima wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe Wizara tunayo sheria ya kulinda mlaji (*Consumer Protection Act)* na kazi ya Sheria ile ni kumlinda mtanzania asiibiwe ambaye anatumia bidhaa hii ya simu na mtandao. Mheshimiwa Waziri anatakiwa kuacha *legacy* kwenye hili na ataacha *legacy* kama atahakikisha kwamba anawalinda watanzania waweze kutumia pesa yao ambayo wamenunua *bundle* au wamenunua muda wa maongezi bila *bundle* lile kuharibika. Na ukisema *bundle* lime-*expire* umeshusha thamani ya pesa ya Tanzania. Kwa sababu kama pesa yangu mimi shilingi 2,000…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** iko mfukoni haija*expire,* ina-*expire vipi pesa ambayo iko kwenye simu? (Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana hoja yako imeeleweka vizuri. Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Ninamuita Mheshimiwa Ester Amos Bulaya aweze kuchangia.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, niseme wazi mimi ni Mwandishi wa Habari na nitawasemea wanahabari, changamoto zao nazijua na nimeziishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na kwa kurudi kwako kaka yangu kuna nafuu, watu wamepata *hope* waandishi wenzangu. Na kwa kauli ya Mheshimiwa Rais imetoa *hope* kwa ile kuonesha dhamira. Tunahitaji dhamira Mheshimiwa Waziri yako na Mheshimiwa dhamira ya Rais sasa ije kwenye vitendo kwa kuleta mabadiliko ya Sheria ya Huduma ya Habari ya mwaka 2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wewe unajua mbali ya kwamba kuna unafuu lakini bado kwenye maeneo mengine waandishi wanatishwa. Bado waandishi hawafanyi kazi kwa uhuru. Mheshimiwa Waziri unajua, leo hakuna *investigation story* si kwenye *print media* wala kwenye *electronic media. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hizi Makala ambazo zinaandikwa ni za kawaida. Sheria hii ililetwa kutakuwa na mijadala ya kujenga, ya kukosoa Taifa letu lakini ya kujenga. Tunataka turudi enzi hizo, tunataka tuone Makala za uchunguzi, tunataka tuone vipindi mbalimbali kwenye Redio na Televisheni ambavyo wachambuzi watakuwa huru kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hayo yote Mheshimiwa Waziri hayawezi kutokea kama hakutakuwa na Sheria bora ya kuwafanya waandishi wa habari kwenye *print media* kwenye *electronic media* wanafanya kazi kwa uhuru. Na kufanya kazi kwa uhuru kukiwa na uwazi ndiyo Taifa letu linasonga. Lakini kwa dhamira tu, leo anaweza akamaliza Mama Samia muda wake ana dhamira njema, wewe una dhamira yako ukatoka lakini akaja wengine ambao hawana dhamira njema bado tukarudi kule kule kwa waandishi kuteswa, kwa waandishi kupigwa, kwa waandishi kunyanyaswa, kwa waandishi kunyimwa habari kwa maslahi ya watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe Mheshimiwa Waziri, najua umeanza kukutana na wadau wa habari ni jambo jema. Lakini nilikuwa naomba zile Sheria zenye ukakasi Serikali ndiyo mzichukue, mzibadilishe kwa sababu ndiyo zinawanyima fursa waandishi wa habari. Kwa mfano Mheshimiwa Waziri wewe unajua, natolea tuu mfano kwenye Sheria ya Huduma ya Habari Kifungu cha 19(20)(21) ambacho chenyewe kinazungumzia kinawatambua watu gani ni waandishi wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye tasnia yetu pia tunawahitaji Wanasheria, kuna watu wataandika habari zinazohusu Sheria. Tunawahitaji Madaktari ambao wataandika habari za afya. Tunawahitaji Wachumi ambao watafanya *analysis* ya masuala ya kiuchumi. Lakini kwa sheria hii inataka mtu mwenye *degree* ya Sheria ya udaktari akija aanze tena *degree* ya habari, hapana. Sisi kwetu tuna taratibu zetu, kwa mfano mimi wakati nipo uhuru pale tulikuwa tunasoma *media law and ethics* kwa sababu gani? Tunajua lazima waandishi wa habari wapate *training* mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hawa wakiwepo Wanasheria wamekuja kutaka kufanya kazi ya habari watapewa mafunzo ya miiko, maadili namna gani ya kuandika habari lakini bado wana taaluma zao. Sasa hayo Mheshimiwa Waziri ni mambo ya muhimu sana na leo kwa mfano kuna kina Jenerali Ulimwengu ni Mwanasheria lakini ni Mwandishi nguli. Tuna Kibanda ni Mwalimu *by profession* lakini ni waandishi wazuri. Kwa hiyo, na sisi tunawahitaji watu wa namna hiyo kuja kufanya uchambuzi wa kina kwenye tasnia yetu. Lakini watapewa miongozo inayohusu habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano pia, Mheshimiwa Waziri wewe unajua kuna Kifungu cha 5(e)(8)(9) kinazungumzia masuala ya leseni. Hiki kifungu kinatoa mwanya kwa Mawaziri wenye nia mbaya kufungia vyombo

vya habari. Hiki kifungu ni kifungu kibaya kuliko vifungu vyote, tunaomba vifanyiwe kazi. Gazeti linatakiwa lisajiliwe tu, sasa kila mwaka leseni, kila mwaka leseni mtu ana kampuni hiki kifungu kibaya kinatengeneza mazingira ya kufungia vyombo vya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mzigo mzito kapewa Mnyamwezi wakati hii Sheria mbovu inatungwa ulikuwepo wewe na umeiona na imetestiwa imekuwa mbaya. Mzigo huu unao wewe mwenyewe wahakikishie kipindi kile kilikuwa kingine, hiki kingine, rekebisha hii Sheria sisi waandishi wa habari tunataka tuwe huru, tulikosoe Taifa letu kwa maslahi ya kujenga ili nchi yetu iende kama nchi zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimuita Profesa Kitila Alexander Mkumbo. Ninamuita Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira wakati Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mheshimiwa Benaya Kapinga na Mheshimiwa Masache Kasaka wanajiandaa.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, niungane na wenzangu kuipongeza sana Wizara hii chini ya uongozi mahiri kabisa wa Mheshimiwa Nape Nnauye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada kubwa sana ambayo Wizara hii inafanya katika kuhakikisha kwamba inaimarisha upatikanaji wa huduma wa mtandao wa *internet* bado kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa huduma ya *internet* hususani katika maeneo ya pembezoni kama vile Kigoma, Kagera, Mtwara, Lindi, Tanga pamoja na Mikoa ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kutambua hilo, napenda kuishauri Wizara itambue mbinu mbadala ya

kufikisha huduma ya *internet* Vijijini ikiwemo na Mikoa yote ya pembezoni. Na njia hii ni kutumia *community networks.* Nchi za wenzetu kama Uganga, Kenya, Zimbabwe, Afrika Kusini wamenufaika sana kwa kutumia *community networks* kufikisha huduma ya *internet* kwenye shule pamoja na Vituo vya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu kabisa, ningependa kuiomba Wizara kufanya mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, chini ya *TCRA* Wizara itambue kundi hili la *community networks.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, chini ya *TCRA* Wizara itambue kundi hili la *community networks.* Jambo la pili, Wizara ipunguze gharama za Bendipana kwa *community networks (broadband costs)*. Jambo la tatu, Wizara iondoe *co-location fee* kwa *community networks*. Yaani unakuta *community networks* wakitaka kuweka vifaa vyao kwenye minara ya *UCSAF* wanachajiwa gharama. Kwa hiyo, Wizara iondoe gharama hiyo kabisa kwa ajili ya *community networks* pale ambapo watataka kuweka vifaa vyao kwenye minara ya *UCSAF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne, Wizara itoe msamaha kwa hizi *community networks* kuchangia katika kapu la Mfuko wa Mawasiliano yaani *UCSAF* kwa sababu kimsingi *community networks* hazifanyi biashara, kimsingi *community networks* zinatoa huduma ya kijamii ili kuwezesha shule pamoja na vituo vya afya vya vijijini na mikoa ya pembezoni iweze kuunganishwa na huduma ya *internet*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo langu la pili, naipongeza sana Wizara pamoja na *UCSAF* kwa kazi kubwa inayofanya ya kuimarisha mawasiliano hapa Tanzania. Pamoja na hayo, naomba niseme kwamba, wakazi wa Bukoba Mjini, Mkoani

Kagera wanapata shida kubwa ya mawasiliano yasiyokuwa na uhakika hususan upatikanaji wa mtandao. Naweza nikasema katika kati ya Kata 14 za Bukoba Mjini, Kata nane za *greenbelt* zinapata changamoto kubwa ya mtandao wa uhakika; Kata hizi ni Buhembe, Nyanga, Kahororo, Nshambya, Ijuganyondo, Kagondo, Kibeta na Kitendagulo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa kabisa, ningependa kumwomba Mheshimiwa Waziri, baada ya Bunge hili la Bajeti afike pale Bukoba Mjini ajionee kero kubwa ya mawasiliano ambayo tunaipata. Hapa ningeomba atakapokuja na dada yangu jembe kabisa Mkurugenzi Mtendaji wa *UCSAF*, dada Justina na yeye afike, aone namna gani ambavyo atatusaidia kuimarisha mawasiliano pale Bukoba Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka, naendelea kuipongeza Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya kwenye anuani ya makazi. Hata hivyo, jambo hilo la anuani ya makazi linaleta changamoto kubwa ya kiusalama, usalama wa taarifa zetu binafsi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri aharakishe utaratibu wa kuleta Sheria ya *Data Protection* hapa Bungeni ili tuweze kuipitia na kuipitisha ili kulinda taarifa zetu binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa natambua zipo Asasi za Kiraia ambazo zimeshaanza mchakato huu, kwa mfano, Jamii *Forum* na wengine na tayari ipo rasimu ambayo imeandaliwa. Kwa kazi iliyobaki ni ndogo, Wizara ichukue jitihada ambazo zimeshaanza ilete Sheria ya *Data Protection* hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ni mtumiaji mkubwa sana wa mitandao ya kijamii, naamini anaona namna gani ambavyo wanawake wanasiasa hususan Wabunge wanawake tunavyopitia ukatili mkubwa wa kijinsia mtandaoni. Jambo hili lipo kwenye Wizara yake, nimwombe

Mheshimiwa Waziri atafute namna ya kutulinda kwenye mitandao ya kijamii; kwanza kwa kuhakikisha kurasa zetu za mitandao zinapata *verification* ili kutuondoa katika hatari ya kudukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Neema Lugangira kwa mchango wako kwa ufupi ndani ya dakika tano.

Mheshimiwa Ali Mohamed Kasinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nitumie fursa hii kumpongeza mdogo wangu Mheshimiwa Nape Moses Nnauye kwa kuteuliwa na kuamini na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara hii ambayo kwa kweli Watanzania tuna Imani naye kubwa sana na nadhani ataendeleza pale ambapo rafiki yangu Dkt. Ndugulile aliachia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi, nianze kwa kushukuru Wizara. Jambo langu la kwanza nilipoingia Bungeni ilikuwa ni kuomba mawasiliano kupitia mnara katika Kata ya Likawage, nashukuru Serikali ya Mama Samia imetekeleza hili. Kupitia mchango wangu, niombe kama ambavyo niliomba katika Mkutano wa Sita uliopita kwamba mnara huu ambao umekamilika kule Likawage utakaohudumia Vijiji vya Nainokoli, Likawage pamoja na Liwiti, basi Mheshimiwa Waziri impendeze aende akazindue rasmi na wana wa Likawage wanamsubiri kwa hamu kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo wanasema kushukuru ni kuomba tena. Pamoja na hayo sisi Wanakilwa

tunaendelea kuomba tena kwamba, mawasiliano haya ya njia ya simu bado ni changamoto katika Kata zetu za Nanjilinji, Chumo, Kandawale, Kinjumbi, Kipatimu pamoja na Kikole. Iwapendeze wenzetu wa Wizara hii ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari katika mpango huu wa 2022/2023, Kata nilizozitaja ziingie katika mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umahususi, niseme kwa masikitiko kidogo kwamba, katika Wizara hii eneo la Shirika la *TBC*, Wilaya ya Kilwa pekee katika Mkoa wa Lindi ndiyo ambao hatuna huduma ya *TBC*, wilaya nyingine zote zilizobaki wanapata huduma hii. Impendeze Mheshimiwa Waziri mdogo wangu Mheshimiwa Nape, awaelekeze watumishi wake, watendaji wenzake katika Serikali, katika Shirika hili la *TBC* na siye wana Kilwa tunahitaji kupata taarifa za Habari kupitia *TBC FM, TBC* Taifa na vyombo vingine vya *TBC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nijikite katika ushauri. Tumeona mikakati ya Wizara kupitia taasisi zake zote nane ni mizuri sana. Hata hivyo, kwa upekee nishauri katika eneo hili la mawasiliano kwamba, kwa muda mrefu eneo la mawasiliano limeachiwa sekta binafsi. Imebainika hapa kwamba, muda si mrefu, Mungu akipenda tunapitisha bajeti ya kutosha, lakini pia bado tuna nafasi ya kukusanya makusanyo mengi kupitia taasisi za Wizara hii. Niwashauri Wizara kwamba eneo hili la mawasiliano libebwe na Wizara kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko kutegemea watoa huduma binafsi pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili niseme kabisa kwamba, Wizara itengeneze sera kama ilivyo katika Wizara zingine kwa mfano Wizara ya Maji, Sera mita 400 maji, mita 400 maji; na Wizara hii ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iweke sera kama ni kila kata ama kila kijiji ama kila umbali wa kilometa kadhaa kadri ambayo utafiti na usanifu

utakavyofanywa na wataalam na kuja na hayo mapendekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mohammed Kassinge kwa mchango wako. Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti ya Wizara hii ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Waziri, kaka yangu Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, kwa kazi nzuri anayoifanya na tunaona Wizara hii kupitia yeye imeendelea kufanya kazi nzuri sana. Kama ambavyo tumekuwa tukisema kwamba lazima Watanzania wapate taarifa mbalimbali, lakini kupitia Wizara hii Waziri ameweka utaratibu mzuri na tumpongeze sana kwamba tuliwahi kumwona siku moja kwenye Aridhio akiendesha kipindi cha karibu nusu saa. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri ndugu yangu *Engineer* Andrea Mathew Kundo kwa namna ambavyo anamsaidia Mheshimiwa Waziri; lakini na timu nzima Katibu Mkuu, pamoja na wasaidizi wao wote katika Wizara na Taasisi zilizopo chini ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu ya muda nitakwenda kwenye mambo mawili tu. Nitaanza na jambo la kuhusiana na kuboresha mawasiliano nchini. Tunajua kabisa kwamba kuna baadhi ya maeneo ambayo yamekuwa na changamoto kubwa, Serikali imefanya kazi kubwa sana ya kupeleka minara. Ukiangalia mwaka wa fedha uliopita minara mingi imewashwa na mingine inaendelea kufanya kazi. Nikiwa Mjumbe wa Kamati tumekuwa tukiona kazi

kubwa inayofanywa na Wizara yetu. Naomba tupongeze sana kwa sababu ni jambo kubwa, kupitia *UCSAF* hawa Mfuko wa Mawasiliano kwa wote umefanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo hayana mvuto wa kibiashara, makampuni mbalimbali yalikuwa hayaendi, lakini kupitia mfumo huu wa Serikali yetu na tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutoa fedha za kwenda kusaidia ruzuku ya kuhakikisha inajenga minara katika maeneo mbalimbali ya nchini kwetu. Kwa sababu, mawasiliano ni haki ya kila mtu, leo hii kila mtu kule kijijini bibi, babu naye unakuta ana simu yake anataka awasiliane na mjukuu wake popote alipo. Hili jambo kubwa limefanyika, lazima tuipongeze Serikali kwa kazi kubwa, hata mwaka huu wa fedha tumeona kuna fedha imetengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru sana sisi watu wa Singida Mashariki tulikuwa na changamoto kubwa katika Bonde la Misughaa, tumepata mnara ambao ulishakuwa tayari. Sasa hivi tunamsubiri Mheshimiwa Waziri aje azindue rasmi ili wananchi waanze kupata mawasiliano. Kwenye hili wananchi wanaomba, Waziri aruhusu na kampuni nyingine za simu ziweze kuweka mawasiliano yao kwenye ule mnara ili waweze kupata na mawasiliano mengine; kwa sababu pale ni mnara wa *TTCL* na wanaomba na mawasiliano ya simu zingine ili waweze kuwa na mawasiliano mbalimbali, wengine wanataka *Airtel, Vodacom* na *Tigo.* Naamini kabisa Waziri akifanya hivyo itakuwa na maana kubwa ya uwekezaji wa Serikali pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili, pia niombe sana tuongezewe tena mnara, katika Kata ya Libwa mawasiliano ni mabaya sana, lakini pale Mang'onyi tunataka tupate mawasiliano kwa ajili ya Mgodi wa Shanta ambao unakwenda kuzinduliwa hivi karibuni, kutakuwa na mwingiliano wa watu wengi sana. Kwa hiyo, niombe sana

watuangalie, tuweze kupata minara angalau mingine miwili katika Jimbo la Singida Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili naomba suala la *data*, tuongeze uwezo wa *data* kwa wananchi, inawezekana kukawa na mawasiliano ya simu, lakini *data* zipo chini, kwa hiyo wamezoea *2G* lakini tukiende *3G, 4G*, kama Mheshimiwa Waziri alivyokuwa anasema hapa, wananchi watakuwa na mawasiliano, kwa sababu leo, mawasiliano ni biashara, kila mtu anaweza kuwa anafanya biashara kupitia simu yake hata akiwa kijijini kule. Pia na hilo Mheshimiwa Waziri akilifanya itatusaidia sana kuongeza uwezo katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo ni jambo la mwisho, nataka niongelee kuhusu *TBC*. *TBC* ndiyo Shirika la Umma; Habari ya *TBC* kokote ikitoka ni ya uhakika kwa sababu imekuwa *edited* na Serikali. Baadhi ya vyombo vinafanya biashara, vinaangalia walaji wanataka nini, lakini *TBC* inajenga umoja wa Kitaifa, ulinzi wa usalama wa nchi, historia ya nchi yetu na mambo mbalimbali. Kwa hiyo, *TBC* ikiwa na uwezo mkubwa itakuwa inajenga umoja wa kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba *TBC* imefanya kazi kubwa toka uhuru, lakini leo hii tunaona namna ambavyo tunauhisha; vipindi mbalimbali vinawekwa, bidhaa mbalimbali zinawekwa kupitia *TBC,* lakini Mkurugenzi Ayubu anafanya kazi nzuri sana. Kwa hiyo niombe sana wapewe fedha ya kutosha, uwekezaji wa kutosha, huko kwenye maeneo ya huko nje kwa maana ya kwenye mipaka ya nchi yetu, kuna baadhi ya watu ambao toka wamezaliwa hawajawahi kusikia *TBC* kwa maana ya Kiswahili, wanaongea lugha za nje, wengine wanasema hao ni Wanyarwanda mpaka kwenye uraia tunapata shida, kwa sababu toka wamezaliwa wanasikia Kinyarwanda tu. Leo hii ukiwawekea *TBC* kwa uhakika, maana yake watu wetu utawasaidia kujua *Radio* yao ya Taif ana Televisheni ya Taifa. Kwa hiyo, niombe

*TBC* wapate fedha ya kutosha ili iweze kufanya kazi nzuri ambayo inaendelea kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge naomba kuwatambulisha wageni waliopo hapa jukwaani mchana huu.

Wapo Wageni wawili wa Mheshimiwa Denis Londo, ambaye ni mwanafunzi Argham Isihaka ambaye ni mshindi wa kwanza kitaifa katika mashindano ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, yaliyofanyika Jijiji Dodoma akiambatana na Mwalimu wake. Mwalimu wake Ndugu Ahmed Mbonde. Tunakupongeza sana Mwanafunzi wetu Argham Isihaka kwa kufanya vizuri sana kwenye masomo ya Sayansi na Teknolojia, lakini pia Mwalimu wake ambaye tunaamini utazidi kumwongoza. *(Makofi)*

Pia, tunao watoto 40 na walezi watano kutoka Shirika la Utoto Mtakatifu, Parokia ya Mwenyeheri Kanisa Katoliki, Jimbo Kuu la Dodoma wakiongozwa na Mlezi wao ndugu Simon Kiyenze. Hawa wamekuja kujifunza, wasimame watoto wote na Mwalimu Simon Kiyenze kiongozi wao karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaendelea, nilimwita Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga wakati huo Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi wanajiandaa.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote niungane na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake lakini na wataalam kwa ujumla. Nampongeza Waziri kwa dhati kabisa

kwa hii *operation* ya *postcode*, Mheshimiwa Waziri amekuja muda mfupi tu, lakini kazi aliyoifanya kila mtu ameiona. Kwa kweli hongera sana kwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mbinga, pamoja na pongezi hizi, kwa upande wa Mbinga nina masikitiko kidogo. Kazi imefanyika vizuri, kwa bahati mbaya tumekwenda kuvuruga miradi iliyokuwa inaendelea. Wilaya ya Mbinga ina shida sana ya barabara, barabara hizi za *TARURA* na unajua Halmashauri ya Mbinga Vijijini ni milima na mabonde. Kwa hiyo, kwa muda mrefu barabara zetu zinapitika kwa shida sana. Zipo barabara tulizitengea fedha kwa bahati mbaya sana barabara zile fedha zimeondolewa zimepelekwa kwenye *postcode*. Sasa sijajua kama na katika maeneo mengine kumefanyika hivyo. Kama maeneo mengine haijafanyika hivyo kwa nini sisi Mbinga; Barabara ya Ngima kwenda Litembo ambako kuna hospitali, Barabara ya Mitawa kwenda Ilela na Daraja la Linyani, fedha za miradi hii imeondoshwa imepelekwa kwenye mradi wa *postcode*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kati ya yale mabao na barabara kipi muhimu zaidi, hivi ni nani anaweza kuvumilia kukosa kuona kibao na kukosa kupita njia nzuri kwenda hospitali? Litembo nilisema hapa ndipo tunapotibiwa sisi, barabara hii inapitiwa na Kata nne za Ngima, Mkumbe, Ukata na Kipololo, lakini pia Kata ya Ukilo zote hizi zinatumia barabara hii. Hali ya barabara hii ni mbaya sana. *(Makofi)*

**MHE. ENG. STELLA M MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu. Nani anazungumza Mheshimiwa Injia Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimshtue kidogo kaka yangu, Mheshimiwa Benaya nadhani kwa uchungu wa zile barabara

zilizokosa fedha amesema hata yale mavibao yana haja gani. Kimsingi kwa kweli anuani za makazi ni muhimu na vile vibao ni muhimu, kwa hiyo ningeomba tu kwamba pamoja na uchungu huo lakini tujiweke vizuri kidogo. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, unaamanisha ni taarifa siyo.

**MHE. ENG. STELLA M MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi tuichukulie ni taarifa.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei hii taarifa yake kwa sababu ananipotezea muda wangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kapinga ngoja kwanza Kiti kinatoa maelekezo. Mheshimiwa *Engineer* Mnyanya; maana Kanuni ya 75(1)(2) mpaka (6) ina uratatibu wake kuhusu kusema kuhusu utaratibu. Maelezo uliyoyatoa ni kama taarifa. Je, Kwenye *Hansard* iwekwe kama Taarifa au Utaratibu?

**MHE. ENG. STELLA M MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa nadhani ni vyema ikakaa kama Utaratibu kwa misingi kwamba, jambo ambalo nimesema limevunja utaratibu ni hili la kusema kwamba yale mavibao yana kazi gani wakati ule ni mradi maalum.

**MWENYEKITI:** Basi kama ni kuhusu utaratibu itabidi utaje Kanuni aliyokiuka; ukienda 75(1) inasema; "*Mbunge anaweza kusimama wakati wowote na kusema neno kuhusu Utaratibu ambapo Mbunge yoyote ambaye wakati huo alikuwa anasema atanyamaza na kukaa chini na Spika atamtaka Mbunge anayedai utaratibu ataje Kanuni au Sehemu ya Kanuni iliyokiukwa*".

**MHE. ENG. STELLA M MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Basi tuipeleke kwenye taarifa kwa

udharura wake kwa sababu mimi Mbunge kushika Kanuni zote kwa wakati mmoja unajua tena siyo lazima niwe na uwezo huo, lakini kimsingi naona kuna jambo limefanyika ambalo haliko sawa kwa umuhimu wa Mradi huu wa Anuani ya Makazi tunaozungumzia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Injinia Stella Martin Manyanya. Mheshimiwa Benaya Kapinga, naomba uendelee.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naomba unilindie dakika zangu. Namheshimu sana dada yangu Injinia Stella Manyanya na ndiyo Mwalimu wangu; lakini kwenye hili sijakaa mradi ule ni mradi mzuri, nafikiri kwenye maelezo yangu ya mwanzo sijui hakunisikia, ni mradi mzuri, lakini nilikuwa nahoji hapa, hivi mtu akikosa kusoma kibao na akakosa barabara, yupi ataumia hapa? Ndiyo hoja yangu ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii mwaka 2020/2021 iliondolewa fedha; tukaitengea fedha 2021/2022 inaondolewa tena fedha, hivi kweli kwa sababu zipi za msingi kiasi hicho? Pia nilikuwa nahoji hapa, hivi ilivyofanyika Mbinga ndivyo yalivyofanyika kwenye Majimbo mengine? Kama sivyo, kwa nini sisi tufanyiwe hivyo. Barabara hii inakwenda kwenye Hospitali pekee ya Halmashauri ya Wilaya Mbinga kwa maana ya Hospitali ya Misheni tunayoitumia sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hapa zaidi ya kata tano zinapita hii barabara na barabara hii utafikiri ni palio la ng'ombe, mashimo mashimo, mawe mawe, haipitiki.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, muda wa Mheshimiwa unakaribia kwisha, ngoja amalizie hoja yake anayoongea.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi wananchi wanalazimika kwenda Mbinga ndiyo waende Hospitali ya Litembo, wanalazimika kwenda Mbinga kilometa zaidi ya 30, wakati pale kuna kilometa 10 tu wanafika hospitalini. Mama Mjamzito anaongezewa safari ya kilometa ya zaidi 30, kwa kweli jambo hili limenisikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uzuri wa mradi huu pamoja na mimi naheshimiana sana na Mheshimiwa Nape, lakini nataka kwenye majumuisho anieleze fedha hizi zitarejeshwaje na miradi hii itatekelezwaje, bila hivi mimi nitaondoka na Siwa hii. Haiwezekani hili Siwa mimi nitatoka nalo ni lazima aniambie Mheshimiwa Nape miradi ile inakwenda kuishaje? *(Makofi)* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kapinga.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naam!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kapinga hebu kaa chini, hebu kaa chini kwanza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge.

## KUHUSU UTARATIBU

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 71(j) lugha inayotumika ambayo kwa kiasi fulani inakera. Mheshimiwa Kapinga ninamheshimu sana na ninafahamu bado ni kijana ni Mbunge wa mara ya kwanza, kwenye *record* zetu hakuna

mtu amewahi kuondoka na Siwa, kwa hiyo, wewe utakuwa ni Mbunge wa kwanza kuondoka na Siwa. Hili Siwa ndilo Bunge lenyewe. Kwa mujibu wa utaratibu wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola Siwa hili limewekwa ndiyo heshima yetu, ndiyo tunalolisalimia hapo na ndiyo inayoshika mamlaka ya Spika. Kwa hiyo, wewe ukiondoka na hili Siwa maana yake umeondoka na hili Bunge lote umekwenda nalo Mbinga. Kwa hiyo, ninakuomba tu ama ufute maneno hayo ili uendelee kutoa mchango wako mzuri na mimi naamini wewe ni Mbunge mzuri sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kapinga.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufuta maneno hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante hata hivyo muda wako umekwisha. Tunaendelea awali nilimuita Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, naomba uendelee kuchangia.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kupata nafasi ya kuweza kuchangia. Nami nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara hii. Kutokana na ufinyu wa muda nijielekeze moja kwa moja upande wa mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye taarifa ya Waziri ambayo ameitoa hapa ameeleza kwamba kwenye huu mwaka wa fedha ambao tunaendelea nao kuna takribani Kata 85 ambazo zilikuwa zimepangwa kuweza kujengwa kwenye huu mwaka wa fedha. Kata hizi ni chache sana kulingana na ukubwa wa jiografia ya nchi hii na tukienda kwa mtindo huo maana yake, hatutoweza kuyafikia maeneo yote kwa kuweza kujengwa minara ya mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, minara hii inajengwa kupitia Mfuko wa Mawasiliano wa *UCSAF* minara ambayo inajengwa kwa *UCSAF* minara mingi wamepewa *TTCL* na *TTCL* hawa wanakwenda kwa hali ya kusuasua, tukienda nao hivi tutafikia hatua ambayo hatutaweza kufikia lengo la kujenga hii minara na kuifikisha kwa wananchi kwa wakati. Kutokana na minara hii na *TTCL* kwenda katika maeneo ambayo kibiashara siyo rafiki sana ambayo Maopareta wengine wanaiogopa hii, sasa tunavyokwenda na *TTCL* maana yake hata ule ushindani na kukua kwao kuweza kupata faida inakwenda kuwa ni ngumu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na *TTCL* kwenda maeneo ambayo kibiashara hayana faida kwao ni kama wanatoa huduma matokeo yake *TTCL* wanakuwa hawafanyi vizuri sana sokoni. Nikiangalia kwenye takwimu ambazo tunazo, kwa watoa huduma saba ambao tuko nao, *Telephone Operators TTCL* ni wa pili kutoka mwisho. Kwenye *market share* wa kwanza anaongoza *Vodacom* ana asilimia 30.5, *Airtel* ana asilimia 27, *tiGo* 25.4, *Halotel* 13.3, *Zantel* asilimia Mbili na *TTCL* ana asilimia 1.7. Kwa hiyo, kuweza kushindana kwenye soko imekuwa ni gumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kushindana huku kunakuwa kugumu tuone namna ambavyo tunaweza kubadilisha Sheria kwa *TTCL* ambayo itaweza kuwabeba ili na wao waweze kufanya kazi yao vizuri. Ninashauri Serikali ili kuweza kuwasaidia *TTCL* tuweze kubadilisha Sheria zetu, *TTCL* wabakie kuwa ni wajenzi wa miundombinu peke yake, wasiingie kama *Telephone Operators* kuweza kushindana na haya makampuni mengine kwa sababu, kwenye ushindani tayari wameshaonesha kwamba hawawezi wameshindwa. Tukiweza kubadilisha sheria wao wakawa wanamiliki miundombinu minara hii wanapewa na minara mingine waendelee kuijenga, baada ya hapo hawa *Telephone Operators* wengine wawe wanapanga kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnara mmoja utaweza kupangwa na makampuni matatu mpaka manne, kwanza itasaidia minara kuwa michache, lakini mnara huo mmoja na makampuni mengine yakipanga hapo na huduma zote maana yake hazitaweza kupatikana vizuri na kwa wakati. *(Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam Mbunge wa Sengerema, taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa tu mchangiaji kwamba *TTCL* hata hiyo minara wameshauza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka unaipokea taarifa?

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hiyo. Tuseme tu *TTCL* wakiweza kumiliki hii minara lakini hata pia kwa usalama wa nchi itaweza kutusaidia sana, maana yake tutakuwa tuna uhakika na usalama na udhibiti mzuri ambao tuko nao. Tukienda hivi tuliona hapa miaka kama miwili iliyopita, wenzetu baadhi ya kampuni fulani tulishindwa kupata mawasiliano hapa, lakini tukiwa na uhakika wa *TTCL* kuweza kumiliki hii hapa hakuna mtu ambaye ataweza kufanya chochote kwenye minara ambayo tunayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa hoja yako ambayo nafikiri pia yamepokelewa na Wizara.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, nilimuita Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga wakati huo Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo na Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi wanajiandaa.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia.

**MWENYEKITI:** Nilimuita Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga nasikia sauti ya kiume. Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi nami nitumie nafasi hii kumpongeza Kaka yangu Mheshimiwa Waziri Nape kwa weledi mkubwa anaoufanya katika sekta ya habari. Kwa kweli uongozi wake wa kusaidia Vyombo vya Habari na sekta nzima ya habari tumeuona na mimi nimtie shime aendelee na mwendo huo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina hoja mbili, kwanza ni kuhusiana na utaratibu wa kuambiwa tuombe *loss reports* pale ambapo unapoteza laini za simu. Kwa hapa tulipo kwa sasa hivi, mtu anavyosajili *line* ya simu anasajili kwa kitambulicho cha *NIDA* na anaweka *finger prints* kwa hiyo, utaratibu wa kuambiwa kutafuta *loss reports* wakati umepoteza laini ya simu naona ni utaratibu unaoleta urasimu ambao hauna maana yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani utaratibu huu labda walivyokuwa wanaweka waliwawekea watu wa Mjini, kwa sababu kwa huko Vijijini tunakotoka mtu tu afike kwenye Kituo cha Polisi kwenda kuomba *loss report* ameshatumia zaidi ya Shilingi 10,000 ama Shilingi 5,000 ama Shilingi 15,000 nauli. Anakwenda kutafuta *loss report* ya Shilingi 500 au siku hizi

tunaambiwa kwamba unaweza kuomba kwenye simu, haya ni mambo ya watu wa Mjini Vijijini kule *internet* inasumbua. Mimi sina mashaka na Mheshimiwa Waziri Kaka yangu Nape haya masuala madogo madogo, yanaleta usumbufu mkubwa sana kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hizi simu ndiyo maisha yetu, haiwezekani mtu akatafute *loss report* zaidi ya siku moja, siku mbili awe nje ya mtandao. Namuomba Mheshimiwa Waziri waweze kuangalia utaratibu huu uweze kuondoka, tayari tunatumia kitambulisho cha *NIDA* kwenye kusajili laini zetu. Kwa hiyo, tunaomba utaratibu wa kuambiwa tutafute *loss report* wakati tumepoteza laini ya simu uweze kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze kwenye suala langu la pili kuhusiana na ulinzi wa taarifa binafsi. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 16 inasema: "kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake, maisha yake binafsi na familia yake, unyumba wake, lakini pia heshima na hifadhi ya maskani yake na mawasiliano yake binafsi". *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia habari ya usiri na ulinzi wa taarifa binafsi za mtu. Kwa nyakati hizi ambazo tunazo, simu zetu zinabeba taarifa zetu nyeti na nzito, ambazo hata watu wetu wa karibu hawazifahamu. Simu zetu zinabeba siri zetu, zinabeba ulinzi wa fedha zetu na maisha yetu kwa ujumla ya kila siku, kwa hiyo, tusipokuwa na ulinzi wa taarifa zetu binafsi ni jambo ambalo kidogo linahatarisha. Naomba nieleze kwa lugha inayoeleweka, kwenye ukusanyaji wa taarifa kuna kitu kinaitwa *data collection* na kuna kitu kinaitwa *data processing*. *Data collection* ama ukusanyaji wa taarifa kwa mfano kampuni ya simu inavyosajili laini yangu inachukua jina langu, inachukua makazi yangu ninapokaa na umri wangu na taarifa za msingi

siyo mbaya kwa sababu ni kwa ajili ya kutupatia huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa inapoanza kuchakata taarifa hapo ndiyo ugumu unapokuja. Kwa sababu, inachakata taarifa ina maana *inazi-process* halafu inawapa watumiaji wengine/makampuni mengine kwa kuyauza. Kwa mfano, unashangaa tu unatumiwa *message* za *betting* kwenye simu, ina maana wamechakata wamewapa wale makampuni ndiyo maana tunatumiwa taarifa. Namuomba Mheshimiwa Waziri, Sheria ile ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi lazima ije hapa *Data Protection and Privacy* ili tuweze kulinda taarifa za watu binafsi, lakini taarifa zetu zinazoenda pia nje ya nchi, kwa sababu taarifa zinatumika bila idhini yetu. Vilevile taarifa zinatumika kwa kuwanufaisha wengine bila sisi kutunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kapinga…

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja namalizia. Kampuni za simu zinatupa *terms of conditions* wakati unasajili laini, zile *terms of conditions* zimeandikwa kwa lugha za kisheria na ngumu mno na tunaambiwa tutazikuta kwenye *website*. Kwa hiyo, tunaomba wakati tunasajili laini tupewe ule mkataba wa namna ya matumizi ili tuweze kuelewa kwamba tunaposajili laini tunajiingiza kwenye vitu gani ambavyo vya msingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsantenaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga kwa mchango wako. Sasa ninamuita Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi aweze kuchangia.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yangu Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya, pia ninampongeza Waziri Kaka yangu Mheshimiwa Nape Nnauye kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya, bila kusahau Naibu Waziri ambaye kimsingi mimi kama Mbunge wa Jimbo la Msalala kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Msalala na hasa Kata ya Jana, Kata ya Mwaruguru ndio Naibu Waziri wa kwanza kufika kwenye maeneo haya. Kwa hiyo, nakupongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambayo umekuja kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natamani nizungumzie habari ya mawasiliano katika Jimbo langu la Msalala na Naibu Waziri nadhani kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, alifanya ziara kwenye Jimbo langu la Msalala kuona hali ya mawasiliano katika maeneo yale. Ni kwamba katika Jimbo la Msalala hali ya mawasiliano ni mbovu sana, minara hakuna, hata kwenye Makao Makuu yetu ya Halmashauri bado Watendaji wanapata taabu sana wnapoenda ku-*load document* inabidi sasa wasafiri waende Manispaa ya Mji ili kuweza kufanya kazi zao za kimawasiliano. Naibu Waziri aliagiza na akaahidi kwamba atatupatia minara Saba na wananchi wanasubiri na niombe sasa Mheshimiwa Waziri unapokuja kufanya *winding up* hapa, utueleze ni lini sasa hiyo minara saba ambayo mlitupatia ambayo itakwenda kujengwa kwenye Kata ya Jana, Kata ya Mwaruguru, Kata ya Mwanase bila kusahau Kata ya Lunguye, Kijiji cha Nyangarasa na Kijiji cha Busolega na Kijiji cha Nyamishiga. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa kuna mtu anataka kutoa taarifa kwenye Jimbo la Msalala, yuko wapi?

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa niko huku.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cherehani.

**T A A R I F A**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampa taarifa mwongeaji kwamba eneo la Halmashauri ya Msalala pia linafanana sana na Halmashauri ya Ushetu, hata Makao Makuu ya Halmashauri ya Ushetu hakuna mawasiliano kabisa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Iddi unapokea taarifa?

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea taarifa hiyo basi nimuombe Waziri tu aweze kuona aipe kipaumbele Wilaya ya Kahama katika Halmashauri hizi, kwa maana ya Halmashauri ya Ushetu lakini *special* kwenye Halmashauri ya Msalala kwa sababu Halmashauri ya Msalala ndiyo *key* ya Majimbo yote haya mawili kwa maana ya Jimbo la Ushetu na Jimbo la Kahama Mji. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ninakuomba utakapokuwa unafanya *winding up* hapa uje utueleze ni lini sasa hawa Wakandarasi watakwenda kuanza kazi ya kujenga minara katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu ili uchumi uweze kukua na hasa katika maeneo yetu ambayo tunatoka katika maeneo ya madini, watu wanahitaji kufanya biashara kila

siku hivyo wanahitaji mawasiliano, jana *nili-share* picha moja nikimuonesha bwana mmoja katika Mgodi wa Nyamishiga Kata ya Runguya, ametengeneza kiti kimoja kirefu sana na amekaa juu na watu wamepanga foleni akiwahudumia kupitia simu yake. Hivyo ni kuonesha dhahiri kwamba bado huduma za mawasiliano katika maeneo hayo hazijafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kuzungumzia habari nzima ya maslahi ya Waandishi wa Habari. Kila mmoja wetu hapa anafahamu kwamba kazi kubwa ambayo inafanywa na waandishi wetu hawa wa Habari; na sisi kama Waheshimiwa Wabunge lakini Viongozi mbalimbali huwatumia hawa waandishi wa habari katika kufanya kazi zetu katika maeneo yale, lakini bado Waandishi wa Habari hawa wamekuwa hawana mikataba ya kudumu. Mheshimiwa Waziri ninakuomba nenda kawalinde waandishi wetu wa habari wanafanya kazi kubwa sana, maslahi yao bado ni madogo mno Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona kwamba kwenye msafara mmoja unaweza kukuta una Waandishi wa Habari mathalani 20 na wanafanya kazi kubwa kweli, kila unapokwenda wao ndiyo wa kwanza kushuka na wao ndiyo wa kwanza kukimbia kurudi kwenye magari na mwisho wa siku baada ya hapo Mheshimiwa Waziri wanaishia kupewa Shilingi 20,000, Shilingi 30,000. Sasa nikuombe Mheshimiwa Waziri hebu nenda sasa… *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa endelea kuzungumza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninakuomba Mheshimiwa Waziri nendeni mkaweke mfumo wa kuwalinda hawa Waandishi wetu wa Habari waweze kuwa na mikataba ya kudumu lakini pia waweze kulipwa

stahiki zao kwa muda. Nilikufuatilia siku moja alipofariki Mwandishi mmoja wa Habari, ulitoa maelekezo aweze kulipwa haki zake, lakini mpaka ninapozungumza hivi bado hajalipwa haki zake. Kwa hiyo, ninakuomba Mheshimiwa Waziri Waandishi wa Habari hawa ndiyo wanafanya kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba, wanatangaza mema yote yanayofanywa na Serikali yetu hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimalizie nizungumzie suala zima la bando. Kuna wizi unaendelea kwenye suala zima la bando, ni kwa nini Mheshimiwa Waziri msitusaidie kwa sababu ukiangalia kilio kikubwa cha wananchi kwa sasa ni bando. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii unakwenda kujiunga bando mathalani ya Shilingi 30,000 na wanakuambia kabisa utapata dakika kwa mfano, 2,500 lakini utapata GB 12, lakini kutokana na hali ya uchumi unajitahidi sasa kujibana uweze kutumia dakika zile vizuri lakini hivyo hivyo unajitahidi kubana utumie *MB* vizuri, lakini mwisho wa siku inapofika siku 30 hujui zile dakika zimekwenda wapi? Sasa nikuombe utakapokuja kufanya *winding up* hapo utueleze, hizi dakika ambazo tunazilipia ambayo ni haki yetu ya msingi tumezilipia huwa zinakwenda wapi? *Either* ni Serikalini au zinakwenda wapi, tufahamu sasa hizi dakika zinazochukuliwa zinakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo ahsante sana, mchango wangu mimi ni mfupi sana kwa siku ya leo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi Mbunge wa Msalala. Nilimuita Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, wakati wafuatao wanajianda akiwemo Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mheshimiwa Godwin

Emmanuel Kunambi, Mheshimiwa Zuena Athuman Bushiri na *Engineer* Mwanaisha Ng'anzi Ulenge.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu ya Teknolojia ya Habari kwa ujumla. Kwanza ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Nape pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri *Engineer* Kundo kwa namna ambavyo Wizara hii wanaisimamia kwa karibu sana, wote tunashuhudia utendaji wao wa kazi kwa karibu na mimi ninawatakia kila la kheri na sisi wa Kishapu tutaendelea kuwaunga mkono kuona kwamba jitihada na juhudi mnazozifanya tunapeana ushirikiano wa karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni jambo zima la uanzishwaji wa kitengo cha mawasiliano ambacho kimeanzishwa na Wizara hii na mwezi wa Julai nadhani kinatarajia kuanza rasmi. Kwanza, niwapongeze kwa sababu ni utaratibu mzuri tumeshuhudia kupitia Msemaji wa Serikali Ndugu yetu Msigwa upashanaji na utoaji wa habari kwa umma umekuwa wa hali ya juu na watanzania wamekuwa wakielewa nini Taifa linatekeleza majukumu yake katika masuala mbalimbali Mtambuka. Sasa jambo hili ni jambo la muhimu sana lakini kitu ambacho ninataka nichangie ni kuhusiana na upungufu, ama uhaba wa watumishi hasa katika eneo hili la Kitengo cha Mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu katika Halmashauri zetu 185, Halmashauri 100 peke yake ndizo zina Wakuu wa Idara hii ama Wakuu wa Vitengo hivi, Halmashauri zaidi ya 85 mpaka 86 hazina wakuu hawa wa vitengo hivi. Kwa hiyo, hii ni changamoto kubwa, kama Wizara ina dhamira ya dhati kuhakikisha kwamba vitengo hivi vifanye kazi zake vinavyotarajiwa kwa uhakika, haiwezekani kama hatutafanya jitihada za haraka sana kuona kwamba suala la kuhakikisha kwamba watumishi hawa wanajitosheleza katika Halmashauri linafanyiwa kazi haraka iwezekanavyo. Kwa

hiyo, ushauri wangu Wizara ifanye kazi ya ziada na kwa haraka zaidi kuhakikisha kwamba watumishi hawa wanajitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba kwa sababu katika Halmashauri tuna baadhi ya watumishi ambao fani zao ama wamejiendeleza katika eneo hili la Habari, kuna haja ya kufanya *recategorization* katika Halmashauri zetu kwa haraka zaidi ili Watumishi tulionao katika ngazi za Halmashauri waweze ku-*cover* maeneo haya ambayo yana matatizo na mapungufu ya aina hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya kufanya *recategorization* katika Halmashauri zetu kwa haraka zaidi ili watumishi tulionao katika ngazi za Halmashauri waweze ku-*cover* maeneo haya ambayo yana matatizo na upungufu wa aina hiyo. Kwa hiyo, nilikuwa naishauri sana Wizara iliangalie hili kwa mapana ilimradi lifanyiwe kazi kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, kwa sababu, tunaye msemaji wetu, kama nilivyozungumza Ndugu Msigwa na amekuwa akifanya kazi kubwa sana, nashauri ifanyike jitihada kubwa ya Wizara kuhakikisha kwamba inatoa mafunzo ya kutosha kwa hawa Maafisa Habari ili nao wawe na uelewa wa kutosha na waweze kuwa wanatoa taarifa hizi katika ngazi za Halmashauri kwa wakati ili Umma wa wananchi katika ngazi za Halmashauri wawe wanaelewa Halmashauri inatenda mambo gani na kwa wakati gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ipo changamoto kubwa ambayo nilikuwa nataka nishauri kuhusu nguvu ya kisheria, kwa sababu katika ngazi za Halmashauri wanaokuwa wasemaji katika ngazi za Halmashauri ni Wenyeviti wa Halmashauri na Wakurugenzi wa Halmashauri. Kwa hiyo, hawa wasemaji wanakuwa wasemaji tu labda katika

mitandao ama wakati mwingine wanasimamia tu vitengo vile kwa ajili ya kutafuta Waandishi wa Habari ili waje wachukue habari katika mabaraza yetu. Kwa hiyo, sasa nilikuwa naomba Wizara iweke utaratibu na mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba inakuja na nguvu ya kisheria ili kuwapa mamlaka hawa wawe wasemaji katika Halmashauri zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la mawasiliano na hasa simu. Kata ya Mwakipoya, Kata ya Mwasubi, Kata ya Masanga, Kata ya Somagedi, Kata ya Mwamalasa na Kata ya Itilima ni kata ambazo zina changamoto ya mawasiliano. Mheshimiwa Kundo aliwahi kuahidi kufika kwenye jimbo langu na kuja kuona changamoto hiyo. Kwa hiyo, kata hizi sita zina matatizo makubwa. Nilikuwa naomba sana kata hizi zipate huduma ya mawasiliano. Nimeona katika taarifa ambayo moja kati ya maeneo ambayo yanaenda kupata huduma hii, lakini maeneo haya bado yana changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, usikivu wa *TBC* bado ni tatizo kubwa katika Wilaya ya Kishapu. Naomba sana Wizara ifanye kazi kubwa kuhakikisha kwamba redio hii iwe inasikika kwa wananchi kwa sababu ni redio mama, na inatoa taarifa muhimu, mtambuka kwa ajili ya Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo. Nilimwita Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, aweze kuchangia.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa sababu ya muda, nilikuwa na mambo mengi,

lakini na-*summaries*. Nina suala la uduni wa mawasiliano Malinyi, kuna suala la *cybercrime* kwa maana ya uhalifu wa mitandao, lakini kuna suala la uhifadhi kwa maana ya suala la mawasiliano katika maeneo ya utalii na uhifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu Malinyi, nazungumza hili kwa kurudia kwani mwaka 2021 nililisema, tuna shida kubwa. Mpaka hivi ninavyozungumza mawasiliano hakuna kwenye Ofisi ya Halmashauri. Utendaji kazi kwa watumishi ni changamoto na wananchi wa eneo lile pia wanapata ugumu sana katika kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Kata kama ya Sofi, Kata ya Kilosa kwa Mpepo ambayo iko mpakani inashikana na Namtumbo - Ruvuma, hakuna mawasiliano. Kwa kifupi hakuna hata kata moja ya Jimbo la Malinyi ambapo kuna uhakika unaweza kuwasiliana kwa asilimia 100 au hata 90. Kwa hiyo, naomba Wizara ilichukue hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2021 tulipata mnara kutoka *UCSAF,* namshukuru Mkurugenzi Mashiba, na tuliambiwa tu mchakato unaanza kwa ajili ya ujenzi, walipewa kazi *TTCL,* lakini mpaka leo bado. Namshukuru Mheshimiwa Waziri Nape ameniahidi, sasa ameingia analivalia njuga, kwa hiyo, ninaamini atafanya kitu kwa ajili ya watu wa Malinyi. Kwa hiyo, tunawaamini, naomba mtusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, suala la *TCRA*. Nadhani uwezo wetu wa mitambo ya kisasa kuweza kudhibiti suala la uhalifu mitandaoni bado ni mdogo. Kwa hiyo, kama shida ni bajeti, basi naomba Mheshimiwa Waziri bajeti ijayo ulete tuwe na mitambo ya kisasa kama ya wenzetu huko nje, tuweze kutatua tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mimi mpaka sasa hivi nilipoteza simu, *tablets* na vitu vingine, lakini

wanaendelea kufuatilia, wanasema tunashughulikia. Mpaka simu iwe hewani ndiyo wanaweza wakaipata, lakini nilidhani ingefaa kabisa tuweze kupata hizi *gadgets* hata kama simu imezimwa, basi ionekane iko sehemu fulani, ila inaonekena kama bado tunabahatisha. Kwa hiyo, naomba tu tujitahidi mwakani kwenye bajeti mlete tuwe na uwezo mkubwa kama wenzetu wa nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine hata kwenye mitandao ya *face book.* Watu wame-*forge account fake,* wametengeneza kama ya kwangu tangu 2018, nimelalamika, nimepewa *RB* iko Iringa, nimeandika barua Serikalini, mpaka leo watu wanaendelea kutapeli watu kwenye mitandao, *accounts* za *face book* zinafanya kazi ambazo ni *fake*. Namba za simu ambazo matapeli wanapokea fedha bado zipo hewani. Sasa unashangaa, inatakiwa tufanye nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama shida ni teknolojia, basi mwakani kwenye bajeti muilete, lakini kwa sasa Mheshimiwa Waziri mtusaidie hili jambo liweze kukoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni suala la mawasiliano kwenye maeneo ya utalii na uhifadhi. Maeneo mengi ya misitu *(TFS),* maeneo yetu ya *game reserves,* maeneo ya *National Parks,* kule kwenye vivutio mawasiliano hakuna. Wageni wanatalii; kwa mfano, Mlima Kilimanjaro pale ni maeneo mazuri ya watu kuona. Mtu anapiga picha na video anataka ku-*share* wakati huo huo dunia ione, iweze kutamani na yenyewe kupanga safari za kuja, lakini hawawezi, mawasiliano hakuna kabisa. Kwa hiyo, mtu akienda kutalii anakuwa kama ameenda sijui maeneo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi kuna haja kubwa sana ya mawasiliano yapatikane kwenye vivutio vyote. Kwa hiyo, Mheshimiwa Nape ushirikiane na watu wa Maliasili,

kwenye vivutio vyetu vyote mawasiliano ya simu yapatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa ni suala la vita dhidi ya ujangili pamoja na mawasiliano. Leo tunafanya doria kama za kienyeji niseme kwa Jeshi la Uhifadhi lote, tunabahatisha kutegemea tu nguvu za miguu na wapiganaji wa kawaida, lakini teknolojia ingeweza kurahisisha ujangili kwa maana ya kupiga vita ujangili. Kupitia mawasiliano ya simu ambayo unayafanya ingekuwa rahisi sana kuwa-*track* majangili, lakini leo kwenye vivutio vya utalii hakuna mawasiliano. Kwa hiyo, zoezi la doria linakuwa gumu, tunafanya kienyeji. Teknolojia ingeweza kutatua tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba niishie hapa kwa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi. Kwenye suala la matapeli, hawa wanao-*hack account,* maana hata mimi mwenyewe wameshani-*hack* za kwangu, nimeripoti sana Mheshimiwa Waziri, lakini bado utekelezaji siyo mkubwa.

Namwita Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, *okay*. Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, wakati huo anajiandaa, atafuatiwa na Mheshimiwa *Eng.* Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mheshimiwa Dkt. Pius Steven Chaya na Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe watamalizia.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Mawasiliano, Teknolojia na Habari. Tunatambua kwamba, Habari na mawasililiano ni kila kitu. Bila mawasiliano hakuna biashara, bila mawasiliano hakuna kazi, bila mawasiliano

hakuna kitu chochote kinachoweza kuendelea katika Mataifa yaliyoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama hapa kwa masikitiko makubwa sana kwamba katika Mkoa wa Kilimanjaro kuna baadhi ya Kata ambazo ziko kwenye mipaka ya mikoa ambazo hazina mawasiliano kabisa. Kenya *Safaricom* imekuwa ikitawala maeneo ya mipakani kwa sababu wananchi wa maeneo hayo hawapati mawasiliano ya nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2021 nilisimama katika Bunge hili nikaongelea maeneo ambayo yameathirika sana ikiwepo Wilaya ya Rombo, maeneo yote ya mpakani; Wilaya ya Mwanga, Kata za Kivisini, Jipe, Kigonigoni, Kwakoa na Toloha. Nasikitika kwamba maeneo haya kwanza yana hatari ya wanyama wakali, lakini pamoja na hatari hiyo hawana mawasiliano kabisa, hawawezi hata kujikwamua katika shida wanazozipata kuwasiliana ili wapate misaada. Naiomba Serikali iangalie maeneo yale ambayo ni hatari kwa wananchi ipeleke minara ile ili wananchi wakapate huduma stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama tena hapa mwaka 2021 nikiongea Habari ya minara katika Hifadhi ya Mkomazi. Hifadhi ile inapita barabara ambayo inaenda katika Makao Makuu ya Wilaya ya Same ambayo inategemea Vijiji vya Ndungu, Maore, Kihurio, Kisiwani, Kadando, Mpirani na vingine vingi vya maeneo ya milimani; wanategemea kupita barabara ile kwenda Makao Makuu ya Wilaya. Pamoja na hayo, wafanyabiashara wengi wa maeneo hayo wanaenda kufungasha mali zao Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pametokea na changamoto ya vijana kuvamia maeneo hayo na kuvamia baadhi ya *Land Rover* zinayopita pale kuiba na kupora mali za wananchi. Naiomba Serikali yangu Sikivu iangalie wananchi

wake taabu wanazopata ili ione umuhimu wa kupeleka minara eneo lile ili wananchi wa maeneo yale wapate huduma stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ikumbukwe kwamba hifadhi ile sasa hivi imekuwa na wanyama wengi sana. Tembo kama tunavyosikia na tunavyoendelea kusema kwamba, tembo wamekuwa ni changamoto kubwa sana. Eneo lile zamani nikiwa mtoto, kwa kuwa ndiko nilikozaliwa, lilikuwa linaitwa kambi ya simba. Kwa hiyo, lina wanyama hatarishi. Inawezekana wananchi wakapata matatizo katika eneo la hifadhi, lakini wanashindwa kujikwamua pa kupata msaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, wakati mtakapokuja kuhitimisha hapa leo, mimi sitashika Shilingi, lakini mtuambie ni lini mtapeleka minara katika maeneo ya mipakani ili wananchi wale nao wakapate huduma stahiki? La kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini pia mtapeleka minara katika maeneo ya hifadhi ya *Mkomazi Game Reserve* ili wananchi nao wakaweze kupata huduma stahiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri. Nilimwita Mheshimiwa *Eng.* Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, aweze kuchangia.

**MHE. *ENG.* MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii ya kuchangia. Awali ya yote namshukuru Mungu na nichukue fursa hii pia kuwapongeza sana Mawaziri wanaofanya kazi kwenye Wizara hii ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kazi kubwa wanayofanya kuhakikisha Taifa letu linakua

kwenye uchumi wa kidijitali, na pia kuhakikisha Taifa letu linakwenda kutekeleza kwa ufanisi majukumu yake mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia hapa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri mikakati mbalimbali ambayo wanayo kuhakikisha wanakwenda kuifanya kazi yao kikamilifu. Naomba nichangie kwenye suala zima la usalama mitandaoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri mikakati yake hapa, lakini kitu ambacho sijakisikia ni *intrusion detection system.* Mara nyingi matukio yanatokea halafu ndiyo watu wanaanza kuhangaika wakati tunaweza kutengeneza *tools* ambazo zitagundua mapema kabla mtu hajaweza kuiba. Wakati anataka kuingia kufanya uhalifu wake, *tools* zile zinaweza ku-*detect.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Wizara hii ikafanye kazi zaidi. Naamini weledi mkubwa wa wataalam waliopo kwenye Wizara hii. Tumempata Dkt. Mwesiga, ni mwalimu wangu, naamini uwezo wake katika mambo haya, pia tuna Dkt. Pido, watu wote hawa ni wataalam wazuri, waje na mifumo ambayo itagundua mapema wizi unaotaka kufanyika kabla tukio halijafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshangaa kuona baadhi ya Ofisi za Serikali watu wanaiba mitandaoni wakati tunaweza kutengeneza *intrusion detection system* zikagundua mapema mambo haya. Kwa hiyo, naomba sana katika mikakati yenu, mbebe na hili tuone tunakuja na mifumo ya kugundua mapema kabla jambo halijatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba kusema kwamba, mwaka 2021 mwishoni tumeona kule Iringa, mfanyakazi wa *Selcom* ameweza kuhamisha Shilingi bilioni mbili na zaidi. Maana yake ni nini? Ni kwamba bado kuna

shida ile ile katika wizi wa mitandaoni. Wakati kama Taifa tunakwenda kusema tunataka uchumi wa kidijitali, kuna mwananchi mmoja mmoja anazoroteshwa uchumi wake kidijitali. Suala la wizi wa mitandaoni ni tishio kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewaaminisha wananchi kwamba tunaweza tukahifadhi fedha zetu mitandaoni, lakini bado kuna hali ngumu kwa sababu wizi huo ni mkubwa mno. Kwa hiyo, naomba niishauri sana Serikali ihakikishe haraka inakuja na ile sera. Sera hii imechelewa sana. Katika nchi 54 za Afrika, ni nchi 28 tu ambazo zimekuwa na sera hii na tunataka Tanzania tuwe miongoni mwao, tusisubiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona nchi za Ulaya wana ile *General Data Protection Regulation,* tunataka na sisi kama Taifa twende kwa mwendo huo. Tunahitaji huduma hizi kwa haraka. Wala tusiridhike na yaliyoletwa na *ITU (International Telecommunication Union)* kusema kwamba sisi tumekuwa wa pili kwa usalama mitandaoni. Jinsi ambavyo wamechukua *survey* ya *data* zile, *is wrong*. Huwezi kuchukua kwa kutumia mfumo wa *questionnaire*. Walitakiwa kutafuta uhakika zaidi. Tatizo hili la usalama mitandaoni ni kubwa. Naomba sana kama Taifa tulibebe kwa uzito wake na juhudi hizo ziongezwe kupata mifumo ambayo itagundua tatizo hilo mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, sisi kule kwetu Kilindi tuna shida kubwa mno ya kukosa mawasilioano. Kwanza naipongeza *Vodacom* kwa *initiative* yake ya mfumo ule wa mama; ile *program* ya mama, ya kuhakikisha inatatua tatizo la dharura mama anapokuwa mjamzito. Ndiyo maana halisi ya Wizara hii, kurahisisha huduma fulani za kijamii. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara hii i-*support initiative* ile ya *Vodacom* kuhakikisha inapeleka minara katika

maeneo yale. Kwekivu, Kimbe, kule Kilindi hakuna kabisa mawasiliano. Yule mama mjamzito hata akipiga simu kwa yule dereva, dereva usiku hapatikani saa 8.00 ya usiku, tunatatua vipi tatizo lile? Inakuwaje katika kutatua tatizo la dharura? Tunaomba tupeleke minara ili wale akina mama waweze kutatua tatizo la kukimbia kwenye vituo vya afya kwa haraka zaidi na mapema zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mweshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, Steven Chaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Olelekeita.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nikushukuru sana kwa kunipa hii nafasi, lakini nichukue nafasi hii nimshukuru sana ndugu yangu Mheshimiwa Nape, Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Vilevile niwashukuru sana ndugu zetu wa *USCAF, TTCL* na timu nzima ya Mheshimiwa Nape ambayo kwa kweli wanafanya kazi kubwa. Hatuna mashaka na Mheshimiwa Nape, tunajua alivyo *aggressive,* alivyo *determined* na amedhamiria kubadilisha hii Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nina mambo machache. La kwanza, naomba nijadili kuhusu umuhimu wa hii Wizara. Sasa hivi ukiangalia Tanzania tulipo, Wizara hii ya TEHAMA ndio *engine* ya maisha yetu ya kila siku, ni *engine* ya uchumi, ni *engine* ya mawasiliano, ni *engine* ya kila kitu. Sasa wakati nafikiria ni jinsi gani nakuja kuchangia kwenye hii Wizara, nilikuwa naangalia hii Wizara nai-*position* wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Wizara zote, zinategemea Wizara ya Mheshimiwa Nape. Watu wa fedha wanamtegemea Mheshimiwa Nape, watu wa afya wanamtegemea Mheshimiwa Nape, watu wa kilimo wanamtegemea Mheshimiwa Nape, watu wa maji wanamtegemea Mheshimiwa Nape. Hii ni Wizara ambayo ni *pivotal.* Ni Wizara ambayo ipo *at the center.* Mheshimiwa Nape ni refa anayehakikisha kwamba ili utoaji wetu wa huduma unaotolewa kwa njia ya TEHAMA, Wizara ya Maji, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Afya, unafanikiwa lazima tumwezeshe Mheshimiwa Nape. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu kubwa ni nini? Sisi kama nchi tunahitaji kui-*brand* hii Wizara. Hii ndio Wizara mama, Wizara ambayo imebeba maisha yetu, Wizara ambayo imebeba uchumi wetu. Hapa tunaongea kwa kutumia hii *technology* ni kwa sababu imewezeshwa na Wizara ya Mheshimiwa Nape. Tunatumia vishikwambi ni kwa sababu ya Wizara ya Mheshimiwa Nape. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wito wangu ni nini kwa Serikali? Kwanza nina mambo mawili; la kwanza, ufike muda sasa tufanye *reformation* ya hii Wizara. Hii Wizara inatakiwa kukaa kwenye muundo upi? Hii Wizara inatakiwa ikae katikati i-*coordinate* zile Wizara zote, lakini sidhani kama hiyo *structure,* hiyo *business modal* na *coordination modal* imekuwa *well defined. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishauri Serikali ifikirie upya tunai-*position* vipi Wizara ya TEHAMA ili kuhakikisha kwamba sasa inajionesha na inatoa ile *coordination support* vizuri sana katika Wizara nyingine? Hilo lilikuwa la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwanza nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri. Mwaka 2021 alinitengea fedha kwa ajili ya kujenga minara ya simu kule

Mangoli na Heka kwa kupitia *TTCL* na tayari tumeshajenga ile minara. Mnara wa Mangoli umeshaanza kufanya kazi, mnara wa Hika umeshakamilika na tunasubiri kuuwasha. Bado kuna maeneo yana shida sana ya mitandao. Kuna Kijiji cha Igwamadete, Simbangulu, Mbweko, Magasai, Kapiti na vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii nimshukuru vilevile Mheshimiwa Waziri, katika bajeti hii hivi vijiji vyote ameviingiza kwenye bajeti, nashukuru sana. Wito wangu ni nini? Wengi wameongea hapa, sidhani kama tunahitaji kujenga kila aina ya mnara, *Vodacom, TTCL* kwenye kila Kijiji. Tunahitaji ku-*integrate* hizi *services.* Kwa hiyo, wito wangu kwa Mheshimiwa Nape, kaa na timu yako m-*brainstorm,* mje na *modal* ambayo itakuwa *very cost effective* kuhakikisha kwamba, *Voda, Halotel, TTCL,* watatumia mnara mmoja, hiyo itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Daktari Pius Stephen Chaya kwa mchango wako, sasa namuita Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe aweze kuchangia.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi kwa ajili ya muda ninaipongeza Serikali pamoja na viongozi wote wa Wizara. Mchango wangu utajielekeza kwenye mapinduzi ya nne ya viwanda *Forth Industrial Revolution* nikimaanisha nataka kuongelea teknolojia ya *Block Chain*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla nijielekeze kwenye mchango wangu naomba nitaje baadhi ya maeneo kwenye Jimbo langu ambayo hakuna mawasiliano ya simu. Kata ya

Mkomba yote *especially* kwenye kijiji cha Ntungwa, kijiji cha Mfuto, Isunda, Lwasho, Kata yote ya Kapela na vijiji vyake Lwate, Ntanga, Ntungwa, Mang'ula pamoja na vijiji vingine kata ya Ivuna Kamsamba na Chiluluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuchangia kwenye *block chain* nataka kuongelea kwenye hili eneo ambalo angalau Benki Kuu yetu imeshaanza kuruhusu mazungumzo na baadhi ya vijana wa kitanzania ambao wanafanya kazi kwenye hii teknolojia nataka niseme toka teknolojia hii imeingia kwenye mapinduzi haya ya nne ya viwanda zaidi ya vijana wa kitanzania 1,000,000 pamoja kwamba siyo rasmi wanajishughulisha na biashara hii na kwa miaka minne au mitano ambayo imepita zaidi ya bilioni 300 za kitanzania zimeshafanyiwa *transaction* lakini unaweza ukaona hakuna namna nzuri ambayo Serikali imeweka ili kuendelea ku-*regulate* hizi *transaction* ili iweze kuzichukulia kodi lakini pia ili kuilazimisha hii sekta na tuweze tufahamu tupate takwimu kwamba ni watanzania wangapi ambao wanajihusisha na hii teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hii *Central Bank Digital Currency* nataka nirejee waraka mmoja ambao umepita kama wiki mbili Benki Kuu walitoa, ambao ulikuwa unasema hivi *Ministry and chamber welcomes discussion on CBDC and clip to asset Minister for Finance and Planning Dr.* Mwigulu Nchemba *has challenge an International Conference on Central Bank Digital Currencies and clip to assets to come up with a clear guidance and whatever countries should regulate or supervise clip to assess or discourage their use.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kwamba hapa wanasema *whether* waone namna nzuri ambayo wanaweza *waka-regulate* au wakaamua *kui-discourage* nataka kusema ni ngumu sana kama Serikali kupitia Wizara hii ambayo inasimamia suala hili kama hawataruhusu kutengeneza chombo maalum ambacho watawaita vijana wa kitanzania

ambao wanauelewa waweze kuwashauri waweze kuwasaidia ndipo ambapo watakuja na njia nzuri ya kuweza kuwasaidia namna ya *ku-regulate* kuwepo kwa hii Benki ya hii *CBDC* yaani tupate *Central Bank* ambayo itajishughulisha na mambo ya *digital currencies*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa ngumu kwa sababu gani? Kwa sababu hoja ya *CBDC* huko duniani ni kuwepo kwa *beat coin* (yaani ni kuwepo kwa zile *digital currencies*) hoja na *idea* na *concept* ambayo iko kwenye *block chain* ambayo iko kwenye *digital currency especially* kwenye *beat coin* ndiyo ambayo huko duniani iliibua hii *CBDC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa itakuwa ngumu sana *kui-regulate* na kuipokea hii *idea* ikiwa kama tu kwanza Serikali haijawahi kumiliki hata *coin exchanger* yoyote hapa tunapoongea sidhani kama Serikali wanajua kuna kitu kinaitwa *Binance*, kuna kitu kinaitwa *Remitano local bitcoin*. Tulitamani kuona angalau kuwe hata na *coin exchanger* yoyote ya majaribio ambayo Serikali imefanya vijana hawa wa kitanzania *wana-practice* na *wana-regulate* sasa hatujawahi *ku-regulate* unafikiri Benki Kuu wataichukulia hii namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwenye Wizara hii ninawaomba mtoe *room under Task Force* yako ita vijana wa kitanzania wakupe ushauri hatupotezi chochote kama tutakubali kujifunza. Naomba nitolee mfano mimi nikiwa *form two* mwaka 2004 tulikuwa tunafundishwa kama siyo *form two form three* kuna *topic* moja ilikuwa inasema *globalization*. Tulikuwa tunaambiwa dunia kiganjani *at that time* kulikuwa hakuna *smart phone* unaposema dunia kiganjani tulikuwa hatujui tutamaanisha nini dunia kiganjani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa hivi tuna-*practice* dunia kiganjani bili tunalipia kwenye kiganja, Bunge tunaendesha kwenye kiganja habari ni kwenye kiganja. Kwa

hiyo, hata hili jambo ili *CBDC* iweze kufanyakazi ni lazima kwanza Serikali iruhusu vijana wa kitanzania ni lazima Serikali iwekeze iweze kuleta *coin exchange* Serikali ifungue *wallet* ifanye majaribio kama ambavyo tunaweza tukasema hatuna vita Jeshini lakini tunatengeneza mabomu kwa kujihami tu kwamba likitokea lolote tufanye, kwa hiyo, tungeweza kufanya mazoezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri Rais wa Salvador ambaye anaitwa Naibu Bukin tarehe 17 Mei Jumanne hii ya wiki hii ambayo tuliyonayo aliitisha mataifa 44 duniani akiziita baadhi ya Benki Kuu kwenye mataifa mbalimbali, lakini akiziita na baadhi ya taasisi za kifedha kwenda kushiriki akaunti yake ya *twitter* iko *verified* wataalam wanaweza wakamtembelea wakaona pale unaweza ukatembelea *page* yake Waziri ukaona alichokifanya na majadiliano yote aliyofanya. Rais huyu aliziita nchi mbalimbali Zambia ilikuwepo, Mauritius ilikuwepo, Bangladesh, Mozambique, Morocco, Sera Leone, Senegal, Nigeria, Jordan, Egypt na nchi mbalimbali kwanini sisi nchi yetu hakutokea hata mwakilishi hata mmoja tunapoteza hela nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunaendelea kulalamika tunasema kwamba ajira ni ngumu kwa watanzania ni kweli ajira ni ngumu na tukiwa hapa Bungeni tunalalamika kila wakati kwamba mfumo wetu wa elimu hau-*support* watu kujiajiri lakini tunashindwa kuendana na teknolojia

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Condester

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja tunashindwa kuendana na teknolojia tuliyonayo ili iweze kuwaajiri vijana wengi wa kitanzania na kupoteza mapato. Wito wangu kwa Serikali kwenye bajeti hii unda chombo kwenye Wizara yako Mheshimiwa Waziri Nape ili vijana wa kitanzania waweze

kukushauri na tuweze kuitumia vizuri *Block Chain Technology* naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako wa kuwazungumzia vijana kwenye nchi yetu. mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Edward Kisau Olekeita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi na kuwa mchangiaji wa mwisho nakushukuru sana. Kwanza kabisa nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara hii. Nimshukuru vile vile Mkurugenzi wa *UCSAF* kwa kweli kati ya wakinamama wanaofanyakazi vizuri sana Wakurugenzi wenye *customer care* inayotisha kwa kweli, kwa kweli anatisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiteto tulikuwa na changamoto kubwa sana ya mawasiliano watanzania wa Kiteto kwa miaka karibu 60 ya uhuru walikuwa hawawezi kufuatilia Redio Tanzania na mitandao ni tabu sana alikuja Mheshimiwa Naibu Waziri Eng. Kundo tarehe 21 Januari kwa kweli tume-*drive* kilomita 240 siku moja kuanzia saa mbili ya asubuhi mpaka karibu saa mbili usiku nafarijika sana kwamba kwenye bajeti hii ukurasa wa 145 vijiji 25 Kiteto ipo kwenye mipango ya mwaka wa fedha 2022/2023 nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri nawashukuruni sana kati ya vijiji ambavyo vilikuwa vinasumbuliwa na mtandao Esuguta, Ndotoi, Laiseri, Nsolosidan, Morokitikiti, Engangware, Amey, Lembampuli, Lolera, Emarti, Nati, Magungu, Kinua, Ndirigish, Taigo, Krash, Ndaleta, Orpopog, Mwitikira, Kiperesa, Asamato, Kimana na Songambele na Loltebes zote ziko kwenye bajeti ya Serikali nawashukuru sana. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Taarifa!

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Redio Tanzania ilikuwa haisikiki kati ya wilaya saba ambazo

imepangwa kwamba wataenda ku-*revolutionize* ili na sisi tupate Redio Tanzania kwa mara ya kwanza Kiteto imo nakushukuru sana Wizara hii kwa kweli tuipitishe hii bajeti kwa haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na suala lingine moja tu dogo Mheshimiwa Waziri kumekuwa na mtandao watu wanatupigia simu wanajifanya ni *customer care* wa makampuni ya simu anajifanya anakupigia anakutapeli watanzania tumekuwa tuki-*volunteer* kuripoti hizi namba kwa makampuni hayo hatupati taarifa kwamba ile namba uliyoripoti tumefanya hivi tukifanya hivyo *take them to task* na sisi tutaendelea kuripoti hizi *crimes* ili watanzania wasitapeliwe nakushukuru sana ahsanteni sana na Mwenyezi Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge nataka kuwakumbusha kwamba kwa mujibu wa kanuni zetu utapewa nafasi ya kutoa taarifa kwa idhini ya Spika. Kwa hiyo, Kiti ndiyo kina-*moderate* mjadala, kwa hiyo kuna wakati ukisema taarifa hukupewa pengine usijisikie vibaya. Tumefika mwisho wa mjadala wetu wachangiaji wote wameshamaliza kabla hatujaendelea naomba nilete matangazo machache.

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge tuna wageni 577 wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima Mbunge ambaye ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ambaye yuko pale ambao ni viongozi wa wamachinga Taifa. Hawa viongozi wa wamachinga Taifa wametoka mikoa mbalimbali ya Tanzania hebu pungeni mikono Waheshimiwa Wabunge wawaone. *(Makofi)*

Lakini wako na uongozi wao wakiongozwa na Mwenyekiti wao ndugu Ernest Masanja yuko wapi? Mwenyekiti wao yuko pale yuko na sutikali, pamoja na Makamu Mwenyekiti ndugu Ally Hamis kutoka Zanzibar, pamoja na Katibu Mkuu ndugu Venatus Magayane. Hivi

Mwenyekiti yuko wapi apunge mkono hayupo, makamu mwenyekiti? Wewe ndiyo makamu? Mwakilishi ahsante sana karibuni sana kwenye Bunge lenu Bunge la Tanzania baada ya maelezo hayo ndugu Waheshimiwa Wabunge sasa ninampisha Mheshimiwa Naibu Spika ili aweze kuendelea na *session*.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari - Ndugu Nape Nnauye na Naibu wake *Engineer* Kundo Mathew na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jimbo langu la Moshi Vijijini kuna maeneo ambayo yana changamoto kubwa ya mawasiliano kutokana na kutokuwa na mvuto wa kibiashara na mashirika ya kibiashara (Tigo, Vodacom, Ttcl, Halotel, Airtel) hayajawekeza kwenye maeneo haya. Maeneo haya yanahusisha vijiji vilivyopakana na Mlima Kilimanjaro katika kata za Kibosho Magharibi, Kibosho Okaoni, Uru Kaskazini na Oldmoshi Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishauri Serikali kupitia kwenye Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote iwekeze na kujenga minara ya mawasiliano katika maeneo haya. Kata hizi ni za kimkakati kwani baadhi zina njia za kitalii za kupeleka watalii katika Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuzuka kwa ugonjwa wa UVIKO-19, mikutano ya ana kwa ana ilisitishwa kwa kuwa nchi nyingi zilijifungia ili kulinda raia wao na maambukizi ya UVIKO-19. Majukwaa maarufu ya *Zoom*, *Skype*, *GoToMeetings*, *Microsoft Teams*, na *Google Hangouts* yalitumika kwenye mikutano kwa njia ya mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukwaa haya yamesaidia sana nchi yetu kwa kiasi kikubwa, hata hivyo, haikua rahisi kuandaa na kushiriki matukio mbalimbali kwa njia hii. Moja ya changamoto kubwa zaidi ni gharama kubwa za mtandao wa *internet* na uwezo hafifu wa mitandao. Pia ni kawaida kwenye maeneo yetu kuona upatikanaji wa huduma ya *internet* ikibadilika mara kwa mara kutegemeana na mahali mtumiaji alipo. Kwa mfano, wakati mtu akiwa kwenye mawasiliano, mitandao hukatika mara kwa mara wakati shughuli zikiendelea na kuwaaacha washiriki njia panda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hizi, ninaishauri Serikali iboreshe miundombinu ya mawasiliano katika maeneo yote muhimu hapa Tanzania. Maboresho haya yatasaidia kuifungua nchi hasa kwa kuzingatia kuwa tunategemea kupata watalii wengi baada ya kampeni ya Rais ya *Royal Tour.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili unahusiana na huduma za habari na mawasiliano kwa watu wenye ulemavu wa usikivu (viziwi) nchini Tanzania. Kwenye hili bado kuna changamoto licha ya juhudi za Serikali za kulisaidia kundi hilo lipatiwe huduma. Viziwi ni moja kati ya makundi ya watu wenye ulemavu wanaohitaji huduma maalumu kupata habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo waliyonayo viziwi huwakwaza katika mawasiliano katika mazingira wanayoishi na hivyo kuwaathiri kwa njia nyingine mbalimbali katika nyanja za elimu, mahusiano na maendeleo ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa matatizo ya viziwi ni ya kimawasiliano na kwa hiyo hayaonekani kwa macho, viziwi wamekuwa wakikabiliwa na tatizo la kusahaulika katika utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali iwekeze kikamilifu na kuweka miundombinu na rasilimali watu ya kutosha ili kundi hili lipate haki yao ya msingi ya kupata habari na kuwasiliana na jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezuka tabia mbaya ya kusambaza taarifa za uongo kwenye mitandao ya *YouTube* na matapeli wa mitandao ya simu kwa kutumia majina ya watu maarufu. Baadhi ya taarifa zimesababisha kero, usumbufu na kuvunja heshima na haki za kibinadamu kwa wahusika kwa kuwasingizia mambo yasiyo na ukweli. Suala hili linasababisha taharuki na kuvuruga haki za kibinadamu kwa walengwa. *Video* hizi za *YouTube* husababisha hasara kwa watumiaji kwani watu hugharamia kununua *bundle* na kuishia kupata habari potofu. Matapeli wa simu wanaotumia majina ya watu maarufu hutapeli watu na kuomba fedha haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali ichukue hatua za haraka kukabiliana na tatizo la taarifa za uongo za waandishi wa *YouTube* na matapeli wa simu kwa mtazamo wa kulinda haki za binadamu kwa waathirika ikizingatia misingi ya kisheria na kisera inayosimamia tasnia ya habari Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na *TCRA* iweke utaratibu wa kuwabaini na kuwachukulia hatua waandishi wanaokiuka maadili kwenye mtandao wa *YouTube* na matapeli wa simu. Adhabu kali zikitolewa, mambo haya yatapotea kwenye jamii yetu ya Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali imeandaa sera na sheria kwenye sekta za TEHAMA, sayansi na ubunifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Serikali iweze kuisimamia vizuri sekta ya TEHAMA tunahitaji kwa haraka sana kuanzisha *ICT Professional Regulation (ICT Commission* haijafanya kazi ya kufanya *regulations*) imara kama wenzetu kwenye sekta zingine mfano wahasibu, afya, na kadhalika. Tumeona CAG akiibua mambo kibao kuhusu mifumo yetu ya taarifa/TEHAMA tunaweza kuhakikisha maadili na weledi kwenye sekta ya TEHAMA bila kuwa na Bodi ya kuwasimamia waatalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna mwingiliano mkubwa wa majukumu kati ya baadhi ya taasisi za Serikali mfano *TCRA, eGA, COSTECH, ICT Commission* na Wizara za Utumishi, Elimu na Mawasiliano. Ni vizuri tukawa na taasisi moja inayosimamia au kupunguza mwingiliano na kutumia vizuri rasilimali

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru Serikali kuanzisha matukio mbalimbali ya kuinua vipaji *(innovation weeks)* kwa mfano MAKISATU ambapo vijana wameonesha matumizi ya TEHAMA na ubunifu mwingine kusaidia sekta za elimu, afya na kadhalika. Changamoto kubwa ni kuweza kuwa na mfumo mzuri wa kitaasisi na endelevu wa kuwatambua na kuwaendeleza wale wenye *products/innovations* ambazo zitakuwa na faida kwa vijana hawa na Taifa kwa ujumla. Iko wapi *Silicon Valley* ya Tanzania? Ahsante.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa kazi nzuri lakini zaidi ushirikiano kuanzia Wizarani hadi watu wa Mfuko wa Mawasiliano na *TCRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafinga tumekuwa wanufaika wa *TCRA,* wameshatusaidia katika shule ya msingi mchanganyiko ya Makalala yenye watoto wenye mahitaji maalum na pia shule ya sekondari Luganga tumeshapata vitendea kazi kutoka *TCRA*. Lakini pia nimeona kwenye bajeti

Kata za Wambi na Bumilayinga zitapata minara. Ni kata muhimu kwa sababu Wambi ndipo yapo Makao Makuu ya Halmashauri na Bumilayinga tumejenga Kituo cha Afya, hivyo ni muhimu kupata mawasiliano. Aidha, *TTCL* wamekamilisha mnara katika Kijiji cha Itimbo, bado kuwasha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nina maombi *TCRA* kwa ajili ya shule mpya ya sekondari ya Upendo ili tuwasaidie vitendea kazi vya TEHAMA.

Pia ninashauri kulitizama kwa ukaribu Shirika la Magazeti ya Serikali kwa kuwawezesha mtambo ili waweze kuchapa magazeti yao kwa rangi na hivyo kuwawezesha kushindana katika soko. Aidha, *Managingi Editor* anakaimu nadhani toka ambaye sasa ni Katibu Mkuu aondoke, Bi. Tuma Abdallah amekulia *TSN,* nadhani ni wakati sasa kumthibitisha ili kumpa morali na ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TBC Radio,* wananchi wa Mafinga wanatamani mno kupata matangazo ya *TBC* lakini inasikika kwa taabu mno, hata redio nyingine hazisikiki, wananchi wa mji huu wa kibiashara kutokana na biashara ya mazao ya misitu wanaomba basi hata redio nyingine zisikike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBC Tv* kwa kweli kazi nzuri, ubunifu wa hali ya juu wa vipindi, nawapongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa kwa kuchangia kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwa moyo wangu wa dhati kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayofanya hasa katika kuwezesha uhuru wa vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii Mheshimiwa Nape na Naibu wake Mheshimiwa Kundo kwa jitahada kubwa zinazofanywa na katika Wizara hii na Serikali ya kuboresha sekta ya habari na mawasiliano nchini bado mkoani Rukwa hususani Jimbo langu la Kwela kuna changamoto bado zinatukabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumfahamisha Mheshimiwa Waziri kuwa Mkoa wa Rukwa ni takribani miaka mitatu sasa hatuna *reporter* wa *television* ya Taifa *(TBC)* toka aliyekuwa *reporter* Mzee Nswima Ernest kustaafu. Mheshimiwa Waziri ifahamike kuwa *TBC* ni kituo kikubwa cha habari katika Taifa letu, hivyo kutosikika kwa takribani miaka mkoani kwetu tunapoteza fursa nyingi zikiwemo za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Waziri kuwa katika Jimbo langu kuna maeneo ambayo mawimbi ya *TBC FM* hayakamati kabisa katika Kata za Milepa, Lusaka na kadhalika, wanapata habari za *TBC* kupitia runinga kwa wale wenye ving'amuzi ambao ni kundi dogo sana hasa wale waliokaribu na miji changamfu. Mkoa wa Rukwa una vivutio vingi vya kiutalii kama *Kalambo falls,* fukwe za Ziwa Tanganyika, *game reserve* na Ziwa Rukwa, lipo Ziwa Kwela na vivutio vingi vya asili vitokanavyo na desturi na tamaduni za Wanarukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa *TBC FM* kwa baadhi ya maeneo, tumepunguza wigo wa kutangaza utajiri wa mkoa wetu kwa ukosefu wa *TBC reporter* na kutokuwepo kwa mawimbi ya *TBC FM* katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni baadhi ya vyombo vya habari vilivyo nje ya Mkoa wa Rukwa kutoa habari zisizo na uhalisia, zenye maudhui ya kutisha wageni na hata wawekezaji juu ya Mkoa wa Rukwa na kusababishia mkoa hasara za kiuchumi. Kwa mfano vyombo

vingi vya habari vimekuwa vikitoa maudhui mbalimbali kwa kutumia jina la Sumbawanga vikihusisha matendo ya kishirikina na uchawi jambo ambalo si sahihi na halipaswi kufumbiwa macho na taasisi kama *TCRA* na nyingine zenye mamlaka husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumuomba Mheshimiwa Waziri apokee changamoto na tatizo kubwa la huduma za mitandao yaani kukosekana kwa minara ya simu inayofanya kazi kwa saa 24 kwa baadhi ya maeneo ya Jimbo la Kwela lililopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa. Kwa mfano kuna tatizo sugu hasa Kata ya Milepa kwa Vijiji vya Milepa, Kinambo, Msia, Kisa na Talanda. Mnara uliopo Kijiji cha Milepa ambacho ndipo yalipo Makao Makuu ya Kata haufanyi kazi saa zote kwani unafanya kazi kwa saa tano tu yaani unawaka kuanzia saa 3:30 asubuhi hadi saa 9:00 alasiri unakuwa umezima na siku kukiwa na mvua au mawingu basi mnara huo hauwezi kuwaka kwa siku nzima tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijiji hiki kinazo taasisi zinazohudumia wananchi kikiwemo Kituo cha Afya Milepa, Kituo cha Polisi, kituo cha kukusanyia mapato ya Halmashauri kilicho na Pashine ya kukusanyia mapato *(POS machine),* sekondari ya kata, shule za msingi zipatazo sita na ofisi za utawala ngazi ya kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma hizi zote zimefungiwa mifumo ya malipo na ya mawasiliano kupitia mitandao, hivyo kuanzia saa 9:00 alasiri hadi kesho yake saa 3:00 asubuhi hakuna huduma inayofanya kazi kupitia mtandao na hivyo husababishwa huduma zote za umma kuzuiwa kufanya kazi kupitia mitandao ikiwa ni pamoja na kutoa risiti zote kupitia mifumo kuanzia huduma za malipo ya ushuru. Usajili wa wagonjwa kimfumo, kutoa risiti kwa wagonjwa wanapokuwa wanataka kulipia gharama za matibabu, kutoa taarifa mbalimbali za kiuhalifu polisi, kutoa taarifa zozote kwenye

Idara za Elimu na Utawala yaani huduma hizi zote husitishwa kutokana na mnara kuzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi zimetokea kesi mbalimbali na kupelekea vifo hasa kwa akina mama wajawazito baada ya kukosekana mawasiliano pindi wanapohitaji huduma ya gari la wagonjwa lililopo Kituo cha Afya Milepa ili likawachukue wajawazito walioshindwa kujifungua kwenye zahanati zilizopo nje ya kituo hicho, lakini huduma hiyo hukosekana kutokana na kutokuwepo kwa mawasiliano kunakotokana na kuzima kwa mnara wa Vodacom ambao ndiyo mnara pekee uliopo kijiji hiki cha Milepa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo hiki cha afya kinahudumia kata zipatazo saba zenye zaidi ya wakazi 108,700 lakini eneo wanalolitegemea kupata huduma muhimu ndilo hili ambalo tatizo la mtandao ni shida kubwa sana. Kutoka Kata ya Milepa kilipo Kituo cha Afya hadi kata ya mwisho ambayo ni Kilangawana ni zaidi ya umbali wa kilometa 125 hivyo utaona ni namna gani mgonjwa hasa mama mjamzito endapo mawasiliano yatakuwa hayapo atakavyoshindwa kuokolewa mapema pindi uhitaji wa gari utakapokuwa unahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo madaktari wanapofanya huduma kubwa hasa za upasuaji huhitaji wakati mwingine kuwasiliana na madaktari bingwa hasa linapotokea tatizo kubwa lakini hushindwa kufanya hivyo kutokana na aidha muda huo kunakuwa hakuna mawasiliano. Pamoja na tatizo hili kuwepo, umeme wa *REA* upo na umepita umbali wa mita 400 kutoka mnara ulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine yenye changamoto za kukosekana kwa mawasiliano kwa njia ya simu ni pamoja na vijiji vya Kizumbi, Kamnyaza na Mpembano Kata ya Lusaka, vijiji vya Katoto na Kazi Kata ya

Lyangalile; vijiji vya Zimba, Misheni Kata ya Zimba; vijiji vya Mtetezi na Kapewa Kata ya Mpui na vijiji vya Msila na Kasekela Kata ya Mfinga vyote vipo ndani ya Jimbo la Kwela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba msaada wa haraka ili kuwasaidia wananchi hawa katika sekta ya mawasiliano kimtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. JUMA OTHMANI HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwako kwa kinipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Makadirio na Mapato ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknnolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimaye kuiwasilisha hotuba hii katika Bunge lako tukufu kwa ufasaha na umakini mkubwa. Hii ni miongoni mwa Wizara muhimu sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo; nikianza na usikivu hafifu katika baadhi ya maeneo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi zinazochukuliwa kwenye tasniya hii ya habari, hivi sasa ulimwengu uko kiganjani. Wananchi wote wanahitaji kupata habari ya kila kinachotokea nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado mpaka leo kuna maeneo katika nchi yetu hawapati habari. Bado usikivu wa

habari katika maeneo yao si wa kuridhisha. Ushauri wangu katika jambo hili kwa Serikali ni kujitahidi kurekebisha hali hii ili wananchi wa maeneo husika wapate haki ya kujua matokeo yanayotokea katika nchi yao na ulimwenguni kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa redio jamii, naipongeza Serikali yetu kwa kutoa uhuru wa habari. Uhuru huu umewasukuma wananchi katika maeneo kadhaa kufungua redio za kijamii. Redio hizi zinasaidia sana katika maeneo hayo. Lakini bado redio hizi uwezo wake ni mdogo sana, haukidhi matakwa ya redio hizo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika jambo hili kwa Serikali ni kuiomba iweze kuweka mpango maalum wa kuzitambua na kuzisaidia redio hizi ili ziweze kukidhi malengo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nimpongeze Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu na Msemaji Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuendeleza mchango wangu kwa kuwashukuru *TBC* kutangaza Wilaya yangu ya Nyasa kupitia *TBC1* na *Safari Channel* chini ya uongozi wa Dkt. Ryoba. Navishukuru pia vyombo vingine vyote vya habari kwa kuwa si rahisi kukitaja kila chombo vikiwemo vyombo vva habari mtandao *(online)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia uboreshaji wa mawasiliano katika Wilaya ya Nyasa, eneo la Kata ya Linga, Mbaha, Kijiji cha Ndonga na Njambe, Mpepo, Kihulunga, Ng'ombo na Mtupale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi maalum ni kuwa tulipata ufadhili wa kompyuta kwa ajili ya shule ya Tingi, lakini

kutokana na mtandao kuwa chini mradi huo unataka kusimamishwa tumepewa miezi miwili tufuatilie uboreshwaji wa mawasiliano hayo. Aidha, Maafisa Habari wanafanya kazi kubwa lakini hawana vitendea kazi vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha kwako maombi ya Wanamufindi kukuomba upatikanaji minara kwenye maeneo yenye kero kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuomba minara ya simu maeneo yafuatayo; Kata ya Maduma, Kata ya Kasanga Makao Makuu ya Kata, Kata ya Kiyowela, Kata ya Makungu sehemu za Kitasengwa, Kata ya Igowole sehemu za Kisasa na Ibatu na Kata ya Nyololo katika baadhi ya sehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna maombi ya kompyuta ili kuunga mkono sera yetu ya *Make Mufindi Digital.* Niombe kompyuta 500 kwa ajili ya shule 10 za kuanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia, ya Habari kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Spika, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa hotuba nzuri iliojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Serikali katika utekelezaji wa ustawi wa jamii na maendeleo endelevu na hii ni mojawapo ya nguzo kuu katika utayari wetu wa ushindani wa Kimataifa *(national competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu".

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na taarifa ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaonesha kuna mafanikio makubwa kwenye sekta za habari, mawasiliano ikiwemo mikakati ya kupunguza gharama za mawasiliano kwa wananchi. Utendaji kazi ulilenga pia kuboresha miundo ya TEHAMA kuwezesha mwelekeo mzuri wa kulea ubunifu ili Tanzania iendane na kasi ya dijitali ya kiuchumi *(digital economy)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza msukumo mkubwa kwenye kuendeleza maboresho ya mtandao wenye kasi zaidi na kuhakikisha matumizi mazuri ya *Data Center* ili kuwezesha ubunifu wa miundombinu ya TEHAMA hasa Serikalini iweze kusomana. Kutokana na kuwepo mifumo tofauti kwenye taasisi za Serikali ni muhimu sana kuunganisha mifumo yote iweze kusoma ili kuleta ufanisi unaoendana na dunia ya leo. Mwelekeo wa dunia ya leo ni kufanya shughuli zote za ki-TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuboresha muundo wa Wizara na Taasisi zake ili kuwepo na idara

mahususi itayoongozwa na Afisa TEHAMA Mkuu *(CIO)* ngazi ya Kamishna. Kuwepo kwa muunganiko wa mifumo yote *(Core Government System),* ni muhimu kuboresha *e-government* na itawezesha ufanisi na kupunguza gharama kwa kiasi kikubwa sana. Kuwepo kwa Mkongo wa Taifa na *Data Center* ni fursa kwa kuwezesha kutengeneza mfumo wa kuratibu na kuendeleza ubunifu katika TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, teknolojia imewezesha huduma ya kifedha juimishi *(financial inclusion)* na hii fursa pia kwa Serikali kuratibu miamala ili iwe sehemu ya mfumo rasmi wa malipo kwa usimamizi wa Benki Kuu na *TCRA*. Napendekeza maboresho kwenye tozo za miamala itakayoongeza mapato ya Serikali lakini ikizingatia kupunguza mzigo kwa wateja. Serikali kwa kushirikisha wadau, itumie uzoefu wa sasa kuboresha huduma za miamala kwa kuoanisha ufanisi kwa huduma ya kifedha juimishi na tozo mbalimbali na mchango wa huduma hii kwenye kukuza uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio makubwa ya utekelezaji wa Wizara ikiwemo zoezi la postikodi, kuna maeneo mengi ambayo bado hayajapata huduma za minara ya mawasiliano na hata kwenye maeneo kadhaa yenye minara katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya hayapati huduma ya mawasiliano. Vijiji vingi ikiwemo katika Kata za Ulenje, Iyunga Mapinduzi, Mshewe, Mjele, Ilembo na Ihango havina minara na vingine kuna minara ambayo kwa muda mrefu haina mawasiliano. Kwa kuzingatia lengo la kupeleka TEHAMA kwa kila shule, Serikali iharakishe kujenga minara maeneo yote kwenye vijiji na vitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, rejea kiambatanisho cha miradi (minara itakayojengwa mwaka 2022/2023) kwenye hotuba *(soft copy)* iliyo katika

Wilaya ya Geita Jimboni Busanda inaonesha Bujila na Nyamalimbe ambayo ni ya mwaka uliopita 2021/2022, kitabu cha hotuba kinaonesha kiambatanisho sahihi ambapo inaonesha ujenzi utafanyika Nyakagomba (Kata ya Nyakagomba) na Msasa (Kata ya Busanda) mwaka 2022/2023. Naomba kiambatanisho kwenye *softcopy* ya hotuba irekebishwe ifanane na *printed hard copy.*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa kwa mamlaka ya kiti naongeza muda mpaka hapo tutakapomaliza shughuli zetu za leo Mheshimiwa Naibu Waziri dakika tano.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii nami nichangie katika mapato na matumizi ya mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Habari na Teknolojia ya Habari. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwa na afya njema, lakini vile vile nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini katika nafasi hii ya Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile nishukuru Bunge lako Tukufu kwa kuendelea kutupatia mchango mawazo maoni ili kuhakikisha kwamba tunaendelea kuboresha katika utekelezaji wa majukumu yetu. Lakini sambamba na hilo nawapongeza sana na kuwashukuru watendaji wote wa Wizara vile vile wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri wangu Mheshimiwa Nape Mose Nnauye lakini vile vile namshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais Dkt. Mpango pamoja na Waziri Mkuu pamoja na Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu lakini pia natambua mchango mzuri sana ambao umetolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wakichangia bajeti yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kabisa kwamba muda hautoshi lakini natambua michango ya Waheshimiwa Wabunge inalenga kwenda kutatua changamoto za wananchi walioko katika Majimbo yao. Lakini tunasema kwamba ili nchi yoyote iweze kuendelea ni lazima kwanza tuwe na huduma bora na za uhakika, lakini kabla ya kuwa na huduma bora za uhakika ni lazima tuwe na miundombinu ambayo inaweza kutoa huduma hizo lakini pia tuwe na sera safi tuwe na utulivu wa kisiasa na sheria nzuri lakini haya yote yanawezekana kutokana na kiongozi mahiri mwenye maono na anayetaka matokeo chanya kwa watanzania ambaye sasa tunaye Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kweli mambo mengi yanafanyika kwa kasi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu zifuatazo; mwaka huu pekee minara 488 inaenda kufanyiwa *upgrading* ambayo ni takriban bilioni 9.76 ambayo imeandaliwa. Lakini vilevile tuna dola milioni 150 ambayo inaenda kutekeleza mradi wa Tanzania ki-*digital* ambapo ukiangalia ni minara 763 inaenda kujenga. Lakini vilevile kuna minara ambayo tayari imeshajenga takriban 161, kuna minara ambayo haijawashwa imeshakamilika 181. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yakishakamilika changamoto zote za Wabunge ambazo leo wameziongea hapa zitakuwa zimeisha kama siyo kupungua kwa kiasi kikubwa sana umeshuhudia Waheshimiwa Wabunge wamesimama hapa wameongelea namna ambavyo tumefika kwenye majimbo yao lakini vile vile maeneo ambayo tumefika katika majimbo yao wamejionea katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri maeneo yao yamejumuishwa katika bajeti yetu. Kwa hiyo, tuwaombe Waheshimiwa Wabunge tuendelee kushirikiana kuhakikisha kwamba tunaendelea kujenga Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa ambacho naweza kuongea hapa ni uelekeo wa Tanzania tunayoenda nayo sasa ni Tanzania ya kidigitali na Tanzania hii inaendana sambamba na ujenzi wa miundombinu ambayo inaenda kutoa huduma hizi. Miundombinu hii ni pamoja na Mkongo wa Taifa, ni ujenzi wa minara kama ambavyo nimetaja, katika zoezi la anuani za makazi na *postcode* ambalo Mheshimiwa Waziri ameongoza timu yetu ya Wizara kuhakikisha tunafikia kiwango cha asilimia 106.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa majukumu yetu haya ni utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi ukurasa wa 98 Ibara 61(j)na(m) ni katika kuhakikisha tunaweka mawasiliano kwa Watanzania ili waweze kufanya biashara zao, waweze kuwasiliana kwa sababu tafsiri yetu ni kwamba mawasiliano ni uchumi, mawasiliano ni usalama na mawasiliano ni haki ya kila mtanzania kuipata. Na sisi wasaidizi wa Mheshimiwa Rais tunaenda kwa kasi kweli kweli kama ambavyo yeye mwenyewe ametuelekeza tufanye kwa utashi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyagusia naomba niyajibu kwa haraka haraka. Suala la *TTCL* ambalo limegusiwa na Mheshimiwa Tabasamu *TTCL* hawajauza minara na kama ambavyo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba *TTCL* tunaenda kuiwezesha ili ikasimamie miundombinu yote ya kimkakati ikiwemo na ujenzi wa minara na usimamizi na Mkongo wa Taifa minara yote na miundombinu mingine yote ya kimkakati *TTCL* inaenda kusimamia. Kwa hiyo, niliomba niweke ufafanuzi kwa namna hiyo katika upande huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile naomba nitolee ufafanuzi jambo moja ambalo liliongelewa na Mheshimiwa Zuena Mheshimiwa Bushiri. Kwenye suala la Mkomazi tayari tumeshaliingiza katika utekelezaji kwa bahati mbaya katika

bajeti iliyopita tulililingiza kwa bahati mbaya watoa huduma hawakuweza kulichagua lakini tumeliingiza kwenye mpango mahsusi wa *National Parks* ambapo sasa tunaenda kuhakikisha kwamba tunaweza utaratibu maalum ili mtoa huduma lazima apatikane kwa ajili ya kufikisha mawasiliano katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile suala jingine ambalao nimeona Mheshimiwa Condester Sichalwe ameliongelea kwa sababu ameongelea masuala ya teknolojia na sisi tunahakikisha kwanza tunaweka Sera safi ambayo ni wezeshi wawekezaji waweze kuja lakini vile vile katika *force industrial Revolution imaging technology* hatuwezi kuzikwepa kwa sasa. *Imaging technology ni kama vile Artificial Intelligence, Block Chain Technology, Internet of Things* haya yote tunaenda kuhakikisha kwamba tunaweka mazingira rafiki ili yote yaweze kufanyika kwa sababu…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** …na sisi ndiyo uelekeo wetu wa Tanzania kwenda katika Tanzania ya kidigitali…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, majibu mazuri!

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Nape karibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Kwa muda toka asubuhi tumekaa hapa tukiwasikiliza ushauri wenu, maoni yetu na

maelekezo yenu. Niwahakikishie mimi na timu yangu tutayazingatia na kuyatekeleza ipasavyo. Maelekezo mengi na ushauri mwingi uliotolewa hapa mwingi umejikita kwenye maeneo makubwa mawili, yapo maeneo yanayogusa Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali tunazotumia katika kuendesha maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili limegusa utendaji wa Serikali, Wizara na Taasisi tunazoziongoza. Kwa sababu ya muda, siwezi kugusa zote lakini niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, Wizara imeandaa Semina kabla ya Bunge hili kuisha kwa maana ya kipindi hiki. Tumeandaa Semina na baada ya kusikiliza michango yote hii Semina tutakayoiandaa itagusa maeneo yote waliyoyazungumza Wabunge ili tukazungumze kwa uwazi, kwa upana, tuone namna ambavyo tutachukua mawazo ya Wabunge. Tutaona hali ya Serikali, halafu tufanye maamuzi yenye tija. Kwa hiyo niwahakikishie, hakuna mchango ambao umepotea, yote tutahakikisha tumeichukua, tumeizingatia na tutaifanyia kazi. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge Semina hiyo itakapotangazwa tushiriki, tuje na maoni hayo, Wizara na Taasisi zetu na wadau wote tutakuwepo kwa ajili ya kuyaweka mambo haya sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo hoja juu ya namna ya kwenda kwenye uchumi wa kidigitali. Tumeeleza hapa jumla ya bajeti yetu inataka kutupeleka kwenye uchumi wa kidigitali wa nchi yetu, sasa tumeanza safari, lakini hii safari wenzetu wameanza siku nyingi sisi tupo kwenye safari hii, tumepanga katika mwaka huu wa fedha kukamilisha *framework* itakayoeleza namna gani uchumi wa kidigitali unajengwa. Katika *framework* hii tutazungumza ushiriki wa kila mmoja, lakini tutapitia Sheria, Sera, Kanuni na Taratibu tutazibadilisha na zipo nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapa mfano mzuri, kaka yangu Mheshimiwa Jerry Silaa, Mbunge wa Ukonga,

amezungumza namna ambavyo Mtanzania leo anatembea na vitambulisho vingi sana. Kuvijumlisha hivi vitambulisho kuna hitaji mabadiliko ya sera, ya sheria ya kanuni na taratibu na sisi tunaona, dunia tunakoenda huitaji kutembea la rundo la vitambulisho, lakini ili ufike huko, lazima utengeneze mabadiliko ya baadhi ya hizi sheria ambazo sasa kwenye *blue print* na hapa nimeeleza tumepata zaidi ya dola milioni mia moja hamsini kwa ajili ya kuchora hii ramani ya huko ambako tunataka kuipeleka Tanzania yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo nadhani muhimu niiguse, nia ya Rais Samia na Serikali ya Awamu ya Sita ni kuongeza na kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa kujieleza katika nchi yetu. Ameingia madarakani yale mambo ambayo hayakuhitaji mabadiliko ya sheria na wote nyie ni mashahidi tumechukua hatua kubwa na wanahabari wanajua. Tumefungulia vyombo Habari yakiwemo magazeti, na mitandao. Baadhi ya sheria ambazo zipo tumeamua kutozisukuma na kuzitekeleza ili mambo yaende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni nia njema na thabiti kwamba jambo hili tunataka tulifikishe. Nataka niahidi nimesikia mchango wa dada yangu Mheshimiwa Ester Bulaya, niwaahidi wanahabari mwaka huu wa fedha tunaouombea fedha sasa tutakamilisha mabadiliko ya Sheria ya Huduma ya Habari kama ambavyo inatakiwa na tumeanza mchakato, tumekutana nao mara. Niwaambie nia ya dhati ipo, tutafanya mabadiliko na tutasonga mbele kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwathibitishie kwamba, zipo sheria Wabunge wamezitaja hapa kwa mfano Sheria ya *Data Protection* Sheria ya *TEHAMA* na sheria mbalimbali. Maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita, Mama hodari kabisa, amesema tupitie sera, sheria na kanuni tuone namna ambavyo zile ambazo zimepitwa na

wakati tuzitengeneze tuzirekebishe. Niwaahidi Wizara yangu sheria zote, sera zote, kanuni zinazohusika na Wizara hii tutawashirikisha vya kutosha wadau ili tutunge sheria zinazotokana na mawazo ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani pia nigusie, nashukuru kwa pongezi walizotupa katika usimamizi wa zoezi la anuani ya watu na makazi. Jambo hili tumelisimamia wote Jambo hili ni la Watanzania pale tulipofikia kuna mapungufu ya hapa na pale, tumeomba fedha na tunaendelea kurekebisha na tutashirikiana pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru usimamizi wa Waziri Mkuu, lakini wa Rais, Rais aliamua kwa makusudi akatoa zaidi ya bilioni 28 kwenda kutekeleza jambo hili. Aliahidi, akatoa na hapa ni vizuri nikasema hoja ya kaka yangu Mheshimiwa Kapinga. Maelekezo hatukuelekeza kuhamisha fedha za miradi ya maendeleo mingine kupeleka kwenye zoezi la anuani na makazi, kama kuna mahali wamefanya hivyo, wamekosea fedha husika zirudishwe kwenye miradi husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulichoelekeza, kwanza kuna fedha zilikwenda na kwa Mbinga tumepeleka zaidi ya milioni mia moja na kitu kwa ajili ya zoezi hili. Sasa kama kuna mahali fedha zimetumika za miradi marufuku kutumia fedha za miradi mingine ya maendeleo kutekeleza zoezi la anuani za makazi. Tumesema fedha zitumike, kama kuna wadau, kama kuna taasisi za Serikali zitumie fedha za dharura na siyo kuhamisha fedha za miradi ya maendeleo, hilo halikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ilitolewa hapa, dada yangu Mheshimiwa Salome ameniambia bando ngoja niseme. Jambo hili tutalieleza vizuri wakati wa semina, lakini hapa niseme jambo, bando kama bando ni huduma ya ziada kwenye huduma ya *data,* ni huduma ya nyongeza,

mtoa huduma anaamua kutengeneza bandos nyingi ili akupe wigo wa kufanya uchaguzi wa huduma unayoitumia. Hapa kwetu asilimia 98 ya watumiaji wa *data* wanatumia hii huduma ya ziada, majirani zetu asilimia kubwa wanatumia *basic tariffs* hawatumii hizi bado kwa sababu bado ni kidogo mno, ni sehemu ndogo na kama ninavyosema ni huduma ya ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji hapa wa hizi *data*, data moja inazalishwa kutoka Sh.2.3 mpaka Sh.9.0. Hapa Tanzania tunauza kwa Sh.1.5 *as we are talking* tunauza chini ya gharama ya kuizalisha hiyo *data.* Sasa watoa huduma walichofanya wakaona katika msingi ukitaka kutumia *basic tariffs* huduma zitakuwa za ghali sana, ndio maana wakaamua kuweka bado nyingi. Sasa bando ni sawa sawa leo ukinunua tiketi yako, tiketi ya kuitumia kwa mwezi mmoja kwenye basi ukiitumia siku moja muda wa mwezi mmoja ukaisha huwezi kwenda kuidai hii tiketi kwa sababu hii umepewa ofa, kama hautaki kutumia ofa ya mwezi mmoja, tumia ya siku moja moja, ndio biashara ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kuna maneno yanasemwa kama vile kuna wizi, kuna wizi. Nasema tumefanya utafiti mwingi wa kutosha na tukatoa wito, kama kuna mtu anadhani ameibiwa, njooni tufanye uchambuzi. Hata hivyo, hebu tujiulize, kampuni zinazotoa na naogopa sana kuwahukumu haya makampuni kwamba wanatuibia, mimi kama Serikali bila kuwa na ushahidi hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu twendeni Kampuni ya *VODACOM*, ya *Tigo*, ya *Airtel* wapo *listed* kwenye soko la hisa, wanafanyiwa ukaguzi, niambieni ni nani anakaa kwenye kampuni hii kubwa ya simu anasema twendeni tukaibe *data*, halafu inapitishwa kwenye kikao, halafu anaambiwa yule mtaalam anaye-*set* kwa sababu wizi lazima u-*set,* ana-*set* wizi, hii fedha inayotokana na wizi nani anachukua, kwamba inaingia kwenye vitabu vya kampuni ambayo ipo *listed*

kwenye makampuni, *serious* Hapana! Nataka kuwaomba Watanzania, twendeni taratibu, naamini uelewa *TCRA* wametoa *press release* nzuri sana, wakaeleza kwa kirefu na hili jambo likapungua kelele zake. Nataka kwenye Semina tutakayoifanya hapa niwaombe …

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nape, dakika moja.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, …Waheshimiwa Wabunge waje na ushahidi halafu waje tufanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakuu wa Taasisi na wataalam ambao kwa kweli wamenisaidia katika kutekeleza majukumu yangu. Natambua mchango wenu na nawashukuru sana. Niwashukuru sana wanahabari wa Tanzania kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kutekeleza majukumu yetu, lakini niyashukuru makampuni ya kutoa huduma na hasa makampuni yanayotoa huduma za simu, hasa simu za mkononi kwa uwekezaji wao, kwa teknolojia wanayoitoa, ulipaji wa kodi na huduma mbalimbali, lakini ajira walizowapatia Watanzania. Kwa niaba ya Serikali naomba tuwapongeze sana na kuwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge, chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Kakoso na Makamu wake Mheshimiwa Mama Anne Kilango kwa usimamizi wao mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana wewe kwa kunipa nafasi na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**NAIBU SPIKA:** Kamati ya Matumizi.

**MWENYEKITI:** Tukae.

Katibu!

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza na Kitabu cha Pili - Matumizi ya Kawaida. Fungu 68 Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Ukurasa wa 448

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 68 – Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*..........Sh. 1,950,459,724

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa nina jina moja tu hapa la mshahara wa Waziri ambaye ni Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na nisiporidhika nitatoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti nyingi za Wizara hii na Wizara ya kazi tumekuwa tukizungumzia maslahi ya Waandishi wa Habari. Waandishi wa Habari wanafanya kazi kwenye mazingira magumu mishahara yao midogo wawe *correspondent* na waajiriwa kwa *level* zote na hatujaona

jitihada za dhati za kuhakikisha Waziri anatengeneza mazingira mazuri ya Waandishi kulipwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio Waandishi hawa hawa wapiga picha, Waandishi hawa ambao wapo viongozi wanazunguka nao kwenye misafara yao ili kutoa habari za kazi zinazofanywa na Serikali na wananchi wanapata. Mbaya zaidi Waandishi hawa michango yao haipelekwi kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na nimelisema hili na kuna Waandishi walishafanya *press,* wakataka kuandamana, wakati Mheshimiwa Jenista alipokuwa kwenye hii Wizara, alikiri na akasema, atafanya ziara kwa kila chombo cha habari kuhakikisha michango ya Waandishi wa Habari ambao wana mishahara midogo, ambao wanafanya kazi kwenye mazingira magumu, lakini hatma yao bado inachezewa, fedha zao hazipelekwi kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiporidhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nitashika shilingi. Je, Serikali inasemaji kuhusiana na jambo hili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nimshukuru dada yangu Mheshimiwa Ester, mwanahabari mkongwe, wa siku nyingi, kwa kuwatetea wanahabari wenzake. Amelelewa na Chama cha Mapinduzi akiwa gazeti la Uhuru, ndiyo maana nakubaliana naye. Ni matumaini yangu kwamba ataruhusu bajeti hii ipite kwa sababu malengo yake ni mema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme hivi, ni kweli wanahabari wa nchi hii wanaishi maisha ya shida na ajira zao hazieleweki. Wengi wao hawana ajira, wengi wao hawana mikataba ya ajira, wengi ni *deiwaka* wanajitolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipoleta Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016, moja ya lengo kubwa illikuwa ni kuitambua tasnia ya habari kama taaluma inayojitegemea ili ipate heshima yake. Katika kuitambua kwenye ile sheria kuna mambo yalipendekezwa moja ilipendekezwa kiwango cha elimu, kwa sababu ikiwa kila mmoja anaweza kwenda akapewa kazi ya kuandika Habari, hatathaminiwa hatapewa mkataba, hatapewa ajira ya maana, atakuwa anajishikiza tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukasema tukiweka kiwango cha elimu, kitasaidia kuwalazimisha waajiri kwanza wawape mikataba, lakini pia waingie kwenye mfumo ambao mafao yao yatalindwa na sheria. Kwa hiyo sheria hii ambayo tumesema tunaifanyia sasa marekebisho, sheria hii itakwenda kukidhi na kujibu haja ya heshima ya wanahabari, mafao yao na stahiki zao. Kwa hali tuliyonayo, tukiendelea nayo hivi hata *product* inayotokana na kazi zao, itakuwa *compromised* kwa sababu maslahi ni madogo, wanakuwa *subjected* kwenye kuendeshwa na wenye fedha ili *product* itoke ile wanayoitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Mbunge apitishe bajeti yangu ili tukafanye marekebisho ya sheria, kwenye sheria hii tutalinda haki na maslahi ya wanahabari. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashika shilingi na natoa hoja Wabunge tujadili jambo hili ni zito sana. Naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bulaya, zaidi ya sheria mpya unafikiri kuna nini kingine kipya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *mmh,* tunataka *commitment,* kuna *commitment* nahitaji hapa, *this is very serious issue*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru…

**MWENYEKITI:** Subiri kwanza, mbona una haraka haraka wewe. *(Kicheko*

Mheshimiwa Kunti na Mheshimiwa Nusrat. Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nadhani suala ambalo ameleta Mheshimiwa Bulaya ni la msingi na lengo lake ni kuisaidia Wizara hususani Waziri. Unavyokuwa na Waandishi wa Habari au waajiriwa…

**MWENYEKITI:** Dakika tatu.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** …ambao wako *secured,* wanaweza kufanya kazi yao kwa weledi zaidi. Kwa hiyo nazidi kusisitiza kwamba ni jambo la msingi sana fedha zao ziweze kuwekwa kwenye Mifuko ya Hifadhi kwa lengo la wao kuwa na *assurance* ya kazi yenyewe wanayoifanya. Tumeona mara nyingi Waandishi wa Habari wakiwa kwenye *risk* na tumeona wengine wakifa wakiwa kazini, sasa kama mtu yupo kwenye *risk* ya aina hiyo bado hajui hatma yake, anakuja kustaafu anaanza kufanya madai kama ambavyo tumekuwa tunaona wastaafu wengine, nadhani hilo jambo siyo sahihi. Mheshimiwa Waziri hapa atuambie ni lini hilo suala litaweza kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunakwenda kikanuni, lakini majibu ya Waziri yalitosha kabisa ku-*satisfy* hoja kamili ya Mheshimiwa Ester Bulaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hakuna *commitment* kubwa unayoweza kuiweka hapa katika mazingira ambayo hawa wanahabari tunaotaka kuwatetea hawana mikataba, hawana haki za kisheria za kuwaweka pale, hata ukienda mahakamani wanashindwa. Ndio maana wengi wenye matatizo haya hawaendi mahakamani, wanataka tutafute *solution* za kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *solution* ya kisiasa ni kutunga sheria itakayowalinda, pitisheni bajeti, tukatunge sheria tuwalinde, kila mwenye nia njema ya kufanya jambo hili liende pitisheni bajeti hapa, tukamalize hii kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kunti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Mheshimiwa Waziri amesema vizuri tunachokitaka sisi hapa suala la sheria si suala la dharura, wala hawa Waandishi wa Habari hawajaanza kazi leo. Mheshimiwa Waziri sio mara yake ya kwanza kuwa Waziri wa Habari, akumbuke miaka mitano iliyopita alikuwa Waziri kwenye Wizara hii hii, alikuwa wapi kuleta sheria hiyo mpaka leo anarudi tena hapa anakuja kutuahidi kwamba ataleta sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vitu ndiyo maana tunasema tunataka Serikali na Mawaziri wanapokuja hapa kuleta hoja zao walete hoja zenye mantiki. Pia wanaposimama kutujibu Wabunge wawe wanasimama ikiwa inatoka ndani ya nafsi zao, kwa sababu hivi vitu inakuwa ni *story* tu ndani ya Bunge

miaka nenda, miaka rudi. Hawa watu wanapata shida, wanaumia, Waziri anakiri hawana mikataba ya ajira, mtu anakufa familia yake inateketea, inaumia huko mtaani, lakini Mheshimiwa Waziri leo anayesimamia Wizara hii akifa familia yake inalindwa na inapata mafao…

**MWENYEKITI:** Ahsante muda wako umekwisha. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Kunti, anaongea hoja za msingi. Nadhani ni suala la uelewa, nilikuwa Waziri hapa, ndiye niliyeleta Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 iliyoshindikana kwa mwaka 23. Nilisimamia nikaileta hapa na kwenye ile sheria tukaweka baadhi ya taratibu ambazo zinakwenda kutatua hili tatizo, shida iliyotokea ni kwamba moja ya kitu kilichowekwa ni elimu, mbili tukasema kuwepo na namna ambayo hawa wanahabari watatenganishwa wanahabari wa taaluma na *citizen journalism*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mhandishi wa Habari kwa kusomea, siwezi nikawaacha Waandishi wa Habari wenzangu wakahangaika. Kwa hiyo, ni jambo ambalo ukisema eti tunapiga blaa blaa, nakuja kupiga blaa blaa kwa maisha ya watu, sikuzoea kufanya hivyo, ndiyo maana tunaileta sheria hapa ili tufanye mabadiliko ili tuwalinde wanahabari. Huko tunakotaka kwenda ndiyo maana nikasema, leo hata akienda mahakamani tukitaka kukaza, tukasema hebu tubanane ambao hawana mikataba waondoke kwenye vyombo vya Habari, wadogo zako, kaka zako ndugu zako watakwenda mtaani. Tumerekebisha hili jambo twende mpaka tukarekebishe sheria ili tuwasaidie na wanahabari wanaunga mkono jambo hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa majibu mazuri sana Mheshimiwa Waziri. Sasa tunaingia kwenye *Guillotine*.

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*..........Sh. 1,950,459,724
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*............Sh.483,378,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit* ................Sh. *667,961,040*
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit* ...........................Sh. 242,028,400
Kifungu 1005 – *Legal Service Unit* ..........................Sh. 270,463,604
Kifungu 1006 – *Government Communication Unit*Sh. 192,585,300
Kifungu 1007 – *Procurement Management Unit*...Sh. 324,999,900
Kifungu 2001 – *Communication Division*..............Sh.1,656,712,632
Kifungu 2002 – *Information, Comm.and Technology*Sh.1,675,009,400
Kifungu 4001 – *Information Services Department*Sh.18,815,748,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahamia kwenye Kitabu cha Matumizi ya Maendeleo Fungu 68 – Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ukurasa wa 194

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tusikilizane, tunajibu hoja hapa tusikilizane, nataka kusikia ndiyo kwa makelele mengi sana. *(Kicheko)*

## MATUMIZI YA MAENDELEO

### Fungu 68 – Matumizi ya Maendeleo

Kifungu 2001 – *Communication Division*............Sh.43,300,000,000
Kifungu 2002 – *Information, Communication and Technology*......................Sh.189,000,000,000
Kifungu 4001 – *Information Services Department*Sh.23,477,440,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi zakeika.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Mtoa Hoja. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia kifungu kwa kifungu Bajeti ya Fungu 68 - Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na kuipitisha bila mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kuhusu hoja ya kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Nikushukuru sana Mheshimwa Waziri wa Habari pamoja na Naibu wako na Katibu Mkuu na timu na taasisi zote ambazo unaziongoza kwa kazi nzuri mliyoifanya. Kwa kweli mabadiliko yapo na hoja hii ya sheria umekuja nayo miaka mingi na ninajua utaiweka vizuri ili Waandishi wa Habari wote waweze kupata haki stahiki za malipo na kazi wanazozifanya.

Nina wageni hapa wa Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani kutoka Singida, Mwenyekiti na Katibu wa Baraza la Wazee wa Mkoa wa Singida naomba kuwakaribisha Bungeni, karibuni. Anaitwa Ndugu Ramadhani Ituji haya popote ulipo ulishatambulika upo rasmi ndani ya Bunge. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge nataka niwakumbushe kuna semina ambayo itaanza sasa hivi kwenye Ukumbi wa Msekwa naomba tukishatoka hapa mwende kwenye semina.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo haya, niahirishe shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 7.25 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 23 Mei, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*